# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA SABA

### Kikao cha Saba – Tarehe 14 Aprili, 2022

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Katibu!

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa George Ranwel Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi.

Na. 58

### Uhaba wa Vifaa vya Maabara kwa Masomo ya Sayansi – Jimbo La Mbozi

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka vifaa vya maabara kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi katika shule za sekondari katika Jimbo la Mbozi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, Mbunge wa Jimbo la Mbozi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikipeleka fedha katika shule za sekondari kwa ajili ya umaliziaji wa miundombinu mbalimbali ikiwemo maabara za masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2022/2023 Serikali imetenga Shilingi bilioni 5.14 kupitia Programu ya *SEQUIP* kwa ajili ya kununua vifaa vya maabara kwa shule 234 za Sekondari za Kata. Hata hivyo, Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na 2021/2022 imepeleka vifaa vya maabara katika shule za

sekondari 1,258 nchini zilizokamilisha ujenzi wa vyumba vya maabara zikiwemo shule 12 za sekondari za Wilaya ya Mbozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kugawa vifaa hivyo nchini ikiwa ni pamoja na shule za Wilaya ya Mbozi kwa kuzingatia mahitaji na upatikanaji wa fedha na wadau mbalimbali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa George.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali. Lakini Wilaya ya Mbozi ina shule za sekondari 44, Serikali imepelekea vifaa vya maabara kwenye shule za sekondari 12 tu. Sasa je, nini *commitment* ya Serikali katika hizi bilioni tano ambazo zimetengwa mwaka huu wa fedha kwa ajili ya kusaidia shule ambazo katika Wilaya ya Mbozi hususan Jimbo la Mbozi ambazo hazijapata vifaa vya maabara? Naomba kuuliza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa ambalo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Mbozi ni kwamba tutapeleka fedha kwa ajili ya shule za sekondari ambazo ameziainisha katika jimbo lake, zile zote ambazo zitakuwa zimemaliza maabara katika mwaka wa fedha unaokuja na zile nyingine ambazo tumeshanunua vifaa tunasubiri tu zile shule ambazo zitaleta taarifa tupeleke.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, natambua kazi njema anayoifanya katika Jimbo la Mbozi na ninajua ameji-*commit* kwa kiwango gani kwa wananchi wake. Kwa hiyo, nimuondoe shaka kwenye hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Jimbo la Mbulu Vijijini ziko sekondari 16 lakini sekondari 11 hatuna vifaa vya maabara ya sayansi.

Je, Mheshimiwa Waziri lini utapeleka vifaa hivyo ili wanafunzi waweze kujifunza vizuri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Flatei Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba kama nilivyojibu katika swali la awali na swali la nyongeza la Mheshimiwa George Mwenisongole, ni kwamba katika maeneo yote ambayo wameshamaliza ujenzi wa maabara sisi tutapeleka vifaa ikiwemo katika Jimbolake la Mbulu Vijijini. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge aondoe wasiwasi katika hilo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko.

Na. 59

**Athari za Watumishi Kuishi Mbali na Watoto Wao**

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA K.n.y. MHE. HUSNA J. SEKIBOKO** aliuliza:-

Je, kuna athari gani za kijamii kwa watumishi wenza kuishi mbali na watoto wao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, familia ni taasisi muhimu sana katika kuleta ustawi kwa jamii na Taifa kwa ujumla. Ni kweli kuwa yapo madhara ya kijamii kwa watumishi wenza kuishi mbali na watoto wao madhara hayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongezeka kwa vitendo vya ukatili kwa watoto majumbani; kukosa malezi chanya inayopelekea watoto kuathirika kisaikolojia; watoto kutokupata lishe bora inayopelekea udumavu na mmomonyoko wa maadili na kuvunjika kwa ndoa kunakosababisha watoto wa mtaani. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Katimba, kwa niaba.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Nashukuru sana kwa majibu ya Serikali amefafanua vizuri kabisa madhara yanayotokana na wenza kutokuwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu, ukiangalia athari ambazo zinatokana na wenza kutokupata nafasi ya kufanya kazi wakiwa wako pamoja, ni kubwa sana na zinaathiri jamii; na sisi tunajua kwamba familia bora ndiyo inajenga jamii bora. *(Makofi)*

Sasa ni nini mkakati wa Serikali wa kukabiriana na hili suala lililopo mbele yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, je, ni nini kauli ya Serikali kwa waajiri wale ambao hawatoi fursa ya kuhakikisha

kwamba wafanyakazi wao wanapata haki ya kufanya kazi wakiwa karibu na wenza wao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zainab kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza linahusu madhara ambayo yanawapata watoto wakati wenza wao mbalimbali. Serikali kupitia MTAKUWWA imeunda Kamati Maalum za kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake kwa ngazi zote. Maafisa wetu wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii wanapita kuelimisha kwa njia za vyombo vya habari, mikutano na makongamano mbalimbali pamoja na midahalo ya kitaifa ambayo inaendelea kila mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, nini tamko la Serikali kuhusu wenza ambao wanakatazwa kuwafuata wenza wao walipo. Kanuni na sheria zipo ambazo zinaeleza kila kitu katika Serikali. Serikali yetu imeunda sera, kanuni na miongozo ambayo inawaelemisha wananchi kufuata sheria zitakazowafanya wapate vibali vya kwenda kukaa na wenza wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelezo zaidi napenda kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge tujifunze kukaa na watoto wetu wakati wowote ule kuwapa muda maalum ambao tunaweza kuwaelimisha elimu ambayo Serikali yetu na utamaduni wetu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri majibu yako mazuri ya kifamilia, hongera sana ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake ambayo yameonesha msingi wa hoja hii muhimu sana ya kuhakikisha kwamba ustawi wa familia kwa maana ya wenza na watoto kuishi pamoja ili kuweka makuzi bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilihakikishie Bunge lako tukufu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma inadhamana ya kuangalia ustawi wa watumishi wote nchini. Baada ya kutambua tatizo hili la wenza kukaa maeneo tofauti tofauti na kusababisha kuwa na athari kubwa katika malezi ya familia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ameshatoa Waraka Namba 452501 kifungu cha 6(b) kimetoa masharti ya kumhakikishia mtumishi ana uwezo wa kuomba kibali cha kuhamia kwa mwenza wake endapo eneo husika litakuwa na nafasi na atakuwa na uthibitisho wa vyeti vya ndoa na nyaraka nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitoe wito kwa waajiri wote kuhakikisha wanazingatia kifungu cha waraka huo ili kusaidia ustawi wa familia, malezi ya watoto na kuhakikisha kwamba wafanyakazi wetu wanakuwa na fursa ya kuishi na wenza kwa kuzingatia taratibu na miongozo iliyowekwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mawaziri wote wawili mmejibu vizuri sana ahsanteni, kapumzike Mheshimiwa Waziri.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma.

Na. 60

**Ujenzi Uwanja wa Ndege Omukajunguti**

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Uwanja wa Ndege Kimataifa wa Omukajunguti ili kuruhusu ndege kubwa kutua Bukoba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango wa kujenga kiwanja kipya cha ndege katika eneo la Omukajunguti, Mkoani Kagera ili kuwezesha ndege kubwa ziweze kuruka na kutua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uthamini wa awali kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi watakaoathirika na utekelezaji wa mradi ulishafanyika. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ikiwa ni maandalizi ya kuanza kwa ujenzi wa kiwanja hicho cha ndege. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ishengoma.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, pamoja na nia nzuri ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na wingi wa abiria wanaotumia uwanja wa ndege wa Bukoba na kutokana na ufinyu na huduma hafifu za uwanja wa ndege wa Bukoba. Uwanja wa Bukoba mwaka 2020 tulipokea abiria zaidi ya 44,000 na mwaka 2021 tumepokea abiria 45,000.

Je, Serikali haioni kuna uharaka wa kujenga Uwanja wa Ndege wa Omukajunguti?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, katika majibu ya Serikali imesema wamefanya tathmini ya kulipa watu watakaopisha ujenzi wa uwanja huo.

Je, ni lini Serikali italipa fidia kwa wakazi wa eneo lile wa Mkajunguti ili waweze kupisha ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Omukajunguti? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na idadi kubwa ya abiria ambao ndio wanatumia uwanja wa Bukoba ndiyo maana Serikali imeamua kwamba kuna haja ya kujenga uwanja mkubwa zaidi kwa sababu uwanja wa Bukoba kwa mahali ulipo hauwezi kuendelezwa kwa maana ya kuipanua na ndio maana Serikali imetafuta eneo jipya ambalo uwanja mkubwa unaweza kujengwa ili kuruhusu ndege kubwa hasa tukizingatia umuhimu wa uwanja huo na abiria walivyo wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala la fidia, Serikali ilishafanya tathmini ya awali ambayo kwa mujibu wa fidia hatuwezi kuitumia tulifanya tathimini ilikuwa inaenda kwenye bilioni tisa. Kwa hiyo, kuna utaratibu tunaufanya tuweze kurudia ile tathmini twende na hali ya sasa na mara tutakapokamilisha basi fidia italipwa kabla ya kuanza ujenzi wa uwanja huo wa ndege wa Omkajunguti. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kihenzile.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru; kwenye Wizara hiyo hiyo ya Ujenzi na Uchukuzi tuna changamoto kubwa sana ya barabara ya Mafinga – Mgololo na Nyororo – Mtangwo ambazo zimeahidiwa kuanzia Serikali Awamu ya Nne mpaka Awamu ya Tano, na tarehe 26 Aprili, 2021 Serikali

Awamu ya Sita imetoa *commitment letter* kuanza kujenga barabara hizo.

Nataka kujua ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa ahadi hii ya kuwajengea barabara wananchi Mufindi Kusini ili waweze kunufaika na barabara hizo? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kihenzile, Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliamuahidi Mheshimiwa Mbunge na ni ahadi ya viongozi wa Kitaifa tangu Awamu ya Kwanza kwamba barabara hii ambayo ni barabara kuu lakini ni barabara kimkakati kwamba tutaijenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge endapo bajeti ambayo tunaenda kuipitisha itapitishwa bila mabadiliko, barabara hii imeweza kuwekwa kwenye mpango ili iweze kujengwa kwa kiwango lami hasa tukizingatia kwamba sehemu kubwa ya mazao ya mbao tunayoyaona Tanzania yanatoka katika eneo hilo.

**NAIBU SPIKA:** Asante Mheshimiwa Agnesta

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, naomba niende moja kwa moja kwenye swali langu dogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uwepo wa viwanja vya ndege gharama au nauli za ndege zimekuwa juu sana nini kauliya Serikali kuhusiana na kuhakikisha nauli hizi zinakuwa himilivu kwa Watanzania hasa baada ya kuwa wamehamasika sana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la nauli ni suala la kibiashara na nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wenzetu wa *ATCL* kuna taratibu ukifanya *booking* mapema bei inashuka lakini kama utanunua tiketi utaratibu wa mashirika mengi ya ndege kama utachelewa kununua tiketi ya ndege siku zote bei inakuwa juu, lakini kama utafanya *booking* mapema basi nauli inakuwa ni ya chini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri inatosha ameshakuelewa. Mheshimiwa Hasunga, jiandae Mheshimiwa Maboto

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naomba kuuliza Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba inakamilisha uwanja wa ndege wa Songwe kwa kuweka vifaa vya kupoozea mazao yaani *cold rooms* ili kusudi wananchi wa Wilaya ya Mbozi na mikoa ya Nyanda za Juu Kusini waweze kuhakikisha kwamba wanasafirisha maparachichi na matunda mengine?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hasunga, Mbunge wa Vwawa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uwanja wa ndege wa Songwe sasa hivi tuko kwenye kukamilisha kuufanya kuwa kati ya viwanja vikubwa vya Tanzania vya ndege ambapo kutakuwa na uwezo wa kupokea ndege zote kubwa zinazoruka katika Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hatua ya pili ni kujenga *storage facility* zikiwepo na hizo za kutunza vifaa ambavyo ni baridi kwa ajili ya kusafirisha nje na ndio maana Serikali ina mpango tayari wa kununua ndege ya kusafirisha mizigo. Kitu cha

kufanya ni kujenga hizo *storage facility* ikiwepo Mkoa wa Mbeya, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Maboto nilishakutaja, jiandae Anatropia

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, barabara ya Buramba – Bunda - Nyamuswa inayotekelezwa kwa kiwango cha lami wananchi wamebomolewa nyumba zao pale. Ni lini Serikali itawalipa fidia yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maboto Mbunge wa Bunda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ilishafanyika, wananchi walishaainishwa na sasa hivi Serikali inafanya kupitia yale malipo ili waweze kulipa fidia hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, licha ya juhudu za Serikali za kuendelea kukarabati viwanja wa ndege bado vingi vimekuwa vinafanya kazi mchana tu. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha viwanja vinafanya kazi saa 24?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anatropia, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa hivi viwanja vyote

tunapoongelea kiwanja cha Mbeya, kiwanja cha Songwe, kiwanja cha Mtwara, kiwanja cha Msalato, kiwanja cha Geita na hata hivyo viwanja vile tunavyojenga Sumbawanga, Kigoma, Tabora na Shinyanga vyote viko kwenye mpango wa kujengewa taa ili viweze kufanya kazi saa 24 na kazi hiyo inaendelea. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara hiyo hiyo Mheshimiwa Christina Christopher Mnzava.

Na. 61

**Ujenzi Uwanja wa Ndege Shinyanga**

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Shinyanga kama ilivyoanishwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali la Mhe. Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga ni miongoni mwa miradi ya ujenzi na upanuzi wa viwanja vya ndege vinne ambavyo ni Kigoma, Tabora, Sumbawanga na Shinyanga inayotarajiwa kutekelezwa kwa ufadhili wa Benki ya Uwekezaji ya Ulaya *(European Investment Bank - EIB)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa matakwa ya kimkataba kati ya Serikali na *EIB* yamekamilishwa na mfadhili tayari ameshatoa fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa miradi hii. Aidha, Mhandisi Mshauri pamoja na mkandarasi wameonesha

utayari wa kuanza kazi na mikataba kati yao na Serikali ilishasainiwa tangu mwaka 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mradi huu umechelewa kuanza kwa wakati, Mhandisi Mshauri pamoja na mkandarasi wameomba ongezeko la fedha katika kipengele cha *price adjustment* ili kuweza kuendana na mabadiliko ya bei ya bidhaa kwa soko la sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imejipanga kuanza utekelezaji wa mradi huu kabla ya mwaka wa fedha 2021/2022 haujaisha, nah ii itatokana na endapo mkandarasi atawasilisha hati ya dhamana ya malipo ya awali kwa wakati. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Eeh majibu yenu ni marefu sana na tulishakubaliana majibu yawe mafupi kwa hiyo *next time* suala hili linaweza likapata mgogoro. Mheshimiwa Dkt. Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli majibu ya Naibu Waziri yananifikirisha sana. Mfadhili ameshapatikana, fedha zimeshatolewa, mkataba umesainiwa mwaka 2017 na wameomba *price adjustment. (Makofi)*

Je, ni lini Serikali itaongeza hizo fedha ili kazi ianze?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili Naibu Waziri amesema kwamba ujenzi utaanza endapo mkandarasi atawasilisha hati ya dhamana ya malipo; ni nini kauli ya Serikali endapo mkandarasi hatawasilisha kwa wakati kama alivyosema kwenye jibu lake la msingi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, *price adjustment* haizuii uwanja kuanza, lakini ni utaratibu kwa kuwa mkataba ulikuwa wa zamani lazima tuwajulishe hawa wafadhili kwamba kutakuwa na

ongezeko la bei na endapo pia hawatataka kuongeza Serikali itaendelea kujenga huu uwanja kwa ile nyongeza ambayo itakuwepo kwani tayari wameshatoa milioni 12 *United States dollars* kwa ajili ya kuanza ujenzi wa viwanja hivyo.

Mheshimiwa Naibu spika, na hati ya dhamana ni kwamba tayari mkandarasi yuko tayari kuanza kujenga na sasa hivi anachofanya tu ni kuandaa hizo hati ili aweze kuziwasilisha baada ya hiyo fedha kutolewa na wafadhili, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Asia Hamlaga.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana ni Asia Halamga, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Naibu Waziri amewahi kuja kukagua eneo la ujenzi wa uwanja wa ndege lililopo kata ya Mwada eneo lenye takribani ya hekari 600 na halina mgogoro wowote.

Je, ni lini Serikali sasa italeta fedha kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa ndege wa Mkoa wa Manyara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asia Halamga, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli uwanja huu utajengwa eneo linaloitwa Mwaga na sasa hivi tunavyoendelea ni kwamba tuko kwenye hatua ya utwaaji wa eneo hilo na pia lilikuwa ni agizo la Mheshimiwa Makamu wa Rais wakati anafungua daraja la Magala kwamba kazi hiyo ifanyike haraka. Kwa hiyo Serikali tuko tunaendelea kulifanyia kazi tuweze kutoa na kuwalipa fidia halafu ujenzi uanze.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kassinge.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi ya swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili kwa bajeti inayoendelea inayoishia Juni, 2022, ilipitisha kwamba kiwanja cha ndege cha Kilwa Masoko kifanyiwe ukarabati na maboresho, mpaka tunazungumza kazi iliyofanyika ni ya kilometa moja kwa kiwango cha changarawe bado mita 950.

Nini maelezo ya Serikali kuhusiana na mita 950 zilizobaki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kassinge Mbunge wa Kilwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali ilivyoahidi tumeshakamilisha kilometa moja na tutaendelea kuzikamilisha hizo kilomita 900 zilizobaki kwa kiwango cha changarawe ili tuweze kutimiza ile ahadi ambayo tuliahidi kuifanya, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Genzabuke, jiandae Sanga.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kigoma ni lango kuu la uchumi wa nchi yetu kwa sababu umepakana na nchi za jirani za DRC Congo na Burundi. Mara nyingi serikaliimekuwa ikiahidi kuja kujenga uwanja wa ndege Kigoma na kuweka taa kwa maaa ya ndege ziweze kuruka usiku.

Sasa nataka Waziri aniambie ni lini Serikali itakuja kuweka taa na kuongeza uwanja wa ndege wa Mkoa wa Kigoma kwa sababu Kigoma imepakana na nchi jirani za Congo na Burundi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Kigoma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanja cha Kigoma ni kati ya viwanja vinne ambavyo ni Kigoma, Tabora, Sumbawanga na Shinyanga ambavyo vinafadhiliwa na *European Investment Bank* na ni kati ya viwanja ambavyo tayari fedha imeshatolewa na moja ya kazi ambayo fedha hii inaenda kufanya ni kujenga uzio, jengo la abiria, *runway* ikiwa ni pamoja na kuweka taa ili kiwanja hiki kiweze kufanya kazi saa 24.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tayari Serikali inaenda kujenga huu uwanja kama ulivyosema. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga, jiandae Mheshimiwa Mtaturu.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante uwanja wa ndege Mkoa wa Njombe haupo kabisa kwenye utekelezaji wa bajeti uliopita na hata bajeti iliyopo ya sasa, lakini kwenye ilani umekuwa ukiutaja kama ni moja kati ya viwanja mnaenda kuvitenga.

Wananjombe wanauliza ni upi mkakati wa Serikali kujenga uwanja wa ndege Mkoa wa Njombe kwa sababu uwekezaji wa parachichi na mambo mengine sasa hivi wanauhitaji mkubwa, lakini wananjombe walioko nje wengi matajiri wanahitaji kusafiri kupitia ndege kurudi Njombe ni upi mkakati wa Serikali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sanga, Mbunge wa Makete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nikweli kwamba uwanja wa Njombe ni muhimu na eneo lipo tayari. Kwa hiyo, nimhakikishie

Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itakapopata fedha na hasa kulingana na umuhimu wa uwanja huo tutaanza kufanya kwanza utwaaji na kulipa fidia lakini pia kuanza usanifu wa kina, lakini hili Mheshimiwa Mbunge itategemea na upatikanaji wa fedha na utekelezaji wa ilani ni wa miaka mitano. Kwa hiyo nikuhakikishie kwamba hata kama kwa sasa hatujaanza kutekeleza lakini utatekelezwa katika miaka hii mitano, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Mtaturu.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Singida uko karibu sana na Makao Makuu ya nchi Dodoma na kwa sababu ya kiusalama uwanja wa ndege wa Singida ni muhimu sana na kwa sababu Marais wote wawili wametaja kwenye hotuba zao hapa Bungeni Rais John Pombe Magufuli pamoja na Rais Samia Suluhu Hassan walisema katika viwanja 11 na kiwanja cha Singida kitajengwa.

Sasa naomba nijue ni lini sasa Serikali itatenga fedha ili kujenga uwanja ule ambao upo karibu na Makao Makuu ya nchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mtaturu, Mbunge wa Singida kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya Mheshimiwa Mbunge ni sahihi na ni kweli kwamba viongozi wameahidi uwanja huu uweze kujengwa na mimi naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara tayari ina mpango wa kuanza kufanya tathmini ya uwanja huu ili iweze kuujenga lakini pia kama ulivyosema ni uwanja ambao upo karibu na Dodoma kwa ajili ya usalama. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba

suala hilo Wizara inalo na muda si mrefu itaanza kulifanyia kazi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Jumbe.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuuliza ni lini uwanja wa Mbeya utaanza kutumika usiku na mchana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, Mbunge wa Kyela kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tunavyoongea uwekaji wa taa kwa uwanja wa Mbeya ambao ni *Songwe airport* upo pengine kwenye asilimia 95 uwekaji wa taa, *runway* imeshakamilika zaidi ya mita 3000, uzio na sasa hivi tunakamilisha pia jengo la kisasa la abiria. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba uwanja huu utaanza kutumika, taa zimeshajengwa na utaanza kupokea ndege usiku na mchana ili kuhakikisha kwamba uwanja huo unatumika kwa asilimia 100, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Waheshimiwam, tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Tarimba

Na. 62

### *Taxpayer, Tax Audit* Kufanyika Kila Mwaka

**MHE. TARIMBA G. ABBAS** aliuliza:-

Je, ni kwa nini Serikali isiweke ulazima wa hitaji la kisheria kuwa *Taxpayer Tax Audit* ifanyike kila mwaka badala ya kusubiri miaka mitatu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Kinondoni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438 kifungu cha 45 imeainisha mamlaka ya Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kufanya ukaguzi au uchunguzi wa masuala ya kodi kwa walipakodi wote, wakati wowote na sio kwa kuzingatia muda wa miaka mitatu isipokuwa ni pale tu inapoonekana kuna viashiria vya upotevu wa mapato ya Serikali ili kukomboa kodi ambayo haijakusanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa viashiria hivyo ni Pamoja na: -Mwenendo usioridhisha wa ulipaji kodi; Mlipakodi kutokufuata Sheria za kodi; aina ya biashara au shughuli ya kiuchumi anayofanya mlipakodi husika; na suala lingine lolote ambalo Kamishna Mkuu ataona ni muhimu ili kuhakikisha kuwa kodi stahiki inakusanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa ili kupunguza ulazima wa Kamishna Mkuu kufanya uchunguzi na ukaguzi wa mara kwa mara kwa walipa kodi ni muhimu walipakodi wote kuzingatia matakwa ya sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya kodi iliyopo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Tarimba.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru Serikali kwa majibu yake lakini nikiangalia majibu haya naona kana kwamba yanakinzana na azma ya *blue print* ambayo inataka wafanyabiashara kwa maana ya walipa kodi waweze kufanya biashara zao wa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Siku zote ukaguzi husababisha *interest* na *penalties* kitu ambacho kinafanya ulipaji wa kodi ule unakuwa mgumu. Kuna ukakasi gani kwa Serikali kuweza kuleta mabadiliko kwamba *tax audit* sasa zifanyike kila mwaka?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kwa kuchelewesha hizi *tax audit* wafanyabiashara wanabambikiziwa makodi makubwa sana kiasi kwamba wanakimbilia kwenda mahakamani, fedha za Serikali hazikusanywi inavyopaswa na kwa wakati. *CAG* anazungumza *trillions of moneys* zimekwama kule katika mahakama. Hivi Serikali haioni kwamba ni wakati sasa kurahisisha shughuli za ukokotoaji wa kodi ili fedha za Serikali ziweze zikapatikana kwa urahisi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abbas Tarimba, Mbunge wa Kinondoni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza tunalichukua kama ushauri, Serikali itaenda kufanya utafiti tukiona kwamba umuhimu wa kuwekwa sheria hiyo basi Bunge lako tukufu tutapeleka mapendekezo yetu na kutunga sheria nyingine ambayo tufanye ukaguzi wa kila mwaka kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali lake la pili pia nalo tunaenda kulifanyia ukaguzi na utafiti kama kweli fedha zinapotea basi atatusaidia na Wabunge wenzangu atatusaidia namna gani ya kuweza kudhibiti na kukusanya fedha hizo kwa wakati stahiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Bulaya, jiandae Mheshimiwa Halima.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, nchi yoyote ambayo inahitaji kukusanya mapato kwa wingi na kuwatengenezea mazingira mazuri wananchi wake wamekuwa wakiweka mazingira mazuri ya kodi yaani kodi zinakuwa rafiki si kubwa kulingana na biashara ya mtu anayoifanya. Lakini hapa katikati kodi zimekuwa kubwa kulingana na biashara ya Watanzania wanazozifanya na kumekuwa na malalamiko mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali inamkakati gani wa kuweka kodi rafiki ili mtanzania ajivunuie kulipa kodi ili kuchangia maendeleo katika Taifa lake?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ester Bulaya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeandaa mazingira rafiki ya ulipaji kodi isipokuwa baadhi ya wafanyabiashara wanakuwa ni wababaishaji katika biashara zao baadhi yao, lakini nalo niseme kwamba tunalichukua kwenda kulifanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la Mheshimiwa Tarimba lilisema Serikali inachukua muda mrefu wa kufanya *Tax Audit* matokeo yake watu wanabambikiziwa kodi kubwa. Waziri umesema unataka ukafanye utafiti, *CAG* ameainisha kwamba kuna kesi za kikodi zenye thamani ya zaidi ya trilioni 350…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima uliza swali lako.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, trilioni 350 zimekwama kwa sababu ya kesi za kikodi. Unahitaji kufanya utafiti gani zaidi juu ya suala la Mheshimiwa Tarimba ni muhimu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima Mdee kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliposema kufanya utafiti lazima tujiridhishe na kama kesi zipo mahakamani tunaiachia mahakama ifanye shughuli zake.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa maswali yamekwisha sasa ni matangazo ya wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Wageni wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI ambao ni Watendaji Wakuu wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo; Profesa Riziki Shemdoe - Katibu Mkuu; Ndugu Gerald Mweli - Naibu Katibu Mkuu – Elimu, Dkt. Sweetbert Mkama - Naibu Katibu Mkuu – TAMISEMI; Dkt. Grace Magembe - Naibu Katibu Mkuu – Afya; Ndugu John Cheyo - Mkurugenzi wa Sera na Mipango; Ndugu Mpamima Madale - Mkuu wa Chuo cha Serikali za Mitaa; Ndugu Edwin Mhede – Mtendaji Mkuu *DART* na *Engineer* Victor Seif – Mtendaji Mkuu *TARURA*. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hatujamuona.

**NAIBU SPIKA:** Yupo pia Ndugu Sigsibert Kaijage - Kaimu Meneja Mkuu Kariakoo; Mwalimu Paulina Mkwama - Katibu *TSC;* Mwalimu Robert Shilingi - Mkurugenzi Mkuu Shirika la Elimu Kibaha na Ndugu Richard Mfugale - Katibu Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa ni mke wake Ndugu Jennifer Bashungwa na kaka yake Ndugu Eliasi Lukumay, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Angelina Mabula Mbunge, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambao ni watoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam, Ndugu Pame Irengo na Ndugu Haida Kavira, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 56 wa Mheshimiwa Fatma Toufiq ambao ni walimu na wanafunzi kutoka shule ya sekondari Dodoma, wakiongozwa na Ndugu Zainab Juma Hamisi, Mkurugenzi wa Sikio la Kike Asasi inayohimiza wasichana wajitambue kwa kusikiliza kwa masikio yao, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 30 wa Mheshimiwa Festo Sanga, ambao ni wanafunzi wanaosoma Chuo Kikuu cha Dodoma wanatoka Wilaya ya Makete Mkoani Njombe, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Miraji Mtaturu ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* Kampasi ya Mwanza, Dodoma na Dar es Salaam; Ndugu Salum Mtaturu, Elisha Lundi, Daud Said na Baraka Mussa, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wwatatu wa Mheshimiwa Furaha Matondo ambao ni familia yake kutoka Mkoa wa Mwanza; Ndugu Omar Omar, Ndugu Yusuph Abdulrahman na Ndugu Baraka Maduhu. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Yustina Rahhi ambao ni walimu kutoka Wilaya ya Mbulu Mkoa wa Manyara; Mwalimu Timotheo Kasmiri na Mwalimu George Ammi. *(Makofi)*

Wageni 10 wa Wabunge wote wa Mkoa wa Manyara ambao ni Wenyeviti wa Halmashauri ya Babati Mkoani Manyara wakiongozwa na Ndugu Peter Sulle - Mwenyekiti wa *ALAT* Mkoa wa Manyara. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Japhet Hasunga, ambao ni ndugu zake kutoka Jimboni Vwawa Mkoa wa Songwe; Ndugu Emmanuel Alphonce na Ndugu Jackline Simbeye, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 22 wa Mheshimiwa Flatei Massay ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Mipango Dodoma wanaotokea Mbulu Vijijini, Mkoa wa Manyara. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Reuben Kwagilwa ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Handeni Ndugu Mussa Mkombati, karibu. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Omar Ali Omar ambaye ni Sheikh Mohamed Alhatmy kutoka Lamu, Kenya, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; mgeni ambaye ni Spika wa Bunge la Serikali ya Wanafunzi ya *Catholic*

*University of Health and Allied Sciences* kutoka Bugando, Jijini Mwanza, karibu. *(Makofi)*

Wawakilishi 10 kutoka Chama cha Viziwi Tanzania *(Tanzania Association of the Deaf)* Tawil la Ikwiriri Mkoani Pwani wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Suleiman Zalala, karibu. *(Makofi)*

Wanafunzi 200 kutoka Taasisi ya Uhasibu Tanzania *(TIA)* ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu anaomba kutaka kutoa taarifa hapa Bungeni kuwa amemteua Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko kukaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**NAIBU SPIKA:** Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa wema na fadhili zake, kwa kutujalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako tukufu sasa likubali kupokea na kujadili, Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI Fungu Namba 56, Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu

Namba 2 na Mafungu 26 ya Mikoa ikijumuisha Halmashauri 184 kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Aidha, naomba Bunge lako tukufu, lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI Fungu Namba 56, Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu Na. 2 na Mafungu 26 ya Mikoa ikijumuisha Halmashauri 184 kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, ninampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake za kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, katika shule za sekondari na vituo shikizi. Fedha hizi zimewezesha kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani. Aidha, jitihada hizo zimewezesha pia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabweni kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule za msingi, ujenzi wa majengo ya wagonjwa mahututi, majengo ya kutolea huduma za dharura, nyumba za watumishi katika sekta ya afya, mashine za mionzi, mitambo ya kuzalisha hewa ya *oxygen*, kituo cha matibabu cha magonjwa ya kuambukiza, na ununuzi wa magari ya kubeba wagonjwa kwa kila Halmashauri, na magari ya usimamizi katika ngazi ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mikoa na Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Spika - Dkt. Tulia Ackson Spika wetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wewe binafsi Naibu Spika na Mbunge wa Jimbo la Ilala, kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuongoza mhimili wa Bunge. Tunawaahidi kuwapa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile kwa kuendelea kukusaidia katika kutekeleza majukumu ya kuongoza Bunge lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini na kuniteua

kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Ninamshukuru pia kwa kuendelea kuwaamini Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange, Mbunge wa Jimbo la Wanging'ombe na Mheshimiwa David Silinde, Mbunge wa Jimbo la Tunduma kwa kuwa Naibu Mawaziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI nawashukuru sana Naibu Mawaziri hawa kwa namna ambavyo wananisaidia katika kusimamia majukumu ambayo Mheshimiwa Rais ametukasimisha na Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wote Tanzania Bara.

Namshukuru Mheshimiwa Rais kuendelea kumuamini Katibu Mkuu, Profesa Riziki Shemdoe, Naibu Makatibu Wakuu; Dkt. Grace Magembe anayeshughulikia Afya, Bwana Gerald Mweli anayeshughulia Elimu na kumteua Dkt. Switbert Zacharia Mkama kuwa Naibu Katibu Mkuu anayeshughulia TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamuahidi Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wetu mpenda Samia Suluhu Hassan na Watanzania wote kuwa tutaendelea kufanya kazi kwa bidii, weledi, ubunifu, uaminifu na utiifu kwake na kwa nchi yetu, katika kumsaidia kusimamia shughuli za utawala na maendeleo katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Tutahakikisha Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaongeza ubunifu kwa kuongeza vyanzo vipya, kuimarisha vyanzo vilivyopo vya mapato na mbinu katika ukusanyaji wa mapato ya ndani bila kusababisha kero kwa wananchi wetu. Vilevile tutaongeza jitihada za kusimamia matumizi ya fedha za umma katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Karagwe kwa kuniamini na kunichagua tena kuwa Mbunge wao. Ninawaahidi Wanakaragwe kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa nguvu zangu zote ili kuifanya Karagwe yetu ipate maendeleo zaidi ya kiuchumi na kijamii. Kipekee, ninaishukuru familia yangu mke wangu Jennifer Bashungwa na watoto wetu Santo, Solana, Sankara na Samora kwa kuniombea na kuwa wavumilivu muda wote ninapokuwa mbali nao katika kutekeleza majukumu ya kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nampongeza Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, Mbunge wa Jimbo la

Mbagala kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Utawala na Serikali za Mitaa; nampongeza Mheshimiwa Dennis Londo, Mbunge wa Jimbo la Mikumi kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati, pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa mchango wao mkubwa katika kuchambua utekelezaji wa mpango na bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, kwa kujadili kwa kina Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu yote 28 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na kupitisha kwa kauli moja. Vilevile Kamati hii imekuwa ikitoa ushauri ambao umesaidia kuboresha utendaji wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI tunawashukuru sana Kamati ya USEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba niipongeze Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wao mahiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na muda mfupi wa kusoma hotuba, eneo la utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 linapatikana na kuelezwa kwa kina katika aya ya 11 mpaka 162 kwenye kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kutokana na sababu za muda,na maelezo ya mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yameelekezwa kwa kina katika aya ya 163 mpaka 194 kwenye kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)* umeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya ujenzi, matengenezo na ukarabati wa barabara za Wilaya. Katika mwaka wa fedha 2019/2020 shilingi bilioni 251.73 ziliidhinishwa, mwaka wa fedha 2020/2021 shilingi bilioni 275.03 ziliidhinishwa na mwaka wa fedha 2021/2022 shilingi bilioni 722.16 ziliidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na ongezeko katika bajeti ya *TARURA* kwa shilingi bilioni 447.13 sawa na asilimia 162.59

kati ya mwaka wa fedha 2020/2021 na 2021/2022 kutokana na Serikali kuongeza vyanzo vya fedha vya tozo ya shilingi 100 kwa kila lita ya mafuta ya petroli na dizeli na fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali ambavyo havikuwepo hapo awali. Nitumie nafasi hii kupongeza Bunge lako tukufu kwa kuiwezesha Serikali kufika hatua hii ya kuiwezesha *TARURA* kuongezewa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wakala umetengewa shilingi bilioni 802.29 kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za ujenzi, ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya barabara. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 11 ukilinganisha na bajeti ya 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, aya ya 165 hadi 177 zimeelezea kwa kina mipango ya utekelezaji wa *TARURA*, kwa sababu ya muda naomba nielezee kwa ufupi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TARURA* imetengewa shilingi bilioni 16.80 kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi wa uboreshaji wa miundombinu katika Halmashauri 45 za Majiji, Manispaa na Miji kupitia Mradi wa *Tanzania Cities Transforming Infrastructure and Competitiveness - TACTIC*.

Waheshimiwa Wabunge mradi huu mmekuwa mkiusubiri kwa muda mrefu na tulipata maelekezo ya Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwamba jitihada za makusudi zifanyike ili mradi huu uanze kwenye mwaka wa fedha wa 2022/2023. Nitumie nafasi hii kumshukuru sana Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa msukumo wake, lakini pia niwapongeze Waheshimiwa Wabunge kwa maelekezo ambayo mliipatia Serikali kwamba mradi huu ni wa muhimu kwa wananchi wetu. Mradi huu utatekelezwa katika Madaraja Matatu yaani *tier 1, tier* 2 *na tier 3*. Mradi huu ni mwendelezo wa Mradi wa Uendelezaji Miji ya Kimkakati nane yaani *Tanzania Strategic Cities Project*, Mradi wa Uimarishaji Miji 18 yaani *Urban Local Government Strengthening Project* ambayo utekelezaji wake umefikia kikomo na pia utajumuisha miji mingine 19 ambayo haikuwepo kwenye awamu zilizopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi zitaelekezwa kwenye uboreshaji wa miundombinu ya barabara kwenye maeneo ya vijijini na mijini kwa lengo la kuimarisha huduma za kiuchumi kwa wananchi wetu. Naomba kutumia fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa namna walivyojitoa katika kusimamia shughuli za ujenzi, ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya barabara katika majimbo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu uliokuwepo awali wa kupata wakandarasi wa ujenzi, matengenezo na ukarabati wa miundombinu ya barabara mchakato wa manunuzi ulikuwa unaanza mwezi Julai. Mara baada ya bajeti ya Serikali kuidhinishwa mwezi Juni ambapo mchakato huo ulikuwa ukienda hadi mwezi Oktoba. Utaratibu huo ulisababisha wakandarasi kwa maeneo mengi kupatikana wakati wa kipindi cha mvua hivyo kusababisha ucheleweshaji wa utekelezaji wa kazi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelekezo ya Bunge lako kupitia Kamati ya Usemi jambo hili tumelipatia dawa. Katika kukabiliana na changamoto ya ucheleweshaji wa ujenzi, matengenezo na ukarabati wa miundombinu ya barabara nilielekeza *TARURA* Wakala kuanzisha utaratibu wa kuanza mchakato wa manunuzi wa asilimia 60 ya kazi zilizopangwa kuanzia mwezi Mei kila mwaka ili fedha zinapoidhinishwa na Bunge mwezi Juni ya kila mwaka, utekelezaji uanze mapema kuliko ulivyokuwa awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itasaidia kuwapa wakandarasi kwa wakati watakaoweza kutekeleza kazi za ujenzi, matengenezo na ukarabati wa miundombinu ya barabara itakayosaidia wananchi kuendelea kutekeleza shughuli zao za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepanga kutekeleza malengo mahsusi yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo; Waheshimiwa Wabunge kwa muda mrefu

mmekuwa mkiiomba Serikali kuongeza bajeti ya Mfuko wa Jimbo, tumekuja na dawa. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu spika, Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo umeongezewa shilingi bilioni 4.99 kutoka shilingi bilioni 11 ambayo imekaa hapo miaka mingi Waheshimiwa Wabunge iliyokuwa katika bajeti ya kuanzia mwaka wa fedha 2016/2017 mpaka 2021/2022 sasa hivi tunaipandisha kutoka bilioni 11 inakuwa bilioni 15.99 kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Waheshimiwa Wabunge hii ni sawa na ongezeko la asilimia 45.36 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi. Mama Samia oyeee. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Oyeee.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa bima ya afya kwa Waheshimiwa Madiwani; Serikali ilianza kulipa posho za Waheshimiwa Madiwani kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo mchango wa bima ya afya haukujumuishwa kwenye posho hizo. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga fedha ya kuchangia mchango wa mwajiri kwa ajili ya Waheshimiwa Madiwani shilingi milioni 607.57 *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarisha usalama na usimamizi wa shughuli za Serikali; Ofisi za Wakuu wa Wilaya zimeongezewa fedha za matumizi mengineyo kutoka shilingi bilioni 17.13 hadi shilingi bilioni 26.68 sawa na ongezeko la shilingi bilioni 9.5 ambayo ni ongezeko la asilimia 55.75 kwa ajili ya kuwawezesha Wakuu wa Wilaya kusimamia usalama na utekelezaji wa shughuli za Serikali katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge *OC* za Wakuu wa Wilaya zilikuwa ndogo na tunataka wasimamie maendeleo katika Wilaya zetu, kwa hiyo Serikali tumewasikia Waheshimiwa Wabunge katika utetezi wa jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikoa imeongezewa fedha za uendeshaji wa vikao vya Kamati za Usalama vya Mikoa kutoka shilingi milioni 416 hadi shilingi milioni 780 sawa na ongezeko la shilingi milioni 364. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mikoa 12 inayopakana na nchi jirani imetengewa jumla ya shilingi milioni 730 kwa ajili ya kuimarisha usalama mipakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mapato ya ndani na uwezeshaji wananchi kiuchumi; katika mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri zinakadiria kukusanya mapato ya ndani ya jumla ya shilingi trilioni 1.01 ikilinganishwa na bilioni 863.85 zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambayo ni ongezeko la shilingi bilioni 148.42 sawa na asilimia 17.18.

Mheshimiwa Naibu Spika, shilingi bilioni 394.8 zimetengwa kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 75.98 ni mikopo ya asilimia 10 na shilingi bilioni 318.82 ni kwa ajili ya miradi mingine ya maendeleo. Mchanganuo wa matumizi ya shilingi bilioni 318.82 unapatikana katika aya ya 195 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, shilingi bilioni 75.97 zinazotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri ambayo ni sehemu ya miradi ya maendeleo zimetengwa kwa ajili ya mikopo ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, suala la asilimi 10 kwenye usimamizi ni eneo ambalo Bunge lako tukufu limekuwa likielekeza Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuja na mikakati ya kusimamia vyema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeweka mikakati mbalimbali ili kuhakikisha mikopo hii inasimamiwa kwa ufanisi. Moja ya mikakati iliyowekwa ni kuweka kigezo cha utoaji wa mikopo, usimamizi wa matumizi ya mikopo hiyo, pamoja na marejesho kuwa sehemu ya kuwapima Wakurugenzi wa Halmashauri ambayo itafanyika kila robo mwaka na tathmini ya kina itafanyika mwisho wa mwaka. Mkakati mwingine ni matumizi ya mfumo wa kielektroniki utakaosaidia kuondoa changamoto katika ukopeshaji, usimamizi na urejeshaji wa mikopo. Hivyo,

itakuwa ni kazi ya Wakurugenzi kuhakikisha mfumo unatumika ipasavyo na kuongeza ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya afya; kuendelea na ujenzi wa Hospitali 28 za Halmashauri ambazo zimetengewa shilingi bilioni 24.65; kuendelea na ujenzi wa Hospitali 31 za Halmashauri ambazo zimetengewa shilingi bilioni 15.5; kuendelea na ukarabati wa Hospitali kongwe 19 za Halmashauri ambazo zimetengewa shilingi bilioni 16.55; ukamilishaji wa ujenzi wa maboma ya zahanati 300 ambazo zimetengewa shilingi bilioni 15; na shilingi bilioni 15.15 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba kwa Zahanati 300, shilingi bilioni 47.7 za ununuzi wa vifaa tiba kwa vituo vya afya 159 na shilingi bilioni 7.1 za ununuzi wa vifaa tiba ya afya ya kinywa na macho kwa ajili ya Hospitali za Halmashauri 71 zilizokamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya elimu; elimu msingi bila malipo kiasi cha shilingi bilioni 346.49 zimetengwa sawa na ongezeko la shilingi bilioni 34.44 ya fedha zilizoidhinishwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambayo ni shilingi bilioni 312.05.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo sera ya elimu msingi bila malipo, Serikali ya Awamu ya Sita tunaendelea nayo na tumeongeza bejeti yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shilingi bilioni 55.57 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 809 za walimu zenye uwezo wa kuchukua kaya 1,916.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, Serikali ya Awamu ya Sita tumeanza sasa kujenga kwa kadri rasilimali zinavyopatikana nyumba za walimu, ni jambo ambalo Bunge hili mmekuwa mkiielekeza Serikali, Serikali ya Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan imewasikia na tumeanza. Tunaanza na nyumba 809 na zitawezesha walimu wetu kaya 1,916 kukaa humo kwenye hizo nyumba hasa hasa shule ambazo ziko mbali na miundombinu itakuwa ni kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naib Spika, kati yake, nyumba za Walimu wa shule za msingi ni 298 za *(3 in1)* ambazo zitajengwa kupitia fedha

za ruzuku kutoka Serikali Kuu kwa shilingi bilioni 30.02 na shilingi bilioni 25.55 zitatumika kujenga nyumba 511 *(2 in1)* za walimu wa shule za sekondari kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Elimu ya Sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa matundu ya vyoo 9,700 katika vituo shikizi 970 ambapo shilingi bilioni 10.67 zimetengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, majimboni kwetu mnafahamu matundu ya vyoo hasa hasa kwenye shule za msingi ni *critical need.* Tumetenga fedha hizi na tutaendelea kutafuta kila aina ya vyanzo kuhakikisha tunakomesha changamoto ya upungufu wa matundu ya vyoo kwenye shule za msingi na sekondari. *(Makofi)*

Pia kuanza Awamu ya Kwanza ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 1,700 katika shule kongwe za msingi shilingi bilioni 34 zimetengwa; ujenzi wa shule mpya 39 za msingi shilingi bilioni 15.6 zimetengwa; ujenzi wa uzio wa mabweni 99 ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ambapo shilingi bilioni 2.97 zimetengwa; ukamilishaji wa maboma ya vyumba vya madarasa 1,911 katika shule za msingi ambapo shilingi bilioni 23.88 zimetengwa na ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba vya maabara 291 katika shule za sekondari ambapo shilingi bilioni 8.73 zimetengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, maswali mengi humu ikiwemo mambo ya maabara tunaenda kukamilisha; ukamilishaji wa mabwalo 86 ambapo mabwalo 80 katika shule za sekondari na mabwalo sita katika shule za msingi shilingi milioni 4.3 zimetengwa; ukamilishaji wa mabweni 461 ambapo mabweni 28 katika shule za msingi zenye wanafunzi wenye mahitaji maalum na mabweni 433 katika shule za sekondari ambapo shilingi bilioni 9.21 zimetengwa; kuwezesha kufanyika kwa mitihani ya Taifa ya darasa la nne, la saba, kidato cha pili, kidato cha nne na kidato cha sita shilingi bilioni 142.33 zimetengwa na shilingi milioni 670 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Tume ya Utumishi wa Walimu pamoja na uundaji wa mfumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, tumefanya hivi ili kuwezesha Tume ya Utumishi wa Walimu kuweza kuhudumia walimu wetu nchini. Kwa hiyo, lazima tuwawekee mazingira mazuri ya kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, programu mbalimbali; jumla ya shilingi bilioni 1.41 zimetengwa kupitia Programu ya Kuimarisha Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kuimarisha Mfumo wa Ugatuaji utakaosaidia kuboresha huduma za jamii, utawala bora na kuwa na maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya shilingi bilioni 135.43 zimetengwa kupitia Programu ya Uboreshaji wa Elimu ya Sekondari yaani *SEQUIP* kwa ajili ya uendelezaji wa ujenzi wa shule 10 za sekondari za wasichana za bweni kwa masomo ya sayansi, shule za sekondari 232 za Kata, ujenzi wa shule mpya za Kata 184, ujenzi wa shule mpya tano za sekondari za wasichana za bweni kwa masomo ya sayansi na fedha kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini.

Aidha, jumla ya shilingi bilioni 55.38 zimetengwa kupitia Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira kwa upande wa elimu na afya kwa ajili ya kuimarisha shughuli za afya na usafi wa mazingira; jumla ya shilingi bilioni 237.36 zimetengwa kupitia Programu ya *BOOST* kwa ajili ya kuimarisha ujifunzaji na ufundishaji katika elimu ya awali na msingi; jumla ya shilingi bilioni 17.27 zimetengwa kupitia *DART* mabasi ya mwendokasi kwa ajili ya kununua mfumo wa kusimamia magari na kusimika vifaa vya kukusanyia nauli kwa mfumo wa kielektroniki na jumla ya shilingi bilioni 83.29 zimetengwa kupitia Programu ya Mfuko wa Pamoja wa Afya kwa ajili ya uboreshaji wa huduma za afya katika vituo vya kutolea huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utawala bora; jumla ya shilingi bilioni 36.11 zimetengwa kwa ajili ya upanuzi, ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa majengo ya ofisi na nyumba za viongozi katika ngazi ya Mikoa, Wilaya na Tarafa. Maelezo ya kina yanapatikana katika aya ya 195 ya hotuba yangu; Serikali imetenga shilingi bilioni 10 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Soko

jipya la Kariakoo na kukarabati Soko Kuu liloungua moto tarehe 10 Julai, 2021.

Aidha, Serikali imetenga shilingi bilioni 8.9 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 111 za Wakuu wa Idara na shilingi bilioni 7.2 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 48 za Wakurugenzi; Halmashauri 83 zimetengewa shilingi bilioni 68.85 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa majengo ya utawala; Halmashauri 13 zimetengewa shilingi bilioni 13 kwa ajili ya ujenzi wa majengo mapya ya utawala; jumla ya shilingi bilioni 2.05 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa boti. Halmashauri za Wilaya za Mafia (boti mbili), Kilwa (boti moja), Ukerewe (boti mbili), Muleba (boti moja), Kalambo (boti moja) na Momba (boti moja) na Halmashauri 20 zimetengewa jumla ya shilingi bilioni 40.11 kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya kimkakati; maswali mengi yamekuwa yakiulizwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuhusu miradi ya kimkakati. Tumejipanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaendelea kusimamia na kuratibu maandiko ya miradi ya kimkakati kwa kushirikiana na timu ya Kitaifa ambayo tumeiunda kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kuratibu maandiko ya miradi inayoweza kukopesheka kupitia Programu ya Ugharamiaji wa Miradi Mbadala. Timu hii imeundwa ili kutatua changamoto ya uandishi wa maandiko ya miradi kutoka katika Halmashauri mbalimbali na hivyo kuzisababishia Halmashauri kutokidhi vigezo vilivyowekwa na Serikali ili kupata fedha za utekelezaji wa miradi hiyo. Naomba kutumia fursa hii kuzielekeza Halmashauri ziibue miradi ili iweze kugharamiwa kupitia utaratibu wa ugharamiaji mbadala wa miradi ikijumuisha Hati Fungani za Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kufanya hivi kuboresha mashirikiano kati ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Wizara ya Fedha na Mipango pia tumejipanga kujenga *capacity* ya Halmashauri zetu kuandika maandiko haya ili kuweza kuwa na utaratibu ambao ni *sustainable*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais - TAMISEMI itazielekeza Halmashauri kuhakikisha zinatekeleza miradi maalum kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri kupitia vipaumbele vilivyopo. Vipaumbele hivyo vitajumuisha ukamilishaji wa ujenzi wa maboma ya vyumba vya madarasa, Zahanati, maabara ya masomo ya sayansi, ujenzi wa matundu ya vyoo kama nilivyosema kwa shule za msingi na sekondari, ununuzi wa vifaa, vifaa tiba na vitendanishi, nyumba za watumishi na kuendeleza ujenzi wa maeneo ya wafanyabiashara wadogo (wamachinga). Vilevile Halmashauri zenye mapato ya ndani zaidi ya shilingi bilioni tano zinaelekezwa pia kuchangia asilimia 10 kwa ajili ya ujenzi wa barabara zinazosimamiwa na *TARURA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zote zinaelekezwa kuendelea na utengaji, uboreshaji, upangaji na ujenzi wa miundombinu ya maeneo ya kufanyia biashara wafanyabiashara wadogo (machinga) pamoja na kuwaunganisha na taasisi za kifedha ili kuwaongezea fursa za kiuchumi na Serikali itanufaika na ushuru pamoja na kodi mbalimbali kupitia shughuli zao. Kwa sasa Halmashauri 11 yakiwemo Majiji sita, Manispaa nne na Halmashauri ya Mji moja zimeanza ujenzi wa miundombinu rafiki kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo (machinga) yatakayowawezesha kurasimisha biashara zao ili watambulike na kuunganishwa na taasisi za kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wanaotarajiwa kuandikishwa kidato cha kwanza Januari 2023, kwa ufaulu wa asilimia 82 ni sawa na wanafunzi 1,257,996 kati ya wanafunzi 1,534,141 waliopo darasa la saba mwaka huu wa 2022. Ongezeko hilo linatokana na wanafunzi wa kundi la kwanza la Mpango wa Elimu Msingi bila Malipo wanaotarajiwa kuhitimu darasa la saba mwaka huu. Kutokana na ongezeko hilo, mahitaji ya vyumba vya madarasa ya wanafunzi wa sekondari yatakuwa 15,186 vyumba vya madarasa vitakavyokuwepo baada ya wanafunzi wa kidato cha nne kuhitimu ni 7,200 na kusababisha upungufu wa vyumba 7,986. Hivyo, Serikali itajenga madarasa haya kupitia ruzuku ya Serikali Kuu, mapato ya ndani ya Halmashauri na fedha za washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kuzielekeza Halmashauri za Serikali za Mitaa kutenga na kupeleka asilimia 20 ya Mapato yatokanayo na tozo za mazao ya kilimo yani *crop cess* kwa ajili ya shughuli za kilimo ikiwemo kuendeleza uzalishaji wa mazao ya kimkakati. Halmashauri zitenge asilimia 15 ya mapato yatokanayo na mazao ya mifugo kwa ajili ya shughuli za kuendeleza ufugaji kwa mujibu wa Waraka wa Rais Na. 01 wa mwaka 2002 kuhusu hatua za kuchukua kuzuia kuenea kwa magonjwa ya mifugo nchini. Vilevile Halmashauri zitenge asilimia tano ya mapato yatokanayo na mazao ya uvuvi kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukurani; kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, naomba kukushukuru wewe binafsi Naibu Spika, na wenyeviti wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kw auongozi imara katika kutekeleza shughuli za Bunge. *(Makofi)*

Vilevile naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa (USEMI) pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa na Kamati zote kwa maoni, maelekezo na maagizo yao katika uboreshaji wa usimamizi wa fedha katika mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia fursa hii pia kuwashukuru viongozi wenzangu katika Ofisi ya Rais; dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Jimbo la Peramiho na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Mheshimiwa George Huruma Mkuchika, Mbunge wa Newala Mjini na Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wenzangu wote kwa ushirikiano walionipa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 na kipekee nimshukuru dada yangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu kwa kunikabidhi kijiti kwenye Ofisi ya Rais – TAMISEMI na ushirikiano ambao ambao anaendelea kunipa akiwa Wizara ya Afya kwa

sababu ni Wizara ambazo tunahitaji ushirikiano wa karibu, nimshukuru kwa ushirikiano wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Profesa Mkend, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, pia ni Wizara ambazo inabidi tushirikiane katika kutekeleza hay ana Mawaziri ote nawashukuru sana kwa ushirikiano wenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya fedha kwa mwaka fedha 2022/2023; sasa naomba Bunge lako tukufu nikubali kuhizinisha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2223 jumla ya shilingi 8,778,607,763,200 (shilingi trilioni nane bilioni mia saba sabini na nane milioni mia sita na saba mia saba sitini na tatu elfu na mia mbili) kwa ajili ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI Fungu Namba 56; Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu Namba 2 na Mafungu 26 ya Mikao yanayojumuisha Halmashauri 184.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hotuba hii yapo majedwali ambayo yanafafanua kwa kina makadirio ya mapato na matumizi ya fedha za Ofisi ya Rais - TAMISEMI Fungu Namba 56, Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu Namba 2 na Mikoa na Halmashauri Mafungu 26 ambayo ni sehemu ya hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hotuba yangu yote iingie kwenye *Hansard. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii ya kuweza kuwasilisha hotuba yangu, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Si unatakiwa utoe hoja? Toa hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, MHESHIMIWA INNOCENT LUGHA BASHUNGWA (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili, Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Fungu 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 2) na Mafungu 26 ya Mikoa ikijumuisha Halmashauri (184) kwa Mwaka wa Fedha 2021/22. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Fungu 56), Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu (Na. 2) na Mafungu 26 ya Mikoa ikijumuisha Halmashauri (184) kwa Mwaka wa Fedha 2022/23.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa heshima na unyenyekevu mkubwa ninampongeza **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake za kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za sekondari na vituo shikizi, fedha hizi zimewezesha kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani. Aidha, jitihada hizo zimewezesha pia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabweni kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule za msingi, ujenzi wa majengo ya wagonjwa mahututi, majengo ya kutolea huduma za dharura, nyumba za watumishi katika sekta ya afya, mashine za mionzi, mitambo ya kuzalisha hewa ya Oksijeni, kituo cha matibabu cha

magonjwa ya kuambukiza na ununuzi wa magari ya kubeba wagonjwa kwa kila Halmashauri na magari ya usimamizi katika ngazi ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mikoa na Halmashauri.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** natoa pole kwako, Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na wapendwa wetu *Mheshimiwa Elias Kwandikwa*, aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Mbunge wa Jimbo la Ushetu; *Mheshimiwa William Tate Olenasha* aliyekuwa Naibu Waziri wa Uwekezaji (Ofisi ya Waziri Mkuu) na Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro; na *Mheshimiwa Khatibu Said Haji* aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Konde Zanzibar). Aidha, napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa wa marehemu, marafiki na watanzania wenzangu kwa kuondokewa na wapendwa wao. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi, Amina.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Naibu Spika *Mheshimiwa Hassan Mussa Zungu* Mbunge wa Jimbo la Ilala kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuongoza Mhimili wa Bunge. Tunakuahidi kukupa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yako.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb) na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile (Mb) kwa kuendelea kukusaidia katika kutekeleza majukumu ya kuongoza Bunge lako.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan** kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI). Ninamshukuru pia kwa kuendelea kuwaamini *Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange*, Mbunge wa Jimbo la Wanging'ombe na *Mheshimiwa David Ernest Silinde*, Mbunge wa Jimbo la Tunduma kuwa Naibu Mawaziri Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wote Tanzania Bara. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Rais kuendelea kumuamini Katibu Mkuu, Profesa Riziki Silas Shemdoe, Naibu Makatibu Wakuu;

Dkt. Grace Elias Magembe (Afya), Bw. Gerald Geofrey Mweli (Elimu) na kumteua Dkt. Switbert Zacharia Mkama kuwa Naibu Katibu Mkuu (TAMISEMI).

8. ***Mheshimiwa Spika,*** tunamuahidi Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na watanzania kuwa tutaendelea kufanya kazi kwa bidii, weledi, ubunifu, uaminifu na utiifu kwake, na kwa nchi yetu, katika kumsaidia kusimamia shughuli za utawala na maendeleo katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, hususan kwa kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaongeza ubunifu kwa kuongeza vyanzo vipya, kuimarisha vyanzo vilivyopo, na mbinu katika ukusanyaji wa Mapato ya Ndani, bila kusababisha kero kwa wananchi. Aidha, Mapato hayo yatumike katika kutekeleza vipaumbele vilivyowekwa, ikijumuisha Miundombinu ya huduma za Afyamsingi na Elimumsingi, barabara, Majengo ya Utawala, Makazi ya Viongozi na watumishi, Ununuzi wa Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi, na kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo. Vilevile, tutaongeza jitihada za kusimamia matumizi ya fedha za umma katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee, nampongeza *Mheshimiwa Abdallah Jaffari Chaurembo,* Mbunge wa Jimbo la Mbagala, kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa; *Mheshimiwa Denis Lazaro Londo,* Mbunge wa Jimbo la Mikumi kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati, pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa mchango wao mkubwa, katika kuchambua utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Fungu 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 2) na Mafungu 26 ya Mikoa ikijumuisha Halmashauri 184 kwa Mwaka wa Fedha 2021/22. Aidha, Kamati ilijadili kwa kina Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu yote 28, kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 na kupitisha kwa kauli moja. Vilevile, Kamati imekuwa ikitoa ushauri ambao umesaidia kuboresha utendaji wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Tume ya Utumishi wa Walimu na Taasisi nyingine zilizo chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee naomba niipongeze Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa

**Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kusimamia kikamilifu, kwa dhati na kwa umakini mkubwa utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 na Malengo Endelevu ya Maendeleo (2030).

## B. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22

11. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zake, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa iliidhinishiwa kukusanya Maduhuli na Mapato ya Ndani, jumla ya **Shilingi bilioni 916.44.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 52.36** ni ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zake, **Shilingi milioni 220.68** ni Maduhuli ya Mikoa, na **Shilingi bilioni 863.85** ni Mapato ya Ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, hadi Februari 2022 jumla ya **Shilingi bilioni 615.61** zimekusanywa, sawa na **asilimia 67.17** ya bajeti iliyoidhinishwa.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Fungu 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 2) na Mafungu 26 ya Mikoa ikijumuisha Halmashauri 184 iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya **Shilingi trilioni 8.56**, ambapo **Shilingi trilioni 4.72** ni Matumizi ya Kawaida, yakijumuisha Mishahara **Shilingi trilioni 3.97**, **Shilingi bilioni 755.85** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, na **Shilingi trilioni 3.84** ni Fedha za Maendeleo ***(Kiambatisho Na. 1)***.

13. ***Mheshimiwa Spika***, hadi Februari 2022 Mafungu 28 ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, yamekusanya na kupokea kiasi cha **Shilingi trilioni 5.33**, sawa na **asilimia 62.26** ***(Kiambatisho Na. 1)***. Mchanganuo kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo: -

**Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zilizo chini yake (Fungu 56)**

14. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zilizo chini yake, iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi trilioni 1.04**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 57.51** ni

mishahara, ambapo **Shilingi bilioni 10.27** ni za Ofisi ya Rais – TAMISEMI Makao Makuu, na **Shilingi bilioni 47.23** ni za Taasisi; **Shilingi bilioni 11.37** ni za matumizi mengineyo ambapo **Shilingi bilioni 10.05** ni kwa ajili ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI Makao Makuu na **Shilingi bilioni 1.31** ni za Taasisi. Aidha, **Shilingi bilioni 973.82** ni za miradi ya maendeleo ambapo fedha za ndani ni **Shilingi bilioni 773.66** na fedha za nje ni **Shilingi bilioni 200.15**.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2022 Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Fungu 56) imepokea jumla ya **Shilingi bilioni 670.36**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 38.17** ni kwa ajili ya mishahara, sawa na **asilimia 66.38** ya fedha zilizoidhinishwa. Aidha, **Shilingi bilioni 8.83** ni matumizi mengineyo, sawa na **asilimia 77.66**, na **Shilingi bilioni 623.35** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, sawa na **asilimia 64.01**. Vilevile, Fedha za Maendeleo zinajumuisha **Shilingi bilioni 526.13** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 97.22** fedha za nje. ***(Kiambatisho Na. 1)***

**Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na.2)**

16. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 14.86**, kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 7.76** ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi bilioni 6.60** ni matumizi mengineyo, na **Shilingi milioni 500.00** kwa ajili ya mradi wa maendeleo.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2022 Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 2) imepokea jumla ya **Shilingi bilioni 9.51**, sawa na **asilimia 64.01** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 5.25** ni kwa ajili ya mishahara, sawa na **asilimia 67.69**, **Shilingi bilioni 3.75** matumizi mengineyo sawa na **asilimia 56.95**, na **Shilingi milioni 500.00** ni kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Tume Makao Makuu Dododma sawa na **asilimia 100** ya fedha zilizoidhinishwa ***(Kiambatisho Na. 1)***.

**Mafungu 26 ya Mikoa ikijumuisha Halmashauri 184**

**Tawala za Mikoa**

18. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Mikoa iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 242.84**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 71.26** ni mishahara, **Shilingi bilioni 57.44** matumizi mengineyo, na **Shilingi bilioni 114.12** miradi ya

maendeleo ambayo inajumuisha **Shilingi bilioni 90.32** fedha za ndani, na **Shilingi bilioni 23.79** fedha za nje.

19. ***Mheshimiwa Spika***, hadi Februari 2022 Mikoa ilipokea jumla ya **Shilingi bilioni 173.99**, kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 45.58** ni kwa ajili ya mishahara, sawa na **asilimia 64.34, Shilingi bilioni 48.03** matumizi mengineyo, sawa na **asilimia 83.62**, na **Shilingi bilioni 80.37** kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na **asilimia 70.42**, ambapo fedha za ndani ni **Shilingi bilioni 71.41** na fedha za nje ni **Shilingi bilioni 8.95 *(Kiambatisho Na. 1)***.

**Halmashauri 184**

20. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Halmashauri ziliidhinishiwa jumla ya **Shilingi trilioni 7.26**, kati ya fedha hizo **Shilingi trilioni 3.83** ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi bilioni 680.42** ni Matumizi Mengineyo yakijumuisha **Shilingi bilioni 147.65** ruzuku kutoka Serikali Kuu, na **Shilingi bilioni 532.77** Mapato ya Ndani ya Halmashauri. Aidha, **Shilingi trilioni 2.75** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ambapo **Shilingi bilioni 957.51** ni ruzuku kutoka Serikali Kuu, **Shilingi bilioni 331.08** ni Mapato ya Ndani ya Halmashauri na **Shilingi trilioni 1.46** ni fedha za nje.

21. ***Mheshimiwa Spika***, hadi Februari 2022 Halmashauri zimepokea jumla ya **Shilingi trilioni 4.47**, kati ya fedha hizo **Shilingi trilioni 2.64** ni kwa ajili ya mishahara, sawa na **asilimia 68.96**, **Shilingi bilioni 492.66** sawa na **asilimia 72.41** ni matumizi mengineyo, yakijumuisha **Shilingi bilioni 122.70** ruzuku kutoka Serikali Kuu, na **Shilingi bilioni 369.96** Mapato ya Ndani ya Halmashauri. Aidha, **Shilingi trilioni 1.34** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, sawa na **asilimia 48.75** zikijumuisha **Shilingi bilioni 696.25** ruzuku ya Serikali Kuu, **Shilingi bilioni 216.11** Mapato ya Ndani ya Halmashauri, na **Shilingi bilioni 429.10** ni fedha za nje (***Kiambatisho Na. 1)***.

**Fedha za Nyongeza za Miradi ya Maendeleo**

22. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Ofisi ya Rais – TAMISEMI iliidhinishiwa fedha za nyongeza **Shilingi bilioni 686.55** ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 512.14** zimetokana na Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO - 19 (TCRP); **Shilingi bilioni 93.00**

zimetokana na Tozo za Miamala ya simu; **Shilingi bilioni 7.76** kutoka kwenye Programu Endelevu ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira (SRWSS)**; Shilingi bilioni 17.25** kutoka Mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu (EP4R).

23. ***Mheshimiwa Spika,*** fedha nyingine za nyogeza ya bajeti ni **Shilingi bilioni 12.62** kutoka Mradi wa Kuimarisha Ufundishaji na Ujifunzaji kwa ElimuMsingi Awamu ya Pili (GPE-LANES); **Shilingi bilioni 8.24** kutoka Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA); **Shilingi bilioni 2.98** kwa ajili ya kulipa madeni ya watumishi (walimu wastaafu); **Shilingi bilioni 9.19** kwa ajili ya utoaji wa chanjo; na **Shilingi bilioni 22.87** ni kwa ajili ya kulipa madeni ya wazabuni katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

24. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari, 2022 zimepokelewa jumla ya **Shilingi bilioni 535.07** ambapo **Shilingi bilioni 360.66** ni kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO - 19 (TCRP); **Shilingi bilioni 93.00** ni za Tozo za Miamala ya simu; **Shilingi bilioni 7.76** kutoka kwenye Programu Endelevu ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira (SRWSS)**; Shilingi bilioni 17.25** kutoka Mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu (EP4R).

25. ***Mheshimiwa Spika,*** fedha nyingine zilizopokelewa ni **Shilingi bilioni 12.62** kutoka Mradi wa Kuimarisha Ufundishaji na Ujifunzaji kwa ElimuMsingi Awamu ya Pili (GPE-LANES); **Shilingi bilioni 8.24** kutoka Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA); **Shilingi bilioni 2.98** kwa ajili ya kulipa madeni ya watumishi (walimu wastaafu); **Shilingi bilioni 9.19** kwa ajili ya utoaji wa chanjo; na **Shilingi bilioni 22.87** ni kwa ajili ya kulipa madeni ya wazabuni katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2021/22**

26. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Halmashauri zimetekeleza shughuli zifuatazo: -

**HUDUMA ZA AFYA YA MSINGI**

27. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Ofisi ya Rais - TAMISEMI iliidhinishiwa **Shilingi bilioni 28.20** kupitia ruzuku ya Serikali Kuu kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa maboma **564** ya Zahanati katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi kufikia Februari 2022, zimepokelewa **Shilingi bilioni 23.32** sawa na **asilimia 82.69** ya fedha zilizoidhinishwa. Ukamilishaji wa ujenzi upo katika hatua mbalimbali **(*Kiambatisho Na. 2)***.

28. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 **Shilingi bilioni 110.60** ziliidhinishwa kupitia ruzuku ya Serikali Kuu kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Vituo vya Afya **304**. Kati ya hivyo, Vituo **52** vilianza kujengwa Mwaka wa Fedha 2019/20 na Vituo **252** vimeanza kujengwa Mwaka wa Fedha 2021/22 ambapo Vituo **18** vimejengwa kwenye Halmashauri zenye Mapato madogo na Vituo **234** vimejengwa katika Tarafa zisizo kuwa na Vituo vya Afya na Kata za Kimkakati kupitia tozo za miamala ya simu. Hadi Februari, 2022 **Shilingi bilioni 108.05** zimepokelewa sawa na **asilimia 97.69** ya fedha zilizoidhinishwa na ujenzi unaendelea ***(Kiambatisho Na. 3)***.

29. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Serikali ilitenga **Shilingi bilioni 81.10** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Hospitali **68** zilizoanza kujengwa mwaka 2018/19, Hospitali **31** zilizoanza kujengwa mwaka 2019/20 na kuanza ujenzi wa Hospitali mpya **28**. Hadi Februari, 2022 **Shilingi bilioni 66.80** sawa na asilimia **82.36** zilikuwa zimepokelewa na ujenzi upo katika hatua mbalimbali ***(Kiambatisho Na. 3)***.

30. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Ofisi ya Rais - TAMISEMI iliidhinishiwa **Shilingi bilioni 11.30** kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaa tiba kwa Hospitali **31** za Awamu ya Pili zilizoanza kujengwa katika Mwaka wa Fedha 2018/19. Hadi Februari, 2022 zimepokelewa **Shilingi bilioni 5.83** sawa na **asilimia 51.59** ambapo fedha hizi zimepelekwa kwenye Halmashauri kumi na moja **(11)** kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaa tiba ***(Kimbatisho Na. 3)***.

**Utekelezaji wa Miradi kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19**

31. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendelea kuimarisha huduma za Afya ya Msingi, katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Ofisi ya Rais – TAMISEMI imepokea **Shilingi bilioni 52.16** kati ya **Shilingi bilioni 203.14** sawa na **asilimia 25.67** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta ya afya kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO 19.

32. ***Mheshimiwa Spika,*** fedha hizo zimeelekezwa katika ujenzi wa majengo **28** ya wagonjwa mahututi (ICUs); majengo **80** ya dharura (EMDs), nyumba **150** (**3 in 1**) kwa ajili ya watumishi wa Afya zinazoendelea kujengwa katika maeneo ya pembezoni; ujenzi wa kituo cha matibabu ya magonjwa ya mlipuko katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu; ajira **150** za mkataba kwa watumishi wa sekta ya Afya pamoja na uhamasishaji wa chanjo dhidi ya UVIKO - 19. Utekelezaji wa ujenzi upo katika hatua mbalimbali na unatarajiwa kukamilika ifikapo Mei, 2022.

33. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Ofisi ya Rais – TAMISEMI ilipokea **Shilingi bilioni 9.19** kutoka Shirika la *Global Alliance for Immunization* (GAVI) kwa ajili ya utoaji wa chanjo ya kukabiliana na mlipuko wa UVIKO – 19 ambapo mafunzo kwa watoa huduma za afya, utoaji wa chanjo kwa njia ya mkoba na tembezi, uhamasishaji wa jamii na usimamizi wa usambazaji wa chanjo za UVIKO – 19 ulifanyika katika Mikoa yote 26 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 184.

**Huduma za Ustawi wa Jamii**

34. ***Mheshimiwa Spika***, kuanzia Julai 2021 hadi Februari 2022 mashauri **57,088** ya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto yaliripotiwa. Kati ya hayo, mashauri **38,464** sawa na **asilimia 67** ni ukatili dhidi ya wanawake na **18,624** sawa na **asilimia 33** ni ukatili dhidi ya watoto. Mashauri **53,199** yalitatuliwa na Ofisi za Ustawi wa Jamii ngazi ya Halmashauri na mashauri **3,889** yalifikishwa mahakamani ambapo mashauri **1,501** sawa na **asilimia 39** yametolewa hukumu.

35. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, mashauri ya migogoro ya kifamilia **79,679** yaliripotiwa, kati ya hayo, mashauri **77,654** sawa na **asimilia 97** yalitatuliwa na Ofisi za Ustawi wa Jamii ngazi ya Halmashauri na mashauri **2,025** sawa na **asilimia 2.5** yalifikishwa mahakamani na kutolewa hukumu.

36. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2021 hadi Februari 2022 jumla ya watoto **692,901** ambapo Wavulana ni **336,809** na Wasichana **356,092** walio katika mazingira hatarishi walitambuliwa na kupewa huduma za chakula, malazi, mavazi, matibabu na wengine **330,250** sawa na **asilimia 48** waliunganishwa na familia zao.

37. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile ununuzi wa pikipiki **268** kupitia wadau wa *USAIDS* Kizazi Kipya na Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO -19 zenye ya thamani ya **Shilingi milioni 789.9** kwa ajili ya Maafisa Ustawi wa Jamii umefanyika, ambapo pikipiki **68** zimenunuliwa kupitia wadau wa *USAIDS* Kizazi Kipya na kusambazwa katika baadhi ya Halmashauri katika Mikoa **21** kwa thamani ya **Shilingi milioni 227.50** na pikipiki **200** kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO -19 ambazo ziko katika hatua ya mwisho ya manunuzi zenye thamani ya **Shilingi milioni 562.40** ambazo zitasambazwa katika maeneo ambayo hayakupata mgao wa pikipiki**.** Aidha, vifaa vya ofisi kwa ajili ya Ofisi za Ustawi wa Jamii katika Halmashauri zikiwemo meza **57,** viti **156,** makabati **1,033** vyote vikiwa na thamani ya **Shilingi milioni 613.07** katika Halmashauri **81**.

38. ***Mheshimiwa Spika***, watoto **3,605** walio kwenye mazingira hatarishi katika Halmashauri **81** walipewa mafunzo ya ufundi

kupitia Vyuo vya Ufundi Stadi (VETA) na kupewa vifaa vya kuanzia kazi vyenye thamani ya **Shilingi bilioni 15.6**. Vilevile, watoto **117,513** wanaoishi katika mazingira hatarishi kwenye kaya **40,487** katika Halmashauri **71** wamepewa Kadi za Mfuko wa Afya ya Jamii iliyoboreshwa (iCHF) zenye thamani ya **Shilingi bilioni 1.71**.

39. ***Mheshimiwa Spika***, hadi Februari 2022 mfumo wa usajili na utoaji wa vyeti vya kuzaliwa bila malipo kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano uliozinduliwa katika Mikoa ya Arusha na Manyara umefanyika jumla ya watoto **634,222** ambao wamesajiliwa. Mpango huu unatarajia kuendelea katika mikoa yote. Aidha, jumla ya Watu Wenye Ulemavu **124,900** wametambuliwa ambapo wanawake ni **59,059** na Wanaume **65,841**. Kati ya hao wanufaika **15,596** wamepatiwa huduma mbalimbali zenye thamani ya **Shilingi bilioni 1.30** zikiwemo vifaa saidizi, huduma za utengamao na matibabu.

**Huduma za Lishe**

40. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kusimamia utekelezaji wa Mkataba wa Lishe unaotekelezwa katika Mikoa na Halmashauri zote nchini ambao ulisainiwa mnamo Desemba 2017 baina ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri na Watendaji wa Kata, Watendaji wa Kata na Watendaji wa Vijiji/Mitaa. Mkataba wa lishe umesaidia kuongeza uwajibikaji na usimamizi wa utekelezaji wa Afua za Lishe.

41. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, **Shilingi bilioni 11.9** zilitengwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kutekeleza afua za lishe ikiwemo kutoa elimu ya lishe ngazi ya jamii, nyongeza ya Vitamin A kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano (5), kutoa vidonge vya kuongeza damu kwa akina mama wajawazito na wanaonyonyesha. Fedha hizo zinatokana na Mpango wa kila Halmashauri kutenga **Shilingi 1,000.00** kwa kila mtoto mwenye umri wa chini ya miaka mitano. Hadi Februari, 2022 **Shilingi bilioni 6.62** sawa na **asilimia 56** zilikuwa zimepokelewa na kutumika kutekeleza afua za lishe. Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaendelea kuratibu na kusimamia utengaji na utolewaji wa fedha hizo katika Halmashauri.

## USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA ELIMU YA MSINGI NA SEKONDARI

42. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kusimamia uimarishaji wa utoaji wa huduma ya elimumsingi. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na:

### Elimumsingi

### Uandikishaji wa Wanafunzi wa Elimu ya Awali

43. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa masomo 2021 wanafunzi wapya wa Darasa la Awali walioandikishwa ni **1,198,564** sawa na **asilimia 94.19** ya lengo la kuandikisha wanafunzi **1,272,513**. Mwaka wa masomo 2022 jumla ya wanafunzi **1,363,834** walitarajiwa kuandikishwa. Hadi Machi, 2022 wanafunzi **1,411,810** sawa na **asilimia 103.52** ya lengo wakiwemo wanafunzi wenye mahitaji maalum **3,511** wameandikishwa. Uandikishwaji huo ni ongezeko la wanafunzi **213,246** sawa na **asilimia 17.79** ikilinganishwa na wanafunzi walioandikishwa kwa kipindi kama hiki kwa mwaka 2021 (***Kiambatisho Na. 4).***

### Uandikishaji wa Wanafunzi wa Darasa la Kwanza

44. ***Mheshimiwa* Spika,** katika mwaka wa masomo 2021 wanafunzi **1,516,598** walitarajiwa kuandikishwa Darasa la Kwanza, walioandikishwa ni wanafunzi **1,549,279** sawa na **asilimia 102.15** ya lengo. Katika mwaka wa masomo 2022 wanafunzi wa Darasa la Kwanza walioandikishwa hadi Machi, 2022 ni **1,726,165** wakiwemo wanafunzi wenye mahitaji maalum **4,723** ambapo wavulana ni **2,618** na wasichana ni **2,105** wenye mahitaji maalum sawa na **asilimia 108.40** ya lengo la kuandikisha wanafunzi **1,592,375** ***(Kiambatisho Na. 5)***.

### Uandikishaji wa Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza

45. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya wanafunzi **907,803** ambapo wavulana ni **467,967** na wasichana **439,836** walichaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza mwaka 2022. Hadi Machi, 2022 wanafunzi **804,269** ambapo wavulana ni **400,469** na wasichana **403,800** wameandikishwa shule sawa na **asilimia 88.60** ya wanafunzi waliochaguliwa. Kati ya wanafunzi walioandikishwa, wanafunzi wenye mahitaji maalum ni **1,247** ambapo wavulana ni **699** na wasichana **548** ***(Kiambatisho Na. 6)***.

### Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne

46. ***Mheshimiwa Spika***, katika matokeo ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne mwaka 2020, jumla ya Wanafunzi **1,551,599** kati ya wanafunzi **1,704,286** sawa na **asilimia 91.04** walikidhi sifa za kuendelea Darasa la Tano. Aidha, katika mwaka 2021 jumla ya wanafunzi **1,681,791 ambapo** wasichana ni **856,860** na wavulana **824,931** walisajiliwa kufanya mtihani wa upimaji wa darasa la nne. Waliofanya mtihani ni wanafunzi **1,561,599** ambapo wasichana ni **808,047** na wavulana **753,552** kati yao wanafunzi waliokidhi sifa za kuingia darasa la tano katika mwaka wa masomo 2022 ni **1,347,554** ambapo wasichana ni **708,203** na wavulana **639,351**.

**Mtihani wa Kuhitimu Elimu ya Msingi**

47. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mtihani wa Kuhitimu Darasa la Saba mwaka 2021 jumla ya wanafunzi **1,132,084** ambapo wasichana ni **584,614** na wavulana **547,470** walisajiliwa kufanya Mtihani wa Kuhitimu Elimu ya Msingi. Watahiniwa **1,108,023** ambapo wasichana ni **574,998** na wavulana **533,025** wakiwemo wanafunzi **3,279** wenye mahitaji maalum walifanya mtihani. Watahiniwa **907,802** ambapo wasichana ni **467,967** na wavulana **439,835** walifaulu wakiwemo wanafunzi wenye mahitaji maalum **2,673** ambapo wasichana ni **1,202** na wavulana **1,471**.

**Elimu ya Sekondari**

**Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili**

48. ***Mheshimiwa Spika*,** takwimu za matokeo ya Upimaji wa Kidato cha Pili zinaonesha kuwa kwa mwaka 2021, jumla ya wanafunzi **555,857** sawa na **asilimia 92.32** kati ya wanafunzi **602,107** katika matokeo ya Upimaji wamepata ujuzi na maarifa ya kuwawezesha kuendelea na Kidato cha Tatu, ambapo wasichana ni **300,492** na wavulana ni **255,365.** Mwaka 2020 wanafunzi **550,979** sawa na **asilimia 91.61** walipata alama za kuwawezesha kuendelea na masomo ya Kidato cha Tatu. Hivyo, ufaulu wa Kidato cha Pili umepanda kwa **asilimia 0.71** ikilinganishwa na mwaka 2020.

**Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne**

49. ***Mheshimiwa Spika*,** kwa upande wa Kidato cha Nne jumla ya Watahiniwa wa Shule **422,388** ikiwa wasichana ni **218,174**

na wavulana **204,214** wamefaulu sawa na asilimia **87.30** ya watahiniwa **483,820** waliofanya mtihani wa kuhitimu Kidato cha Nne mwaka 2021. Mwaka 2020 watahiniwa **373,958** sawa na **asilimia 85.84** ya Watahiniwa wa Shule walifaulu mtihani huo. Hivyo, ufaulu wa Watahiniwa wa Shule mwaka 2021 umeongezeka kwa **asilimia 1.46** ikilinganishwa na mwaka 2020.

**Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Sita**

50. ***Mheshimiwa Spika***, ufaulu wa Kidato cha Sita kwa mwaka 2021 ulikuwa ni **asilimia 99.62** ambapo watahiniwa **79,596** kati ya watahiniwa **80,302** waliofanya mtihani walifaulu ikilinganishwa na mwaka 2020 ambapo watahiniwa **73,537** kati ya **74,284** ya waliofanya mtihani walifaulu sawa na **asilimia 99.51** ya watahiniwa. Ufaulu wa Kidato cha Sita umeendelea kuwa bora zaidi kila mwaka.

**Wanafunzi waliochaguliwa Kidato cha Tano mwaka, 2021**

51. ***Mheshimiwa Spika***, jumla ya wanafunzi **87,663** ambapo wasichana ni **41,885** na wavulana **45,778** sawa na asilimia **58.67** ya wanafunzi **148,127** wenye sifa walichaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule **476** za Serikali. Kati yao wanafunzi wenye mahitaji maalumu walikuwa ni **288** wakiwemo wasichana **123** na wavulana **165** sawa na **asilimia 100** ya wenye mahitaji maalum waliokuwa na sifa za kujiunga Kidato cha Tano. Kati ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano, wanafunzi **41,504** wakiwemo wasichana **17,646** na wavulana **23,858** sawa na **asilimia 47.34**, wamechaguliwa kusoma tahasusi za Sayansi na Hisabati; wanafunzi **46,159** wakiwemo wasichana **24,239** na wavulana **21,920** sawa na asilimia **52.66** wamechaguliwa kusoma tahasusi za masomo ya Sanaa na Biashara.

**Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi**

52. ***Mheshimiwa Spika,*** uandikishaji wa wanafunzi wa Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA) umeendelea kupungua mwaka hadi mwaka. Matokeo ya uandikishaji kwa wanafunzi hao hadi mwezi Februari 2022 yanaonesha kupungua ambapo wanafunzi **12,421** wakiwemo wavulana **6,880** na wasichana **5,541** wameandikishwa. Idadi hiyo imepungua kwa **asilimia 75.25**

ikilinganishwa na wanafunzi **50,192** wakiwemo wavulana **27, 819** na wasichana **22,373** walioandikishwa mwaka 2021.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** kupungua kwa uandikishaji kunatokana na mafanikio ya utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi Bila Malipo ambapo kuanzia mwaka 2015 hadi Februari, 2022 mpango umewezesha wanafunzi wenye umri wa kwenda shule kuandikishwa kutokana na kuondolewa kwa ada na michango mbalimbali ambayo ilikuwa ni miongoni mwa vikwazo vilivyopunguza kiwango cha uandikishaji. Sababu nyingine ni kutokana na kusogeza huduma za Elimumsingi karibu na wanafunzi kwa kujenga na kuboresha Vituo shikizi vilivyowapunguzia wanafunzi kutembea umbali mrefu kufuata huduma ya elimu. Hii inaashiria kwamba wanafunzi waliokuwa wanakosa nafasi ya elimu katika mfumo rasmi sasa wanapata fursa hiyo. Aidha, uandikishaji wa watoto wenye umri wa kwenda shule unafanyika kwa wakati.

**Elimu Maalum**

54. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI inasimamia Shule Maalum **37** za bweni, Vitengo Maalum **710** vinavyoshughulikia wanafunzi wenye mahitaji maalum katika Shule za Msingi na Shule Jumuishi **3,956** zenye wanafunzi wenye mahitaji maalum wa Shule za Msingi. Kwa upande wa Sekondari, kuna Shule Maalum moja ya Patandi na Shule Jumuishi **127**. Vilevile, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Serikali imeajiri walimu **766** waliosomea taaluma ya Elimu Maalum ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wenye mahitaji maalum wanapata elimu sawa na wanafunzi wengine. Aidha, Serikali imenunua na kusambaza vifaa visaidizi **82,919** vyenye thamani ya **Shilingi bilioni 4.6** kwenye shule zenye wanafunzi wenye mahitaji maalum.

**Michezo kwa Shule za Msingi na Sekondari**

55. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais -TAMISEMI imeendelea kuhimiza na kusimamia maendeleo ya michezo katika Shule za Msingi na Sekondari ikiwemo ufundishaji wa somo la Elimu kwa michezo darasani. Katika mwaka wa masomo 2021 ufaulu wa somo la Elimu kwa michezo kwa wanafunzi wanaomaliza Kidato cha Nne umeongezeka kutoka asilimia **45.3** mwaka 2020 hadi **asilimia 83** mwaka 2021 ambapo watahiniwa **1,702** walifanya

mtihani wa somo la elimu kwa michezo ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi **1,669** wa mwaka 2020. Aidha, mashindano ya michezo ya Umoja wa Michezo na Taaluma Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA) na Umoja wa Michezo Shule za Sekondari Tanzania (UMISSETA) yaliendelea kufanyika kwa ubora zaidi na hivyo kuendelea kuwa kitalu cha kuendeleza na kuvuna wanamichezo wa kuunda timu za taifa za michezo mbalimbali kwa vijana.

**Tathmini ya Mahitaji ya Walimu kwa Shule za Msingi na Sekondari**

56. ***Mheshimiwa Spika***, takwimu zilizopo zinaonesha kuwa kuna jumla ya Shule za Msingi **17,034** zenye jumla ya wanafunzi **12,033,594** wakiwemo wanafunzi wenye mahitaji maalum **60,825** na Shule za Sekondari **4,175** zenye jumla ya wanafunzi **2,607,142** wakiwemo wanafunzi wenye mahitaji maalum **11,106**. Jumla ya walimu waliopo ni **258,291** wakiwemo walimu wa Shule za Msingi **173,591** na Sekondari walimu **84,700.**

57. ***Mheshimiwa Spika***, hadi Machi, 2022 mahitaji ya walimu katika Shule za Msingi ni **274,549** kwa kutumia uwiano wa **1:60** (Mwalimu mmoja kwa wanafunzi 60) walimu waliopo ni **173,591** na upungufu ni **100,958** sawa na **asimilia 36.77** ya mahitaji. Aidha, mahitaji ya walimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa Shule za Msingi ni walimu **3,631**, waliopo ni **1,517** na upungufu ni walimu **2,143** sawa na **asilimia 59.02** ya mahitaji. Vilevile, mahitaji ya walimu kwa Shule za Sekondari ni **159,443** waliopo ni **84,700** na upungufu ni walimu **74,743** sawa na asilimia **46.87.**

58. ***Mheshimiwa Spika*,** katika kukabiliana na upungufu wa walimu uliopo, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeomba kibali cha kuajiri walimu **10,000** wa Shule za Msingi na Sekondari. Kati ya hao, walimu **5,000** ni kwa ajili ya shule za Awali na Msingi na **5,000** kwa ajili ya Shule za Sekondari. Hii itapunguza mahitaji ya walimu wa Shule za Sekondari kwa **asilimia 6.56** na elimu ya Awali na Msingi kwa **asilimia 10.65**. Ili kutoa elimu yenye ubora katika maeneo yote, Serikali itaendelea kuajiri walimu katika Shule za Msingi na Sekondari kulingana na upatikanaji wa fedha ikiwa ni pamoja na kutoa ajira mbadala kwa walimu wanaoondoka kwenye utumishi wa umma kwa sababu mbalimbali.

**Ujenzi na Ukamilishaji wa Miundombinu ya Elimu ya Msingi na Sekondari**

**Ujenzi wa Miundombinu ya Elimu**

59. ***Mheshimiwa Spika***, kipekee nichukue fursa hii kumshukuru **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuzipatia Mamlaka za Serikali za Mitaa **Shilingi bilioni 304.00,** kutokana na mkopo wenye masharti nafuu kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kwa ajili ya kukabiliana na athari za kiuchumi zilizotokana na ugonjwa wa UVIKO-19.

60. ***Mheshimiwa Spika***, fedha hizi zimetumika katika ujenzi wa vyumba vya madarasa **12,000** katika Shule za Sekondari, vyumba vya madarasa **3,000** katika Vituo shikizi na mabweni **50** kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum. Hadi Februari, 2022 vyumba vya madarasa **11,988** kati ya vyumba **12,000** vya Shule za Sekondari vimejengwa na kukamilika sawa na **asilimia 99.99**. Vilevile, vyumba vya madarasa **2,978** kati ya **3,000** vimejengwa na kukamilika katika Vituo shikizi sawa na **asilimia 99.26**. Aidha, mabweni **49** yanaendelea kujengwa na yanategemewa kukamilika ifikapo tarehe 30 Aprili, 2022. Kupitia Mpango huo, ofisi za walimu **3,184**, matundu ya vyoo **557** yamejengwa, ajira zilizozalishwa **21,872** wakiwemo wanaume **17,354** na wanawake, **4,518**, madawati **47,149** na seti ya meza na viti **451,918** vimetengenezwa.

61. ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa mpango huo umepunguza uhaba wa miundombinu ya shule katika Shule za Msingi na Sekondari. Hii imewezesha wanafunzi wote **907,803** waliofaulu mtihani wa darasa Saba mwaka 2021 kupata nafasi ya kuanza Kidato cha Kwanza Januari, 2022 bila kuwa na chaguo la pili.

62. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2021/22 kupitia Programu ya Uboreshaji wa Elimu katika Shule za Sekondari (Secondary Education Quality Improvement Program-SEQUIP) jumla ya **Shilingi bilioni 30** zimepokelewa ambapo kila Shule imepokea **Shilingi bilioni 3.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Shule za Sekondari za masomo ya sayansi kwa Wasichana **(*Kiambatisho Na. 7)***.

63. ***Mheshimiwa Spika***, katika Awamu ya Kwanza ujenzi unafanyika katika shule **10** kati ya shule **26** za Sekondari za Wasichana za bweni kwa masomo ya sayansi (shule moja kwa kila Mkoa) ambapo katika awamu hii ujenzi umeanza kwa kujenga miundombinu ya Kidato cha Tano na Sita. Shule hizi zitakapokamilika zitakuwa na uwezo wa kuchukua kati ya wanafunzi **1,000** hadi **1,200.**

64. ***Mheshimiwa Spika***, kupitia SEQUIP katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepokea **Shilingi bilioni 109.57** kwa ajili ya ujenzi wa Shule za Sekondari **232** ambazo zitajengwa kwenye kata zisizokuwa na Shule za Sekondari kwa Awamu ya Kwanza ambapo kila Shule imepokea **Shilingi milioni 470** kwa ajili ya kuanza ujenzi huo. Aidha, Shule moja kati ya shule hizo imepokea **Shilingi bilioni 1.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa shule ya sekondari ya Kidato cha Tano na Sita **(*Kiambatisho Na. 7)***.

65. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Ofisi ya Rais – TAMISEMI imepokea **Shilingi bilioni 8.24** kutoka Mamlaka ya Elimu Tanzania (Tanzania Education Authority-TEA) kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya Shule za Msingi na Sekondari. Miundombinu itakayojengwa ni pamoja na vyumba vya madarasa **210** katika shule **65** (Shule za Msingi **53** na Sekondari **12**), ujenzi wa maabara **sita (6)** katika Shule za Sekondari mbili **(2)**, matundu **1,920** ya vyoo katika shule **80** (Shule za Msingi **58** na Sekondari **22**), miundombinu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule **9** ambapo Shule za Msingi **8** na shule moja (1) ya Sekondari na ofisi za walimu katika shule mbili (2) za Sekondari.

66. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Ofisi ya Rais – TAMISEMI imepokea jumla ya **Shilingi bilioni 17.25** kwa ajili ya ujenzi wa Shule mpya za Sekondari **15** na Shule za Msingi **9** kupitia Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo (Education Performance for Results - EP4R).

67. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Ofisi ya Rais – TAMISEMI imepokea **Shilingi bilioni 12.37** kupitia Mradi wa

Kuimarisha Ufundishaji na Ujifunzaji katika Elimu ya Msingi (Global Partnership for Education - GPE LANES II). Kazi zinazoendelea kufanyika ni ujenzi wa vyumba **304** vya madarasa, mabweni nane (**8)** ya wanafunzi wenye mahitaji maalum katika Shule za Msingi, nyumba **11** za walimu, matundu **548** ya vyoo, ujenzi wa shule mpya **10** za Msingi na majengo manne **(4)** ya utawala.

**Ukamilishaji wa Ujenzi wa Maboma ya Madarasa na Maabara kupitia Ruzuku ya Serikali Kuu**

68. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Serikali iliidhinisha jumla ya **Shilingi bilioni 23.16** kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa maboma ya vyumba vya madarasa **1,853** katika Shule za Msingi. Hadi Februari 2022, **Shilingi bilioni 20.31** zimetolewa sawa na **asilimia 87.71** ya fedha iliyoidhinishwa. Aidha, ukamilishaji wa ujenzi wa maboma ya vyumba vya madarasa unaendelea (***Kiambatisho Na. 8).***

69. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 jumla ya **Shilingi bilioni 23.00** ziliidhinishwa kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba **1,840** vya madarasa katika Shule za Sekondari. Hadi Februari, 2022 zimetolewa **Shilingi bilioni 23.00** sawa na **asilimia 100** ambapo ukamilishaji wa ujenzi wa madarasa haya upo katika hatua mbalimbali. (***Kiambatisho Na. 8)***

70. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha Elimu ya Sayansi kwa Vitendo Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya ukamilishaji ujenzi wa vyumba vya maabara ya masomo ya sayansi katika Shule za Sekondari. Katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Ofisi ya Rais - TAMISEMI iliidhinishiwa **Shilingi bilioni 26.07** kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba **869** vya maabara za masomo ya sayansi. Hadi Februari, 2022 zimetolewa **Shilingi bilioni 22.27** sawa na **asilimia 85.42** ya fedha zilizoidhinishwa na ukamilishaji wa ujenzi upo katika hatua mbalimbali (***Rejea Kiambatisho Na. 8).***

71. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Serikali ilianzisha tozo ya miamala ya simu kwa ajili ya ujenzi wa

miundombinu ya kutolea huduma ambapo Ofisi ya Rais - TAMISEMI ilipokea jumla ya **Shilingi bilioni 7.00** kwa ajili ya kukamilisha maboma **560** ya vyumba vya madarasa katika Shule za Sekondari ambapo utekelezaji upo katika hatua mbalimbali (***Kiambatisho Na. 8).***

**ElimuMsingi bila Malipo**

72. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 ziliidhinishwa jumla ya **Shilingi bilioni 312.05** kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi Bila Malipo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 142.72** ni kwa ajili ya Shule za Msingi na **Shilingi bilioni 169.33** kwa Shule za Sekondari. Hadi Februari, 2022 jumla ya **Shilingi bilioni 192.44** zimepelekwa katika shule sawa na **asilimia 61.67** ambapo **Shilingi bilioni 89.62** ni kwa ajili ya Shule za Msingi na **Shilingi bilioni 102.82** kwa ajili ya Shule za Sekondari. Fedha hizi ni zinatumika katika maeneo ya uendeshaji wa shule, chakula kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum wa Shule za Msingi na wanafunzi wa bweni wa Shule za Sekondari, fidia ya ada kwa wanafunzi wa kutwa na bweni wa Kidato cha Kwanza hadi cha Nne na posho ya madaraka kwa Wakuu wa Shule na Maafisa Elimu Kata (***Kiambatisho Na. 9 & 10).***

**Ajira katika Sekta ya Afya na Elimu**

73. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na upungufu wa watumishi katika sekta ya afya na elimu chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI Serikali imeendelea kutoa ajira za watumishi katika maeneo hayo. Katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Serikali kupitia Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imetoa vibali vya nafasi za ajira **17,412** ambapo **7,612** ni ajira za watumishi wa kada za afya na **9,800** ni ajira za walimu wa shule za msingi na sekondari. Naomba nitumie fursa hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ***Mheshimwa Samia Suluhu Hassan*** kwa kutoa kibali cha ajira hizo za watumishi.

**MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI**

74. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22 Halmashauri ziliidhinishiwa kukusanya **Shilingi bilioni**

**863.85** kutoka kwenye vyanzo vyake vya Mapato ya Ndani ikiwa ni ongezeko la **Shilingi bilioni 48.94** ikilinganishwa na bajeti ya **Shilingi bilioni 814.96** ya Mwaka wa Fedha 2020/21.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari, 2022 Halmashauri zimekusanya jumla ya **Shilingi bilioni 586.07** sawa na **asilimia 67.84** ya makisio kwa Mwaka wa Fedha 2021/22. Makusanyo haya ni ongezeko la **Shilingi bilioni 112.13** ikilinganishwa na makusanyo ya **Shilingi bilioni 473.94** yaliyokusanywa kwa kipindi kama hiki mwaka 2020/21 (***Kiambatisho Na. 11).***

76. ***Mheshimiwa Spika***, kuongezeka kwa Mapato kumetokana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka mikakati ya pamoja ya kubuni vyanzo vipya, kuimarisha vilivyopo na mikakati zaidi ya ukusanyaji wa mapato.

77. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais – TAMISEMI itaendelea kuzisimamia Halmashauri ili ziongeze wigo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani. Mikakati iliyowekwa ni pamoja na kuwajengea uwezo maafisa wanaokusanya mapato, kuboresha mfumo wa ukusanyaji mapato na utambuzi wa fursa na uibuaji wa vyanzo vipya vya mapato. Aidha, utendaji wa Halmashauri utapimwa kwa kuzingatia upelekaji wa asilimia 40/60 za fedha zinazotokana na makusanyo ya mapato ya ndani yasiyolindwa katika miradi ya maendeleo, utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, na urejeshaji wa mikopo na ujibuji wa hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa wakati.

**Miradi ya Maendeleo iliyotekelezwa kupitia Fedha za Mapato ya Ndani ya Halmashauri**

78. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 ziliidhinishwa jumla ya **Shilingi bilioni 331.08** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia fedha za Mapato ya Ndani ya Halmashauri. Hadi Februari, 2022 jumla ya **Shilingi bilioni 216.11** sawa na **asilimia 65.27** zimetumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwa ni **asilimia 40/60** ya Mapato yasiyolindwa kulingana na makundi ya Halmashauri.

79. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Ofisi ya Rais -TAMISEMI iliidhinishiwa **Shilingi bilioni 17.68** kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa maboma **1,415** ya vyumba vya madarasa kwa Shule za Msingi kupitia Mapato ya Ndani ya Halmashauri. Hadi Machi, 2022 jumla ya **Shilingi bilioni 19.43** zimetolewa sawa na **asilimia 109.89** ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba madarasa. Ongezeko hilo limetokana na baadhi ya Halmashauri kuanza kujenga madarasa mapya kutokana na kutokuwa na maboma ya madarasa ya kumalizia.

80. ***Mheshimiwa Spika****,* katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Ofisi ya Rais - TAMISEMI iliidhinishiwa **Shilingi bilioni 9.95** kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa Zahanati **199** kupitia Mapato ya Ndani ya Halmashauri. Hadi Machi, 2022 **Shilingi bilioni 4.06** sawa na **asilimia 40.84** ya fedha zilizoidhinishwa zimetolewa kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa Zahanati ambao upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. (***Kiambatisho Na. 2)***.

81. ***Mheshimiwa Spika****,* katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Ofisi ya Rais – TAMISEMI iliidhinishiwa **Shilingi bilioni 51.50** kupitia Mapato ya Ndani ya Halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya **103**. Hadi Machi, 2022 kiasi cha **Shilingi bilioni 17.90** kimetolewa sawa na **asilimia 34.14** kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya ambavyo vipo katika hatua mbalimbali za ujenzi (***Kiambatisho Na. 3)***.

**Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi Kutokana na Asilimia 10 ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri**

82. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kusimamia utoaji wa Mikopo ya Uwezeshaji kwa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kwa mujibu wa Kifungu cha **37A** cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura **290** na Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu za mwaka 2019 kwa ajili ya utoaji wa mikopo na riba isiyo na riba kwa vikundi hivyo.

83. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2022 Halmashauri zimekopesha kiasi cha **Shilingi bilioni 35.55** ambapo **Shilingi bilioni**

**19.36** zimetolewa kwa vikundi vya Wanawake **2,881**, **Shilingi bilioni 13.51** zimetolewa kwa vikundi vya Vijana **1,441** na **Shilingi bilioni 2.68** zimetolewa kwa vikundi **580** vya Watu Wenye Ulemavu.

84. ***Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 fedha zilizokusanywa kutokana na marejesho ni **Shilingi bilioni 34.81** kutoka kwenye vikundi **29,443**. Fedha zilizorejeshwa kiasi cha **Shilingi bilioni 28.80** zimekopeshwa kwa vikundi **2,950** vya Wanawake, Vikundi **1,334** vya Vijana na Vikundi **322** vya Watu Wenye Ulemavu. Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Taasisi nyingine inaandaa mkakati wa kuimarisha ukopeshaji na urejeshaji wa fedha hizo.

85. ***Mheshimiwa Spika*,** baadhi ya miradi mikubwa iliyotekelezwa kupitia fedha za asilimia 10 ni pamoja na Kikundi cha *MIOMBO Beekepers Iniciateves Group* kilicho katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora. Kikundi hiki kilikopeshwa **Shilingi milioni 50.00** kwa ajili ya kuanzisha kiwanda cha kuchakata mazao yanayotokana na asali; Ujenzi wa kiwanda kidogo cha kutengeneza sabuni na dawa za usafi kinachomilikiwa na Kikundi cha Wanawake cha Juhudi ambapo kikundi hiki kilikopeshwa **Shilingi milioni 380**; Kiwanda cha kutengeneza Batiki kinachomilikiwa na Kikundi cha Wanawake cha *Hand Product of Tanzania* kilichokopeshwa **Shilingi milioni 150**; na Kikundi cha *NURU Disabled* kinajishughulisha na usafirishaji wa mizigo kwenda mikoani, kikundi hiki kinamiliki Lori aina ya SCANIA na kilikopeshwa **Shilingi milioni 100**. Vikundi vyote hivi vinapatikana katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. Aidha, kikundi cha *Bulldozer Youth Group* kutoka Halmashauri ya Jiji la Tanga kinachojihusisha na shughuli za uvuvi na uuzaji wa samaki kimepata mkopo wa **Shilingi milioni 50.00** na kununua boti ya uvuvi. Kikundi hiki kinafanya vizuri na kimetoa ajira za kudumu kwa vijana **kumi (10)** na kinatarajia kutoa ajira zaidi kwa anawake na vijana katika eneo linapojengwa bomba la mafuta. Nitumie fursa hii kutoa maelekezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kutoa elimu ya ujasiriamali na kutoa mikopo kwenye miradi yenye tija ili kuhakikisha fedha hizi zinaleta mabadiliko chanya kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.

**Maboresho ya Miundombinu ya Wafanyabiashara Wadogo (Machinga)**

86. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19 Ofisi ya Rais – TAMISEMI imepokea **Shilingi bilioni 5.00** mwezi Machi, 2022 kwa ajili ya kufanya maboresho ya miundombinu ya maeneo ya wafanyabiashara wadogo (machinga) katika Halmashauri. Halmashauri zilizonufaika na fedha hizo ni za Majiji ya Dar es Salaam (**Shilingi milioni 263.13**), Arusha (**Shilingi milioni 500.00**), Mwanza (**Shilingi milioni 500.00**), Mbeya (**Shilingi milioni 540.96**), Dodoma (**Shilingi milioni 500.00**) na Tanga (**Shilingi milioni 540.34**); Halmashauri za Manispaa za Morogoro (**Shilingi milioni 490.20**), Kinondoni (**Shilingi milioni 441.89**), Temeke (**Shilingi milioni 441.94**), Ubungo (**Shilingi milioni 398.50**); na Halmashauri ya Mji Tunduma (**Shilingi milioni 383.00**). Utekelezaji wa miradi hiyo unaendelea katika maeneo yote yaliyopokea fedha. Serikali itaendelea kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu ya machinga kwenye maeneo mengine ili yaweze kunufaika na mpango huo.

**Miradi ya Kimkakati**

87. **Mheshimiwa *Spika*,** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 ziliidhinishwa jumla ya **Shilingi bilioni 68.70** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati ili kuziwezesha Halmashauri kuongeza mapato kwa lengo la kupunguza utegemezi wa Serikali Kuu, miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa stendi za kisasa za mabasi, maegesho ya malori, ujenzi wa viwanda vya chaki na vifungashio pamoja na masoko yanayojengwa katika Halmashauri mbalimbali.

88. ***Mheshimiwa Spika*,** hadi Februari, 2022 jumla ya **Shilingi bilioni 22.01** sawa na **asilimia 32.03** zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo. Halmashauri **12** ambazo zinaendelea na utekelezaji wa miradi ni; Halmashauri za Majiji ya Dar es Salaam (ujenzi wa Soko la kisasa Kisutu umekamilika kwa **asilimia 97)**, Tanga (ujenzi wa kituo cha mabasi Kange umekamilika kwa **asilimia 80**) na Mwanza (ujenzi wa soko la mjini kati katika Kata ya Pamba umekamilika kwa **asilimia 71** na ujenzi wa kituo cha

mabasi Nyegezi umekamilika kwa **asilimia 73**); Halmashauri za Manispaa za Kinondoni (ujenzi wa soko la kisasa Tandale umekamilika kwa **asilimia 70**) na Iringa (ujenzi wa machinjio ya kisasa Ngelewala umekamilika kwa **asilimia 93**).

89. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile miradi mingine ya kimkakati inaendelea kutekelezwa katika Halmashauri za Miji ya Tunduma (ujenzi wa maegesho ya malori mpakani mwa Tanzania na Zambia umekamilika kwa **asilimia 95** na ujenzi wa kituo cha mabasi Mpemba umekamilika kwa **asilimia 70**), Kibaha (ujenzi wa soko la kisasa katika eneo la kitovu cha Mji umekamilika kwa **asilimia 90**), Halmashauri za Wilaya za Maswa (ujenzi wa kiwanda cha chaki umekamilika kwa **asilimia 99**), Hanang (ujenzi wa kituo cha mabasi Kateshi Mjini umekamilika kwa **asilimia 5**) na Biharamulo (ujenzi wa kituo cha maegesho ya magari makubwa Nyakanazi umekamilika kwa **asilimia 98**). Aidha, miradi ya ujenzi wa kituo cha mabasi na maegesho ya malori katika Kata ya Nyamhongolo Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela na Soko la Magomeni katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imekamilika.

## UTAWALA BORA, USIMAMIZI WA RASILIMALI, UJENZI WA MAJENGO YA UTAWALA NA NYUMBA ZA VIONGOZI

### Utawala Bora na Usimamizi wa Rasilimali

90. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kusimamia Utawala Bora katika Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na maeneo yaliyopatiwa kipaumbele kama ifuatavyo: -

### Ushughulikiaji wa Kero na Malalamiko ya Wananchi katika Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

91. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendelea kuimarisha Utawala bora, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeendelea kutekeleza dhana ya ‘‘TAMISEMI ya Wananchi’’. Katika kutekeleza dhana hiyo, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kuimarisha Kituo cha Huduma ya Mawasiliano kwa Mteja (Call Centre) kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi bila ya kuhitajika kufika katika Ofisi ya Rais - TAMISEMI Dodoma.

92. ***Mheshimiwa Spika***, hadi Februari 2022, Kituo hiki kimehudumia jumla ya wananchi **126,000** kuhusu kero, malalamiko na ufafanuzi tangu kilipoanza kutoa huduma tarehe 06 Agosti, 2020. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Kituo hiki kimesaidia kupunguza changamoto ya upatikanaji wa taarifa zinazohitajika kwa wananchi, naendelea kuwasisitiza Waheshimiwa Wakuu Mikoa kuanzisha Vituo vya Huduma ya Mawasiliano kwa Wateja (Call Centre) katika maeneo yao ili kuwapunguzia wananchi adha ya kusafiri umbali mrefu kutafuta huduma.

93. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kuboresha na kuimarisha utendaji kazi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ili zitoe huduma bora kwa wananchi. Katika kutekeleza azma hii, watumishi waliokaa kwenye vituo vya kazi kwa muda mrefu hususan Wakuu wa Idara na Vitengo wameanza kuhamishwa kutoka vituo vya zamani na kupelekwa katika vituo vipya. Aidha, Ofisi ya Rais – TAMISEMI itaendelea kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi wasiozingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za kazi ikiwa ni pamoja na kuwashusha vyeo na kuwaondoa kazini **watumishi wazembe na wabadhirifu wa mali za umma**.

94. ***Mheshimiwa Spika***, kupitia Bunge lako Tukufu naomba nitoe maelekezo kwa watumishi wote wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Taasisi zilizo chini yake, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria na Taratibu.

**Usimamizi wa Fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa**

95. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kutoa maelekezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu usimamizi wa fedha kwa kuzingatia Sheria, Taratibu na Miongozo inayotolewa mara kwa mara ili kujenga nidhamu ya matumizi ya fedha za umma. Lengo ni kuhakikisha kazi zinazotekelezwa zinalingana na thamani ya fedha iliyotumika. Aidha, taarifa kwa umma kuhusu mwenendo wa makusanyo ya Mapato ya Ndani

katika Halmashauri zote imeendelea kutolewa kupitia vyombo vya habari kila robo mwaka.

96. ***Mheshimiwa Spika***, taarifa ya ukaguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(Controller and Auditor General - CAG)* kuhusu Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2020/21 imebainisha Halmashauri **178** sawa na **asilimia 96** zimepata Hati Safi, Halmashauri **6** sawa na **asilimia 3** zimepata Hati Zenye Shaka na Halmashauri **1** sawa na asilimia **1** imepata Hati Mbaya.

97. ***Mheshimiwa Spika,*** matokeo ya ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2020/21 yanaonesha mwenendo mzuri wa aina ya Hati za Ukaguzi zilizotolewa ikilinganishwa na ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha wa 2019/20 ambapo Halmashauri zilizopata Hati Safi zilikuwa **124** sawa na **asilimia 67**, Halmashauri zilizopata Hati Zenye Shaka zilikuwa **53** sawa na **asilimia 29** na Halmashauri zilizopata Hati Mbaya zilikuwa **8** sawa na **asilimia 4.**

98. ***Mheshimiwa Spika***, matokeo hayo mazuri yametokana na jitihada mbalimbali zilizofanywa na Serikali, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa (USEMI) na wadau wengine katika kuhakikisha kuwa changamoto zilizojitokeza katika ukaguzi uliotangulia wa mwaka wa fedha 2019/20 zinafanyiwa kazi kama ilivyoshauriwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu hatua zinazochukuliwa dhidi ya vitendo vya matumizi mabaya ya fedha za umma kwenye baadhi ya Halmashauri ni kwamba, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imekuwa ikiratibu na kusimamia uchukuaji wa hatua stahiki za kinidhamu na kisheria kwa Watumishi, Wakandarasi, Wahandisi Washauri na Wazabuni wengine ambao wamekuwa wakibainishwa kwenye taarifa za ukaguzi kujihusisha na vitendo vya ubadhirifu wa fedha za umma.

100. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2022, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imepokea na kuchambua taarifa za ukaguzi maalum uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

kwenye Halmashauri **64**. Ofisi za Wakuu wa Mikoa zimeelekezwa kusimamia uchukuaji wa hatua stahiki za kinidhamu kwa watumishi zaidi ya **1,000** waliotajwa kuhusika na kasoro mbalimbali zilizobainishwa kwenye taarifa hizo.

101. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI tayari imewasiliana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ili izifanyie kazi taarifa hizo kwenye maeneo yanayohusu ubadhirifu wa fedha na mali za Halmashauri. Vile vile, Ofisi ya Rais – TAMISEMI inakamilisha uchambuzi wa Wakandarasi na Wahandisi Washauri wote waliotajwa kwenye taarifa za ukaguzi ili wafikishwe kwenye Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) kwa hatua stahiki kufuatia ukiukaji wa maadili ya taaluma zao.

**Matumizi ya Fedha za Mfuko wa Jimbo**

102. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Ofisi ya Rais –TAMISEMI iliidhinishiwa **Shilingi bilioni 11.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Majimbo ya Uchaguzi **214** ya Tanzania Bara. Hadi Februari, 2022 fedha zote zilizokuwa zimeiidhinishwa zilikuwa zimetolewa sawa na **asilimia 100**. Fedha za Mfuko wa Jimbo zimeelekezwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyoanzishwa kwa nguvu za Wananchi ikiwa ni pamoja na ukamilishaji wa ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za kijamii hususan katika sekta ya afya na elimu.

**Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA**

103. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kuimarisha mifumo ya kielektroniki na miundombinu ya TEHAMA kwenye Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi zilizo chini yake na vituo vya kutolea huduma ambayo imeongeza ufanisi na uwajibikaji. Mifumo mbalimbali imefanyiwa usanifu na kusimikwa kwenye maeneo ya kutolea huduma nchini.

104. ***Mheshimiwa Spika***, Mifumo iliyosanifiwa na kusimikwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI ni pamoja na Mfumo wa Kuandaa Mipango, Bajeti na Utoaji wa Taarifa (PlanRep); Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani katika Mamlaka za Serikali za

Mitaa (LGRCIS); Mfumo wa Usimamizi wa Fedha na Utoaji wa Taarifa za Kihasibu (FFARS); Mfumo wa Usimamizi na Uendeshaji wa Vituo vya Kutolea Huduma za Afya (GoTHOMIS) na Mfumo wa Takwimu za Elimumsingi (BEMIS). Aidha, Ofisi ya Rais - TAMISEMI inaendelea kukamilisha Mfumo wa Mikopo ya asilimia Kumi (10% LMIS) ambao utapunguza changamoto zilizopo.

105. ***Mheshimiwa Spika,*** mifumo mingine inayosimamiwa na Ofisi ya Rais-TAMISEMI ni Mfumo wa Maombi ya Ajira TAMISEMI; Mfumo wa Tovuti za Serikali (GWF); Kituo cha Kutoa Huduma kwa Wananachi (Call Centre), Mfumo Jumuishi wa Ufuatiliaji na Tathmini (iMES) na Mfuko wa Afya ya Jamii Uliyoboreshwa (iCHF). Matumizi ya mifumo hii imeiwezesha Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoa huduma kwa wakati na ufanisi.

106. ***Mheshimiwa Spika***, hadi Februari, 2022 mifumo imefanyiwa maboresho ili kuongeza ufanisi katika Mipango na Bajeti na ukusanyaji na usimamizi wa fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ni pamoja na Mfumo wa Kuandaa Mipango, Bajeti na Utoaji Wa Taarifa (PlanRep); na Mfumo wa Usimamizi wa Fedha na Utoaji wa Taarifa za Kihasibu (FFARS). Mifumo hii imeboreshwa ili kuwezesha Kata, Vijiji na Mitaa kupanga mipango na bajeti na kufanya matumizi.

107. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha Wizara na Idara za Serikali zinashirikiana na kupunguza wingi wa mifumo, Mfumo wa PlanRep unaboreshwa ili kuweza kuanza kutumika katika kupanga Mipango na Bajeti Tanzania Bara na Visiwani. Vilevile, mfumo huu unatumika katika Taasisi **236** zinazosimamiwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina.

**Ujenzi wa Majengo ya Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Wilaya na Tarafa**

108. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Ofisi za Wakuu wa Mikoa ziliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 31.72** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Ofisi za Wakuu wa Wilaya na Ofisi za Maafisa Tarafa. Hadi Februari, 2022 jumla ya **Shilingi bilioni 16.50** sawa na **asilimia 52.01** ya bajeti iliyoidhinishwa na utekelezaji wa miradi hiyo upo katika hatua mbalimbali.

**Ujenzi wa Nyumba za Viongozi katika Tawala za Mikoa**

109. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Ofisi za Wakuu wa Mikoa ziliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 21.65** kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi za Viongozi katika Mikoa na Wilaya. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 2.89** ziliidhinishwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa nyumba za Wakuu wa Mikoa **12** ya; Arusha, Dar es Salaam, Kagera, Iringa, Geita, Katavi, Manyara, Mtwara, Njombe, Rukwa, Ruvuma na Shinyanga. Aidha, **Shilingi bilioni 8.71** ni kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa nyumba za Wakuu wa Wilaya **39, Shilingi bilioni 10.05** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa nyumba **11** za Makatibu Tawala wa Mikoa, Makatibu Tawala Wasaidizi **11**, Makatibu Tawala wa Wilaya **26**, Ikulu Ndogo **sita (6)** na Maafisa Tarafa **19**.

110. ***Mheshimiwa Spika,*** kufikia Februari, 2022 jumla ya **Shilingi bilioni 9.13** zimetolewa sawa na **asilimia 42.17** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 4.20** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa nyumba za Wakuu wa Mikoa **12** na nyumba za Wakuu wa Wilaya **39.** Vilevile, **Shilingi bilioni 4.93** ni kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa nyumba **11** za Makatibu Tawala wa Mikoa, Makatibu Tawala Wasaidizi **11**, Makatibu Tawala wa Wilaya **26**, Ikulu Ndogo **sita (6)** na Maafisa Tarafa **19**.

**Ujenzi wa majengo ya Utawala katika Halmashauri**

111. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2021/22 jumla ya **Shilingi bilioni 85.22** ziliidhinishwa kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya utawala **90**. Hadi Februari, 2022 jumla ya **Shilingi bilioni 64.42** sawa na **asilimia 75.59** zimetolewa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi pamoja na ukamilishaji wa majengo ya utawala ambapo jumla ya majengo **12** yamefikia **asilimia 90** ya ujenzi, majengo **9** yamefikia asilimia **80** na mengine yapo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. (**Kiambatisho Na. 12)**

112. ***Mheshimiwa Spika,*** majengo hayo yapo katika hatua mbalimbali za ujenzi ambapo majengo sita **(6)** ya Halmashauri za Wilaya za Mkalama, Malinyi, Madaba, Itilima, Wanging'ombe na Chalinze yamekamilika na yanatumika, Majengo saba **(7)** ya Halmashauri za Wilaya za Songwe, Misungwi, Kakonko, Nsimbo,

Pangani, Chamwino na Mji Geita yanaendelea na ujenzi. Aidha, majengo nane **(8)** yapo katika hatua za ukamilishaji. Majengo **61** yapo katika hatua mbalimbali za ujenzi ikiwemo kuta, usimikaji wa nguzo na hatua za msingi.

113. ***Mheshimiwa Spika***, ujenzi wa majengo **12** ya utawala katika Halmashauri za Wilaya za Nzega, Kigoma, Kwimba, Ulanga, Kisarawe, Kilwa, Kongwa, Ukerewe pamoja na Manispaa za Moshi na Shinyanga haujaanza kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo Halmashauri kuchelewa kukubaliana eneo la ujenzi. Halmashauri zilizokuwa na changamoto hii ni Halmashauri za Wilaya za Kigoma, Nzega na Kisarawe. Aidha, kwa sasa makubaliano yamefikiwa na ujenzi upo katika hatua za awali za kusafisha eneo na kupima udongo.

**Ujenzi wa Nyumba za Viongozi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa**

114. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 jumla ya **Shilingi bilioni 10.60** ziliidhinishwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Wakurugenzi na Wakuu wa Idara. Hadi Februari, 2022 jumla ya **Shilingi bilioni 6.55** sawa na **asilimia 61.79** zimetolewa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa nyumba hizo **106** (***Rejea Kiambatisho Na. 12).***

115. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Ofisi ya Rais- TAMISEMI iliidhinishiwa **Shilingi bilioni 12.58** kwa ajili ya ununuzi wa magari **70** ya Wakurugenzi na Wakuu wa Idara wa Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini. Hadi Februari 2022 jumla ya **Shilingi milioni 801** zimepokelewa sawa na **asilimia 6.52** na taratibu za manunuzi zinaendelea. Aidha, kufuatia maelekezo ya Serikali magari mengine yaliyobaki utaratibu wa manunuzi unaendelea na magari hayo yatanunuliwa kwa pamoja.

116. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Ofisi ya Rais- TAMISEMI iliidhinishiwa **Shilingi bilioni 3.88** kwa ajili ya ununuzi wa magari **14** kwa ajili ya Viongozi wa Tawala za Mikoa. Hadi Februari, 2022 zimepokelewa **Shilingi milioni 900.00** kwa ajili ya ununuzi wa magari matatu **(3)** Ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma

na Makatibu Tawala wa Mikoa ya Mbeya na Pwani na taratibu za ununuzi wa magari hayo zinaendelea.

**Huduma za Kiuchumi na Uzalishaji**

117. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Wadau mbalimbali imeendelea kuratibu huduma za ugani. Hadi Februari 2022, jumla ya mashamba darasa **116** yameandaliwa katika Mikoa ya Katavi, Dar es salaam, Mwanza, Simiyu, Tabora, Rukwa, Iringa, Morogoro, Arusha, Geita na Songwe ili kutoa elimu kwa vitendo kwa wakulima kuhusu mbinu bora za kilimo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

118. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kushirikiana na Taasisi ya AGRA imekamilisha kuandaa Mipango ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa **37** kwenye Mikoa **12** ikiainisha maeneo ya kipaumbele kwenye sekta za kilimo-mazao, mifugo na uvuvi. Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Wizara za Kisekta na Washirika wengine wa Maendeleo katika kuhakikisha kuwa rasilimali fedha zinapatikana ili kuwezesha utekelezaji wa afua hizo.

**Maliasili na Mazingira**

119. ***Mheshimiwa Spika*,** Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera na mikakati mbalimbali ya kuhifadhi maliasili na usimamizi wa mazingira katika ngazi ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali. Hadi Februari, 2022 Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeratibu na kusimamia shughuli za upandaji miti ambapo jumla ya miti **milioni 127.5** imepandwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

120. ***Mheshimiwa Spika*,** sambamba na jitihada za upandaji miti, wananchi wamekuwa wakihimizwa kutunza misitu ya asili kwa ajili ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na uuzaji wa hewa ukaa. Biashara ya hewa ukaa imeanza katika Mkoa wa Katavi katika Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika. Hadi Februari, 2022 jumla ya **tani 403,500** zimeuzwa kwa **Shilingi bilioni**

**2.30** ambapo jumla ya wananchi **21,000** katika vijiji nane (**8**) kutoka katika Halmashauri Wilaya ya Tanganyika wamenufaika na biashara ya hewa ukaa.

121. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mitaji ya Maendeleo (United Nation Capital Development Fund-UNCDF) imewajengea uwezo wananchi kuhusu kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Hadi Februari, 2022 jumla ya **Shilingi milioni 413.88** zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa kusaidia jamii kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika Halmashauri za Wilaya ya Chamwino, Kondoa na Mpwapwa katika Mkoa wa Dodoma.

122. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuzisimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuhakikisha zinatenga maeneo kwa ajili ya shughuli mbalimbali za uzalishaji. Hadi Februari, 2022 jumla ya hekta **7,186,312.44** zimetengwa kwa ajili ya shughuli mbalimbali ikiwemo hekta **175,951.19** kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda, **hekta 3,003,352.03** kwa ajili ya malisho ya mifugo, hekta **261,897.30** kwa ajili ya machimbo ya madini, hekta **29,644.79** kwa ajili ya biashara za aina mbalimbali na hekta **3,715,467.13** kwa ajili ya kilimo.

123. ***Mheshimiwa Spika****,* Serikali imekuwa ikifanya kazi na Asasi za Kiraia katika kuboresha huduma kwa jamii ambapo hadi Februari, 2022, Ofisi ya Rais TAMISEMI imeratibu AZAKI **265** kwa kutoa vibali ili zikatekeleze majukumu yake kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwenye Mikoa mbalimbali nchini.

124. ***Mheshimiwa Spika****,* Ofisi ya Rais - TAMISEMI imefanya ufuatiliaji wa shughuli za Wadau hao katika Mikoa ya Mara, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Dodoma, Morogoro, Mwanza, Kagera, Tabora, Tanga, Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe, Rukwa na Katavi. Miradi iliyotembelewa ni ya Kilimo, Ufugaji, Ujasiliamali Utunzaji wa Mazingira, Maji na Usafi wa Mazingira. Ofisi ya Rais - TAMISEMI inazipongeza AZAKI zote kwa namna zinavyotoa ushirikiano katika uboreshaji wa huduma kwa jamii.

**Uendelezaji wa Miji na Vijiji**

125. ***Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea*** kushirikiana na Wizara za Kisekta katika kuandaa na kutekeleza mipango ya Uendelezaji wa Vijiji na Miji nchini. Hadi Februari, 2022. Mipango kabambe imekamilika na kusajiliwa kwa Majiji **5** ya Arusha, Mwanza, Dodoma, Tanga na Mbeya; Manispaa **14** za Ilemela, Kigoma – Ujiji, Mtwara – Mikindani, Lindi, Songea, Iringa, Morogoro, Singida, Tabora, Bukoba, Musoma, Mpanda, Sumbawanga na Shinyanga na Miji **6** ya Babati, Njombe, Geita, Korogwe, Kibaha na Bariadi. Aidha, Ofisi ya Rais TAMISEMI inaendelea kuandaa Mipango Kabambe kwa Halmashauri zilizobakia.

126. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeendelea kubainisha majina ya mitaa, njia na barabara, kusimamia ukusanyaji wa taarifa za nyumba, wakazi na makazi na uwekaji wa miundombinu kwenye majengo na barabara kwa kuwashirikisha wananchi wenyewe kwenye maeneo yao. Utekelezaji wa kazi hizo ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Anwani za Makazi ambao utatumika wakati wa zoezi la Sensa ya Watu na Makazi linalotarajiwa kufanyika Agosti, 2022.

**UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA TAASISI ZILIZO CHINI YA OFISI YA RAIS - TAMISEMI**

127. ***Mheshimiwa* Spika,** Ofisi ya Rais-TAMISEMI inasimamia Taasisi Saba **(7)** ambazo ni Chuo Cha Serikali za Mitaa (LGTI), Shirika la Elimu Kibaha (KEC), Shirika la Masoko ya Kariakoo (KMC), Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART), Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa (LGLB) na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC). Aidha, utekelezaji uliofanyika katika Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi Februari, 2022 kwa kila taasisi ni kama ifuatavyo: -

**Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA)**

128. ***Mheshimiwa Spika***, mtandao wa barabara chini ya TARURA una jumla ya kilomita **144,429.77** ambazo zimetangazwa

rasmi kwenye **Gazeti la Serikali Na. 463 la tarehe 25 Juni 2021**. Mtandao wa barabara unaosimamiwa na TARURA una jumla ya madaraja **3,191**, makalavati **69,317**, barabara za lami zenye urefu wa kilomita **2,473.55**, barabara za Changarawe zenye urefu wa kilomita **30,756.51** na barabara za udongo zenye urefu wa **kilomita 111,199.72**.

129. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2021/22 TARURA iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 900.45** kwa ajili ya ujenzi, matengenezo na ukarabati wa miundombinu ya barabara za Wilaya, kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 722.16** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 178.29** ni fedha za nje. Fedha za ndani **Shilingi bilioni 722.16** zinajumuisha **Shilingi bilioni 272.50** kutokana na fedha za Mfuko wa Barabara, **Shilingi bilioni 322.16** kutokana na tozo ya mafuta ya **Shilingi 100** kwa kila lita ya mafuta ya petroli/diseli na **Shilingi bilioni 127.50** kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali.

130. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, TARURA ilipanga kujenga barabara za lami zenye urefu wa kilomita **232.94**, changarawe **kilomita 13,727.76**, madaraja **736**, na utunzaji wa barabara kilomita **22,202.84**. Hadi Februari 2022, **Shilingi bilioni 461.75** zimepokelewa na kukamilisha ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilomita **129.02**, changarawe kilomita **1,198.78**, madaraja **181**, na matengenezo ya barabara kilomita **19,257.76**.

**Ujenzi wa Barabara katika Mji wa Serikali Mtumba**

131. ***Mheshimiwa Spika***, TARURA inaendelea na ujenzi wa barabara kilomita **51.2** kwa kiwango cha lami katika Mji wa Serikali Mtumba, mradi huo ulianza kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2019/20 kwa gharama ya **Shilingi bilioni 89.13**. Mradi umekamilika kwa **asilimia 90** na hadi Februari 2022, malipo ya **Shilingi bilioni 76.16** yamefanyika. Kazi zilizokamilika ni pamoja na Ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilomita **51.2**, taa za barabarani **196** na ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua kilomita **62.8**. Aidha, Wakala unaendelea na ukamilishaji wa kazi ndogo ndogo zilizobakia.

**Mradi wa Uboreshaji Miundombinu katika Jiji la Dar es Salaam (DMDP)**

132. ***Mheshimiwa Spika***, katika mradi wa DMDP Serikali imetoa jumla ya **Shilingi bilioni 83.11** kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita **16** kwa kiwango cha lami na ujenzi wa mifereji ya Maji ya mvua kilomita **17.9** katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, Temeke na Jiji la Dar es Salaam; Ununuzi wa magari **20** ya kusomba taka ngumu pamoja na vyombo **65** vya kukusanyia taka (skip bucket). Hadi Februari, 2022, ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kilomita **5.39**, mifereji ya maji ya mvua kilomita **4.75** imekamilika pamoja na soko la Mtoni Kijichi katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke.

**Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka, Dar es Salaam**

133. ***Mheshimiwa Spika***, hadi Februari, 2022 Wakala umefanya mapitio ya mtandao wa usafiri kwa kuongeza barabara za Kimara hadi Kibamba kilomita **13.7** na Mbagala Rangi Tatu hadi Vikindu kilomita **4.5** ambazo zimejumuishwa kwenye awamu ya sita ya mradi na hivyo kuwa na mtandao wa barabara zenye jumla ya urefu wa kilomita **154.4**.

134. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na mtandao huo wa barabara, jumla ya vituo vikuu vipatavyo **24** vitahitajika. Aidha, mpango huu mpya umeainisha maeneo **14** kwa ajili ya kujenga karakana zitakazohitaji kuhudumia awamu zote sita **(6)** za mradi. Tayari maeneo yote haya yameainishwa na kuingizwa kwenye mpango wa utwaaji wa maeneo ya mradi.

135. ***Mheshimiwa Spika***, Wakala umefanya Tathmini ya mahitaji ya usafiri wa umma katika Mkoa wa Dar es Salaam ambayo imeonesha kuongezeka kwa mahitaji ya usafiri wa umma ambapo hadi mwaka 2025 kutakuwepo na watumiaji wa usafiri wa umma **2,590,000** kwa siku ambapo kutahitajika jumla ya mabasi **1,975**. Kati ya mabasi hayo, mabasi **695** ni yenye urefu wa mita **18** na mabasi **1,280** ni yenye urefu wa mita **12**.

136. ***Mheshimiwa Spika***, Mradi wa DART awamu ya pili unatekelezwa kupitia ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa kiasi cha **Dola za Kimarekani milioni 141.71**. Serikali imelipa fidia ya **Shilingi bilioni 30.25** kwa wananchi **92** ambao maeneo yao yaliathiriwa na utekelezaji wa mradi huu. Aidha, kwa kazi za barabara zimepangwa kutekelezwa kwa muda wa miaka mitatu **(3)** kwa gharama ya **Shilingi bilioni 217.48**. Ujenzi ulianza rasmi mwezi Mei, 2019 na umefikia **asilimia 48** ambapo unatarajia kukamilika ifikapo Machi, 2023.

137. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Wakala umeendelea na Awamu ya Pili ya ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka katika Mkoa wa Dar es Salaam ambapo miradi inayohusika ni ujenzi kuanzia Mjini Kati hadi Mbagala Rangitatu na kutoka Mgulani hadi Magomeni kupitia Chang'ombe na Kawawa barabara yenye urefu wa **kilomita 20.3**. Kazi nyingine zinazoendelea kutekelezwa katika awamu hii ni ujenzi wa vituo **28** vya mabasi, karakana moja **(1)** na madaraja ya juu mawili katika barabara za Kilwa na Mandela na makutano ya barabara ya Chang'ombe na Nyerere, vituo mlisho vinne (**4**), vituo vikuu viwili (**2**) katika eneo la Mbagala Rangitatu na Gerezani Kariakoo na daraja moja **(1)** katika eneo la BP.

138. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango na Wakala wa Serikali Mtandao unatengeneza mfumo wa kielektroniki wa kukusanya nauli. Kazi hiyo inaendelea na mfumo umeanza kufanya kazi ambapo mpaka sasa vituo ishirini **(20)** vya DART vinatumia mfumo mpya vikiwemo vituo vikuu vyote, na vingine vitakamilisha kuwekewa mfumo huo mwezi Juni 2022, baada ya kukamilisha ununuzi wa vifaa.

**Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC)**

139. ***Mheshimiwa Spika***, Dhima ya Tume ya Utumishi wa Walimu ni kuhakikisha walimu wa Shule za Msingi na Sekondari Tanzania bara wanapata huduma bora kuhusu masuala ya ajira, kupandishwa vyeo na kukuza maadili katika Utumishi wa walimu. Katika kutekeleza Dhima hiyo, walimu **6,949** kati yao walimu **3,949** wa Shule za Msingi na walimu **3,000** wa Shule za Sekondari

walioajiriwa mwezi Juni, 2021 walisajiliwa na kupewa namba za TSC, Walimu **591** walipewa vibali vya kustaafu, mikutano **223** ya Kisheria imefanyika kati ya mikutano **278** iliyopangwa kufanyika kwa mwaka.

140. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mikutano hiyo ya kisheria iliyofanyika, Walimu **1,872** walipandishwa vyeo ambapo walimu **914** wa shule za msingi na **958** wa shule za sekondari; walimu **222** walithibitishwa kazini na walimu **460** walibadilishiwa vyeo. Vilevile, mashauri ya kinidhamu ya walimu **642** kati ya **793** yalihitimishwa, na mashauri ya walimu **151** yapo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Aidha, hadi Februari, 2022 rufaa za walimu **147** kati ya rufaa **152** zilitolewa uamuzi na Tume. Pia, malalamiko ya walimu **405** kuhusu upandishwaji vyeo, ubadilishwaji vyeo na mashauri ya kinidhamu yalipokelewa na kushughulikiwa.

141. ***Mheshimiwa Spika***, Tume ya Utumishi wa Walimu imeanza kutekeleza ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu katika eneo la Njedengwa, Dodoma utakaogharimu **Shilingi bilioni 3.86** hadi kukamilika. Katika Mwaka wa Fedha 2021/22 jumla ya **Shilingi milioni 500** ziliidhinishwa. Hadi Februari 2022, **Shilingi milioni 500** zimepokelewa sawa na **asilimia 100** ya fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka husika ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 386** zimetumika kumlipa Mkandarasi SUMA – JKT ikiwa ni malipo ya awali na kazi imeanza.

142. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Utumishi wa Walimu katika kutekeleza majukumu yake imekuwa ikikabiliana na changamoto mbalimbali za walimu ikiwemo: upungufu wa walimu **100,958** wa shule za msingi na walimu **74,743** wa shule za sekondari hususan masomo ya sayansi; malalamiko ya walimu ikiwemo kutopandishwa vyeo kwa wakati; na wastaafu kucheleweshewa kulipwa stahili na mafao yao baada ya kustaafu.

143. ***Mheshimiwa Spika***, Tume ilipandisha vyeo walimu **126,346** na Serikali inaendelea kushughulikia walimu **23,457** ambao wamechelewa kupandishwa vyeo kutokana na sababu mbalimbali.

144. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kushughulika kero za wastaafu, Tume ya Utumishi wa Walimu imeanzisha dawati maalumu la kupokea malalamiko na kero za wastaafu. Aidha, Tume inaendelea na ujenzi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Masuala ya Walimu (*Teachers Service Commission Management Information System -TSC-MIS)* ambao utasaidia kurahisisha utoaji wa huduma kwa walimu.

145. ***Mheshimiwa Spika***, Tume ya Utumishi wa Walimu imesaidia kupunguza kero na malalamiko ya walimu nchini ambapo tathmini iliyofanywa imeonesha kwamba **asilimia 69** ya wadau hasa walimu wanaridhishwa na huduma zinatolewa na Tume ya Utumishi wa Walimu. Aidha, ajira za walimu zimepanda kutoka **10,629** mwaka wa fedha 2018/19 hadi kufika **14,949** mwaka wa fedha 2020/21 sawa na **asilimia 40.66**. Vilevile, Kamati za Wilaya **139** za Tume ya Utumishi wa Walimu zimejengewa uwezo ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi katika mwaka 2021/22.

**Shirika la Elimu Kibaha**

146. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Shirika la Elimu Kibaha limeendelea kuwa mstari wa mbele katika kutimiza malengo ya kuanzishwa kwake ambayo ni kupambana na maadui watatu wa maendeleo yaani **Maradhi**, **Ujinga** na **Umaskini**. Hadi Februari, 2022, Elimu ya Kinga na tiba kupitia Hospitali Teule ya Rufaa ya Mkoa Pwani (Tumbi) ilitolewa kwa wagonjwa wa nje **60,867** sawa na wastani wa wagonjwa **338** kwa siku ambao ni **asilimia 68** ya malengo, kati ya idadi hiyo, wazazi wa watoto chini ya umri wa miaka mitano walikuwa **10,064**.

147. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeendelea kusimamia utoaji wa huduma za afya ambapo hadi Februari, 2022 wagonjwa **4,264** walilazwa ikiwa ni pamoja na watoto chini ya umri wa miaka mitano **491** na watoto wachanga **641**. Vilevile, huduma kwa wazazi waliojifungua kawaida walikuwa **452**, waliojifungua kwa njia ya upasuaji walikuwa **582** na wazazi **3** walipoteza maisha wakati wa kujifungua kutokana na kupoteza damu nyingi.

148. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali pia imeendelea kutoa huduma kwa waraibu wa madawa ya kulevya ambapo kuanzia Julai 2021 hadi Februari, 2022 waraibu **273** wamesajiliwa na wanaendelea na tiba. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya majeruhi **810** wa ajali za barabarani walihudumiwa.

149. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Shirika limeendelea kutoa Elimu ya utabibu na uuguzi kupitia Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Kibaha kwa wanachuo **514.** Aidha, huduma nyingine zinazotolewa katika Hospitali Teule ya Tumbi ni mafunzo tarajari ambapo madaktari **79**, wauguzi **20** na wafamasia **10** wanaendelea na mafunzo.

150. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali Teule ya Tumbi ni miongoni mwa Hospitali za Rufaa za Mikoa, ambazo zimehamishiwa Wizara ya Afya kutokana na agizo la aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Awamu ya Tano alilolitoa tarehe 25 Novemba, 2017 ili kuimarisha utendaji na utoaji wa huduma bora za Afya kwa wananchi.

151. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Shirika limeendelea kutoa Elimu kwa wanafunzi **3,013** wakiwemo wanafunzi **825** wa Shule ya Sekondari Kibaha, **819** Shule ya Sekondari Tumbi, **339** Shule ya Sekondari ya Wasichana Kibaha, **890** Shule ya Msingi Tumbi pamoja na watoto **140** wa elimu ya awali. Kwa mwaka wa masomo 2021 kuna ongezeko la wanafunzi **111** ikilinganishwa na wanafunzi wa mwaka wa masomo 2020 ambao walikuwa **2,902**. Ongezeko hili limetokana na ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Kibaha na Shule ya Sekondari Tumbi ambapo vimejengwa vyumba viwili vya madarasa kwa kila shule.

152. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Shirika limeendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi ya nadharia na vitendo kupitia Chuo cha Maendeleo ya Wananchi kwa wanachuo **330** ambao wamesajiliwa (Wanaume **210** na Wanawake **120**). Mafunzo yaliyotolewa ni Kilimo, Mifugo, Ujenzi, Ushonaji, Upishi, Ufundi wa Magari, Uundaji na Uungaji vyuma na Umeme wa majumbani. Katika mwaka wa masomo 2021/22, kuna ongezeko la wanachuo **38** ikilinganishwa na Mwaka wa Masomo

2020/21 ambapo walikuwa Wanachuo **292** kutokana na kuongeza wigo wa kukitangaza Chuo.

153. ***Mheshimiwa Spika***, mafunzo mengine yaliyotolewa ni mafunzo ya muda mfupi kwa wahitaji **476** yakijumuisha udereva kwa wahitaji **68** ambapo wanaume ni **55** na wanawake **13**, wanajamii **408** ambapo Wanaume ni **101** na wanawake **307** ambao walijengewa uwezo kupitia mafunzo ya Ujasiriamali, Elimu ya kifedha-Mikopo na Kilimo cha Bustani kwa njia ya matone. Mwaka 2020/21 walikuwa wanufaika **267** ambapo kwa Mwaka 2021/22 kuna wanufaika **476** sawa na ongezeko la wanufaika **209** kutokana na kuanza kutoa mafunzo kwa wanufaika wa mikopo inayotolewa na Halmashauri kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.

**Chuo Cha Serikali za Mitaa**

154. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Chuo cha Serikali za Mitaa kimeendelea kutekeleza kazi na majukumu yake yakiwemo mafunzo, utafiti na ushauri. Katika mwaka wa masomo 2021/22 Chuo kimedahili jumla ya wanafunzi **5,166** ambapo kati yao wanafunzi wa Astashada ya awali (*National Technical Award* 4) ni **1,930**, Astashahada ya kati (*National Technical Award* 5) ni **1,925,** Stashahada (*National Technical Award* 6) **1,997** na Shahada (*National Technical Award* 7-8) **214**. Aidha, Chuo kimeendesha mafunzo katika programu kuanzia ngazi ya Astashahada mpaka Shahada ya kwanza. Programu hizo ni Utawala na Uongozi katika Serikali za Mitaa; Menejimenti ya Rasilimali watu, Maendeleo ya Jamii; Uhasibu na Fedha katika Serikali za Mitaa; Nyaraka na Utunzaji wa Kumbukumbu na Ununuzi na Ugavi.

155. ***Mheshimiwa Spika***, Chuo kimeendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi ya kujenga uwezo kwa Halmashauri mbalimbali nchini. Hadi Februari, 2022 Chuo kimetoa mafunzo ya kuwajengea uwezo jumla ya Waheshimiwa Madiwani **482** wa Halmashauri **14** za Tanzania Bara zikijumuisha Halmashauri za Wilaya ya Bahi (**27**); Same (**54**); Meru (**36**); Karatu (**27**); Hai (**27**); Mbinga (**27**); Ushetu (**27**) na Buhigwe (**27**). Pia, mafunzo hayo yalijumuisha Halmashauri ya Mji Mbinga (**25**); Manispaa za Songea (**27**), Kinondoni (**61**) na Ilemela

(**27**). Vilevile, mafunzo hayo yalijumuisha Halmashauri za Majiji ya Dar es Salaam (**54**) na Arusha (**36**). Nitumie fursa hii, kuwaelekeza Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini kutumia Chuo hiki katika kuwajengea uwezo Waheshimiwa Madiwani, Watendaji na Viongozi wengine katika Halmashauri zao.

156. ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo kimeendesha mafunzo ya Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo Ulioboreshwa (*Improved Oppotunities & Obstacles to Development – O&OD*) kwa Halmashauri **184** nchini na mafunzo kwa Wenyeviti wa Mitaa **11** wa Manispaa ya Kinondoni kwa lengo la kuimarisha uwezo wa kutekeleza majukumu yao. Nitumie fursa hii tena, kuwaelekeza Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini kutumia Chuo hiki katika kuwajengea uwezo Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji katika Halmashauri zao.

157. ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo kimetoa mafunzo kwa viongozi na watendaji wa Halmashauri mbalimbali kwa kutumia Mfumo wa Ujifunzaji Kielektroniki (MUKI). Washiriki wa mafunzo hayo ni pamoja na Waheshimiwa Madiwani **757**, watumishi wapya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa **1,103**, Watendaji wa Kata **8** na wasimamizi wa vituo vya kutolea huduma za Afya **25**. Naendelea kuelekeza Wakurugenzi wa Halmashauri kuhakikisha wanatumia Mfumo huo kuwajengea uwezo viongozi na watendaji wa Halmashauri katika ngazi zote.

158. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 chuo cha Serikali za Mitaa kimetekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, ikiwemo ujenzi na ukamilishaji wa madarasa pacha ya wanafunzi **500** kwa gharama ya **Shilingi milioni 500** na ukarabati wa majengo ya chuo uliogharimu **Shilingi milioni 550** kwa kutumia fedha ya Mapato ya Ndani.

**Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa**

159. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa imetoa mikopo ya **Shilingi milioni 300** kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe kwa ajili ya ujenzi wa vibanda vya biashara vinavyozunguka Kituo cha Mabasi katika Makao Makuu ya Halmashauri. Hadi Februari 2022,

Bodi imeratibu urejeshwaji wa mikopo jumla ya **Shilingi milioni 147.00** kutoka katika Halmashauri. Vilevile, Bodi imeendelea kukusanya michango ya akiba na nyongeza ya mtaji ambapo kiasi cha **Shilingi milioni 83.50** kimekusanywa kuanzia Julai 2021 hadi Februari 2022. Nachukua fursa hii kuziagiza Halmashauri zote zilizokopa kurejesha Mikopo yake kama ilivyo kwenye Mikataba yao na kuchangia Michango yao ya Akiba kwa Mujibu wa Sheria.

**Shirika la Masoko ya Kariakoo**

160. ***Mheshimiwa Spika*****,** Shirika la Masoko Kariakoo lilianzishwa kwa Sheria ya Bunge **Na. 36** ya Mwaka 1974 kwa lengo la kusimamia na kuendesha masoko ya mazao ya chakula, zana za kilimo na pembejeo za kilimo katika Mkoa wa Dar es salaam. Tarehe 07 Julai, 2021 kulitokea ajali ya moto katika jengo kuu la Shirika la Masoko ya Kariakoo. Moto huo uliteketeza bidhaa zote za wafanyabiashara **224** ambapo kati yao **120** walikuwa wanaendesha biashara zao katika ghorofa ya chini, wafanyabiashara **100** katika ghorofa ya kwanza na wafanyabiashara wanne (**4**) maeneo ya matangazo. Naomba kutumia fursa hii kutoa pole kwa wafanyabiashara wote waliopoteza mali zao katika janga hilo la moto. Aidha, ajali hiyo iliteketeza mali zote za Shirika ambazo ni Ofisi **31,** samani, vifaa na nyaraka zote za kumbukumbu.

161. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mujibu wa tathmini iliyofanywa na Kampuni ya Ushauri ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (BICO) imebaini kuwa Jengo halikuathirika kiasi cha kutoweza kukarabatiwa. Katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Serikali imetenga **Shilingi bilioni 26.28** kwa ajili ya ukarabati wa jego lililoungua na ujenzi wa soko jipya. Hadi Februari, 2022 ukarabati wa soko lililoungua umefikia **asilimia 40** na ujenzi wa soko jipya umefikia **asilimia 15.** Aidha, fedha zilizotolewa na kulipwa kwa Mkandarasi ESTIM CONSTRUCTION ikiwa ni malipo ya awali ni **Shilingi bilioni 3.94** na mradi unategemewa kukamilika mwezi Oktoba, 2023. Baada ya mradi kukamilika jumla ya wafanyabiashara **2,313** wataweza kupata nafasi za biashara ikilinganishwa na wafanyabiashara **1,598** waliokuwepo kabla ya soko kuungua ikiwa ni ongezeko la wafanya biashara **715.**

162. ***Mheshimiwa Spika***, natoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ***Mheshimwa Samia Suluhu Hassan***, kwa kusikia kilio cha wafanyabiashara wa Soko la Kariakoo waliokuwa wanafanya biashara mbalimbali katika soko hilo ambalo linahudumia wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, Mikoa mingine na wafanyabiashara kutoka nchi za jirani kwa kutoa fedha za ujenzi wa soko jipya na kukarabati soko lililoungua.

## C. MPANGO NA BAJETI YA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23 KWA OFISI YA RAIS - TAMISEMI (FUNGU 56), TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (FUNGU NA. 2) NA MAFUNGU 26 YA MIKOA IKIJUMUISHA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA 184

163. ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/23 umeandaliwa kwa kuzingatia Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020, Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Awamu ya Sita, ***Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan***, aliyoitoa katika Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/23, maelekezo ya Viongozi wengine wa Kitaifa, Sera za Kisekta, Miongozo ya Serikali na Mipango Mikakati iliyohuishwa ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI Fungu 56, Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu Na. 2 na Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa Mafungu 26 kwa kipindi cha 2021/22-2025/26.

164. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imepanga kutekeleza Mipango na Bajeti kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo: -

i) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa Elimumsingi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ikijumuisha utekelezaji wa Elimumsingi Bila Malipo;

ii) Kuratibu na kusimamia Mkakati wa kuongeza ukusanyaji wa mapato na kudhibiti matumizi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

iii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa Huduma za Afya ya Msingi, Lishe na Ustawi wa Jamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

iv) Kushughulikia malalamiko ya walimu ikiwemo kutopandishwa vyeo kwa wakati; na wastaafu kucheleweshewa kulipwa stahili na mafao yao baada ya kustaafu ambapo Tume ya Utumishi wa Walimu imeanzisha dawati maalumu la kupokea malalamiko na kero za wastaafu;

v) Kuchochea na kuhimiza ukuaji wa uchumi shindani kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla kwa kuiwezesha Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji, hasa katika Kilimo, Mifugo na Viwanda. Utekelezaji wa jambo hili utahusisha uimarishaji wa sehemu ya uchumi na uzalishaji katika ngazi ya Mikoa kwa kuhakikisha kuna rasilimali watu wenye weledi pamoja uwepo wa fedha na vitendea kazi. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa maafisa ugani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Wizara za kisekta ili kuboresha mazingira ya kilimo, mifugo, uwekezaji, viwanda na biashara;

vi) Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI ikiwa ni pamoja na kufanya Ukaguzi, Ufuatiliaji na Tathmini kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali, Taasisi, Programu na miradi katika ngazi ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

vii) Kusimamia matumizi ya TEHAMA katika ngazi zote za Ofisi ya Rais -TAMISEMI.

viii) Kuendeleza rasilimaliwatu katika ngazi zote za Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa kuwaongezea ujuzi kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utendaji kazi;

ix) Kuratibu shughuli za utendaji kazi kwa Taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI;

x) Kuratibu ujenzi, ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya maeneo ya utawala ya Mikoa, Wilaya, na Halmashauri;

xi) Kusimamia matumizi ya rasilimali fedha katika ngazi zote za Ofisi ya Rais-TAMISEMI;

xii) Kuratibu shughuli za kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na

xiii) Kusimamia shughuli za utawala bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na Ugatuaji wa Madaraka kwa Umma (D by D).

**MALENGO YA TAASISI ZILIZO CHINI YA OFISI YA RAIS-TAMSEMI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23**

**Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA)**

165. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) umeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya ujenzi, matengenezo na ukarabati wa barabara za Wilaya. Katika Mwaka wa Fedha 2019/20 **Shilingi bilioni 251.73** ziliidhinishwa, 2020/21 **Shilingi bilioni 275.03** ziliidhinishwa na Mwaka wa Fedha 2021/22 **Shilingi bilioni 722.16** ziliidhinishwa.

166. ***Mheshimiwa Spika,*** kumekuwa na ongezeko katika bajeti ya TARURA kwa **Shilingi bilioni 447.13** sawa na **asilimia 162.59** kati ya Mwaka wa Fedha 2020/21 na 2021/22 kutokana na Serikali kuongeza vyanzo vya fedha vya tozo ya **Shilingi 100** kwa kila lita ya mafuta ya petroli/dizeli na fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali ambavyo havikuwepo hapo awali.

167. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wakala umetengewa **Shilingi bilioni 802.29** kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za ujenzi, ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya barabara. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/23, Wakala unatarajia kujenga barabara za lami **Kilomita 411.80,** barabara za changarawe **kilomita 10,666.11,** matengenezo ya barabara **kilomita 24,015.77** madaraja na vivuko **322** pamoja na matengenezo ya miundombinu ya barabara zenye urefu wa **mita 12,542.50.**

168. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wakala umetengewa **Shilingi bilioni 257.04** kutoka Mfuko wa Barabara kutekeleza kazi za matengenezo ya barabara **kilomita 24,015.77,** ujenzi wa barabara za lami **kilomita 40.78,** ujenzi wa barabara za changarawe **kilomita 2,532.51** na madaraja **28.**

169. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wakala umetengewa **Shilingi bilioni 325.77** kutokana na tozo ya mafuta kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za ujenzi wa barabara za lami **kilomita 157.49,** changarawe **kilomita 5,735.42**, madaraja **218** na mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa **mita 4,093.5.**

170. ***Mheshimiwa Spika****,* katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wakala umetengewa **Shilingi bilioni 127.50** kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za ujenzi wa barabara za lami **kilomita 94.33,** changarawe **kilomita 2,326.93**, madaraja **75** na mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa **mita 8,449**.

**Miradi Inayotekelezwa kupitia Benki ya Dunia na Jumuiya ya Nchi za Ulaya**

171. ***Mheshimiwa Spika****,* katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wakala umetengewa **Shilingi bilioni 9.68** kutoka Benki ya Dunia kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu Dar es Salaam (DMDP) kwa ajili ya kuendelea kukamilisha ujenzi wa kilomita **3** za lami, mifereji ya maji ya mvua na gharama za maandalizi ya miradi mipya ya *Tanzania Cities Transforming Infrastructure competitiveness* (TACTIC) na Bonde la Msimbazi.

172. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka wa fedha 2022/23, TARURA umetengewa **Shilingi bilioni 6.00** kutoka Benki ya Dunia kupitia Mradi wa Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji Jamii na Ufunguaji Fursa za Kijamii na Kiuchumi Vijijini (Roads to Inclusion and Social Economic Opportunities – RISE). Mradi huu utatekelezwa kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2022/23 utahusisha ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami urefu wa kilomita **530** katika kipindi kizima cha mradi. Mradi pia utahuisha matengenezo ya maeneo korofi katika Halmashauri zote nchini na matengenezo ya kawaida ya barabara kwa kutumia vikundi vya jamii inayoishi kandokando ya barabara husika. Katika mwaka wa fedha 2022/23 kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa barabara za Wenda – Mgama kilomita **19** na Mtili – Ifwagi kilomita **14** katika Halmashauri za Wilaya za Iringa na Mufindi mtawalia;

173. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wakala umetengewa bajeti ya **Shilingi bilioni 16.08** kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya uboreshaji wa Bonde la Mto Msimbazi. Mradi huu utahusisha ujenzi wa daraja jipya la Jangwani, kupanua, kuongeza kina na kuimarisha kingo za mto Msimbazi.

174. ***Mheshimiwa Spika,*** TARURA imetengewa **Shilingi bilioni 16.80** kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi wa uboreshaji wa Miundombinu katika Halmashauri **45** za Majiji, Manispaa na Miji kupitia mradi wa *Tanzania Cities Transforming Infrastructure and Competitivenes -TACTIC*. Mradi huu utatekelezwa katika Madaraja Matatu (*Three Tiers – Tier 1, Tier 2 na Tier 3*). Mradi huu ni mwendelezo wa Mradi wa Uendelezaji Miji ya Kimkakati nane (**8)** (Tanzania Strategic Cities Project – TSCP), Mradi wa Uimarishaji Miji **18** (Urban Local Government Strengthening Project-ULGSP) ambayo utekelezaji wake umefikia kikomo na pia utajumuisha Miji mingine **19** ambayo haikuwepo kwenye awamu zilizopita. Aidha, **Shilingi bilioni 30.45** zimetengwa kutoka Mapato ya Ndani ya TARURA kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kilomita **3.2**, ujenzi wa barabara kwa kiwango cha changarawe kilomita **71.25**, ujenzi wa daraja **moja**, ukamilishaji wa mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani ya TARURA pamoja na utelekezaji wa ahadi za Viongozi;

175. ***Mheshimiwa Spika,*** fedha hizi zitaelekezwa kwenye uboreshaji wa miundombinu ya barabara kwenye maeneo ya Vijijini na Mijini kwa lengo la kuimarisha huduma za kiuchumi (uzalishaji) na kijamii (huduma za afya na elimu) kwa wananchi. Naomba kutumia fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa namna wanavyojitoa katika kusimamia shughuli za ujenzi, ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya barabara katika majimbo yao.

176. ***Mheshimiwa Spika,*** utaratibu uliokuwepo awali wa kuwapata Makandarasi wa ujenzi, matengenezo na ukarabati wa miundombinu ya barabara mchakato wa manunuzi ulikuwa unaanza mwezi Julai, mara baada ya Bajeti ya Serikali kuidhinishwa mwezi Juni ambapo mchakato huo ulikuwa ukienda hadi mwezi Oktoba. Utaratibu huo ulisababisha Makandarasi kwa maeneo mengi kupatikana wakati wa kipindi cha mvua, hivyo kusababisha ucheleweshaji wa utekelezaji wa kazi hizo.

177. ***Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na changamoto ya ucheleweshwaji wa ujenzi, matengenezo na ukarabati wa miundombinu ya barabara, Wakala umeanzisha utaratibu wa kuanza mchakato wa ununuzi wa Kandarasi kuanzia mwezi Mei kila mwaka ili fedha zinapoidhinishwa na Bunge Mwezi Juni ya kila mwaka utekelezaji uanze mapema kuliko ilivyokuwa awali. Hii itasaidia kuwapata Makandarasi kwa wakati watakaoweza kutekeleza kazi za ujenzi, matengenezo na ukarabati wa miundombinu ya barabara itakayosaidia wananchi kuendelea kutekeleza shughuli zao za kiuchumi na kijamii.

**Tume ya Utumishi wa Walimu**

178. ***Mheshimiwa Spika***, Tume ya Utumishi wa Walimu imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa mujibu wa Sheria Sura 448, Kanuni za Mwaka, 2016, Taratibu na miongozo inayohusu kusimamia ajira, maadili na maendeleo ya walimu nchini.

179. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuiongezea Tume Bajeti ya matumizi mengineyo (OC) ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake. Kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 Tume ilitengewa

**Shilingi bilioni 4.62**, mwaka wa fedha 2019/20 **Shilingi bilioni 6.00**, Mwaka wa fedha 2020/21 **Shilingi bilioni 6.10** na mwaka wa fedha 2021/22 Tume ilitengewa **Shilingi bilioni 6.60**.

180. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa fedha 2022/23 Tume imetengewa **Shilingi bilioni 6.70** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake ya msingi. Aidha, Tume imetengewa **Shilingi milioni 670.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa ofisi ya Tume Makao Makuu na kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa Mfumo wa TSC- MIS. Vilevile, Tume itaendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa wafanyakazi kwa kuwaongezea ujuzi, kuwapatia Ofisi na vitendea kazi.

**Chuo cha Serikali za Mitaa**

181. ***Mheshimiwa Spika***, Chuo cha Serikali za Mitaa kimeendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu ambapo Waheshimiwa madiwani **2,688** na Watendaji wa Kata na Vijiji **3,547** wamepewa mafunzo juu ya uongozi, usimamizi na uendeshaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi. Naomba nichukue fursa hii kuwaelekeza Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha wanatenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuwajengea uwezo Waheshimiwa Madiwani na Watumishi wa kada mbalimbali ili kuboresha utendaji kazi wao ili Chuo hiki kitumike kwa malengo ya kuanzishwa kwake.

182. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Chuo kitaendelea na majukumu yake ya kutoa elimu, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalam. Katika kutekeleza jukumu la kutoa mafunzo ya muda mrefu Chuo kimepanga kudahili wanafunzi wapya **7,300** kwa ngazi mbalimbali na kuanza kufundisha Shahada ya Kwanza ya Menejimenti ya Rasilimali watu. Pia, Chuo kimepanga kuandaa mitaala ya Shahada ya Kwanza katika Nyaraka na Utunzaji Kumbukumbu na kuanza mchakato wa kuanzisha Shahada ya Uzamili ya Maendeleo ya Jamii, kuandaa Mtaala wa Mafunzo ya "*Local Economic Development*" na kuanza hatua za awali za uanzishaji wa Kampasi ya Tanzania Zanzibar.

183. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Chuo kimepanga kuanza ujenzi wa jengo la Utawala la chuo lenye ghorofa mbili litakalogharimu **Shilingi milioni 907.09** na ujenzi wa majengo ya Chuo cha Serikali za Mitaa Kampasi ya Dodoma Mjini kwa gharama ya **Shilingi milioni 255**. Ujenzi wa majengo hayo utagharamiwa kwa fedha za mapato ya ndani.

**Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka, Dar es Salaam**

184. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka, Dar es Salaam umeendelea kuboresha huduma za usafiri wa umma katika Mkoa wa Dar es Salaam, ambapo muda wa kusafiri umepungua kutoka masaa **matatu na nusu** hadi **dakika arobaini** kutoka Kimara kwenda Kivukoni ambao ndio umbali mrefu unaohudumiwa na mabasi ya mwendo kasi. Aidha, abiria **180,000** wanatumia usafiri huu kwa siku. Napenda kuchukua fursa hii kumshukuru **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamhuri wa Tanzania** kwa kutoa fedha kwa ajili ya kuongeza mtandao wa huduma ya usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka.

185. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka, Dar es Salaam utaendelea na uboreshaji wa huduma za usafiri katika Mkoa wa Dar es Salaam na maeneo ya jirani ikiwa ni pamoja na kuendelea na usimamizi wa utoaji wa huduma ya usafiri wa Haraka Mkoani Dar es Salaam awamu ya kwanza, kukamilisha taratibu za manunuzi ya Mtoa Huduma wa Mabasi **95** ya nyongeza kwenye awamu ya kwanza ya BRT; Kubadilisha mfumo wa uendeshaji na ulipaji wa watoa huduma kutoka kupokea tozo ya kupita katika mfumo wa DART na kuanza kutumia utaratibu wa malipo ya umbali ambao mabasi yatakuwa yanatembea.

186. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Serikali itaendelea kuongeza Mtandao wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka, Dar es Salaam (BRT) kwa kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya BRT Awamu ya Pili **(2)** yenye urefu wa **kilomita 20.6** unaojumuisha barabara za Kilwa (kutoka mzunguko wa Mtaa wa Bandari hadi Mbagala Rangi Tatu); Barabara ya Chang'ombe (kutoka mzunguko wa Mgulani JKT

katika barabara ya Kilwa hadi makutano ya Barabara ya Nyerere); Barabara ya Kawawa (kutoka makutano ya Barabara ya Nyerere hadi Magomeni); Mtaa wa Gerezani, Sokoine Drive (kutoka kwenye makutano ya mitaa ya Railway na Gerezani hadi Mtaa wa Zanaki, na Mtaa wa Bandari.

187. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Serikali itaanza ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Mkoani Dar es Salaam awamu ya tatu **(3**) yenye urefu wa **kilomita 24.3** itakayojumuisha barabara za Nyerere hadi Gongo la Mboto; barabara ya Mandela kutoka TAZARA hadi makutano ya barabara ya Uhuru na Mandela; barabara ya Uhuru kutoka Makutano ya Barabara ya Mandela hadi makutano ya Mtaa wa Shaurimoyo; Mtaa wa Shaurimoyo kutoka makutano ya Barabara ya Uhuru hadi Mtaa wa Lindi; Mtaa wa Lindi kutoka makutano ya Mtaa wa Shaurimoyo hadi Kituo Kikuu cha Gerezani – Kariakoo; Nkurumah kutoka makutano ya Barabara ya Nyerere hadi makutano ya Mtaa wa Bibi Titi; Mtaa wa Maktaba na Mtaa wa Azikiwe hadi makutano na Barabara ya Kivukoni.

188. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendelea kuboresha huduma ya usafiri katika mkoa wa Dar es Salaam, DART itaendelea kukamilisha usanifu ambapo awamu ya nne **(4)** itahusu barabara za Bibi Titi, Alli Hassan Mwinyi na Bagamoyo hadi Tegeta pamoja na barabara ya Sam Nujoma yenye urefu wa **kilomita 30.1**; awamu ya tano (5) itajumuisha barabara za Nelson Mandela kuanzia Ubungo hadi daraja la Mwalimu Nyerere – Kigamboni; Tabata na Kigogo kuanzia Tabata Segerea kupitia Tabata Dampo, Kigogo hadi barabara ya Kawawa zenye urefu wa **kilomita 27.6;** usanifu wa awamu ya sita itajumuisha barabara ya Mwai Kibaki hadi Kawe; nyongeza ya Barabara ya Morogoro kutoka Kimara hadi Kibamba na Barabara ya Kilwa kutoka Mbagala Rangi tatu hadi Vikindu yenye urefu wa **kilomita 26.5**.

**Shirika la Elimu Kibaha**

189. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Shirika la Elimu Kibaha litaendelea kutoa elimu ya uuguzi na utabibu katika Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Kibaha kwa kuongeza udahili kutoka wanachuo **500** kwa mwaka hadi **700**

kupitia kozi mpya mbili za Ufamasia na Maabara zinazotarajiwa kuanzishwa.

190. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Elimu Kibaha litaendelea kubuni na kuibua fursa mbambali za kuwawezesha wananchi hasa Vijana, Wanawake na Watu Wenye Ulemavu kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi kupitia Chuo cha Maendeleo ya Wananchi ikiwa ni pamoja na kilimo, ufundi, na biashara ili kuongeza thamani katika shughuli zao za kujikomboa na umasikini na kuongeza pato la taifa.

**Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa**

191. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa imetengewa **Shilingi bilioni 2.67** zikiwemo ruzuku kutoka Serikali Kuu **Shilingi milioni 61.95** na Mapato ya Ndani **Shilingi bilioni 2.61** ambazo zitatumika kutoa mikopo ya **Shilingi bilioni 2.38** kwa Halmashauri zitakazokidhi vigezo vya kukopeshwa, kusimamia na kuratibu urejeshwaji wa mikopo ya **Shilingi milioni 940.02** kutoka Halmashauri **9** zinazodaiwa deni hilo, kusimamia na kuratibu ukusanyaji wa michango ya akiba na nyongeza ya mtaji ambapo **Shilingi bilioni 1.44** zitakusanywa na **Shilingi milioni 233.40** zitakusanya kutoka vyanzo vingine vya mapato.

**Shirika la Masoko ya Kariakoo**

192. ***Mheshimiwa Spika***, Soko la Kariakoo lipo kwenye kitovu cha biashara katika Jiji la Dar es Salaam na linabeba historia ya biashara ya mji Mkuu wa biashara nchini. Uendeshaji wa Soko hili umekuwa na changamoto mbalimbali ikiwemo uchakavu wa majengo na miundombinu ya mifumo ya maji na umeme. Kutokana na changamoto hizo, Serikali imefanya mabadiliko makubwa ikiwa ni pamoja na kubadilisha Menejimenti ya Shirika, kujenga soko jipya badala ya soko la zamani ambalo miundo mbinu yake ilichakaa kwa kiasi kikubwa na kukarabati soko kuu lililoungua moto.

193. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umelenga kubadilisha kabisa mandhari ya soko la Kariakoo, kuongeza maeneo ya biashara, kuboresha mazingira ya kufanyia biashara, kuongeza idadi ya wafanyabiashara na wateja watakaohudumiwa na soko hili kutoka ndani na nje ya nchi wakiwemo watalii pamoja na kuongeza ajira zisizo za moja kwa moja zipatazo **4,626.** Faida nyingine itakayopatikana ni kuongeza mapato ya Shirika na Serikali kwa ujumla.

194. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Shirika la Masoko ya Kariakoo limetengewa **Shilingi bilioni 10.00** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam. Mradi huu una sehemu kuu mbili ambapo sehemu ya kwanza ni ukarabati wa soko lililoungua na sehemu ya pili ni ujenzi wa soko la ghorofa sita (**6**) za juu na ghorofa mbili (**2**) za chini katika eneo lilipokuwa soko dogo ambalo limebomolewa. Aidha, Shirika litaendelea kusimamia maeneo mengine ya Shirika yaliyopo Tabata Bima, Mbezi Beach Makonde na kuweka mikakati na mifumo thabiti ya uendeshaji wa biashara.

## D. MALENGO MAHSUSI YALIYOPANGWA KUTEKELEZWA NA OFISI YA RAIS – TAMISEMI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2022/23

195. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Ofisi ya Rais -TAMISEMI imepanga kutekeleza malengo mahsusi yafuatayo: -

### Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo

(i) Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo umeongezewa **Shilingi bilioni 4.99** kutoka **Shilingi bilioni 11.00** iliyokuwa katika bajeti ya kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 - 2021/22 hadi **Shilingi bilioni 15.99** kwa mwaka wa fedha 2022/23 sawa na ongezeko la **asilimia 45.36** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi;

### Mchango wa Bima ya Afya kwa Waheshimiwa Madiwani

(i) Serikali ilianza kulipa posho za Waheshimiwa Madiwani kwa mwaka wa fedha 2021/22 ambapo mchango wa bima ya afya haukujumuishwa kwenye posho hizo. Kwa Mwaka wa Fedha 2022/23, Serikali imetenga fedha ya kuchangia mchango wa mwajiri kwa ajili ya Waheshimiwa Madiwani **Shilingi milioni 607.57**;

**Kuimarisha Usalama na Usimamizi wa Shughuli za Serikali**

(i) Mikoa imeongezewa fedha za uendeshaji wa vikao vya Kamati za Usalama vya mikoa kutoka **Shilingi milioni 416.00** hadi **Shilingi milioni 780.00** sawa na ongezeko la **Shilingi milioni 364.00**;

(ii) Mikoa **12** inayopakana na nchi jirani imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 730.00** kwa ajili ya kuimarisha usalama mipakani;

(iii) Ofisi za Wakuu wa Wilaya zimeongezewa fedha za matumizi mengineyo kutoka **Shilingi bilioni 17.13** hadi **Shilingi bilioni 26.68** sawa na ongezeko la **Shilingi bilioni 9.55** ambalo ni ongezeko la **asilimia 55.75** kwa ajili ya kuwawezesha kusimamia usalama na utekelezaji wa shughuli za Serikali katika maeneo yao;

**Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA)**

(i) Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) imetengewa **Shilingi bilioni 802.29** kwa ajili ya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya barabara ambapo barabara za lami zenye urefu wa kilomita **411.80**, changarawe urefu wa kilomita **10,666.11,** ujenzi wa mifereji ya maji yenye urefu wa **mita 12,542.50,** matengenezo ya barabara **kilomita 24,015.77** na madaraja na vivuko **322** vitajengwa. Aidha, TARURA itaanza taratibu za ununuzi mwezi Mei, 2022 ya **asilimia 60** ya kazi zilizopangwa ili utekelezaji ufanyike kwa wakati;

**Mapato ya Ndani na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

(i) Katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Halmashauri zinakadiria kukusanya Mapato ya Ndani ya jumla ya **Shilingi trilioni 1.01** ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 863.85** zilizoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 ambayo ni ongezeko la **Shilingi bilioni 148.42** sawa na **asilimia 17.18**. Ongezeko hili limetokana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka mikakati ya pamoja ya kubuni vyanzo vipya, kuimarisha vilivyopo na mikakati zaidi ya ukusanyaji wa mapato **(*Kiambatisho Na. 11*)**;

(ii) **Shilingi bilioni 394.80** zimetengwa kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 75.98** ni mikopo ya **asilimia 10** na **Shilingi bilioni 318.82** ni kwa ajili ya miradi mingine

ya maendeleo kama ifuatavyo:- **Shilingi bilioni 35.32** zitatumika kuboresha miundombinu ya afya. Miradi itakayotekelezwa ni pamoja na kuendeleza ujenzi na ukarabati wa wa Hospitali **6** za Halmashauri, vituo vya afya **101,** zahanati **205,** vituo vya kukusanyia taka **59,** majengo ya huduma kwa wagonjwa wa nje (OPD) katika vituo vya afya na Hospitali **9** pamoja na huduma za lishe na ununuzi wa madawa; **Shilingi bilioni 25.89** zitatumika kuboresha miundombinu ya biashara ikiwemo ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa stendi **74**, masoko **110,** maegesho ya magari **38,** kuweka mazingira wezeshi ya viwanda vidogo **26,** maeneo ya kupumzikia **4** pamoja na kuboresha vituo vya kukusanyia mapato **61; Shilingi bilioni 51.52** zimetengwa kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya elimu ikiwemo ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa vyumba vya madarasa **2,935,** matundu ya vyoo **4,787,** daharia (hosteli) **102**, maabara za masomo ya sayansi **78,** mabwalo ya chakula **20** na kutengeneza madawati **56,049; Shilingi bilioni 7.57** zitatumika kuboresha miundombinu ya kilimo, mifugo na uvuvi ikiwemo ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa machinjio **124,** miundombinu ya umwagiliaji **50,** maghala **12,** majosho **52**, mashamba darasa **28,** mabwawa ya samaki **31**, malambo **10** na mashine za usindikaji **8; Shilingi bilioni 93.71** zitatumika kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi ikiwemo ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa majengo ya utawala yakijumuisha ofisi za walimu na ofisi za Halmashauri **482,** nyumba za watumishi **303**, uzio wa majengo **87,** ofisi za kata **113,** kumbi **30,** ofisi za vijji **98,** ofisi za Mitaa **16,** ununuzi wa pikipiki **65,** malori **manne (4),** ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo na utoaji wa mafunzo, mifumo ya umeme na TEHAMA; **Shilingi bilioni 13.32** zitatumika kwa ajili ya mipango miji na matumizi bora ya ardhi, vituo vya utalii na viwanja vya michezo; na **Shilingi bilioni 21.95** zitatumika kwa ajili ya matengenezo ya barabara, madaraja **20,** uwekaji wa taa za barabarani na ujenzi wa mifereji ya maji; na **Shilingi bilioni 68.99** zimepangwa kutumika katika miradi mingine;

(iii) **Shilingi bilioni 75.97** zinazotokana na **asilimia 10** ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri ambayo ni sehemu ya miradi ya amendeleo zimetengwa kwa ajili ya mikopo ya vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ambayo ni sehemu ya fedha za maendeleo zinazotokana na asilimia 40/60. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 30.39** ni kwa ajili ya vikundi vya

Wanawake, **Shilingi bilioni 30.39** ni kwa ajili ya vikundi vya Vijana na **Shilingi bilioni 15.19** ni kwa ajili ya vikundi vya Watu Wenye Ulemavu ***(Kiambatisho Na. 13)***. Aidha, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeweka mikakati mbalimbali ili kuhakikisha mikopo hii inasimamiwa kwa ufanisi. Moja ya mikakati iliyowekwa ni kuweka kigezo cha utoaji wa mikopo, usimamizi wa matumizi ya mikopo hiyo pamoja na marejesho kuwa sehemu ya kuwapima Wakurugenzi wa Halmashauri ambayo itafanyika kila robo mwaka na tathmini ya kina itafanyika mwisho wa mwaka. Mkakati mwingine ni matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki utakaosaidia kuondoa changamoto katika ukopeshaji, usimamizi na urejeshaji wa mikopo. Hivyo, itakuwa ni kazi ya Wakurugenzi kuhakikisha mfumo unatumika ipasavyo na kuongeza ufanisi; na

(iv) Jumla ya **Shilingi bilioni 4.76** zimetengwa kwa ajili ya uratibu wa Huduma Ndogo za Fedha ambapo Taasisi na vikundi vinavyojishughulisha na shughuli za fedha ambavyo siyo rasmi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa vitarasimishwa kupitia utaratibu huu;

**Sekta ya Afya**

(i) Kuendelea na ujenzi wa Hospitali **28** za Halmashauri ambazo zimetengewa **Shilingi bilioni 24.65 (*Kiambatisho Na. 14)***;

(ii) Kuendelea na ujenzi wa Hospitali **31** za Halmashauri ambazo zimetengewa **Shilingi bilioni 15.50 (*Kiambatisho Na. 14)***;

(iii) Ukarabati wa Hospitali kongwe **19** za Halmashauri ambazo zimetengewa **Shilingi bilioni 16.55 (*Kiambatisho Na. 14)*;**

(iv) Ukamilishaji wa ujenzi wa maboma ya Zahanati **300** ambazo zimetengewa **Shilingi bilioni 15.00 (*Kiambatisho Na. 14)***;

(v) **Shilingi bilioni 15.15** zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa Vifaa Tiba kwa Zahanati **300, Shilingi bilioni 47.70** za ununuzi wa Vifaa Tiba kwa Vituo vya Afya **159** na **Shilingi bilioni 7.10** za ununuzi wa Vifaa Tiba ya afya ya kinywa na macho kwa ajili ya hospitali za Halmashauri **71** zilizokamilika **(*Kiambatisho Na. 15)***;

**Sekta ya Elimu**

(i) Elimumsingi Bila Malipo kiasi cha **Shilingi bilioni 346.49** zimetengwa sawa na ongezeko la **Shilingi bilioni 34.44** ya fedha zilizoidhinishwa mwaka wa fedha 2021/22 ambayo ni **Shilingi bilioni 312.05 (*Kiambatisho Na 16)***;

(ii) **Shilingi bilioni 55.57** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba **809** za walimu zenye uwezo wa kuchukua kaya **1,916**. Kati yake, nyumba za walimu wa shule za msingi ni **298** za **(3 in1)** ambazo zitajengwa kupitia fedha za ruzuku kutoka Serikali Kuu kwa **Shilingi bilioni 30.02** na **Shilingi bilioni 25.55** zitatumika kujenga nyumba **511 (2 in1)** za walimu wa shule za sekondari kupitia mradi wa Uboreshaji wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP) (***Kiambatisho Na. 17)*;**

(iii) Ujenzi wa matundu ya vyoo **9,700** katika Vituo shikizi **970** ambapo **Shilingi bilioni 10.67** zimetengwa ***(Kiambatisho Na. 17)***;

(iv) Kuanza Awamu ya Kwanza ya ujenzi wa vyumba vya madarasa **1,700** katika Shule Kongwe za Msingi **Shilingi bilioni 34.00** zimetengwa ***(Kiambatisho Na. 17)* ;**

(v) Ujenzi wa Shule Mpya **39** za Msingi **Shilingi bilioni 15.60** zimetengwa ***(Kiambatisho Na. 17)*;**

(vi) Ujenzi wa uzio wa mabweni **99** ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ambapo **Shilingi bilioni 2.97** zimetengwa ***(Kiambatisho Na. 17)*;**

(vii) Ukamilishaji wa maboma ya vyumba vya madarasa **1,911** katika Shule za Msingi ambapo **Shilingi bilioni 23.88** zimetengwa ***(Kiambatisho Na. 18)*;**

(viii) Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba vya maabara **291** katika Shule za Sekondari ambapo **Shilingi bilioni 8.73** zimetengwa ***(Kiambatisho Na. 18)***;

(ix) Ukamilishaji wa mabwalo **86** ambapo mabwalo **80** katika shule za sekondari na mabwalo **sita (6)** katika Shule za Msingi **Shilingi milioni 4.30** zimetengwa ***(Kiambatisho Na. 18)*;**

(x) Ukamilishaji wa mabweni **461** ambapo mabweni **28** katika shule za Msingi zenye wanafunzi wenye mahitaji maalum na mabweni **433** kwa Shule za Sekondari ambapo **Shilingi bilioni 9.21** zimetengwa ***(Kiambatisho Na. 18)*;**

(xi) Kuwezesha kufanyika kwa mitihani ya Taifa ya Darasa la Nne, la Saba, Kidato cha Pili, Kidato cha Nne na Kidato cha Sita **Shilingi bilioni 142.33** zimetengwa **(*Kiambatisho Na. 19)***;

(xii) **Shilingi milioni 670.00** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Tume ya Utumishi wa Walimu pamoja na uundaji wa mfumo;

**Utawala Bora**

(i) Jumla ya **Shilingi bilioni 36.11** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa majengo ya ofisi na nyumba za viongozi kama ifuatavyo: **Shilingi bilioni 1.15** zimetengwa kwa ajili ya upanuzi wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa 3 ya Dodoma, Kilimanjaro na Singida; **Shilingi bilioni 3.58** kwa ajili ya ukarabati wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa **9;** Wakuu wa Wilaya **15** na Ofisi moja (1) ya Afisa Tarafa; **Shilingi milioni 967.89** zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa nyumba mbili **(2)** za Wakuu wa Mikoa, nyumba **18** za Wakuu wa Wilaya, nyumba moja **(1)** ya Katibu Tawala wa Mkoa na nyumba **4** za Makatibu Tawala wa Wilaya; **Shilingi bilioni 2.38** zimetengwa kwa ajili ya Ujenzi na ukamilishaji wa Ikulu ndogo saba **(7)** na ukarabati wa Ikulu Ndogo tatu **(3)**; **Shilingi bilioni 6.75** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa nyumba za Viongozi **40**; **Shilingi bilioni 19.43** kwa ajili ya ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa majengo ya ofisi **61** yakiwemo ya Wakuu wa Mikoa **10**; Wakuu wa Wilaya **19** na ofisi za Tarafa **32.**

(ii) Serikali imetenga **Shilingi bilioni 10.00** kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Soko jipya la Kariakoo na kukarabati Soko Kuu liloungua moto tarehe 10 Julai, 2021;

(iii) Serikali imetenga **Shilingi bilioni 8.90** kwa ajili ya ujenzi wa nyumba **111** za Wakuu wa Idara na **Shilingi bilioni 7.20** kwa ajili ya ujenzi wa nyumba **48** za Wakurugenzi ***(Kiambatisho Na. 20)***;

(iv) Halmashauri **83** zimetengewa **Shilingi bilioni 68.85** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa majengo ya utawala ***(Kiambatisho Na. 20)***;

(v) Halmashauri **13** zimetengewa **Shilingi bilioni 13.00** kwa ajili ya ujenzi wa majengo mapya ya utawala ***(Kiambatisho Na. 20)***;

(vi) Jumla ya **Shilingi bilioni 2.05** zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa boti: Halmashauri za Wilaya za Mafia **(boti mbili)**, Kilwa (**boti moja**), Ukerewe (**boti mbili**), Muleba (**boti moja**), Kalambo (**boti moja**) na Momba (**boti moja**);

(vii) Halmashauri **20** zimetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 40.11** kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kimkakati ***(Kiambatisho Na. 21)***;

**Programu mbalimbali**

(i) Jumla ya **Shilingi bilioni 1.41** zimetengwa kupitia Programu ya Kuimarisha Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kuimarisha Mfumo wa Ugatuaji utakaosaidia kuboresha huduma za jamii, utawala bora na kuwa na maendeleo endelevu;

(ii) Jumla ya **Shilingi bilioni 135.43** zimetengwa kupitia Programu ya Uboreshaji wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP) kwa ajili ya uendelezaji wa ujenzi wa shule **10** za sekondari za wasichana za bweni kwa masomo ya sayansi, shule za sekondari **232** za Kata, ujenzi wa shule mpya za kata **184**, ujenzi wa shule mpya **tano (5)** za sekondari za wasichana za bweni kwa masomo ya sayansi na fedha kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini;

(iii) Jumla ya **Shilingi bilioni 55.38** zimetengwa kupitia Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira (SRWSS) kwa upande wa elimu na Afya kwa ajili ya kuimarisha shughuli za afya na usafi wa mazingira;

(iv) Jumla ya **Shilingi bilioni 237.36** zimetengwa kupitia Programu ya BOOST kwa ajili ya kuimarisha ujifunzaji na ufundishaji katika elimu ya awali na msingi;

(v) Jumla ya **Shilingi bilioni 17.27** zimetengwa kupitia DART kwa ajili ya kununua Mfumo wa kusimamia magari na kusimika vifaa vya kukusanyia nauli kwa mfumo wa kielektroniki; na

(vi) Jumla ya **Shilingi bilioni 83.29** zimetengwa kupitia Programu ya Mfuko wa Pamoja wa Afya kwa ajili ya uboreshaji wa huduma za afya katika vituo vya kutolea huduma.

196. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais – TAMISEMI itaendelea kusimamia na kuratibu maandiko ya miradi ya kimkakati kwa kushirikiana na Timu ya Kitaifa iliyoundwa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kuratibu maandiko ya miradi inayoweza kukopesheka kupitia Programu ya ugharamiaji wa miradi mbadala. Timu hii imeundwa ili kutatua changamoto ya uandishi wa maandiko ya miradi kutoka katika Halmashauri mbalimbali na hivyo kuzisababishia Halmashauri kutokidhi vigezo vilivyowekwa na Serikali ili kupata fedha za utekelezaji wa miradi hiyo. Naomba kutumia fursa hii kuzielekeza Halmashauri ziibue miradi ili iweze kugharamiwa kupitia utaratibu wa ugharamiaji mbadala wa miradi ikijumuisha Hati Fungani za Halmashauri.

197. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI itazielekeza Halmashauri kuhakikisha zinatekeleza miradi maalum kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri kupitia vipaumbele vilivyopo. Vipaumbele hivyo vitajumuisha: ukamilishaji wa ujenzi wa maboma ya vyumba vya madarasa, zahanati, maabara ya masomo ya sayansi, ujenzi wa matundu ya vyoo kwa Shule za Msingi na Sekondari, ununuzi wa vifaa, vifaa tiba na vitendanishi, nyumba za watumishi na kuendeleza ujenzi wa maeneo ya wafanyabiashara wadogo (wamachinga). Vilevile, Halmashauri zenye Mapato ya Ndani zaidi ya **Shilingi bilioni 5.00** zinaelekezwa pia kuchangia **asilimia 10** kwa ajili ya ujenzi wa barabara zinazosimamiwa na TARURA.

198. ***Mheshimiwa Spika,*** Halmashauri zote zinaelekezwa kuendelea na utengaji, uboreshaji, upangaji na ujenzi wa miundombinu ya maeneo ya kufanyia biashara wafanyabiashara wadogo (machinga) pamoja na kuwaunganisha na Taasisi za kifedha, ili kuwaongezea fursa za kiuchumi na Serikali itanufaika na ushuru pamoja na kodi mbalimbali kupitia shughuli zao. Kwa

sasa Halmashauri kumi na moja **(11)** yakiwemo Majiji **sita (6)** Manispaa Nne **(4)** na Halmashauri ya Mji **moja (1)** zimeanza ujenzi wa miundombinu rafiki kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo (machinga). yatakayowawezesha kurasimisha biashara zao ili watambulike na kuunganishwa na Taasisi za kifedha.

199. ***Mheshimiwa Spika***, wanafunzi wanaotarajiwa kuandikishwa Kidato cha Kwanza Januari 2023, kwa ufaulu wa **asilimia 82** ni **1,257,996** kati ya wanafunzi **1,534,141** waliopo darasa la saba mwaka 2022. Ongezeko hili linatokana na wanafunzi wa kundi la kwanza la mpango wa elimumsingi bila malipo wanaotarajiwa kuhitimu darasa la saba mwaka 2022. Kutokana na ongezeko hilo, mahitaji ya vyumba vya madarasa ya wanafunzi wa sekondari yatakuwa **15,186** vyumba vya madarasa vitakavyokuwepo baada ya wanafunzi wa Kidato cha Nne kuhitimu ni **7,200** na kusababisha upungufu wa vyumba **7,986.** Hivyo, Serikali itajenga madarasa haya kupitia ruzuku ya Serikali Kuu, mapato ya ndani ya Halmashauri na fedha za Washirika wa maendeleo wakiwemo SEQUIP.

200. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kuchukua fursa hii kuzielekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga na kupeleka **asilimia 20** ya Mapato yatokanayo na tozo ya mazao ya kilimo (*crop cess*) kwa ajili ya shughuli za kilimo ikiwemo kuendeleza uzalishaji wa mazao ya kimkakati. Aidha, Halmashauri zitenge **asilimia 15** ya mapato yatokanayo na mazao ya mifugo kwa ajili ya shughuli za kuendeleza ufugaji kwa mujibu wa Waraka wa Rais Na.01 wa mwaka 2002 kuhusu hatua za kuchukua kuzuia kuenea kwa magonjwa ya mifugo nchini. Vilevile, Halmashauri zitenge **asilimia tano (5)** ya mapato yatokanayo na mazao ya uvuvi kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009.

## E. SHUKRANI

201. ***Mheshimiwa Spika,*** kabla ya kuhitimisha Hotuba yangu, naomba kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi imara katika kutekeleza shughuli za Bunge. Vilevile, naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa (USEMI)

inayoongozwa na Mheshimiwa Abdallah Jaffari Chaurembo Mbunge wa Jimbo la Mbagala, Mwenyekiti wa Kamati, na Mheshimiwa Denis Lazaro Londo Mbunge wa Jimbo la Mikumi, Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa kazi nzuri katika kusimamia utendaji wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Maoni na ushauri wa Kamati umesaidia kuleta mageuzi makubwa yaliyotokea katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na utoaji wa huduma katika Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

202. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kumshukuru Mheshimiwa Daniel Barran Sillo Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na Mheshimiwa Omary Mohammed Kigua Makamu Mwenyekiti na wajumbe wa Kamati kwa maoni, maagizo na maelekezo mengine ambayo wanaendelea kutuelekeza kuhusu utekelezaji wa Mipango na Bajeti.

203. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) inayoongozwa na Mheshimiwa Grace Victor Tendegu Mbunge wa Viti Maalum, Mwenyekiti wa Kamati na Mheshimiwa Selemani Jumanne Zeddy Mbunge wa Jimbo la Bukene Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa maoni, maelekezo na maagizo yao katika uboreshaji wa usimamizi wa fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

204. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa Wadau wa Maendeleo katika utekelezaji wa Programu, Miradi na shughuli mbalimbali za Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Washirika hawa ni pamoja na Benki ya Dunia (WB), Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA), Jumuiya ya Ulaya (EU), *Global Partnership for Education,* Shirika la Maendeleo la Uingereza (Foreign, Commonwealth and Development Office-FCDO), Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), Shirika la Kuleta Mapinduzi ya Kijani (AGRA) na Nchi zinazochangia kupitia Mfuko wa Pamoja wa Afya ambazo ni Denmark, Ireland, Jamhuri ya Korea (KOICA), Shirika la Maendeleo (SIDA), Global Partnership for Education-

(GPE), Switzerland na Shirika la Umoja wa Mataifa na Mitaji na Maendeleo (UNCDF).

205. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaendelea kushirikiana na Wadau wa Maendeleo katika utekelezaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii ili kuboresha utoaji wa huduma na kupunguza umaskini. Aidha, ninawashukuru wananchi kwa mchango mkubwa katika utekelezaji wa Miradi na Programu mbalimbali kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

206. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutambua mchango mkubwa wa Viongozi wenzangu katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI. Kipekee, nawashukuru Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange, Mbunge wa Jimbo la Wanging'ombe na Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Jimbo la Tunduma, kwa msaada mkubwa wanaotoa kwangu katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

207. ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, namshukuru Katibu Mkuu, Prof. Riziki Silas Shemdoe kwa mchango wake katika kufanikisha maandalizi ya Mpango na Bajeti na Naibu Makatibu Wakuu Bw. Gerald Geofrey Mweli, Dkt. Grace Elias Magembe na Dkt. Switbert Zacharia Mkama katika usimamizi wa majukumu ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Vilevile, nimpongeze Bi. Paulina Mbena Nkwama Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kusimamia vyema Tume ya Utumishi wa Walimu. Aidha, ninawashukuru Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Waheshimiwa Madiwani, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI, Wakurugenzi wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Watumishi wote wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zake kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

208. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutumia fursa hii pia kuwashukuru Viongozi wenzangu katika Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama Mbunge wa Jimbo la Peramiho, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Utumishi wa Umma na Utawala Bora; na Mheshimiwa George Huruma Mkuchika Mbunge wa Jimbo la

Newala Mjini, Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais.

209. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wenzangu wote kwa ushirikiano walionipa katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/22 katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais –TAMISEMI.

210. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa heshima na unyenyekevu mkubwa ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Karagwe kwa kuniamini na kunichagua tena kuwa Mbunge wao. Ninawaahidi wana Karagwe kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa nguvu zangu zote ili kuifanya Karagwe yetu ipate maendeleo zaidi ya kiuchumi na kijamii. Kipekee, ninaishukuru familia yangu kwa kuniombea na kwa uvumilivu wao muda wote ninapokuwa mbali nao katika kutekeleza wa majukumu ya kitaifa.

## F. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

### Maduhuli na Makusanyo ya Mapato ya Ndani

211. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Taasisi zilizo chini yake, Mikoa **26** na Halmashauri **184** inaomba idhini ya kukusanya Maduhuli na Mapato ya Ndani jumla ya **Shilingi Trilioni moja Bilioni Sabini na Moja Milioni Mia Saba na Thelathini Mia Nane na Themanini na Sita Elfu Mia Nne na Kumi na Tano na Senti Hamsini (Shilingi 1,071,730,886,415.50)**. Makusanyo haya yatatokana na mauzo ya vifaa chakavu, ada za wanafunzi, tozo na ushuru unaotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kulingana na Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290. Mchanganuo wa makusanyo ya mapato hayo ni kama ifuatavyo:

| **Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Maduhuli na Mapato ya Ndani kwa Mwaka wa Fedha 2022/23** | |
|---|---|
| **OFISI/TAASISI** | **MAKADIRIO** |
| Ofisi ya Rais – TAMISEMI | 0 |
| Taasisi | 59,195,516,103.50 |

| | |
|---|---|
| Mikoa | 249,281,312.00 |
| Halmashauri | 1,012,286,089,000.00 |
| **JUMLA KUU** | **1,071,730,886,415.5** |

212. ***Mheshimiwa Spika,*** sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 jumla ya **Shilingi Trilioni Nane Bilioni Mia Saba Sabini na Tisa Milioni Mia Nane Thelathini na Saba Mia Saba Sitini na Tatu Elfu na Mia Mbili (Shilingi 8,779,837,763,200.00)** kwa ajili ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI Fungu **56**, Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu **Na. 2** na Mafungu **26** ya Mikoa yanayojumuisha Halmashauri **184**.

213. ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya fedha zinazoombwa, **Shilingi Trilioni Tano Bilioni Mia Tano Kumi na Moja Milioni Mia Nane Arobaini na Tano Mia Moja Tisini na Tatu Elfu (Shilingi 5,511,845,193,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida yanayojumuisha Mishahara **Shilingi Trilioni Nne Bilioni Mia Sita Ishirini na Sita Milioni Mia Mbili Hamsini na Tatu Mia Nane Sitini na Nane Elfu** (**Shilingi 4,626,253,868,000.00)** na **Shilingi Bilioni Mia Nane Themanini na Tano Milioni Mia Tano Tisini na Moja Mia Tatu Ishirini na Tano Elfu (Shilingi 885,591,325,000.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, jumla ya **Shilingi Trilioni Tatu Bilioni Mia Mbili Sitini na Saba Milioni Mia Tisa Tisini na Mbili Mia Tano Sabini Elfu na Mia Mbili (Shilingi 3,267,992,570,200.00** zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo kati ya fedha hizo **Shilingi Trilioni Mbili Bilioni Mia Moja Arobaini na Saba Milioni Mia Sita Themanini na Sita Mia Tatu Sabini na Moja Elfu na Mia Mbili (Shilingi 2,147,686,371,200.00** ni fedha za ndani na **Shilingi Trilioni Moja Bilioni Mia Moja Ishirini Milioni Mia Tatu na Sita Mia Moja Tisini na Tisa Elfu (Shilingi 1,120,306,199,000.00)** ni fedha za nje *(Mchanganuo wa fedha zinazoombwa katika Mwaka wa Fedha 2022/23 umeoneshwa katika* ***Jedwali Na. 2***.

**Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Makisio katika Mafungu 28 ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2022/23**

| AINA YA MATUMIZI | BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23 |
|---|---|
| **Matumizi ya Kawaida Ofisi ya Rais -TAMISEMI** | |
| **Mishahara** | |
| Mishahara Makao Makuu | 9,556,977,000.00 |
| Mishahara ya Taasisi | 53,823,523,000.00 |
| **Jumla Mishahara Ofisi ya Rais - TAMISEMI** | **63,380,500,000.00** |
| | |
| **Matumizi Mengineyo** | |
| Makao Makuu | 12,494,284,000.00 |
| Taasisi | 2,643,670,000.00 |
| **Jumla ya Matumizi Mengineyo** | **15,137,954,000.00** |
| **Jumla Matumizi ya Kawaida** | **78,518,454,000.00** |
| | |
| **TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)** | |
| Mishahara | 8,276,293,000.00 |
| Matumizi Mengineyo | 6,708,202,000.00 |
| **Jumla ya Matumizi ya Kawaida TSC** | **14,984,495,000.00** |
| | |
| **MIKOA NA HALMASHAURI** | |
| **MIKOA:** | |
| Mishahara | 76,205,297,000.00 |
| Matumizi Mengineyo | 79,829,078,000.00 |
| **Jumla ya Matumizi ya Kawaida** | **156,034,375,000.00** |
| | |
| **HALMASHAURI** | |
| Mishahara | 4,478,391,778,000.00 |
| Matumizi Mengineyo (SK) | 166,430,744,000.00 |
| Matumizi Mengineyo (MSM) | 617,485,347,000.00 |
| **Jumla Matumizi ya Kawaida** | **5,262,307,869,000.00** |
| | |
| **MIRADI YA MAENDELEO** | |

| AINA YA MATUMIZI | BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23 |
|---|---|
| OFISI YA RAIS -TAMISEMI | |
| Fedha za Ndani | 758,726,035,200.00 |
| Fedha za Nje | 124,312,896,000.00 |
| **Jumla Maendeleo** | **883,038,931,200.00** |
| | |
| **TUME YA UTUMISHI WA WALIMU** | |
| Fedha za Ndani | 670,000,000.00 |
| **Jumla** | **670,000,000.00** |
| | |
| **MIKOA** | |
| Fedha za Ndani | 66,018,770,000.00 |
| Fedha za Nje | 18,508,243,000.00 |
| **Jumla Maendeleo** | **84,527,013,000.00** |
| | |
| **HALMASHAURI** | |
| Fedha za Ndani (SK) | 927,470,824,000.00 |
| Fedha za Ndani (MSM) | 394,800,742,000.00 |
| Fedha za Nje | 977,485,060,000.00 |
| **Jumla Maendeleo Halmashauri** | **2,299,756,626,000.00** |
| **JUMLA KUU** | **8,779,837,763,200.00** |

***SK –*** *Serikali Kuu na* ***MSM*** *– Mapato ya Ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa*

214. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na hotuba hii yapo majedwali ambayo yanafafanua kwa kina makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI Fungu 56, Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu Na. 2, Mikoa na Halmashauri Mafungu 26 ambayo ni sehemu ya hotuba hii.

215. ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba hii inapatikana pia kwenye Tovuti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI ambayo ni www.tamisemi.go.tz.

216. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, hoja imeungwa mkono, ahsante sana Waziri Bashungwa kwa kazi nzuri unayoifanya wewe na timu yako. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tulivyokuwa tunatangaza majina ya wageni wageni wakuu wa Wizara hii akiwemo Katibu Mkuu walikuwa na dharula nyingine hasa kutokana na unyeti na umuhimu wa wageni hawa wanne nitakaowatambulisha kwenu ili mtambue na wao wamo ndani.

Naomba sasa nimtambulishe Profesa Riziki Shemdoe - Katibu Mkuu, Dkt. Grace Magembe - Naibu Katibu Mkuu Afya, Ndugu John M. Cheyo Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Ndugu Herineema Kaaya - Mkurugenzi wa *ALAT,* karibuni sana. *(Makofi)*

Tumewapa kipaumbele kwa sababu ni Wizara nzito na Taifa linawategemea sana kufikisha matakwa ya wananchi kutokana na utendaji wenu mzuri. *(Makofi)*

Naomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge na watumishi wa Ofisi ya Bunge kuwa wale wote waliopima na kuhitaji *frame* za miwani za kisasa tayari *frame* hizo zimeletwa, hivyo mnatakiwa kuwaona madaktari hao kwenye eneo la viwanja vya Bunge nyuma ya Ukumbi wa Msekwa. Aidha leo ni siku yao ya mwisho kuwa hapa Bungeni hivyo mnatakiwa kwenda kuchukuwa leo hii.

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu Bunge na Utawala Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

**MHE. DENNIS L. LONDO – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2021/2022, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 naomba kuwasilisha kwako taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na maoni ya kamati kuhusu makadirio na mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne; sehemu ya kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi, muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati hii ilivyofanya kazi; sehemu ya pili inaripoti matokeo ya uchambuzi na tathmini kwa kuchanganua utekelezaji wa malengo ya mpango wa ofisi hii, ukusanyaji wa maduhuli, upatikanaji wa fedha na uzingatiaji wa ushauri wa Kamati. Aidha sehemu ya tatu inayoripoti maoni na ushauri wa Kamati kutokana na uchambuzi; lakini sehemu ya nne na ya mwisho inayohitimisha na kulishauri Bunge kuhusu hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais -TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa Kamati kuchambua Makadirio ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni Masharti ya kifungu cha 6(4) kikisomwa kwa pamoja na kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Aidha, Kanuni ya 117(4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yaliyotaka taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa hapa Bungeni. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa na kwamba naliomba Bunge hili liijadili hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa pamoja na taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa zilizochambuliwa, zinagusa jumla ya mafungu 28, kati ya mafungu hayo Fungu moja ni Fungu la Ofisi ya Rais -TAMISEMI na la pili ni Fungu la Tume ya Utumishi wa Walimu, mafungu 26 ni ya Mikoa ya Tanzania Bara na kwa mawanda hayo nitangulie kusema kuwa nitasoma taarifa hii kwa muhtasari, lakini naomba taarifa yote kama ilivyowasilisha mezani iingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Kwa sababu hiyo, ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa wasilisho hili, naomba kubainisha mambo makuu mawili yaliyochambuliwa. Mambo hayo ni taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022; na makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilichambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI baada ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, uchambuzi huo ulilenga kujenga msingi wa kufanya ulinganisho wa makadirio kwa mwaka wa fedha 2022/2023, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2021/2022 Ofisi ya Rais - TAMISEMI, iliidhinishiwa kukusanya jumla ya shilingi 916,445,409,198.50 hata hivyo kufikia mwezi Februari, 2022 Ofisi hii ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi 615,603,870,037.65 ambayo ni asilimia 67 ya lengo lililokusudiwa mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekana katika Jedwali Na. 1 kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha uchambuzi wa makusanyo ya maduhuli unaonyesha kwamba moja, jumla ya makusanyo ya maduhuli umefikia asilimia 56 ya lengo hadi kufikia Februari, 2022. Hii ikiwa ni ndani ya robo tatu ya utekelezaji wa majukumu.

Mheshimiwa Naibu Spika mbili, mwenendo wa makusanyo ya maduhuli ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa umefikia asilimia 67 ya lengo na mikoa imefikia asilimia 51 ya lengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kwa kipindi hiki kilichobaki cha utekelezaji ni vigumu kufikia lengo kwa kuwa ni kipindi kilichokwisha katika utekelezaji karibu asilimia 75.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, mikoa na TAMISEMI yenyewe wamekusanya nyuma ya lengo kwa kufikia chini ya asilimia 60 ya lengo ndani ya kipindi hicho ambacho ni asilimia 75 ya kipindi cha utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa ukusanyaji maduhuli kwenye mikoa taarifa zinaonesha kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2022 mikoa yote kwa pamoja ilifikia lengo la makusanyo kwa asilimia 75, mwenendo huu wa makusanyo unaendana na matarajio ya malengo, aidha, uchambuzi unaonyesha kuwa Mbeya ni Mkoa unaoongoza kufikia lengo kwa kufikia asilimia 98 ya lengo hadi mwezi Februari, 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikoa mingine miwili iliyofuatia Mbeya kwa kufikia lengo ni Kagera, kwa asilimia 95 na Ruvuma iliyofikia lengo kwa asilimia 92. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchambuzi huo ni dhahiri kuwa mwenendo wa makusanyo kwa ujumla si mzuri hata hivyo mwenendo wa makusanyo kwa mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa unatoa mwelekeo wa kufikia lengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka wa fedha 2021/2022 ofisi hii inatekeleza jumla ya miradi 14 ya Fungu Namba 56 na miradi mingine kwenye mikoa na Serikali za Mitaa. Jumla ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya kugharamia miradi hiyo ni shilingi 3,840,453,728,770 sawa na asilimia 44.8 ya bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu na Mikoa 26.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa madhumuni ya kuzingatia masharti ya Kanuni ya 171(1) ya kanuni za Bunge kamati ilitembelea miradi 10 ya Wizara hii miradi hiyo ni kama ilivyooneshwa kwenye taarifa iliyowekwa mezani mapema leo asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na miradi hiyo ipo pia miradi iliyotekelezwa kwa kutumia fedha zilizotolewa na Serikali katika mpango wa maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano ya UVIKO-19.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufuatiliaji wa Kamati unaonyesha kuwa zipo dalili kwamba baadhi ya Halmashauri hazikuteleza miradi iliyopangwa kwenye bajeti zao za ndani, badala yake

zimetumia fedha za UVIKO kuendeleza miradi hiyo hali hiyo kwa maoni ya Kamati si jambo linalofaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu pamoja na mikoa 26 waliidhinishiwa jumla ya shilingi 4,728,008,207,000 sawa na asilimia 55 kwa matumizi ya kawaida, aidha, kufikia Februari 2022 kiasi cha fedha kilichopokelewa ni kiasi cha shilingi 3,287,355,817,601.06 sawa na asilimia 69. 5 ya kiasi kilichoidhinishwa, mchanganuo wa upokeaji wa fedha unaonekana katika Jedwali Na. 2.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi unaonyesha kuwa mwenendo wa jumla wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida si mbaya, hata hivyo upatikanaji wa fedha hizo kwa ajili ya uendeshajiwa Tume ya Utumishi wa Walimu hauridhishi, hadi kufikia mwezi Februari, 2022 Tume hiyo ilipokea kiasi ambacho ni asilimia 56 tu ya bajeti yake ikiwa ni robo tatu za kipindi za utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, angalau mafungu ya mikoa kwa ujumla wake yaliweza kupokea asilimia 72 ya bajeti yake hadi kufikia Februari, 2022, lakini Tume ya Utumishi wa Walimu na Mamlaka za Serikali za Mitaa zilipokea pungufu ya asilimia ya 72 hadi kufikia mwezi Februari, 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kuzingatia ama kupitia na kuidhinisha makadirio na mapato ya matumizi ya Ofisi ya Rais- TAMISEMI Kamati ilishauri kuhusu mambo mbalimbali naomba kulijulisha Bunge lako hili kuwa taarifa ya mtoa hoja ilionesha kwamba Serikali imezingatia sehemu kubwa ya ushauri huo, mfano ushauri wa Kamati uliozingatiwa ni kuhusu kusaidia vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu na Halmashauri kubuni vyanzo vipya vya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya utekelezaji zilionesha kuwa baadhi ya Halmashauri zimeboresha mikopo kwa vikundi hivyo, aidha, zipo halmashauri zilizobuni vyanzo vipya vya mapato kwa mfano Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ilijenga soko la madini ambalo ni chanzo kipya cha mapato ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja uzingatiaji mzuri wa ushauri upo ushauri uliotolewa na Kamati ambao unahitaji kufanyiwa kazi na Serikali, kwa mfano suala la kuhakikisha Halmashauri zinasimamia vyama mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu linahitajika kuboreshwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya maduhuli kwa matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa  Kamati ilifanya uchambuzi kwa makadilio kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Uchambuzi huo ulifanyika kwa kulinganisha na bajeti iliyopita kama inavyooneka katika sehemu ya pili ya taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi wake kamati ilibaini kuwa makadirio ya maduhuri kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yameongezeka kwa asilimia 14.4 ikilinganishwa na lengo la maduhuli kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Mchanganuo wa makadirio hayo unaoneshwa kuwa katika Jedwali Na. 3 na taarifa iliyowasilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchanganuo huo unaonesha kwamba moja kwa ujumla makadirio ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yameongezeka kwa asilima 14.4 ikilinganishwa na lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili kutokana na mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kuonesha kufika asilimia 56 ndani ya robo tatu za kipindi cha utekelezaji, haitakuwa rahisi kufikia lengo la makusanyo lililowekwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ikizingatiwa kuwa uzoefu uliopatikana kwa mwaka wa fedha uliotangulia hali haikuwa hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchambuzi huo, kamati ina maoni kwamba uwekaji wa lengo la makusanyo utakuwa na tija iwapo utazingatia uhalisia.  Kwa mfano katika 2021/2022, Mikoa ilifikia lengo la makusanyo chini ya asilimia 55 hadi kufikia mwezi Februari, 2022; lakini kwa mwaka wa fedha 2022/2023 lengo la

maduhuli kwa mikoa limeongezeka kwa asilimia 11.4, ni dhahiri kuwa kama hakuna maelezo ya kutosha kwa lengo hilo la makusanyo miaka hiyo haitafikiwa lengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa matumizi ya kawaida; makadirio ya matumizi ya jumla ya kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, yameongezeka kwa asilimia asilimia 16.5 ikilinganishwa na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Hali hiyo ililinganishwa na uzoefu wa upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2021/2022 ili kuonesha uwezekano katika hali halisi. Naomba kulijulisha Bunge lako kuwa, Kamati ilibaini kwamba iwapo mwenendo wa upatikanaji wa fedha utakuwa kama ulivyo kwa mwaka wa fedha unaoisha, ukadiriaji huu wa matumzi ya kawaida unaweza kukosa uhalisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi umeonesha kuwa katika bajeti ya Mikoa kuna ongezeko la bajeti kwa asilimia 20.6 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2021/2022 kama mchanganuo wa makadirio hayo unavyooneka katika Jedwali Na. 4

Mheshimiwa Naibu Spika, mchanganuo wa makadirio ya matumizi ya kawaida kwa taasisi zilizo chini ya TAMISEMI, unaonesha kuwa bajeti ya *TARURA* kwa matumizi ya kawaida imeongezeka kwa asilimia 14.7 hii ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2021/2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, taasisi yenye bajeti iliyoongezeka kwa kiasi kikubwa zaidi ya nyingine ni *DART* yenye ongezeko la asilimia 16.9 mchanganuo huo unaonekana katika Jedwali Na. 5.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchanganuzi huo, ni wazi kwamba uendeshaji wa shughuli za *TARURA* na *DART* umeongezewa msukumo katika bajeti. Hata hivyo, uhalisia wa uzito maalumu uliojitokeza katika makadirio kwa shughuli za Serikali na taasisi hizo utaonekana wakati wa utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati ilichambua pia makadirio na matumizi ya kugharamia miradi ya maendeleo iliyopangwa

kutekelezwa na TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu na Mikoa 26 kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio hayo ni pungufu kwa asilimia 14.9 ikilinganishwa na bajeti iliyowasilishwa hapa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kama inavyooenekana katika Jedwali Na.06.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, bajeti ya maendeleo kwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa, Serikali za Mitaa kwa ujumla imepungua kwa asilimia 15. Punguzo hili lina maana kwamba idadi, thamani na ukubwa wa miradi inayotekelezwa imepungua ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, miradi inayotekelezwa na mikoa imepungua zaidi kwa asilimia 25.9 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, miradi iliyopungua lakini kwa kiasi kidogo ikilinganishwa na punguzo la Mikoa na Tawala za Serikali za Mitaa ni miradi ya TAMISEMI na Tume ya Utumishi wa Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchambuzi huo ni wazi kuwa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa itatekeleza miradi kwa idadi ndogo, thamani ndogo au msisitizo mdogo ikilinganishwa na utekelezaji ulivyokuwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati; pamoja na uchambuzi huo Kamati inayo maoni ambayo ni msingi wa ushauri nitakaouleza naomba kutoa maoni hayo kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya fedha za asilimia 10 inayotokana na mapato ya ndani ya Halmashauri yasipowekewa utaratibu mzuri ya ufuatiliaji na usimamizi hayatatoa tija iliyokusudiwa. Kwa sasa taarifa za matumizi ya fedha hizo nazo zinatofautiana kwa kiasi kikubwa na kuacha mashaka kuhusu uaminifu katika matumizi yake.

(b) Kukosekana kwa mfumo wa TEHAMA katika matumizi ya fedha za asilimia 10 kunaweza kuwa chanzo cha ubadhirifu wa fedha hizo.

(c) Ujenzi au ukarabati wa shule utakuwa na tija zaidi iwapo barabara zinazofikia shule hizo zitaboreshwa ili zipitike vizuri, kwa mfano ujenzi wa shule ya *Chief Rocket Mwashinga* katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya unahitaji juhudi za dharura kuboresha barabara hiyo inayokwenda kwenye miundombinu hiyo.

(d) Ukarabati na ujenzi wa shule za Umma utakuwa na manufaa zaidi iwapo utafanyika sambamba na kuhakikisha kuwa shule hizo zinajengewa uzio kwa kutumia mapato ya ndani ya Halmashauri zinazohusika.

(e) Uhamasishaji mzuri na usimamizi bora wa uendeshaji wa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa namna inavyofanikisha urejeshaji wa mikopo unaweza kuongeza uwezo wa Halmashauri kuvisaidia vikundi vingine vyenye sifa, hivyo kukidhi madhumuni ya mikopo hiyo.

(f) Kuvisaidia vikundi vinavyopatiwa mikopo na Halmashauri nchini kwa kuvipa uwezo na maarifa ya kufanya biashara kwa ufanisi ni jambo linaloweza kufanikisha adhma ya utaratibu wa mikopo hiyo.

(g) Idara ya Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii na Biashara kwenye Halmashauri nchini zisipotumika kikamilifu kuviwezesha vikundi vinavyopata mikopo, utaratibu wa matumizi ya asilimia 10 ya mapato ya ndani unaweza kukosa tija.

(h) Miradi inayotekelezwa na Halmashauri nchini ambayo inafaa kuwa na barabara zinazofikika itakuwa na manufaa makubwa kwa wananchi iwapo *TARURA* itapanga ujenzi wa barabara kwa kuipa vipaumbele miradi hiyo.

(i) Ujenzi wa barabara bila kukamilisha uwekaji wa taa za barabarani na alama za barabarani kutokana zabuni

kutokujumuisha kazi hizo unafifisha manufaa ya barabara nyingi zinazojengwa na *TARURA*. *(Makofi)*

(j) Ujenzi wa madaraja yanaunganisha mawasiliano katika maeneo mbalimbali ya vijijini, usipozingatia hali ya udongo wa eneo linalohusika unaweza kuathiri tija *TARURA* kutekeleza baadhi ya miradi.

(k) Utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa vituo vya afya katika Halmashauri nchini usipozingatia ramani na miongozo inayotolewa na TAMISEMI unaweza kutofautiana kwa kiasi kikubwa na viwango vinavyotakiwa. Aidha, kukosekana kwa barabara zinazopitika kwenda kwenye vituo vinavyojengwa kunaweza kukwamisha madhumuni ya ujenzi wa vituo hivyo.

(l) Utekelezaji wa miradi ya maendelo uliokuwa umepangwa katika bajeti za Halmashauri ni jambo lenye umuhimu kama ilivyo kwenye utekelezaji wa miradi chini ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa Mapambano Dhidi ya UVIKO-19. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umuhimu huo ukaguzi maalumu wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Halmashauri kwa utaratibu wa fedha za mapato ya ndani unaweza kusaidia udhibiti wa hatari wa matumizi mabaya ya fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa Kamati; kwa kuzingatia maoni yaliyobainishwa naomba kutoa ushauri kama ifuatavyo; Mikoa kutokana na maoni ya Kamati ushauri kuhusu Sekretarieti za Mikoa nchini ni kama ifuatavyo:-

(a) Sekretarieti za Mikoa zipange kwa kuzingatia vipaumbele ambavyo vitatekeleza kwa wakati.

(b) Halmashauri zote katika kila Mkoa zielekezwe namna bora ya kutumia utaratibu wa *force account* wakati wa kutekeleza miradi ya maendeleo ili kuto kununua vifaa vya ujenzi kutoka nje ya Halmashauri zinazohusika. *(Makofi)*

(c) Halmashauri katika kila Mkoa zihimizwe na kusimamiwa ili zizingatie maelekezo na viwango vya ujenzi wa miundombinu inayojengwa.

(d) Halmashauri zote katika kila Mkoa zitafute namna bora ya kuwezesha upatikana wa taulo za watoto wa kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, TAMISEMI na taasisi zake, kuhusu mipango ya TAMISEMI na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Serikali iandae taarifa maalum ya matumizi ya fedha za asilimia 10 inayotoka na mapato ya ndani ya Halmashauri zinazotokana na mapato yasiyolindwa. Taarifa hiyo aidha, ionyeshe kiasi kilichokusanywa tangu mwaka 2018 hadi 2022, kiasi kilichorejeshwa, kiasi kilichotumika kwa usimamizi wa pamoja na fedha za marejesho kwa kila Halmashauri.

(b) Serikali kupitia Wakala Mtandao itengeneze mfumo maalum utakaokuwa unatoa taarifa na kuidhinisha malipo ya asilimia 10 kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

(c) TAMISEMI itoe maelekezo ya utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu inayotakiwa kutekelezwa kutokana na fedha za asilimia 40 na 60 zinayotokana na mapato ya ndani ya kila Halmashari.

(d) TAMISEMI iwezeshe Wabunge kushiriki kwenye Kamati za Kisekta katika ngazi ya Halmashauri ili ushauri na usimamizi wa utekelezaji wa mipango na bajeti katika Halmashauri hizo uzingatie nafasi za Wabunge katika maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitarudia, TAMISEMI iwezeshe Wabunge kushiriki kwenye Kamati za Kisekta katika ngazi ya Halmashauri ili ushauri na usimamizi wa utekelezaji wa mipango na bajeti katika Halmashauri hizo uzingatie nafasi za Wabunge katika maeneo yanayohusika. *(Makofi)*

(e) TAMISEMI ifuatilie utekelezaji wa Sera ya Ardhi nchini katika maeneo ya uwekezaji ili kuwezesha mwekezaji kupata

huduma zote muhimu zinazohitajika, kama vile maji, barabara na umeme.

(f) Serikali iwezeshe upatikanaji wa fedha kulingana na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Aidha, utekelezaji wa malengo ya bajeti usimamiwe kama inavyostahili.

(g) Serikali ichukue hatua kali dhidi ya Wakurugenzi na viongozi wote ambao kwa makusudi hawakutekeleza maagizo ya Serikali yaliyopo kwenye bajeti, ikiwemo ujenzi wa vituo vya afya, zahanati na madarasa. Aidha, viongozi waliotekeleza maagizo ya Serikali chini ya kiwango wachukuliwe hatua stahiki. *(Makofi)*

(h) TAMISEMI wapange watumishi kwa uwiano stahiki baina ya maeneo ya mijini na yale ya vijijini au yasiyovutia.

(i) TAMISEMI itumie vyuo vya Serikali kutoa mafunzo kwa watendaji wa ngazi za chini hasa Watendaji wa Kata na Watendaji wa Vijiji.

(j) TAMISEMI iweke utaratibu wa kutoa vipindi vya luninga kwa masomo ambayo hayana walimu wa kutosha.

(k) Serikali itoe mwongozo kuhusu uendeshaji wa shule maalum ili kutoathiri uendeshaji wa shule nyingine kwa kuwa shule hizo ni za kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha ufanyike ukaguzi maalum wa utekelezaji wa miradi iliyopangwa kwenye bajeti za Halmashauri kutokana na vyanzo vya ndani na Halmashauri zinazohusika ni ambazo zimeacha kutumia bajeti zao na badala yake zimetumia fedha za UVIKO kuendeleza miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, kama inavyofahamika Ofisi ya Rais - TAMISEMI ni muhimu katika kuziwezesha Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kuongeza uwezo wa uboreshaji wa huduma kwa wananchi. Kwa kuzingatia hayo Kamati imefanya mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na kuchambua makadirio ya mapato na

matumizi ya TAMISEMI kama nilivyobainisha awali, uchambuzi huo umewezesha maoni na ushauri niliouelezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani, baada ya kufanya hivyo naomba kuwashukuru kwa dhati wajumbe wote wa Kamati ya Bunge, Utawala na Serikali za Mitaa kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya Ofisi hii hadi kukamilika kwa taarifa hii. Kwa kuzingatia ukweli kwamba Kamati hii ndiyo ambayo inashughulikia mafungu mengi ya bajeti yaani mafungu 36 ukilinganisha na kamati nyingine za Bunge na kwa kuzingatia muda mfupi uliotengwa kwa ajili ya uchambuzi, ni wazi wajumbe walilazimika kufanya kazi kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umuhimu wake ningetamani kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa kumtaja jina mmoja mmoja, hata hivyo kwa kuzingatia ufinyu wa muda majina hayo naomba yabaki kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge kama nilivyoomba awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumshukuru sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI Mheshimiwa Innocent Bashungwa kwa ushikiriano mkubwa kwa kamati ambayo umechangia kwa kiasi kikubwa kuwezesha kamati kutekeleza shughuli zake. Aidha, utendaji na Naibu Mawaziri wake wawili Mheshimiwa David Ernest Silinde na Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange, umedhihirisha jinsi walivyohazina kubwa kwa ustawi na maendeleo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini na maendeleo ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru pia kwa watendaji wote Ofisi ya Rais - TAMISEMI chini ya Uongozi wa Katibu Mkuu Profesa Riziki Silas Shemdoe akisaidia na Naibu Katibu Wakuu - Ndugu Gerald Mweli, Dkt. Grace Magembe na Ndugu Sweetbert Mkama kwa ushirikiano wao kwa kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani za Kamati ziwaendee pia Wakuu wa Mikoa yote ya Tanzania Bara, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri zote nchini kwa utekelezaji makini wa bajeti ya mwaka unaoisha na uwasilishaji mzuri wa taarifa ya makadirio ya

mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka ujao wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee naomba nimshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc*, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Bunge Ndugu Gerald Magili, Makatibu wa Kamati Ndugu Angelina Sanga na Ndugu Sikudhani Mbinga, wakisaidiwa na Ndugu Pauline Mavunde kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya taarifa hii kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 MAELEZO YA JUMLA**

**1.1 Utangulizi**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, pamoja na

Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/ 2023.

**Mheshimiwa Spika**, kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge kufuatilia mtiririko wa uwasilishaji wangu, naomba kulijulisha Bunge kwamba, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu zifuatazo:-

(a) Sehemu ya **Kwanza** inayotoa maelezo ya jumla kuonesha msingi, Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

(b) Sehemu ya **Pili** inayoripoti matokeo ya uchambuzi na tathmini kwa kuchanganua utekelezaji wa malengo ya mpango wa Ofisi hii, Ukusanyaji wa Maduhuli, Upatikanaji wa fedha na uzingatiaji wa ushauri wa Kamati;

(c) Sehemu ya **Tatu** inayoripoti Maoni na Ushauri wa Kamati kutokana na uchambuzi; na

(d) Sehemu ya **Nne** na ya mwisho inayohitimisha na kulishauri Bunge kuhusu hoja ya Waziri wa nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

### 1.2 Msingi wa Uchambuzi wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa Kamati kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni Masharti ya Kanuni za Bunge. Kifungu cha 6 (4) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo. Aidha, Kanuni ya 117(4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yaliyotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa na kwamba, naliomba Bunge hili lijadili hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa pamoja na Taarifa hii.

### 1.3 Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi iliyochambuliwa, inagusa jumla ya Mafungu ishirini na nane. Kati ya Mafungu hayo, mafungu mawili

ni Mafungu ya Wizara na Tume ya Utumishi wa Walimu na mafungu mengine ni ya mikoa ishirini na sita.

**SEHEMU YA PILI**

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu Hoja hii ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI. Kwa sababu hiyo, ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa wasilisho hili, naomba kubainisha mambo makuu mawili yaliyochambuliwa. Mambo hayo ni:-

(a) Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022; na

(b) Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

### 2.2 Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022

**Mheshimiwa Spika**, ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Ofisi ya Rais TAMISEMI baada ya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo. Uchambuzi huo ulilenga kujenga msingi wa kufanya ulinganisho na makadirio kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Mambo yaliyochambuliwa ni Ukusanyaji wa maduhuli, Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya kugharimia miradi ya maendeleo na Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Uchanganuzi huo ni kama ifuatavyo:-

#### 2.2.1 Uchambuzi wa Ukusanyaji Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Ofisi ya Rais - TAMISEMI iliidhinishiwa kukusanya jumla ya **Sh. 916,445,409,198.50.** Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Februari, 2022, Ofisi hii ilikuwa

imekusanya jumla ya **Sh. 615,603,870,037.65** ambazo ni asilimia **67.17** ya lengo lililokusudiwa. Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekana katika **Jedwali Na. 01**.

**Jedwali 1: Kiasi cha Fedha kilichokadiriwa kukusanywa na kiasi kilichokusanywa na TAMISEMI na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2021/2022**

| Wizara/ Taasisi /Mikoa | Makadirio ya makusanyo | % jumla kwa wizara | Makusanyo hadi Februari 2022 | % Lengo la taasisi | % Jumla ya makusanyo |
|---|---|---|---|---|---|
| TAMISEMI | 52,366,725,886.50 | 5.7 | 29,420,500,356.65 | 56 | 4.8 |
| TSC | - | - | - | - | - |
| MIKOA | 220,683,312.00 | 0.02 | 113,369,680.00 | 51 | 0.02 |
| MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA | 863,858,000,000 | 94.3 | 586,070,000,000.00 | 67.84 | 95.2 |
| **JUMLA** | **916,445,409,198.50** | | **615,603,870,037.65** | **56.16** | **100** |

**Chanzo**: Randama ya Fungu 56, Fungu 02 na Mafungu ya Mikoa

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa makusanyo ya maduhuli unaonesha kwamba: -

(a) Jumla ya makusanyo ya Maduhuli imefikia asilimia 56.16 ya lengo hadi kufikia Februari, 2022 ikiwa ni ndani ya robo tatu za utekelezaji wa majukumu;

(b) Mwenendo wa makusanyo ya maduhuli ya Mamlaka za Serikali za Mitaa umefikia asilimia 67.84 ya lengo na Mikoa imefika asilimia 51 ya lengo;

(c) Kwa kipindi kilicho baki cha utekelezaji, ni vigumu kufikia lengo kwa kuwa kipindi kilichokwisha katika utekelezaji ni karibu asilimia 75; na

(d) Mikoa na TAMISEMI yenyewe wamekusanya nyuma ya lengo kwa kufika chini ya asilimia 60 ya lengo ndani ya kipindi ambacho ni asilimia 75 ya kipindi cha utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa ukusanyaji wa maduhuli kwenye Mikoa, Taarifa zilionesha kuwa, hadi kufikia mwezi Februari, 2022, mikoa yote kwa pamoja ilifika lengo la makusanyo kwa asilimia 75. Mwenendo huu wa makusanyo unaendana na matarajio na malengo. Aidha, Uchambuzi umeonesha kuwa Mbeya ni Mkoa unaoongoza kufikia lengo kwa kufika asilima 98.04 ya lengo hadi mwezi Februari, 2022. Mikoa mingine miwili iliyofuatia Mbeya kwa kufikia lengo ni Kagera iliyofikia lengo kwa asilima 95 na Ruvuma iliyofikia asilimia 92.67.

**Mheshimiwa Spika,** Mkoa wa mwisho katika kufikia lengo ni mkoa wa Singida uliofika asilimia 60 ya lengo. Hata hivyo katika uwekaji wa lengo la Maduhuli, Mkoa wa Singida haukuwa wa mwisho kwa kuwa uliweka lengo la kukusanya Sh. 16,998,296,912.00 lakini mkoa wa Rukwa uliweka lengo la kukusanya Sh. 9,635,108,000.00 ambalo ni dogo kuliko lengo la mkoa wa Singida.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa uchambuzi huo, ni dhahiri kuwa mwenendo wa makusanyo kwa ujumla si mzuri. Hata hivyo mwenendo wa makusanyo kwa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa unatoa mwelekeo wa kufikia lengo.

### 2.2.2 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Ofisi hii inatekeleza jumla ya miradi 14 ya Fungu 56, mradi 1 Fungu Na. 2 na miradi mingine kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Jumla ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya kugharimia miradi hiyo ni **Sh. 3,840,453,728,770.00** sawa na **asilimia 44.82** ya bajeti ya Ofisi ya Rais TAMESEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu na Mikoa ishirini na sita.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa madhumuni ya kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilitembelea miradi 10 ya Wizara hii. Miradi hiyo ni: -

(a) Mradi wa Ujenzi wa Shule ya Msingi ya Kingereza ya Chief Rocket Mwashinga iliyoko Halmashauri ya Jiji la Mbeya iliyojengwa kwa fedha za Mapato ya ndani;

(b) Mradi wa ufugaji wa kuku wa Kikundi cha Wanawake cha Wafipa Lumbila katika Jiji la Mbeya unaotokana na asilimia kumi ya mapato ya ndani ya Halmashauri;

(c) Mradi wa kikundi cha Jiweze (Watu wenye Ulemavu) kinachojishughulisha na Ushonaji wa nguo, kukamua alizeti na utengenezaji wa viatu kutokana na Mkopo wa asilimia kumi ya mapato ya ndani ya Halmashauri ya Mbeya Vijijini;

(d) Mradi wa kikundi cha Vijana wanaojishughulisha na Usafirishaji wa Abiria kwa kutumia Bajaji (VIWABA) kutokana na Mkopo wa asilimia kumi ya mapato ya ndani ya Halmashauri;

(e) Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya Sangambi unaojengwa kwa kutumia mapato ya Ndani katika Halmashauri ya Chunya;

(f) Mradi wa ujenzi wa Soko la Madini unaojengwa kwa kutumia mapato ya Ndani katika Halmashauri ya Chunya;

(g) Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Masebe - Bugoba - Lutete (Km 7.2) kwa kiwango cha lami unaojengwa na TARURA uliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe na Jiji la Mbeya ;

(h) Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Masebe DSP - Mpuguso TTC - Bugoba Kibaoni Km. 5 kwa Kiwango cha lami unaojengwa na TARURA katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe;

(i) Mradi wa Daraja la Mwasanga lililopo katika Jiji la Mbeya;

(j) Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya Chimala uliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali unaojengwa kwa kutumia mapato ya Ndani;

(k) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Afya Mtwango;

(l) Mradi wa Usagaji Kokoto wa Kikundi cha Vijana Mtwango;

(m) Mradi wa Ufugaji Ng'ombe wa Kikundi cha Kinamama Njombe; na

(n) Mradi wa Duka la Jumla na Rejareja wa Kikundi cha Watu wenye Ulemavu, Njombe.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na miradi hiyo, ipo pia miradi iliyotekelezwa kwa kutumia fedha zilizotolewa na serikali katika mpango wa maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi UVIKO – 19. Ufuatiliaji wa Kamati umeonesha kuwa zipo dalili kwamba, baadhi ya Halmashauri hazikutekeleza miradi iliyopangwa kwenye bajeti zao za Ndani, badala yake zimetumia fedha za UVIKO kuendeleza miradi hiyo. Hali hiyo kwa maoni ya Kamati si jambo linalofaa.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi unaonesha kwamba, kwa ujumla upatikanji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo haukuwa kama ulivyotarajiwa. Hali hiyo, si dalili nzuri kwa utekelezaji bora wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa. Ni maoni ya Kamati kuwa ubora wa miradi utakuwa na maana iwapo utekelezaji wake unakwenda kama ilivyopangwa. Aidha, utekelezaji wa miradi unategemea pamoja na mambo mengine, upatikanaji wa fedha iliyoidhinishwa kwa wakati.

### 2.2.3 Uchambuzi wa Taarifa za Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu pamoja na mikoa ishirini na sita waliidhinishiwa jumla ya Sh. **4,728,008,207,000.00** sawa na asilimia 55.17 kwa matumizi ya kawaida. Hadi kufikia mwezi Februari 2022, kiasi cha fedha zilizopokelewa ni Sh. **3,287,355,817,601.06** sawa na **Asilimia 69.53** ya kiasi kilichoidhinishwa. Mchanganuo wa upokeaji wa fedha unaonekana katika **Jedwali Na. 02**.

**Jedwali 2: Hali ya Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya TAMISEMI, TSC, Mikoa na Serikali za Mitaa**

| a. | TAASISI | MAKADIRIO KWA MWAKA 2021/2022 | KIASI KILICHOPATIKANA HADI MWEZI FEBRUARI, 2022 | ASILIMIA YA MAKADIRIO |
|---|---|---|---|---|
| | TAMISEMI | 68,887,652,000 | 47,010,184,560.33 | 68 |
| | TSC | 14,368,770,000.00 | 9,012,765,307.08 | 56.89 |
| | MIKOA | 128,718,142,000,00 | 93,621,437,994.66 | 72.73 |
| | MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA | 4,516,033,643,000.00 | 3,137,711,429,738.99 | 69.48 |
| | **JUMLA** | **4,728,008,207,000.00** | **3,287,355,817,601.10** | **69.53** |

**Chanzo**: Randama ya Fungu 56, Fungu 02 na Mafungu ya Mikoa

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi unaonesha kwamba:

(a) Mwenendo wa jumla wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida si mbaya. Hata hivyo, Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya uendeshaji wa Tume ya Utumishi wa Walimu hauridhishi. Hadi kufikia mwezi Februari, 2022 Tume hiyo ilipokea kiasi ambacho ni asilimia 56 tu ya bajeti yake ikiwa ni robo tatu za kipindi cha utekelezaji.

(b) Angalau mafungu ya mikoa kwa ujumla wake yaliweza kupokea asilimia 72 ya bajeti yake hadi kufikia mwezi Februari, 2022. Lakini Tume ya Utumishi wa Walimu na Mamlaka za Serikali za Mitaa zilipokea pungufu ya asilimia 72 hadi kufikia mwezi Februari, 2022.

### 2.2.4 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais TAMISEMI, Kamati ilishauri kuhusu mambo mbalimbali. Naomba kulijulisha Bunge hili kuwa, Taarifa ya Mtoa hoja ilionesha kwamba, Serikali imezingatia sehemu kubwa ya Ushauri. Mfano wa Ushauri wa Kamati uliozingatiwa ni kuhusu kusaidia Vikundi vya Wananwake, Vijana na Watu wenye Ulemavu na Halmashauri kubuni vyanzo vipya vya mapato.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa za utekelezaji zilionesha kuwa baadhi ya Halmashauri zimeboresha mikopo kwa Vikundi hivyo. Aidha,

zipo Halmashauri zilizobuni vyanzo vipya vya mapato. Kwa mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ilijenga Soko la Madini ambalo ni chanzo kipya cha mapato yake ya ndani.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na uzingatiaji mzuri wa ushauri, upo ushauri uliotolewa na Kamati ambao unahitaji kufanyiwa kazi na Serikali. Kwa mfano, suala la kuhakikisha Halmashauri zinasimamia vyema mikopo kwa vikundi vya Wananwake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, linahitaji kuboreshwa zaidi.

### 2.3 Makadirio ya Maduhuli na Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu na Mikoa ishirini na sita imekadiria kukusanya maduhuli na bajeti ya matumizi. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kulinganisha na bajeti iliyopita. Uchanganuzi wa Maduhuli na makadirio ya matumizi hayo ni kama ifuatavyo:-

#### 2.3.1 Makadirio ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** Mtoa hoja alieleza kuwa, Jumla ya Sh. **1,071,730,886,508.50** zinakadiriwa kukusanywa na TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu na Mikoa Ishirini na Sita kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kiasi hicho ni ongezeko la asilimia 14.48 ikilinganishwa na lengo la maduhuli kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Mchanganuo wa makadirio hayo unaoneshwa katika **Jedwali Na. 03.**

**Jedwali 3: Mchanganuo wa Makadirio ya TAMISEMI, TSC na Mikoa kuhusu Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ikilinganishwa na mwaka 2021/2022**

| Na | Wizara/ Taasisi /Mikoa | Makadirio ya Maduhuli kwa mwaka 2021/2022 | % Jumla kwa | Makadirio kwa mwaka 2022/2023 | Ongezeko | Ongezeko kwa Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | TAMISEMI | 52,366,725,886.50 | 5.71 | 59,195,516,103.50 | 6,828,790,217.00 | 13.04 |
| 2. | TSC | 0 | 0 | 0 | **0** | **0** |
| 3. | MIKOA | 220,683,312.00 | 0.02 | 249,281,312.00 | 28,598,000.00 | 11.47 |
| 4. | MAMLAKA | 863,858,000,0 | 94. | 1,012,286,089,0 | 148,428,089,0 | 17,18 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | ZA SERIKALI ZA MITAA | 00.00 | 26 | 93.00 | 93.00 | |
| **JUMLA** | | **916,445,409,198.50** | | **1,071,730,886,508.50** | **155,285,477,310.00** | **14.48** |

**Chanzo:** Randama za Fungu 56, Fungu 02 na Randama za Mikoa Ishirini na Sita.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi umeonesha kwamba:

(a) Kwa ujumla makadirio ya Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yameongezeka kwa asilima 14.48 ikilinganishwa na Lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

(b) Kutokana na mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kuonesha kufika asilimia 56.16 ndani ya Robo tatu za kipindi cha utekelezaji, haitakuwa rahisi kufikia lengo la makusanyo linalowekwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ikizingatiwa uzoefu uliopatikana kwa mwaka wa fedha uliotangulia.

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kwamba, uwekaji wa lengo la makusanyo utakuwa na tija iwapo utazingatia uhalisia. Kwa mfano kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Mikoa ilifikia lengo la makusanyo chini ya asilimia 55 katika kipindi cha robo tatu ya muda wa utekelezaji, lakini lengo linalowekwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 limeongezeka kwa asilima 11.49. Ni dhahiri kuwa kama hakuna maelezo ya kutosha kwa lengo la makusanyo linalowekwa, TAMISEMI itakuwa na lengo la maduhuli ambalo halitekelezeki.

**2.3.2 Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023, TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) na Mikoa nishirini na sita wanakadiria matumizi ya kawaida ya Shilingi **5,511,015,193,000.00**. Kiasi hicho ni ongezeko la matumizi kwa asilimia **16.56** ikilinganishwa na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Hali hiyo ililinganishwa na uzoefu wa upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2021/2022 ili kuona uwezekano katika hali halisi. Naomba kulijulisha Bunge kuwa, Kamati ilibaini kuwa iwapo mwenendo wa upatikanji wa fedha utakuwa kama ilivyo kwa

mwaka wa fedha unaoisha, Ukadiriaji huu wa matumzi ya kawaida unaweza kukosa uhalisia.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi umeonesha kuwa katika bajeti ya Mikoa kuna ongezeko la bajeti kwa asilimia 20.65 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2021/2022. Mchanganuo wa Makadirio hayo unaonekana katika **Jedwali Na. 04.**

**Jedwali 4: Mchanganuo wa Makadirio ya Matumizi ya TAMISEMI, TSC, na mikoa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ikilinganishwa na Bajet iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022**

| Na. | TAASISI | MAKADIRIO KWA MWAKA 2021/2022 | MAKADIRIO KWA MWAKA 2022/2023 | ASILIMIA KATIKA ONGEZEKO |
|---|---|---|---|---|
| 1. | TAMISEMI | 68,887,652,000.00 | 78,518,454,000.00 | 13.98 |
| 2. | TSC | 14,368,770,000.00 | 14,984,495,000.00 | 3.58 |
| 3. | MIKOA | 128,718,142,000.00 | 155,304,375,000.00 | 20.65 |
| 4. | MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA | 4,516,033,643,000.00 | 5,262,307,869,000.00 | 16,52 |
| **JUMLA** | | **4,728,008,207,000.00** | **5,511,115,193,000.00** | **16.56** |

**Chanzo:** Randama za Fungu 56, Fungu 02 na Randama za Mikoa Ishirini na Sita

**Mheshimiwa Spika,** Mchanganuo zaidi wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaidia kwa Taasisi zilizo chini ya TAMISEMI unaonesha kuwa TARURA imekadiriwa kutumia kiasi cha Sh. **35,865,840,000/-** sawa na ongezeko la asilimia 14.71 ikilinganishwa na Bajeti ya mwaka 2021/2022. Aidha, Taasisi yenye Bajeti iliyoongezeka kwa kiwango kikubwa zaidi ya nyingie ni DART yenye ongezko la asilimia **16.93**. Mchanganuo huo unaonekana katika **Jedwali Na. 05**

**Jedwali 5: Mchanganuo wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida ya Kawaida kwa Taasisi zilizochini ya Taasisi zilizochini ya**

**TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022**

| Na. | TAASISI | MAKADIRIO KWA MWAKA 2021/2022 | MAKADIRIO KWA MWAKA 2021/2023 | ASILIMIA KATIKA ONGEZEKO |
|---|---|---|---|---|
| | KEC | 10,011,527,000.00 | 10,670,147,000.00 | 6.57 |
| | DART | 2,259,127,000.00 | 2,641,718,000.00 | 16.93 |
| | LGTI | 4,956,471,000.00 | 5,586,231,000.00 | 12.70 |
| | LGLB | 61,952,000.00 | 61,652,000.00 | -0.48 |
| | TARURA | 31,265,784,000.00 | 35,865,840,000.00 | 14.71 |
| | **JUMLA** | **48,554,861,000.00** | **54,825,588,000.00** | 12.91 |

**Chanzo:** Randama za Fungu 56 na Fungu 02

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na uchanganuzi huo, ni wazi kwamba, uendeshaji wa shughuli za TARURA na DART umeongewa msukumo katika bajeti. Hata hivyo, uhalisia wa uzito maalumu uliojitokeza katika makadirio kwa shughuli za Taasisi hizo utaonekana wakati wa utekelezaji. Kamati ina maoni kuwa kukadiria vizuri bajeti ya matumizi hakuna maana sana kama utekelezaji wake hautaendana na mipango iliyopo. Kwa mtazamo huu, ni dhahiri kuwa upo umuhimu wa hatua madhubuti za Serikali kuziwezesha Taasisi hizo kupata fedha kama inavyoidhinishwa na Bunge.

### 2.3.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua makadirio ya jumla ya Sh. **3,266,292,570,200.00** kwa ajili ya kugharimia miradi ya Maendeleo inayopangwa kutekelezwa na TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu na Mikoa ishirini na Sita kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Makadirio hayo ni pungufu kwa asilimia 14.95 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kama inavyooenekana katika **Jedwali Na.06**.

**Jedwali 6: Mchanganuo wa Makadirio ya Bajeti ya Maendeleo itakayotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022**

| Na | TAASISI | MAKADIRIO KWA | MAKADIRIO KWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|

| | | MWAKA 2021/2022 | MWAKA 2022/2023 | KATIKA ONGEZEKO |
|---|---|---|---|---|
| 1. | TAMISEMI | 973,820,371,932.00 | 883,038,931,200.00 | -9.3 |
| 2. | TSC | 500,000,000.00 | 670,000,000.00 | 34 |
| 3. | MIKOA | 114,126,978,614.00 | 84,527,013,000.00 | -25.9 |
| 4. | MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA | 2,752,006,378,224.00 | 2,299,256,626,000.00 | 16.45 |
| **JUMLA** | | **3,840,453,728,770.00** | **3,267,492,570,200.00** | -15.0 |

**Chanzo:** Randama za Fungu 56, Fungu 02 na Randama za Mikoa Ishirini na Sita

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi unaonesha kwamba,
a) Bajeti ya maendeleo kwa Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ujumla imepungua kwa asilimia 15. Punguzo hili lina maana kwamba idadi, thamani na ukubwa wa miradi inayotekelezwa imepungua ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2021/2022.

b) Miradi inayotekelezwa na Mikoa imepungua zaidi kwa asilimia 25.9 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2021/2022.
c) Miradi iliyopungua lakini kwa kiasi kidogo ikilinganishwa na punguzo la mikoa na Tawala za Serikali za Mitaa ni miradi ya TAMISEMI na Tume ya Utumishi wa Walimu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo ni wazi kuwa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa itatekeleza miradi kwa idadi ndogo, thamani ndogo au msisitizo mdogo ikilinganishwa na utekelezaji ulivyokuwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Ni maoni ya Kamati kuwa, utekelezaji wa miradi ya maendeleo nchini unaweza kuwa na matokeo ya moja kwa moja kwa Wananchi iwapo utasimamiwa na Mikoa na Tawala za Serikali za Mitaa zinazohusika.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maelezo

**Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi huo, Kamati inayo maoni ambayo ni msingi wa Ushauri nitakaoueleza. Naomba kutoa maoni hayo kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya fedha za asilimia 10 inayotokana na mapato ya ndani ya Halmashauri yasipowekewa utaratibu mzuri wa ufuatiliaji na usimamizi, hayatatoa tija iliyokusudiwa. Kwa sasa, taarifa za matumizi ya fedha hizo zinatofautiana kwa kiasi cha kuacha mashaka kuhusu uaminifu katika matumizi yake;

(b) Kukosekana kwa Mfumo wa TEHAMA katika usimamizi wa fedha za asilimia 10 kunaweza kuwa chanzo cha ubadhirifu wa fedha hizo;

(c) Ujenzi au ukarabati wa Shule utakuwa na tija zaidi iwapo barabara zinazozifikia Shule hizo zitaboreshwa ili zipitike vizuri. Kwa mfano, Ujenzi wa Shule ya Msingi ya Chief Rocket Mwashinga katika Halmshauri ya Jiji la Mbeya unahitaji juhudi za TARURA kuboresha barabara inayokwenda kwenye shule hiyo;

(d) Ukarabati na Ujenzi wa shule za Umma utakuwa wa manufaa zaidi iwapo utafanyika sambamba na kuhakikisha kuwa shule hizo zinajengewa Uzio kwa kutumia mapato ya ndani ya Halmashauri zinazohusika;

(e) Uhamasishaji mzuri na usimamizi bora wa uendeshaji wa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kwa namna inayofanikisha urejeshaji wa mikopo, unaweza kuongeza uwezo wa Halmashauri kuvisaidia vikundi vingine vyenye sifa, hivyo, kukidhi madhumuni ya mikopo hiyo.

(f) Kuvisaidia vikundi vinavyopatiwa mikopo na Halmashauri nchini kwa kuvipa uwezo na maarifa ya kufanya biashara kwa ufanisi, ni jambo linaloweza kufanikisha azma ya utaratibu wa mikopo hiyo.

(g) Idara ya Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii na Biashara kwenye Halmashauri nchini, zisipotumika kikamilifu kuviwezesha vikundi vinavyopata mikopo, utaratibu wa matumizi ya asilimia 10 ya mapato ya ndani unaweza kukosa tija;

(h) Miradi inayotekelezwa na Halmashauri nchini, ambayo inafaa kuwa na barabara zinazofikika itakuwa na manufaa

makubwa kwa Wananchi iwapo TARURA itapanga ujenzi wa barabara kwa kuipa kipaumbele miradi hiyo;

(i) Ujenzi wa barabara bila kukamilisha uwekaji wa taa na alama za barabarani kutokana na zabuni kutojumisha kazi hizo, unafifisha manufaa ya barabara nyingi zinazojengwa na TARURA;

(j) Ujenzi wa Madaraja yanayounganisha mawasiliano katika maeneo mbalimbali ya vijijini usipozingatia hali ya udongo wa eneo linalohusika, unaweza kuathiri tija ya TARURA kutekeleza baadhi ya miradi;

(k) Utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa vituo vya afya katika Halmashauri nchini usipozingatia ramani na miongozo inayotolewa na TAMISEMI, unaweza kutofautiana kwa kiasi kikubwa na viwango vinayotakiwa. Aidha, kukosekana kwa barabara zinazopitika kwenda kwenye vituo vinavyojengwa kunaweza kukwamisha madhumuni ya vituo hivyo;

(l) Utekelezaji wa miradi ya maendeleo uliokuwa umepangwa katika bajeti za Halmshauri, ni jambo lenye umuhimu kama ilivyo kwa utekelezaji wa miradi chini ya Mpango wa Maendeleo kwa ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO – 19. Kwa umuhimu huo, Ukaguzi maalumu wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Halmshauri kwa utaratibu wa vyanzo vya fedha za ndani ya Halmashauri, unaweza kusaidia udhibiti wa hatari ya matumizi mabaya ya fedha za umma.

## 3.2 Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia maoni yaliyobainishwa, naomba kutoa ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

### 3.2.1 Mikoa

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na Maoni ya Kamati, Ushauri kuhusu Sekretarieti za Mikoa nchini ni kama ifuatavyo:-

(a) Sekretarieti za Mikoa zipange kwa kuzingatia vipaumbele ambavyo vitatekelezeka kwa wakati;

(b) Halmashauri zote katika kila mkoa zielekezwe namna nzuri ya kutumia utaratibu wa "force account" wakati wa kutekeleza miradi ya maendeleo ili kutokununua vifaa vya ujenzi kutoka nje ya Halmashauri zinazohusika;

(c) Halmashauri katika kila mkoa zihimizwe na kusimamiwa ili zizingatie maelekezo na viwango vya ujenzi wa miundombinu; na

(d) Halmashauri zote katika kila mkoa zitafute namna bora ya kuwezesha upatikanaji wa taulo za watoto wa kike.

### 3.2.2 TAMISEMI na Taasisi zake

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu mipango ya TAMISEMI na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Serikali iandae taarifa maalum ya matumizi ya fedha za asilimia 10 inayotokana na mapato ya ndani ya Halmashauri zinazotokana na mapato yasiyolindwa. Taarifa hizo zioneshe kiasi kilichokusanywa tangu mwaka 2018 hadi 2022, kiasi kilichokopeshwa, kiasi kilichorejeshwa, kiasi kilichotumika kwa usimamizi pamoja na fedha za marejesho kwa kila Halmashauri;

(b) Serikali (eGA) itengeneze mfumo maalum utakaokuwa unatoa Taarifa na kuidhinisha malipo ya asilimia 10;

(c) TAMISEMI itoe maelekezo ya utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu inayotakiwa kutekelezwa kutokana na fedha za asilimia 40/60 zinazotokana na mapato ya ndani ya Halmashauri;

(d) TAMISEMI iwezeshe Wabunge kushiriki kwenye Kamati za Kisekta katika ngazi ya Halmashauri ili ushauri na usimamizi wa utekelezaji wa mipango na bajeti katika Halmashauri uzingatie nafasi ya Wabunge katika maeneo yanayohusika;

(e) TAMISEMI ifuatilie utekelezaji wa Sera ya Ardhi nchini katika maeneo ya uwekezaji ili kumwezesha Mwekezaji kupata huduma zote muhimu zinazohitajika, kama vile maji, barabara na umeme;

(f) Serikali iwezeshe upatikanaji wa fedha kulingana na bajeti inayoidhishwa na Bunge. Aidha, Utekelezaji wa malengo ya Bajeti usimamiwe inavyostahili;

(g) Serikali ichukue hatua kali dhidi ya Wakurugenzi na Viongozi wote ambao kwa makusudi hawakutekeleza maagizo ya Serikali yaliyopo kwenye bajeti, ikiwemo ujenzi wa Vituo vya Afya, Zahanati na Madarasa. Aidha, viongozi waliotekeleza maagizo ya Serikali chini ya kiwango, wachukuliwe hatua stahiki;

(h) TAMISEMI wapange Watumishi kwa uwiano stahiki baina ya maneo ya mijini na yale ya Vijijini au yasiyovutia (maeneo ya pembezoni);

(i) TAMISEMI itumie vyuo vya Serikali kutoa mafunzo kwa Watendaji wa ngazi za chini (Watendaji kata na Watendaji wa vijiji);

(j) TAMISEMI iweke utaratibu wa kutoa vipindi vya Luninga kwa masomo ambayo hayana Walimu wa kutosha; na

(k) Serikali itoe mwongozo kuhusu uendeshaji wa Shule Maalum ili kutoathiri uendeshaji wa Shule nyigine kwa kuwa shule hizi ni za kibiashara;

(l) Ufanyike Ukaguzi maalumu wa utekelezaji wa miradi iliyopangwa kwenye bajeti za Halmashauri kutokana na vyanzo vya Ndani. Hamlashauri zinazohusika ni ambazo zimeacha kutumia bajeti zao na badala yake zimetumia fedha za UVIKO kuendeleza miradi hiyo.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Maelezo ya Kuhitimisha

**Mheshimiwa Spika,** kama inavyofahamika, Ofisi ya Rais TAMISEMI ni muhimu katika kuziwezesha Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kuongeza uwezo wa kuboresha huduma kwa Wananchi. Kwa msingi huo, TAMISEMI ni mwezeshaji na mratibu muhimu wa kufanikisha matokeo bora ya utekelezaji wa mipango ya nchi na Ilani ya CCM ya Uchaguzi wa mwaka 2020. Kwa kuzingatia hayo, Kamati imefanya mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na kuchambua makadirio ya Mapato na Matumizi ya TAMISEMI kama nilivyobainisha. Uchambuzi huo umewezesha maoni na ushauri nilioueleza.

**4.2 Shukurani**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kufanya hivyo, naomba kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya ofisi hii hadi kukamilika kwa Taarifa hii. Kwa kuzingatia ukweli kwamba, Kamati hii ndiyo inayoshughulikia mafungu mengi ya bajeti (36) ikilinganishwa na Kamati nyingine za Bunge, na kwa kuzingatia muda mfupi uliotengwa kwa ajili ya uchambuzi, ni wazi Wajumbe walilazimika kufanya kazi kwa muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa umuhimu wake ningetamani kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa kutaja majina yao. Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo: -

1. Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo, Mb – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Dennis Lazaro Londo, Mb – **Makamu Mwenyekiti**
3. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb
4. Mhe.Mwantum Mzamili Zodo, Mb
5. Mhe. Dkt. Thea Medard Ntara, Mb
6. Mhe. Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mb
7. Mhe. Festo Richard Sanga, Mb
8. Mhe. Rehema Juma Migila, Mb
9. Mhe.Mwatum Dau Haji, Mb
10. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb
11. Mhe. Amandus Julius Chinguile, Mb
12. Mhe.Sebastian Simon Kapufi, Mb

13. Mhe. Michael Constatino Mwakamo, Mb
14. Mhe. Lazaro Justin Nyamoga, Mb
15. Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb
16. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb
17. Mhe. Shanif Jamal Mansoor, Mb
18. Mhe. Zacharia Paul Issaay, Mb
19. Mhe. Seif Salum Seif, Mb
20. Mhe. Constantine John Kanyasu, Mb
21. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis, Mb
22. Mhe. Tunza Issa Malapo, Mb
23. Mhe. William Vangimembe Lukuvi, Mb
24. Mhe. Prof. Palamagamba Aidan Mwaluko Kabudi, Mb

**Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kumshukuru sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mhe. Innocent Bashungwa (Mb) kwa ushirikiano mkubwa kwa Kamati ambao umechangia kwa sehemu kubwa kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake. Utendaji wake na Naibu Mawaziri wake, Mhe. David Ernest Silinde (Mb) na Mhe. Dkt. Festo John Dugange (Mb) umedhihirisha jinsi walivyo hazina kubwa kwa ustawi na maendeleo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini na maendeleo ya Taifa hili.

Nawashukuru pia Watendaji wote wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI chini ya uongozi wa Katibu Mkuu Prof. Riziki Silas Shemdoe, akisaidiana na Naibu Makatibu Wakuu, Ndg. Gerald Mweli, Dkt. Grace Maghembe na Sweetbert Mkama kwa ushirikiano wao kwa Kamati.

Shukrani za Kamati ziwaendee pia Wakuu wa Mikoa yote ya Tanzania Bara, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri zote nchini, kwa utekelezaji makini wa Bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha, na uwasilishaji mzuri wa Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka ujao wa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc*; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, *ndc,* Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Bunge Ndg. Gerald Magili; Makatibu wa Kamati Ndg. Angelina Sanga na Ndg. Sikudhani Mbinga, wakisaidiwa na Ndg. Pauline Mavunde, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati

ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii kwa wakati.

Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Abdalla J. Chaurembo (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA UTAWALA**
**NA SERIKALI ZA MITAA**
14 Aprili, 2022

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa kusoma vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuna wachangiaji 17 na kwa mujibu wa Kanuni ya Tano nitaisoma; "5.-(1) Katika kutekeleza majukumu yake yaliliyotajwa katika Ibara ya 84 ya Katiba, Spika ataongozwa na Kanuni hizi na pale ambazo Kanuni hazikutoa mwongozo, basi Spika atafanya kazi kwa kuzingatia Katiba, Sheria nyingine za nchi, Kanuni nyingine zilizopo, maamuzi ya awali ya Maspika wa Bunge, pamoja na mila na desturi za Mabunge mengine yenye utaratibu wa Kibunge unaofanana na utaratibu wa Bunge la Tanzania."

Kwa Kanuni hii nawachangiaji hawa, uchangiaji wetu utakwisha mchana huu na tutajaribu kuwamaliza kabla ya saa nane na baada ya hapo tutaliahirisha Bunge mpaka tarehe na muda ambao tutatangaza hapa kwenye kiti. *(Makofi)*

Tunaanza kuchangia Mheshimiwa Jerry Silaa, jiandae Mheshimiwa Edward Olelekaita, jiandae Mheshimiwa Mtenga, jiandae Mheshimiwa Abdallah Chaurembo.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mezani ya Ofisi ya Rais TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kuipongeza sana Wizara ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kazi nzuri sana wanayoifanya. Nampongeza kaka yangu Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Mbunge kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuiongoza Wizara hii na Naibu Mawaziri wake Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange na Mheshimiwa David Silinde kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa kuwa karibu na Wabunge kwa kutusikiliza na kuwa wanyenyekevu katika kutumikia Taifa letu. Binafsi niwaahidi ushirikiano, vijana wenzetu tupo tutawalinda, tutawatetea katika kutekeleza majukumu yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nimpongeze Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuleta fedha nyingi za maendeleo kupitia kwenye Wizara hii. Tumesikia kwenye Hotuba ya Waziri, fedha zilizokuja za barabara kupitia *TARURA* kila Jimbo tumepata fedha hizi, tunaishukuru na kumpongeza sana Rais. Tumepata pesa za tozo kujenga vituo vya afya, Jimbo la Ukonga tumepata bilioni 1.5, Kituo cha Afya Kipunguni kinajengwa, Kituo cha Afya Majohe na Kituo cha Afya cha Zingiziwa tunaishukuru na kuipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuleta fedha za elimu bila malipo, shilingi bilioni 1.2 kwenye elimu ya msingi na shilingi bilioni 3.84 kwenye elimu ya sekondari kwenye Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam zimepokelewa, tunaishukuru na kuipongeza Serikali. Ujenzi wa zile shule za kimkakati kwenye Mradi wa *SEQUIP* fedha zimeanza kupokelewa na kule Jimbo la Ukonga shule itajengwa kwenye Kata ya Mbondole na kuna mpango mwingine wa shule nyingine kwenye Kata ya Kitunda, tunaishukuru sana Serikali.

Naomba Serikali, niiombe sana tuendelee kutenga fedha hasa za barabara kwenye majimbo yote lakini kwenye Jimbo la Ukonga tunaomba sana Serikali, uendelezaji wa mradi wa *DMDP* awamu ya pili ambacho ndiyo kilio kikubwa cha wananchi wengi wa Jimbo la Ukonga na Mkoa wa Dar es Salaam kama wenzetu

tulivyosikia hapa kwenye hotuba ya Waziri, mradi wa *TACTIC* ambao ni uendelezaji wa mradi wa *Tanzania Strategic City Project* ambao umeanza, tunaiombe Serikali ijitahidi kuongeza kasi ya mazungumzo na Benki ya Dunia ili Mradi wa *DMDP* awamu ya pili na wenyewe uweze kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Dar es Salaam na kule Jimbo la Ukonga pamoja na fedha hizi za *TARURA* zilizoletwa na Mheshimiwa Rais, Wabunge wengi hapa alivyotambulishwa *Engineer* Seif wamepiga makofi kutokana na fedha zile kupokelewa kwenye majimbo karibia yote nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuiombe sana Serikali barabara nyingi za Dar es Salaam kile kigezo cha *traffic density,* cha wingi wa magari yanayotumia barabara kimezidi yale magari 400 ya kujenga barabara kwa kiwango cha changarawe na kiukubwa ni kujenga barabara kwa kiwango cha lami. Barabara za Pugu - Majohe, barabara za Banana - Kitunda - Kivule tunategemea kwenye mradi huu wa *DMDP* tukipata fedha zitajengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la barabara niombe mambo mawili; jambo la kwanza niiombe sana Serikali inapogawa fedha hizi basi vigezo vya kitaalam vya wenzetu vya *TARURA* vizingatiwe. Majimbo mengi yanatofautiana urefu wa kilometa za barabara, majimbo mengi yanatofautiana changamoto za ujenzi wa vivuko na madaraja. Nikuombe radhi hata humu Bungeni kwako ikitokea unagawa huduma yoyote ya mpango ya uzazi salama hauwezi Bi. Asha Mshua ukamuweka kundi moja na Ng'wasi Kamani, lazima utaweka kwa vigezo vyao na umri wao kutokana na hali halisi ya mazingira ya uzazi salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe sana kwenye mgao wa fedha hizi ombi la pili na wenzetu wa Zanzibar kwa mahusiano mazuri ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mnapogawa fedha hizi za barabara, basi kama tulivyofanya kwenye fedha za UVIKO na wenzetu wa majimbo ya Zanzibar nao muangalie jinsi ya kuweza

kuwafikishia fedha za barabara ili kuwe na usawa wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nizungumzie *system* za *structures* za Serikali za Mitaa, leo hapa tumeombwa zaidi ya trilioni 4.6 kama mishahara kwenye Serikali za Mitaa kwa jumla ya watumishi zaidi 319,000, tumeombwa fedha za maendeleo zaidi ya shilingi trilioni 3.26 ambazo zinaenda kutekelezwa kwenye Serikali za Mitaa. Lakini Serikali za Mitaa zimeundwa kwa mujibu wa Katiba, zinapata mamlaka yake kwenye Ibara ya sita, Ibara ya nane, Ibara ya 145 na Ibara ya 146 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wananchi wa Tanzania wenyewe ndiyo wameamua kwenda kutengeneza Serikali za kusimamia maendeleo yao. Fedha hizi zinaenda kule chini kuna Wenyeviti wa Vijiji, kuna Wenyeviti wa Mitaa, kuna Waheshimiwa Madiwani, tujiulize swali moja la msingi je, mifumo na miundo ya Halmashauri hizi inawapa mamlaka ya kutosha ya kusimamia uwezo wa miradi hii ya maendeleo? Halmashauri hizi zinawezeshwa na watendaji hawa kwenda kusimamia watumishi hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi kubwa inapaswa kufanyika, kazi ya kwanza kwenye miundo. Muundo wa Halmashauri zetu tukitoka hapo nje getini ukamtafuta Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa kama ana ufahamu wa bajeti hii inayosomwa na Waziri, nadhani majibu yake utayapata. Kuna kazi kubwa ya kurekebisha muundo wa Halmashauri, ili Waheshimiwa Madiwani wapate fursa ya kujadili bajeti hizi kwa kina kabla hazijafika hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwenye Halmashauri imekuwa ni desturi ya bajeti hizi kupita kwa kasi na kuwa na haraka ya kupita yale malengo ya *Regional Secretariat* na kuleta Bungeni.

Mhshimiwa Naibu Spika, lakini la pili; je, Wenyeviti wa Mitaa, Vijiji na Vitongoji; je, Waheshimiwa Madiwani wanapata mafunzo ya kutosha ya kuweza kusimamia rasilimali fedha na rasilimali watu kule kwenye Halmashauri zetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la tatu niipongeze Serikali toka mwaka fedha uliopita imeanza kulipa posho za

Madiwani. Lakini je, posho hizi zinatosha? Je, posho za Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji zinatosha? Hivi kweli Mwenyekiti wa Mtaa analipwa posho ya shilingi 100,000 kwa mwezi, ataacha kuwa-*charge* wananchi gharama za kuandika barua ofisini? Ataweza kweli kusimamia maendeleo kwenye eneo lake?

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme ifike wakati Serikali itengeneze muundo mzuri wa kuwawezesha kimuundo, kimafunzo, lakini kimaslahi viongozi wetu hawa wa Mitaa, Vijiji na Vitongoji na Waheshimiwa Madiwani waweze kusimamia majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni Halmshauri zenyewe Serikali kuzitendea haki. Mwaka 2019/2020 kodi ya majengo *(property tax)* ilikuwa inakusanywa na Halmashauri zetu; na pale Halmashauri nyingi za Dar es Salaam tulikusanya shilingi bilioni tisa, lakini mwaka 2021zilipelekwa *TRA*. Fedha hizi hazikukusanywa wala hazikuletwa kwenye Halmashauri kuja kutekeleza majukumu yetu. Mwaka 2021/2022 zimepelekwa kwenye LUKU, sijui hii mwaka 2022/2023 mtazileta wapi? Niiombe sana Serikali tuziwezeshe Halmashauri zetu, tuzipe mamlaka ya kukusanya mapato yake, zitengenezewe malengo na zisimamiwe kuweza kutekeleza majukumu kwa wananchi wake. Hata hao Wenyeviti wa Mitaa, Wenyeviti wa Vijiji, Waheshimiwa Madiwani, wawekewe malengo ya kukusanya mapato, kuwe na sera ya *retention* ili waweze kuendesha shughuli zao kwenye ofisi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Mtaa inapokuwa na *retention* ya kodi ya majengo haitam-*charge* mwananchi barua ya dhamana kulipia kwenda kumtoa ndugu yake aliyekuwa na matatizo mahakamani. Watakuwa na uwezo wa kujiendesha, kutoa mafunzo kwa wananchi wao, hata kusimamia vikundi vya kina mama na vijana na walemavu wanaopata mikopo ya Halmashauri hata kuwaandikia katiba, kuwasajilia vikundi; na huu uwezeshaji wa wananchi utafika kwenye maeneo ya mitaa, vijiji na vitongoji na Waheshimiwa Madiwani leo watakuwa na uwezo wa kusimamia halmashauri zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuheshimi muda na kwa wachangiaji waliopo leo, naomba niseme naunga mkono hoja

iliyowekwa mezani na Waziri wa Nchi, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, namuita Mheshimiwa Edward Olelekaita, ajiandae Mheshimiwa Mtenga, Mheshimiwa Chaurembo na ajiandae Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii na kabla ya yote kabisa nimpongeze sana Mama yetu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa aliyofanya kwa mwaka mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru pia Makamu wa Rais, Dkt. Isdor Mpango na Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa kwa kuendelea kumsaidia Rais wetu kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nimshukuru sana Waziri wa TAMISEMI na timu yake yote kwa hotuba nzuri sana. Nimshukuru vilevile jirani yangu hapa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge na Makamu wake na timu yote na Kamati yote ile kwa kuendelea kuwakilisha Bunge vizuri kusimamia TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiteto peke yake kwa mwaka huu uliopita, tumepata miradi ya zaidi ya shilingi bilioni saba hongereni sana. Wananchi wa Kiteto wamepanga na wameniomba nije niwashukuru sana kwa miradi na heshima kubwa mliyoijengea Kiteto. Madarasa ya shule shikizi peke yake ni shilingi 1,140,000,000 tumejenga madarasa 57; madarasa ya sekondari madarasa 44, shilingi milioni 880; vituo vya afya bilioni moja, vituo viwili vya afya vya tarafa zile na sisi tumepanga, nimeongea Mkurugenzi wangu asubuhi hii. Sisi tutamaliza hiyo kazi tarehe 20 Mei, mwezi mmoja kabla ambao mmetuwekea na nakukaribisha sana Mheshimiwa Waziri ututembelee ili vituo vile vingine vitatu vya tarafa tulivyokubaliana, hapa tulishakubaliana tujenge kwenye tarafa zote, Tarafa ya Makame, Dosidosi na Kibaya. Kwa hiyo, sisi sasa tunawadai tatu tu na kwa kweli kwa *speed* tunayokwenda nayo na nakualika Mheshimiwa Waziri uje uone ili mtupatie hizo fedha zingine tumalize biashara ya Tarafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata fedha shilingi 1,500,000,000 kwa *TARURA* tunawashukuru sana. Na namshukuru sana kumuona *Engineer* Seif hapa, nimualike atembelee Kiteto. Kiteto ni jimbo kubwa sana ni kubwa kuliko Mkoa wa Kilimanjaro na tuna Meneja pale mzuri sana, shida yetu ni gari. *Terrain* ya Kiteto, jiografia na umbali wake, kwa kweli mtuletee *Landcruiser* moja nzuri sana ili kazi hii iendelee kufanyika vizuri zaidi. Namualika vilevile Mkurugenzi Mkuu wa *TARURA* atembelee Kiteto, karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tumepata shule za sekondari mbili mpya shilingi 1,200,000,000 na kazi zinaendelea. Bado sasa na kama kata nne hivi hazina sekondari na kwa kuwa tulishapanga tujenge sekondari kwa kata zote; tukiendelea na kasi hii Kata za Makame, Leseri, Lolela na Ndiligish na uzuri Mwenyekiti wangu wa Halmashauri yupo hapa juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaushauri sana ambao nilishakuutoa siku nyingi kidogo; ipo miradi, miradi ya wananchi ambayo imejengwa na nguvu za wananchi na niitumie nafasi hii kuwapongeza sana wananchi Kiteto. Mheshimiwa Waziri nipo na karatasi hapa miradi zaidi ya 119 ipo kwenye *stage* mbalimbali ambazo zimejengwa na nguvu za wananchi. Wakati tunapata fedha za UVIKO-19 tulitamani zile fedha zingemalizia miradi ile iliyojengwa na wananchi, lakini kutokana na masharti ya fedha za UVIKO tulimuelewa sana aliyekuwa Waziri wa TAMISEMI kwamba kwa sababu ya masharti tusingeweza kumalizia majengo yale. Lakini kwa kweli kwa juhudi hii iliyooneshwa na wananchi madarasa tu peke yake kwa mfano tu Kiteto tuna miradi 80 inaendelea kwenye vijiji 50 kati ya vijiji 63 vya Wilaya ya Kiteto. Lakini kwenye miradi ya shule shikizi bado tuna uhitaji wa madarasa 26. Lakini kwa zahanati 13 hizi nguvu za wananchi wa Kiteto kwa kweli zina-*deserve* Serikali iwaunge mkono, kwani tulishatoa ushauri Mheshimiwa Waziri *I am sure* kwa kweli m-*consider* hizi nguvu za wananchi ili wananchi waendelee kupata ari ya kuchangia miradi kwa kweli tutafarijika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni la watumishi; ripoti ya CAG inaniambia Kiteto tuna upungufu wa watumishi 651. Sasa

watumishi wakipungua kwa kweli ufanisi wa kazi utapungua nao zaidi. Kwa hiyo, naomba na ninafurahi sana kuona kwamba Waziri wa Utumishi ametoa ajira zile na ametoa *breakdown* kwamba walimu nafasi 12,000, afya 10,000, kilimo 814, mifugo 700, uvuvi 204, maji 261, sheria 53; tunachowaomba ajira hizi zinavyotoka mtumia *formula* mliyotumia wakati mnagawa fedha za Uviko, wote tupate. Heshima mliyowajengea Wabunge kwa fedha kwa hizi za UVIKO-19 mkifuata *formula* hii *wallah* nawaambia wale wanaotaka majimbo haya watapata taabu sana huko mbele kwa sababu mtakuwa mmewajengea heshima Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile maslahi ya watumishi, yakiangaliwa yanaongeza ufanisi zaidi. Na wameyazungumza Waheshimiwa Mabunge hapa kuhusu maslahi ya Madiwani kwa kweli Madiwani wetu wanafanya kazi nzuri zaidi. Tuwaangalie namna ya kuboresha maslahi yao. Lakini vilevile Wenyeviti wa Vijiji na Wenyeviti wa Mitaa wanafanya kazi kubwa sana tuwaangalie namna ya kuwasaidia ili kujenga ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini walikwisha kusema wengine hapa, tukiwapa uwezo, tukitengeneza zile semina za kuwajengea uwezo Madiwani na Wenyeviti, itaongeza ufanisi zaidi katika kusimamia miradi. Kwa hiyo, zile semina za kuongeza uwezo zitasaidia sana msiziache. Kwa kweli Madiwani wetu wangekuwa wanapata *from time-to-time* wapate semina kama hizo itaongeza ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni la *TARURA;* nawashukuru sana kwa kuongeza fedha kwa *TARURA,* lakini ni kweli Ilani ya Chama cha Mapinduzi tulishasema hivyo, tunataka tuongeze fedha nyingi zaidi najua mmeongeza fedha karibu bilioni 100 tena nawapongeza sana. Tunataka fedha za *TARURA* ziendelee kuwa nyingi zaidi ili barabara za vijijini na mijini zikapate kufunguka; barabara zitaongeza kasi ya uzalishaji. Kwa hiyo, kwa kweli endeleeni kuangalia *TARURA* kila wakati ikipatikana fedha muongeze fedha kwa ajili ya *TARURA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna majengo haya ya Halmashauri; Kiteto tunajengo la Halmashauri ambalo sasa

linaendelea kwa muda mrefu kidogo na kuna fedha karibu milioni kama 400 hivi bado; na mkandarasi anasema kwa kuwa malipo yamechukua muda mrefu kidogo tangu mwaka 2016 anaanza kufikiri kwamba zile fedha ni kidogo. Kwa hiyo, nawaombeni sana, hii miradi mkitoa fedha kwa utaratibu ili zisichelewe mtatuepusha sisi na matatizo ya huko ya kuanza kugombana na wakandarasi. Kwa hiyo, mkitugawia milioni 400 hiyo lile jengo tulimalizie kwa sababu mmeshatumia fedha nyingi sana na tunawashukuru sana. Kwa hiyo, nakukumbusha Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nyingine, kwenye ajira hizi hasa za walimu muangalie sana namna ya kuwajali walimu ambao wamekuwa wakijitolea kwa miaka mingi kidogo; hiyo iwe *criteria* kabisa namba moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wetu ambao wamemaliza elimu zao na wakaona wasikae bure nyumbani waendelee kutusaidia wanafanya kazi kubwa sana. Mkiweka hiyo kama *criteria* wale wote ambao wana-*volunteer* na wanaendelea kutufundishia watoto wetu hiyo iwe *criteria* namba moja. Mheshimiwa Waziri usikubali kabisa kumuacha mwalimu ambaye ana *record* ya kuendelea ku-*volunteer,* mkifanya hivyo mtakuwa mmetenda kazi nzuri sana; na tuangalie wafanyakazi wetu wote wanao-*volunteer* kwenye sekta fulani fulani kila mtu anaye-*volunteer* nia yake ikitokea kanafasi basi apewe *priority*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli baada ya kusema haya, mimi nakushukuru sana naunga mkono TAMISEMI mtakijengea heshima Chama cha Mapinduzi kwa sababu ukisoma ilani...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa mchango mzuri.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nakushukuru sana naunga mkono hoja ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtenga, jiandae Mheshimiwa Chaurembo na Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini mimi niungane na wenzangu kumshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya na hasa anavyotusikiliza Wabunge tunavyokuwa kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano na vilio vyetu huwa anavisikia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niende nimshukuru Mheshimiwa Waziri, Ndugu yangu Innocent, kwa kweli Waziri huyu sijui niseme nini kwenye Bunge lako hili tukufu. Ni kijana msikivu, lakini ni kijana ambaye anaelewa matatizo ya kila Mbunge kwenye jimbo lake, ni kijana ambaye simu yake saa 6, saa 8 za usiku anakupokelea simu; kwa hiyo, tumpongeze sana na Mungu ambariki. Lakini vilevile wasaidizi wake wamekuwa ni marafiki sana kwa Wabunge wote wawili, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nishukuru katika jimbo langu nimepata shilingi milioni 440 za madarasa ya sekondari, naishukuru sana Serikali, namshukuru Mheshimiwa Rais. Lakini nashukuru nimepata shilingi milioni 260 kwa kituo cha afya pale Kata ya Ufukoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka nianzie kwa kituo cha afya. Kituo hiki cha Afya ili kikamilike kinahitaji lazima tuwe na jiko ambalo linawezekana likawepo pale lakini tuwe na eneo la kufulia nguo, *ambulance,* sasa tayari kile kituo kimekamilika lakini wauguzi bado hatujawapata. Kwa hiyo, niombe tunapoelekea kwenye kutekeleza haya mambo adimu kwa wananchi, huduma za wananchi tunapozimaliza kwenye majengo twende kwenye huduma nyingine ya watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, Jimbo la Mtwara Mjini tulikuwa tuna mradi wa kufunga taa barabarani; na mradi huu ulikuwa mwaka 2017/2018. Lakini kwenye bajeti ya mkandarasi ya malipo kwenye mradi huu ilielekezwa apewe shilingi 1,065,000,000, lakini kwa sintofaham Mkurugenzi na watumishi wengine ambao wana uwezo au wana mamlaka ya kulipa fedha hizo walilipa fedha 1,653,000,000; kuna fedha karibu milioni 588 ambazo zimelipwa nje ya mkataba. Fedha hizi ni fedha

za wananchi, na *CAG* alishaelekeza fedha hizi zirudishwe lakini mpaka leo ninapozungumza fedha hizi zipo mikononi kwa watu na hakuna hatua yoyote ambayo imechukuliwa mpaka sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niishukuru Serikali hasa kupitia *TARURA*, lakini nataka nitoe angalizo au nitoe ushauri majimbo yapo tofauti, Jimbo la Mtwara Mjini huwezi kulinganisha na Jimbo la Nanyamba, Jimbo la Mtwara Mjini huwezi kulilinganisha na Jimbo la Kilombero, haya majimbo yapo tofauti. Lakini tunaingia kwenye migao ya fedha tunasema kwenye *package* ya migao ya kila jimbo *TARURA* tupeleke labda shilingi 1,500,000,000 au tupeleke shilingi bilioni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo manispaa, zinakusanya almost zaidi ya shilingi bilioni 60 kwa mwaka na zipo Halmashauri hazina uwezo wa kukusanya hata shilingi milioni 200 kwa mwaka. Kwa hili mimi nilikuwa naiomba Wizara twendani tuangalie kwenye mazingira haya kama tunataka kuziinua hizi Halmashauri na manispaa basi tuangalie ni manispaa gani, Halmashauri gani ambayo ipo chini sana ili tuweze kuzisaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu ya mradi ya *TACTIC* wenzangu wamezungumza, miradi hii inatakiwa iende na wakati. Jimbo la kwangu Mtwara Mjini, ikinyesha mvua leo hapa Bungeni mimi nakuwa na wasiwasi, nitapigiwa simu ngapi mafuriko! Mradi huu tunauomba uende kwa wakati kwa sababu toka tumesikia mradi huu zaidi ya miaka miwili, kila siku mazungumzo yanafanyika. Ni mazungumzo yapi yasiyokwisha? Kwa hiyo, nikuombe mtusaidie kwa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna jambo la Madiwani, tulikaa kwenye Bunge letu hili hapa tukaelekeza kwamba tufike mahala kwamba Serikali Kuu mishahara yao ipitie kwenye Serikali Kuu. Lakini pamoja na hizi posho ambazo zinapita kupitia kwenye Serikali Kuu, hali ya Madiwani ni mbaya, ni mbaya. Hali ya Madiwani kwa kweli inapelekea Diwani anashinda kwenye Halmashauri utafikiri yeye labda ni mtumishi pale; sasa kwa namna moja ama nyingine Diwani huyu hawezi kwenda kuhoja chochote chenye maslahi ya wananchi kwenye eneo husika. Hili

mimi naomba tuliangalie sana, Madiwani hawa waongezewe posho, wanafanyakazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nishukuru kwa Hospitali ya Rufaa pale Mtwara Mjini. Nataka niombe kwa ridhaa yako nilizungumzie hili, hospitali imejengwa pale, lakini leo tukihitaji huduma ya simu kwenye jengo lile huduma ya simu haipatikani. Lakini unapozungumza na wahusika wanakueleza kwamba mkitaka kupata mnara basi mamlaka zinazohusika zaidi ya miezi sita watoe kibali. Jamani tupo nchi gani? Kibali cha mnara mmoja kinachukua takribani miezi sita! Hivi leo tupo pale tunataka sasa tufungue ile hospitali yetu, kuna wagonjwa, Hospitali ya Rufaa itaunganisha na mkoa mmoja wa Mtwara, Lindi na Ruvuma; mtu yupo Ruvuma anataka kujua mgonjwa wake anaendeleaje tunampataje? Hebu sasa kwenye huduma hizi nikuombe tufike mahali sasa tujiwekeze kwenye mambo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumejenga shule na tunaishukuru sana Serikali na iendelee kutusaidia kwenye majimbo yetu. Shule hizi tayari zimeshajengwa, lakini walimu kwenye shule hizi hakuna, majengo yale yapo lakini walimu hawapo. Kwa hiyo, Serikali ichukue hatua za kila aina tuweze kupatiwa walimu kwenye haya madarasa mapya ambayo tumejenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye Jimbo la Mtwara Mjini sisi tunatofauti ya walimu shule za msingi tunataka tusaidiwe walimu zaidi ya 200 katika shule zetu za msingi. Lakini shule za sekondari katika Jimbo zima tunahitaji tupate zaidi ya walimu 300. Kwa uwiano huu mnaouona je, tuna elimu kabisa ambayo inawezekana mbadala wake watu wakapata elimu sahihi? Kwa hiyo, nilikuwa ninaliomba hilo ili tusaidiwe na sisi inawezekana tukafika mahali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hili ni janga ambalo nataka nilizungumze wako wakandarasi wanapewa na *TARURA* kwenye maeneo yetu; na sielewi kwenye hii mikataba ni sheria gani ambazo zinatumika. Mkandarasi anashinda *tender,* anaposhinda *tender* kabla hajaingia *site* anawezekana akapewa *period* yake, labda ndani ya wiki mbili kwa mujibu wa sheria au mwezi mmoja

haingii *site*. Lakini inafika takribani mpaka miezi minne, miezi mitano mpaka miezi sita mkandarasi hajaingia *site*, lakini tayari *TARURA* wameshampatia mkandarasi asilimia fulani ya mradi ule. Matokeo yake wanatuambia bwana mkandarasi ameshindwa kutengeneza barabara, lakini katika fedha ambazo tumeshampatia nadhani ana-*insurance bank* yatalipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo ni kweli tumefikia hapa na kama sheria zipo hivyo kwa nini tusiingie hapa tukabadilisha hizo sheria? Kwa hiyo, nataka nikuambie haya mambo yanafanyika na kwenye Jimbo langu ndio mchezo ambao unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niwashukuru sana Mameneja wa *TARURA* pale wa Wilaya na ninamshukuru kwa sababu amekuwa ni mtu ambaye anapambana sana na wakandarasi na shida ipo. Kwamba, leo mkandarasi anatoka anakotoka yeye…*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante ya pili, hiyo mengine andika.

Mheshimiwa Chaurembo, jiandae Mheshimiwa Sanga, jiandae Mheshimiwa Kanyasu. *(Makofi)*

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia, lakini leo mchango wangu utaongozwa sana na maneno ya dini. Mtume wetu Muhammad Swalallahu Allah Wasalaam amesema; "*Lamiyashukurillaha Mallam yashukurunasi*" hatopatikana mtu atakayemshukuru Mungu wakati hataki kuwashukuru watu. Lakini vilevile, kwenye Zaburi 138:1 inasema; "Nitashukuru kwa moyo wangu wote na mbele ya Mungu nitakuimbia Zaburi". *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeanza na maneno haya ya dini kwa maana, ni vyema tumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri na kubwa anayoifanya. Mwaka jana wakati kama huu nilizungumza sana kuhusiana na vilio mbalimbali katika sekta ya elimu, afya na barabara katika Jimbo langu la Mbagala. Lakini

hapa ninapozungumza matatizo mengi yameenda kutatuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano katika elimu msingi, shule tatu mpya zimejengwa katika Jimbo la Mbagala, yYamejengwa madarasa katika shule zilizopo zaidi ya madarasa 50, kwenye sekondari fedha za UVIKO nimepata madarasa 87, lakini mapato ya ndani tumejenga shule mpya mbili za sekondari na vilevile fedha zilizoletwa katika shule maalum nimeletewa fedha kwa ajili ya kujenga shule katika kata zisizokuwa na sekodnari. Sasa naogopa nisije nikaendelea kumshukuru Mungu bila kuwashukuru watu hawa ambao wamewezesha mambo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye afya; sasa hivi hapa ninapozungumza kule Mbagala umeme ukikatika ukirudi tunasema huooo, sasa hivi kule Mbagala kila dakika tunasema hizooo fedha za Rais. Sasa hivi hapa wananchi wangu wananiambia hizooo shilingi bilioni mbili za kujenga Hospitali ya Wilaya zimeingia jana. Wananchi wa Mbagala wana kila namna ya kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa maana jana peke yake tumepata shilingi bilioni mbili za kujenga Hospitali ya Wilaya pale Mbagala Zakhiem ambayo ilikuwa ina msongamano mkubwa sana na mwaka jana nililizungumza hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo vya afya; ndani ya Jimbo langu kwa mwaka huu mmoja vituo vitatu vya afya vinajengwa ambavyo vina thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 1.5; zahanati kila kata sasa hivi tunakwenda kuwa na zahanati ambayo tunakoelekea sasa, tunaelekea kwa kila Mtaa nina kila sababu ya kuendelea kumshukuru Rais wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Nabu Spika, kuhusu barabara za *TARURA* tumepata fedha nyingi za kutengeneza barabara zetu za *TARURA*. Lakini ombi ambalo limebaki kwa wananchi wa Jimbo la Mbagala upande wa *TARURA* na Serikali kwa ujumla, tunao ule mradi wa uboreshaji wa Jiji la Dar es Salaam awamu ya pili. Tunaiomba sana Serikali kilio chetu kikubwa sasa hivi Dar es Salaam hasa Temeke na Jimbo langu la Mbagala katika Kata za Chamazi, Charambe, Mianzini, Kiburugwa, Kibondemaji, Kilungule,

Mbagala Kuu, Kijichi, Mbagala pamoja na Toangoma tatizo letu kubwa sasa hivi ni barabara. *(Makofi)*

Kwa hiyo, niombe sana ule mradi unaotokana na uboreshaji wa Jiji la Dar es Salaam awamu ya pili, uharakishwe ili matatizo ya watu wa Mbagala yaende kuwa historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie utekelezaji wa miradi hii yote ambayo Mheshimiwa Rais ameileta. Niwashukuru sana kuanzia Wenyeviti wa Mitaa, Waheshimiwa Madiwani, Watendaji wa Halmashauri, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya pamoja na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa. Kazi nzuri wameifanya katika kusimamia miradi hii na ndio maana leo hii tunasimama kifua mbele kusifia miradi imefanyika vizuri.

Sasa hapa ombi langu Wenyeviti wa Mitaa wanafanya kazi kubwa na nzuri sana, sasa hivi kila jambo unalolitaka, lazima upige simu kwa Diwani au Mwenyekiti wa Mtaa akuelezee uhalisia wa maeneo hayo. Nitakupa mfano wakati tunapata fedha za kujenga vituo vya afya kwa haraka haraka ilionekana maeneo ya kujenga hakuna, lakini tulipowapigia simu Madiwani na Wenyeviti wa Mitaa wametuonesha maeneo mengi ambayo yametengwa na Serikali kwa ajili ya huduma za jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuone tayari ni namna gani watu hawa walivyokuwa muhimu, lakini tuangalie na maslahi ambayo wanayapata. Nikuombe sana Wenyeviti hawa wa Serikali za Mitaa tutengeneze mazingira mazuri ya kuweza kupata maslahi yao hasa posho. Ninaamini Mheshimiwa Waziri hapa anasikia na anaweza akatoa maelekezo huko baadaye, kuhakikisha Wenyeviti hawa wa Mitaa walau tunawaongezea *morale* ya kufanya kazi. Anuani za makazi hizi tunazozishughulikia sasa hivi ambao wako mstari wa mbele ni Wenyeviti wa Mitaa pamoja na Madiwani. Sasa niombe sana Wenyeviti wa Mitaa, Wenyeviti wa Vijiji nao waone namna ambayo tunaweza tukawaongeza maslahi yao ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa Madiwani; mimi nilikuwa Diwani, ili tuwe na Madiwani wazuri ni lazima pia tuangalie maslahi yao. Tumeanza Udiwani tukiwa tunalipwa shilingi 120,000 lakini sasa hivi imefika shilingi 350,000; ndugu zangu kutokana na hali halisi ya maisha ya sasa hivi bado ni fedha ndogo sana. Tuwaombee Madiwani hawa waongezewe fedha ili nao waweze kusimamia vizuri miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa NaibU Spika, nimalizie, tuna suala zima la kujifunza Madiwani, tuombe TAMISEMI ielekeze Mikoa, Madiwani pale ambapo Halmashauri zao zina fursa za kutosha wapewe nafasi ya kwenda kujifunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi hapa Dodoma inatengenezwa *open market* kwa ajili ya wamachinga. Kule Dar es Salaam tuna tatizo kubwa sana la wamachinga, ni wakati muafaka sasa Madiwani wa maeneo tofauti tofauti, wakaenda maeneo mbalimbali kujifunza ili mradi waone namna wenzao wanavyofanikisha mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini hili Mheshimiwa Waziri atalitolea maelezo ili mradi tu kama fedha wametenga kwenye bajeti zao na fedha wanazo, sioni kwa nini wawe na vikwazo vya kupewa ruhusa ya kwenda kujifunza katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante na Mheshimiwa Waziri hongera sana kwa mpango wa machinga Dodoma, wewe na wenzako mnafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Festo Sanga, ajiandae Mheshimiwa Kanyasu, ajiandae Mheshimiwa Leah Komanya. *(Makofi)*

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia, lakini nimpe hongera sana na pongezi nyingi sana Mheshimiwa Rais Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi nyingi ambazo anazifanya Makete, lakini

Mheshimiwa Waziri kaka yangu Innocent Bashungwa ni mmoja ya Mawaziri ambao sisi vijana tunajivunia sana kwa jinsi ambavyo anatusikiliza na anatupa nafasi kwenye wakati tofauti tofauti ambapo tunakuwa na matatizo, lakini pia Naibu Mawaziri wake wote wanatupa ushirikiano mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nimpongeze sana Mkuu wangu wa Wilaya Ndugu Juma Sweda anafanya kazi nzuri sana, Mkurugenzi wangu Ndugu William Makufu anafanya kazi nzuri sana kule Makete, lakini na Watendaji wote wa Halmashauri wanatupa ushirikiano mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Serikali hii sisi wana Makete tunaipongeza kwa sababu kuna mambo ambayo yamefanyika kwa muda ambao Halmashauri ya Makete ilikuwepo haya mambo hayakufanyika. Mimi nimeingia nikiwa Mbunge wa Makete tulikuwa na vituo vitatu tu vya afya, ninavyozungumza leo tumejengewa vituo vitatu vingine vya afya vya shilingi bilioni 1.5. Lakini tuna kata ambazo zilikuwa hazina shule Kata ya Bulongwa, Kata ya Mlondwe na Kata ya Kigala, tayari tumeanza mkakati Serikali imetupatia fedha, tunajenga shule ya Mlondwe na bado shule mbili mradi wa zaidi shilingi bilioni 1.8; lakini tuna shughuli nyingi ambazo tunaendelea nazo kwenye ujenzi wa madarasa ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Makete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niombe Wizara mtukumbuke sana Makete kwenye suala la ukarabati wa shule za msingi. Tuna shule za msingi nyingi ni kongwe kwenye nchi hii hazijakarabatiwa kwa muda mrefu, tuna shule ya Misiwa, tuna shule ya Igorwa, tuna shule ya Asunzi tuna shule nyingi ndani ya Wilaya ya Makete, tunaomba Wizara itukumbuke ili shule hizi ziweze kufanyiwa ukarabati na kujengwa. Lakini tuna vituo vya afya kwa mfano Kituo cha Afya cha Lupila, wananchi wa Makete wanasafiri zaidi ya kilometa 100 kutoka Lupila kwenda Makete Mjini, kwa ajili ya kufuata huduma za afya pale ambapo kwenye kituo cha afya imeshindikana, hawana *ambulance* hawa wote wanatumia bodaboda kilometa 100, tunaomba mtukumbuke *ambulance* kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Lupila. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nizungumze mambo mawili makubwa leo. Leo nina jambo kubwa la *TARURA;* kwanza niwapongeze *TARURA* kwa kazi ambayo wanaifanya na nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri maana *break* yake ya kwanza baada ya kuteuliwa breki ya kwanza ilikuwa Makete kwa ajili ya shughuli ya *TARURA*. Mheshimiwa Waziri uliona hali ya Makete ya barabara sisi Wilaya ya Makete inaitwa Wilaya ya Kazi wananchi wetu ni wachapakazi wakubwa, lakini changamoto kubwa tuliyonayo sisi ni barabara za vijijini hazipitiki, uliona hali halisi. Nawapongeza *TARURA* kwa yale wanayoendelea nayo, lakini ninaushauri na hii kwa Mheshimiwa Waziri unaweza ukawa ndio *game changer* wa *TARURA* ndani ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2019 TAMISEMI mliandika barua kwenda kwenye Halmashauri mkizuia, kuna Halmashauri ambazo tulikuwa tayari kukopa mitambo ya kujenga barabara kwenye Halmashauri zetu. TAMISEMI wakazuia kwamba Halmashauri zisinunue wala zisikope kwa namna ya kwamba mnataka kulinda *local constructors* (wakandarasi wa ndani) waliopo ndani. Lakini nikuombe Mheshimiwa Waziri kama ambavyo leo Wizara ya Maji wananunua mitambo kwa ajili ya kuchimba mabwawa, ni wajibu sasa na ni wakati sasa *TARURA* kwa sababu ni *department* na ni Wakala, ruhusuni wawe na mitambo ya ujenzi wa barabara kwenye Miji na Halmashauri ambazo tuna mazingira magumu kama Makete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii mwananchi wa kutoka Lupila kwenda Makete kupita Kipengele anasubiri fedha ya *maintenance* ya barabara kutoka Mkoani hadi ije ikamilike masika imepita, watu wamefariki, mazao yameozea shambani. Lakini tungekuwa na mitambo ya barabara pale Makete kutoka *TARURA* tungeenda na mitambo yetu, tungemwaga kifusi, tungesafisha barabara. Kwa ununuzi wa fedha za Serikali mitambo hata shilingi bilioni mbili haizidi mngefanya kwa nchi nzima, mngekuwa mmeokoa mambo mengi sana na fedha ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawasihi na ninawaomba tusije tukaja na hoja ya kulinda hawa wakandarasi kwamba

wakandarasi wadogo tutawazuia. Mheshimiwa Waziri wajibu wa kwanza wowote wa Serikali ni kuhudumia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la watu wa *private sector* hilo ni hatua nyingine ninyi nendeni mkajenge barabara hawa nao watapata nafasi zao. Kwa sababu, mmejenga vituo vya afya msingejenga tungetegemea hospitali binafsi tungefika leo hapa? Tunaomba *TARURA* wawezeshwe… *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napenda tu kumpa taarifa Mheshimiwa Sanga anaongelea hoja ambayo ni *valid* sana, ukizingatia barabara hizi ambazo ziko chini ya Halmashauri au *TARURA* ni takriban asilimia 85 na tunajua kabisa kwamba upande wa maji kule tuna *DDCA*. Kwa hiyo, ni mbadala sasa hivi kuweza kuhakikisha kwamba wale ambao wanajiweza kununua mitambo wanunue mitambo. Kwa sababu kama *DDCA* ipo na haizuii *contractor* hawa ambao ni *local* kwa nini mzuie kwa upande wa Halmashauri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga taarifa hiyo.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipokea taarifa hiyo na ninaomba Mheshimiwa Waziri ataandika historia kwenye Taifa hili, ni mmoja kati ya vijana ambao tunawategemea ni kuruhusu jambo kama hili lifanyike kwenye nchi yetu. Halmashauri zenye uwezo wa kuwa na *excavator,* kuwa na ma-*roller,* kuwa na ma-*tiper* ziruhusiwe. Wataalam watakudanganya tu hapa kukupiga bumbuwazi ili watengeneze *chain* na watu ambao ni *constructors* ambazo ni *private sector*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninakuomba simamia msimamo huo kama Mheshimiwa Aweso anavyokwenda kuchimba mabwawa, anza kujenga barabara vijijini na tutakuja kukushukuru.

Mheshimiwa NaibU Spika, barabara vijijini ndio sera ya Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan anasema tuwezeshe barabara vijijini zipitike. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri una nafasi ya kuyafanya haya mambo ndani ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo ninataka kuzungumza ni kwenye asilimia 10 kwenye *10 percent* ambazo zilianzishwa na sheria yetu hapa nchini kwa makusudi mazuri sana ya kuona tunasaidia vijana, akina mama na watu wenye ulemavu. Hii sheria ilianzishwa kwa ajili ya kusaidia watu hawa ambao ni vijana wenzetu, lakini *10 percent* ambayo tumekuwa tukitenga kwa ajili ya vijana wa Taifa hili, kwa ajili ya akina mama wa Taifa hili imegeuka ni *10 percent* ya watu ambao wana uwezo na sio vijana wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumza kwa *data* ukisoma kwenye hotuba ya Waziri kwenye moja kati ya maelekezo toka tuanze kukopesha *10 percent* mwaka 2017/2018 hadi 2021 nchi hii tumekopesha zaidi ya shilingi bilioni 300 kwa asilimia 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini toka tumeanza kukopesha tuna zaidi ya shilingi bilioni 222 ziko kwenye mikono ya wanyang'anyi na ninataka nikupe mfano Mheshimiwa Waziri; mfano ni Mkoa wa Tabora toka mwaka 2018 hadi 2021 wamekopesha shilingi bilioni 5.7, lakini fedha zilizorudi hadi leo ni shilingi bilioni mbili tu fedha zingine zote ziko mifukoni kwa watu. Ukienda Mkoa wa Pwani mwaka 2018 hadi 2021 wamekopesha shilingi bilioni 11 lakini hadi leo wamerudisha shilingi bilioni nne tu fedha zingine zimepotea. Ukienda Mkoa wa Mwanza wamekopesha shilingi bilioni 8.9, wamefanikiwa kurudisha shilingi bilioni 3.9 tu fedha zingine zote zimepotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Mkoa wa Dar es Salaam wamekopesha bilioni 52.3 wamefanikiwa kurudisha bilioni 14 tu fedha nyingine zote zimepotea; ukienda Mkoa wa Mbeya anakotoka Spika wa Bunge wamekopesha bilioni 12 toka mwaka 2018 hadi leo wamerudisha bilioni saba tu fedha nyingine zote zimepotea; achana na Simiyu wamekopesha bilioni nne imerudi bilioni moja, achana na Geita wamekopesha bilioni sita zimerudi bilioni tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi zipo kwenye mikono ya wanasiasa, zipo kwenye mikono ya watumishi wa Serikali ambao wanatengeneza vikundi vya vijana, wanawa-*lob,* wakifika pale wanakopeshwa fedha zinaingia mifukoni mwao, vijana hawafaidiki chochote. Kwa hiyo… *(Makofi)*

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba, anachokiongea ni *very valid* na kuna muongozo wa *10%* ambao uliandaliwa na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, mpaka tunavyozungumza bado haujapelekwa kwenye Halmashauri kwa ajili yak u-*guide* na muongozo huo ungekuwa suluhisho kwenye matatizo ambayo anazungumza mzungumzaji anayechangia sasa hivi, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga, Taarifa, unaipokea?

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini nataka kuzungumza, Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, anaweza kuzifuatilia fedha hizi zaidi ya bilioni 222 zilizoko mikononi kwa wahuni. Kwa nini nasema ziko kwenye mikono ya wahuni?

Mheshimiwa Naibu Spika, nenda ukafuate Halmsahauri ya Temeke ufuatilie fedha ziko kwa nani…

*(Hapa kipaza sauti kilizimwa)*

**NAIBU SPIKA:** Tayari, muda wako umekwisha.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, bado sijamaliza, bado dakika moja. Naomba dakika moja tu.

**NAIBU SPIKA:** Aah, sekunde tatu, sekunde tatu maliza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuomba Mheshimiwa Waziri fedha hizi shilingi bilioni 222 zilikuwa zina uwezo wa kutafutwa na zikaenda kutatua matatizo ya barabara, kuweza kununua mashine za kufyatulia tofali mkawapa vijana, mkaenda mkanunua mitambo mingine ambayo imeandikwa kwenye *project* ikasaidia vijana. Tafuta bilioni 222 ziko wapi zisaidie nchi yetu kwa sababu ni fedha ambazo ziko kwa viongozi wa taasisi, zipo kwa wanasiasa… *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, umeeleweka, ahsante sana. Ahsante Mheshimiwa Sanga.

Mheshimiwa Kanyasu, jiandae Mheshimiwa Komanya, jiandae Mheshimiwa Jesca.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi na mimi naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema kuweza kusimama hapa leo, lakini kipekee naomba nitumie nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri sana anayofanya ya kutuletea maendeleo Watanzania, lakini pia ya kuongoza Serikali vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na timu yake nzima. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Utawala na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba nikiri kwamba, Waziri anatupa nafasi ya kutosha kutusikiliza, anatoa ushirikiano mkubwa, lakini ni mtu ambaye yuko *accessible,* unaweza kumpata muda wowote unapomuhitaji. Kwa hiyo, yeye pamoja na timu yake nzima, Katibu Mkuu na wasaidizi wake tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijasahau mdogo wangu Mheshimiwa Sanga amezungumzia mitambo ya kutengeneza barabara na akatamani Halmashauri ziruhusiwe kununua. Natamani sana aje ajifunze Geita, tulitenga shilingi bilioni 1.4 kila halmashauri kununua mitambo na ile mitambo haijawahi kuonesha *value for money*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasikitika sana hiyo mikoa yote naweza nikakutajia Mwanza wanayo, Sengerema wanayo, yote yako *grounded,* kwa nini, na ni mapya? Yote ni kutoka *CAT - Caterpillar*, lakini huwezi ku-*manage* matumizi yake, wakienda *site* wale wanaoendesha wanabadilisha *pump,* anabadilisha *roller,* anabadilisha hiki, matokeo yake yale madude yanakuwa *grounded* siku mbili hayana kazi. Sasa ni vizuri kuja kujifunza kabla ya jambo hilo.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpe taarifa mzungumzaji, hatuwezi kuacha kufanya maendeleo kwa kuogopa uzembe wa baadhi ya watu ambao hawasimamii wajibu wao waliopewa na Serikali. Kwa sababu watu wa Geita kama hawasimamii hayo ma-*caterpillar* wanaachia watu wanaenda kuiba na kuchukua vitu haizuwii Halmashauri kama alivyosema Mheshimiwa Mheshimiwa Sanga kununua ma-*caterpillar* kwa halmashauri nyingine zinazofuata. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu, hiyo taarifa, umeipokea?

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikia na Watanzania wamemsikia, lakini nimesema akajifunze Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili. Ntaka kuipongeza sana Serikali, ilisema katika Bunge hili kwamba, itatangaza ajira 30,000 na zimetangazwa…

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga, Taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa Taarifa mzungumzaji kwamba Makete tulinunua *excavator* toka mwaka 1998 na tunalo hadi leo. Anavyosema kwamba tukajifunze kwa watu ambao wame-*fail*, hakuna utamaduni wa kujifunza kwa watu walio-*fail*, tunajifunza kwa watu waliofanikiwa, kwa hiyo, hatuwezi kwenda kujifunza Geita kwa watu walio-*fail*. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Na mnaweza mkajifunza kwa Mheshimiwa Jerry Silaa mpaka leo analo bado. *(Makofi)*

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa yake siipokei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema naipongeza Serikali ilipotimiza ahadi yake ya kuajiri watumishi zaidi ya 32,000 na ninaipongeza kwa sababu tumekuwa na uboreshaji na uongezaji wa miundombinu katika maeneo mbalimbali kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kutoa mfano na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, tulipata fedha za UVIKO, tumejenga madarasa katika Halmashauri ya Mji wa Geita, madarasa zaidi ya 63, lakini kutokana na mapato ya ndani tumejenga shule karibu sita mpya, shule tatu za sekondari na shule mbili za *primary*. Tunahitaji walimu wa kutosha, lakini kwa bahati mbaya shule zile nyingi zina walimu wachache kwa sababu hapakuwa na *staff,* hatukuwa na walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaipongeza Serikali, lakini namuomba Mheshimiwa Waziri aje sasa na taarifa inayoonesha uwiano wa mahitaji pamoja na ajira iliyotolewa ili tuweze kujua tume-*cover* kwa asilimia ngapi. Kwa sababu tunaweza kuajiri 32,000; lakini mahitaji ya mpaka tunaahirisha Bunge mwezi wa pili ilikuwa ni walimu 120,000 lakini pia aje na mkakati tunaziba vipi hilo *gape* ambalo sasa litakuwepo?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaipongeza sana Serikali kwa kazi nzuri na tunashukuru kwa hizo ajira ambazo zimetangazwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo nataka kuzungumza, Geita Mji imekuwa na ahadi ya kuwa Manispaa tangu mwaka 2018. Tumezungumza na Waheshimiwa Mawaziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wote waliokuwepo na ahadi mbalimbali zimetolewa. Nataka nitoe vigezo ambavyo vinasababisha Halmashauri kuwa Manispaa; la kwanza ni kuwa na watu wasiopungua laki moja sisi tuna watu takribani laki tatu, lakini la pili asilimia 30 ya wakazi wake wawe na ajira isiyohusiana na kilimo. Sisi pale asilimia 80 ni wafanyabiashara ya madini na biashara nyingine ambazo hazina uhusiano na kilimo, tuko mjini, lakini la tatu inasema kuwe na walau kiwanda kikubwa kimoja, tuna mgodi mkubwa pale ulioajiri zaidi ya watu 12,000; lakini la nne inasema tuwe na uwezo wa asilimia 70 ya uwezo wa kujitegemea Halmashauri, Halmashauri ya Geita Mjini ina uwezo wa kujitegemea kwa asilimia 83, maana yake tumeshavuka hiyo habari, lakini lingine inasema kuwepo na huduma mbalimbali ya kwanza elimu ya watu wazima tunayo, hospitali ya rufaa tunayo, chuo kikuu tunacho, ukumbi wa mikutano tunao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kumwambia Mheshimiwa Waziri tunataka Geita ipewe hadhi yake ya kuwa Manispaa. Mlituongezea sharti moja tu la kupata *master plan,* tumekamilisha *master plan* na tayari Geita tunayo *master plan*. Sasa tunakuomba tupewe hadhi ya kuwa manispaa kwa sababu, mnatuchelewesha kuendelea, tunakusanya zaidi ya bilioni 15 kwa mwaka kwa hiyo, tunataka sisi tukimbie ninyi mnatusimamisha, tunaomba tupewe tuweze kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kuongea ni jambo la *TARURA*. Kwanza naipongeza sana Wizara imefanya kazi vizuri, naipongeza sana Serikali, kwa mujibu wa takwimu kwa miaka minne yote mfululizo *TARURA* walikuwa wanapewa kwa wastani wa fedha wanazoomba; walianza kuomba mwaka 2019 shilingi bilioni 639 walipata fedha kwa asilimia 25 takribani, mwaka 2020 waliomba shilingi bilioni 699 wakapata asilimia 24 na asilimia 38 asilimia 35, lakini mwaka huu wa fedha unaoisha waliomba shilingi bilioni 717 wakapata kwa zaidi ya asilimia 96, naipongeza sana Serikali kwa jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo nataka kusema hapa *TARURA* inasimamia mtandao wa barabara zaidi ya asilimia 90 Tanzania kwa hiyo, ni chombo ambacho lazima kitazamwe upya kiongezewe uwezo ili kiweze kusaidia miundombinu, lakini jambo moja Mheshimiwa Waziri Halmashauri zote uliziongezea pesa, ulitoa mwanzo milioni mia tano-mia tano fedha za jimbo za barabara ukapandisha bilioni moja, lakini Geita Mjini ukaiacha na milioni 500.

Mheshimiwa ninaomba hiyo pesa iongezeke ili tuweze kutengeneza barabara, barabara ni mbaya na Geita imekaa kwenye muinuko kila mvua inayonyesha maji yanaenda kwenye miji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niipongeze pia Serikali kwa mradi wa *TACTIC,* tumeusubiri kwa miaka mingi sana, tumekaa tukiusubiri, lakini sasa unakuja. Hoja yangu hapa Mheshimiwa Waziri wakati ule tunatekeleza mradi wa *LGSP* tulijikuta mradi una-*phase out* fedha ziko kwenye *account*. Sasa tunataka tuiombe Serikali *this time* kwa sababu tunakwenda kwa pamoja tutakaposema tunaanza paa, miradi yote iliyotajwa kwenye mradi itangazwe ili tusiache fedha kwenye *account,* lakini barabara zitengezwe. Tumeipongeza sana Serikali kwa mradi huo na tunaomba jambo hilo liweze kufanyiwa mchakato mapema ili tuweze kuendelea vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kuchangia ni kuhusu *Machinga Complex*. Nampongeza sana

Mheshimiwa Mwenyekiti wa kwetu wa Kamati amezungumzia kuhusu Dodoma, tulikwenda kutembelea machinga inayojengwa hapa Dodoma, mimi nikataka kukuuliza Mheshimiwa Waziri, hawa viongozi wetu wa mikoa wanakwenda kwenye semina tofauti?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia *modal* waliyoitumia Dodoma, namna walivyo-*handle* machinga ni tofauti na machinga nchi nzima. Ukienda mikoa yote machinga wamekuwa *displaced,* wamepelekwa kwenye maeneo ambayo wamefilisika, Dodoma wameachwa wanafanya kazi zao, mpaka leo tunavyozungumza wako barabarani, lakini wanajengewa miundombinu na miundombinu ile inaonesha wazi kwamba kuna mtu amekaa ame-*plan.* Sasa Dodoma walikuwa na *formula* tofauti na mikoa mingine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kitu kingine cha mwisho Mheshimiwa Waziri, nimeona Dodoma Mheshimiwa Rais ametoa shilingi bilioni 2.5 kwa ajili ya kujenga machinga. Naamini tu sababu ni makao makuu, unakuja na *package* gani ya mikoa mingine ya Halmashauri nyingine ili kama hazina uwezo wa kutenga fedha hizo kwa sababu kundi hili ni muhimu ziweze kutengewa fedha kujenga kwa sababu, sasa hivi ninavyozungumza na wewe machinga *almost* wamefilisika na watu wengi sasa usije ukashangaa ujambazi ukaongezeka kwa sababu hawana kazi ya kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo nataka kuzungumza hapa ni hoja ya mifumo. Ilikuja moja ya idara zinazoshughulikiwa na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni eneo la uboreshaji wa mapato. Halmashauri yangu na Halmashauri nyingine wamebinafsisha ukusanyaji wa mapato, sasa nataka kutoa mfano; mmempa uzabuni wa kukusanya takataka mwananchi kwenye mitaa miwili ukamwambia kwa mwezi akusanye milioni tano, lakini asilimia 80 ya fedha ni za kwake, anakusanya anapata kwenye mashine yake inasoma alikusanya milioni 3.8, zile fedha unazikataa unasema hapana kalete milioni tano, akizikosa anawekwa ndani mpaka ifike milioni tano, lakini akishaweka milioni tano unamrudishia milioni nne na laki mbili. Kwa nini watu wa mifumo wasi-*develop system* ambayo *computer* iwe ina-*tally* ambazo zinatakiwa zipokelewe na Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kama ninatakiwa kwenye shilingi mia hela ya Serikali ni shilingi ishirini, *computer* imuoneshe mzabuni kupeleka shilingi ishirini kuliko kumng'ang'aniza apeleke milioni kumi anawekwa ndani, anakopa halafu baada ya siku mbili unamrudishia milioni tisa, kazi zimesimama mwezi mzima. Sasa hivi mji wangu wa Geita ni mchafu kwa sababu wazabuni wote wamekimbia, kwa nini, kwa sababu mwingine anadaiwa laki tano, anadaiwa laki nne, lakini katika milioni kumi hela ya kwetu ya Serikali ni shilingi milioni 1.2. Mfumo unaweza kutengenezwa ili kuweza kudhibiti suala hilo. Pesa inayopokelewa pale iwe ni ile ambayo kisheria inayotakiwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kushukuru sana kwa nafasi na ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Leah Komanya, jiandae Mheshimiwa Jesca Msambatavangu.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu katika hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuipongeza Serikali ya Chama Cha Mapinduzi chini ya Mheshimiwa Mama Samia kwa kazi nzuri inayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha huu tunaoutekeleza fedha nyingi sana zimeletwa katika majimbo yetu na mimi katika Jimbo la Meatu tumeshapokea wastani wa shilingi bilioni 10 katika miradi mbalimbali, elimu, afya, maji, barabara na miradi mingine mbalimbali ikiwemo mifugo pamoja na kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa unyenyekevu wake mkubwa kwa Wabunge wenzake. Ni kipindi kirefu nimekuwa nikifuatilia kutekelezwa kwa ahadi

aliyoitoa Mheshimiwa Samia Suluhu wakati akiomba kura, akiwa mgombea mwenza mwaka 2015, Meatu, aliahidi kujengwa kwa daraja la Mto Semu katika Kijiji cha Mwamanongu, lakini muda mfupi tu alipoingia nilivyomueleza jambo hili nishukuru tayari juzi tumeshapokea shilingi bilioni 43 kwa ajili ya kufanya usanifu wa daraja hilo, lakini nimshukuru pia *Engineer* Seif kwa ushirikiano wake mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niombe tu tusiishie katika usanifu kila tunapouliza maswali tuambiwe usanifu unaendelea. Kwa kuwa sisi Wilaya ya Meatu katika Mfuko wa *TARURA* tumetenga shilingi bilioni 2.7 katika miradi ya maendeleo kwa ajili ya kuanza ujenzi wa daraja hilo la Mto Semu katika Kijiji cha Mwamanongu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niiombe Serikali mwaka jana mwezi wa tisa iliniahidi kupanua shule ya Sekondari Nghoboko. Naomba wafanye utekelezaji huo kwa sababu, tulijipanga toka mwaka 2008 kupandisha hadhi shule ya Sekondari Nghoboko kuwa ya kidato cha tano na sita kwa sababu, tayari madarasa manne tumekamilisha, ofisi tatu, bwalo linahitaji kupauliwa, tunaomba bweni pamoja na maktaba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu leo kwa kiwango kikubwa nitajikita katika mapato. Tumeona Mheshimiwa Waziri amesema kutakuwa na ongezeko la asilimia 17.1 katika mapato ya Halmashauri ni jambo jema, lakini katika mapato ya Halmashauri yamekuwa na changamoto nyingi katika ukusanyaji wake ikiwemo mapato mengi ya Halmashauri yanakusanywa nje ya mfumo rasmi wa Halmashauri kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilianza ikatoa *property tax* ambayo ilipaswa ikusanywe na Serikali za Mitaa. Tumeona wameondoa *parking fees,* wametoa tozo za maji ambazo zote zilipaswa kukusanywa na Serikali za Mitaa na sasa kwa asilimia kubwa ushuru wa huduma unakusanywa na *TRA.* Mapato haya yalitakiwa yalindwe yakusanywe na Serikali za Mitaa kwa sababu zina mahitaji mengi na ni makubwa. Tumekuwa tunaziongezea mapato, lakini mapato yake yamekuwa yakipungua kila mwaka

kwa kadri tunavyokwenda. Naomba hili suala liangaliwe kwa kina, Halmashauri zetu zinakuwa hazistawi katika mapato wakati kazi zake ni nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na katika taarifa iliyopita ya Julai/Disemba kwa mwaka wa fedha uliopita ushuru wa huduma ulionekana kuongoza kuwa chanzo chake kikubwa kwa sababu asilimia 19 ilikuwa imekusanywa ya mapato yote, lakini chanzo hiki kika changamoto nyingi. Mwanzo kazi za kandarasi zilikuwa zikilipwa Halmashauri, ushuru wa huduma ulikuwa ukibakia Halmashauri, lakini *certificates* sasa zinalipwa Hazina za miradi ya maji, miradi ya barabara, kwa hiyo, ushuru wa huduma umeendelea kukusanywa na *TRA*.

Niombe namna Serikali inavyoweza kurudisha katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na kuweza kuzirudishia Halmashauri ziweze kujitegemea kwa mapato kwa sababu Halmashauri zimeendelea kutegemea Serikali kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna miradi mikubwa pia kimkakati ambayo haikusanywi vizuri. Kwa mfano tulivyofanya ziara Kamati ya Bajeti, *SGR* hawajaanza kukusanya ushuru wa huduma, basi miradi kama hiyo ikibaki hata Serikali Kuu ikakusanywa irudishwe katika Serikali Kuu iweze kuzisaidia Halmashauri kwa sababu, tunaona watendaji wetu wa kata hawana ofisi, baada ya mradi ule wa undelezaji mtaji kusitishwa, kwa hiyo, yamebakia maboma. Warudishiwe basi zile fedha watendaji wetu wapate ofisi, wapate hata vitendea kazi kama pikipiki, waweze kusimamia vizuri ukusanyaji wa mapato kama ushuru wa mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chanzo cha pili kulichoonekana ni kikubwa ni ushuru wa mazao, lakini ushuru huu umekuwa na changamoto nyingi katika ukusanyaji wake. Nishukuru Wizara ya Kilimo kwa kuamua kuwapatia pikipiki Maafisa Ugani waweze kusimamia uzalishaji wa mazao, lakini wameenda zaidi wakawawezesha kwa posho, jambo ambalo litasaidia uzalishaji wa mazao ambayo yanachangia kupata ushuru wa mazao tofauti na mwanzo mafaili yalikuwa yakibaki pale kwa

Wakurugenzi mpaka msimu unakwisha hawajawaona wakulima wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niombe na sisi TAMISEMI tuige jambo lililofanywa na Wizara ya Kilimo kwa kuwawezesha watendaji wetu wa kata. Watendaji wa Kata ndiyo asilimia kubwa wanasimamia ukusanyaji wa ushuru wa mazao, lakini hawana pikipiki, hawalipwi posho, tumepewa shilingi 100,000; lakini shilingi 100,000 hii wakati mwingine inapita miezi miwili haijalipwa. Basi tuone namna inavyoweza kulipwa na Serikali kuu kwa sababu wenyewe hawawezi kumshinikiza Mkurugenzi kwa sababu ni mwajiri wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia ushuru huu wa mazao kumekuwa na uvujaji wa mapato kwa sababu katika hoja za ukaguzi tumeona fedha zimetumika zikiwa mbichi na moja ya sababu inayochangia kwa kuwa hawalipwi fedha za ukusanyaji wakati mwingine wanajilipa kabla zile fedha hazijafika Halmashauri. Kwa hiyo, tukiwawezesha mianya hii ya uvujaji haitakuwepo kwa sababu fedha inayotumiwa kabla haijafika Halmashauri haiwezi kutambulika katika vitabu vya Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namba tatu katika ukubwa wa mapato ya Halmashauri ni uchangiaji wa huduma ya afya, tumeona wananchi wamekuwa na mwitikio, lakini wananchi wamekuwa wakishindwa kuchangia kikamilifu, tukisimamia vizuri uchangiaji mapato yatakuwa zaidi kuliko mlivyoyategemea 13%. Yapo matatizo kwa sababu kuna upotevu mkubwa wa madawa, lakini Serikali tumekuwa tukiangalia tu upotevu wa dawa lakini pia kuna fedha ambazo hazilipwi na bima ya afya kwa sababu ya ujazwaji mbaya wa fomu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka miwili mfululizo Halmashauri zimepoteza bilioni mbili kwa ujazaji mbaya wa fomu za bima ya afya. Niiombe Serikali iwasaidie weledi katika ujazaji wa fomu watumishi wetu ili yale mapato yasiendelee kupotea, yale mapato yakiendelea kuwepo yatasaidia kuwa-*revolving* katika Halmashauri zetu wananchi wakienda hawatakosa dawa, wataendelea kujiunga na bima ya afya tutaisaidia Serikali siku

ambapo itashindwa kupeleka fedha sisi tayari tutakuwa na fedha za *revolving* ambazo zitasaidia kuendeleza upatikanaji wa dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika *service levy* pia kuna mapato mengi ambayo hayakusanywi kutokana na kwamba tu ofisi za makampuni haziko Halmashauri ambapo wametekeleza miradi hiyo. Lakini pia kuna halmashauri zinakusanya ushuru huo bila kujua ni faida kiasi gani kilipatikana katika yale makampuni ni kwa sababu hazina *access* ya kupata *turnover* ya ile kampuni husika. Niiombe Serikali kupitia TRA na mwenyekiti wa mapato wa mkoa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwosha muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Haya malizia sekunde mbili.

**MHE. LEAH K. KOMANYA:** Azisaidie Halmashauri kupata takwimu cha kiasi ambacho Halmashauri zinatakiwa kutozwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Jesca, jiandae Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi pia niungane na Wabunge wengine kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungnao wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayofanya katika Taifa letu na hasa kwa kuangalia wananchi wetu wa chini kuhakikisha kwamba anashughulika zaidi na masuala ya elimu na afya na tumeona kwa vitendo siyo kwa maneno. Nimtie moyo kwamba tupo nyuma yake na tutaendelea kupigana na kuhakikisha kwamba kazi inaendelea na zaidi sana kwa kuwa amesimama kama taa ya mabinti zetu na sisi wanawake tutahakikisha haizimi, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nitakuwa naongea mambo mawili na hayo yote yanahusu ukatili. Jambo la kwanza

nitaongelea ukatili wa kijinsia lakini dhidi ya watoto, lakini nitaongelea pia ukatili wa kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa leo tumekaa hali ya watoto wetu kwenye Taifa hili si salama hata kidogo. Mheshimiwa Waziri amesema hapa kati ya mashtaka yaliyopelekwa mahakamani ya ukatili wa kijinsia asilimia 33 ni kwa ajili ya watoto na 67% ni kwa wanawake. Lakini nimuongezee hajasema wanaume, lakini upo ukatili pia dhidi ya wanaume na tafiti zinaonesha kabisa kiwango cha wanaume kupigwa kimeongezeka mpaka 71.7% wakati wanawake wamepigwa kwa 73.5%. Ukichukua takwimu hizo zinaonesha wanaume wanashuka kwa sababu wao walikuwa juu zaidi kwenye kiwango cha kupiga na wanawake wanapanda kwa kasi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu hizi zote zinaonyesha namna gani sasa athari inakwenda kuangukia kwa Watoto, kwa sababu vipigo vinavyoendelea usitahimivu wa ndoa unakuwa haupo, watu wanaachana wanaacha watoto katika hali hatarishi. Katika hiyo 33% watoto wa kiume waliofanyiwa ukatili ni 11.5% na watoto wa kike ni 22%. Tunaposema watoto wa kiume wamefanyiwa ukatili wa kingono maana yake wameingiliwa kinyume cha maumbile. Ipo miaka kumi inayokuja usishangae kuona mtoto wako wa kiume anakuja nyumbani na mkwe wako wa kiume na tusije tukaanza kuleta maneno *astaghfilillah,* tusije tukaanza kuleta maneno *God* for *bid,* tusije tukaanza kuleta maneno Mungu niepushie mbali, atakuwa hajakuepushia mtoto wako wa kiume, atakuwa amekuja na mwanaume mwenzie na anataka kumuoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu katika watoto waliofanyiwa ukatili 3% ndiyo waliopata ushauri nasihi na kutibiwa, 7% wako mitaani na wale wanageuka kuwa makonki *master* na watoto wa kike 13% tu ndiyo waliopata ushauri. Nasema hivi kwa sababu sisi Iringa tumepata tatizo hili, mtoto mmoja ambaye ameweza kuwalawiti wenzie 19 ndani ya mwezi mmoja, sasa wale saba wanaobaki ambao hawajafanyiwa matibabu wala ushauri nasihi wanarudi mitaani na wanaendeleza ile tabia. Nilivyoongea na yule mtoto aliniambia kwa uchungu sana akaniambia nilifanyiwa matendo haya nikiwa *nursery school* miaka mitano, leo

hii tumepata takwimu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri watoto walioandikishwa *nursery school* ni karibu 1,198,564 lakini watoto walio nje ya shule kwa maana ya *pre-primary* kwa *data* zilizoko na utafiti ulioko wa *UNICEF* ni 61.8%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatujaona mpango hapa tumesema tumewaandikisha hawa ni awali na tunapongea awali hawa ni watoto wa shule ya msingi miaka sita chini ya hapo wako nyuma na yule mtoto anasema alifanyiwa akiwa chini ya miaka sita.

Leo aliachwa amekwenda mtaani na akaniambia Mheshimiwa Mbunge nikasema nikusaidiaje kama Mbunge wako maana mtoto ana miaka 13; akaniambia naomba uhamishe watoto wote wanaokaa lile eneo uwapeleke shule ya bweni au uwapeleke kwenye vituo maana yake pale watoto wote ndiyo tunachofanya.

Sasa nikawa nasoma pia maendeleo ya wenzangu Wizara mpya ambayo mama ametuanzishia ya Maendeleo ya Jamii, wanasema wameanzisha kamati za kulinda watoto na wanawake. Kamati 18,186 kati ya kamati 20,750 walizotaka kuanzisha kwenye nchi hii kwa ajili ya kulinda wanawake kwenye mitaa na vijiji, kamati hizo hazipo na hazifanyikazi, hatujaziona. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Jambo hili la ulawiti kwa watoto wadogo, ukatili wa kijinsia kwa Watoto, limeshika kasi sana katika nchi yetu na kumekuwa na kesi nyingi sana ambazo mwisho wake haueleweki kumekukuwa na rushwa mbalimbali na hakuna hatua madhubuti ambazo zinachukuliwa mimi niombe sasa kupitia hili kwamba Mheshimiwa Mbunge anachokisema ni sahihi kabisa na wale wote watakaobainika basi wahasiwe iwe ndiyo adhabu kubwa ikiwa ni pamoja na kifungo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa hiyo?

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea kasoro ile ya kuhasiwa. Sipokei ya kuhasiwa kwa sababu tuna namna tutawashughulikia na kuwashughulikia hawa kwa sababu zipo sababu zinazosababisha wafanye mambo haya ikiwepo ukata, nitaongezea yaani yale mambo ya uchumi yale.

Sasa hivi mapenzi au huduma ya mapenzi ni *product* kama *product* zingine watu wamepunguza *purchasing power* hawana nguvu ya kununua kwa hiyo wanakwenda kwenye kundi la watoto wadogo na kuwaonea. Kwa nini wamepunguza *purchasing power*? Ni kwa sababu ya ukatili mbalimbali unaofanyika kwenye jamii kiuchumi ikiwepo pamoja naweza nikasema sasa hivi na sisi tunachangia kama kuna Wizara hapa inafikiria kutowapa kipaumbele Watanzania katika miradi inayotolewa na Serikali hao ndiyo wanaosababisha matatizo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ukiniambia nguzo za umeme zitanunuliwa nje ya nchi una maana vijana wangu wote walioko Iringa, Songwe, Tanga wote wamepanda miti wakose fedha, watakapokuwa wanahitaji la mapenzi watafanya nini? Kwa sababu kiuhakika sasa hivi hamna mwanamke atakupenda sura kwa sababu wanaume kwanza hawana sura nzuri unampendaje mwanaume sura. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanamme anapendwa kitu alichonacho anapendwa fedha leo tunapoharibu mazingira ya utendaji kazi wa machinga hatuangalii kama mimi Mheshimiwa Bashungwa Iringa hujanipa hela yoyote ya kuandaa mazingira ya machinga. Wanakaa katika mazingira hatarishi wanapoteza mitaji wale ni watoto wa kiume rijali unategemea unaenda wapi? Inapofika hatua anataka hamu ya mapenzi anafanyaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndiyo tunayoyasema, lakini pia kuendelea kuwanyanyasa vijana wetu waliojiajiri kwa mfano kwenye bodaboda, kwenye bajaji wanafanya kazi zao unawabana unawanyanyasa kwa leseni wasifanyekazi vizuri una

mnyanyasa yule kijana akikosa hela atafanya nini? Huo ndiyo unyanyasaji wa kiuchumi.

Sasa tuhakikishe kwamba Watanzania wanajengewa mazingira mazuri ya kufanyakazi, wanajengewa mazingira mazuri ya tiba, mimi naomba vijana wangu pale watibiwe vizuri zile hela za vijana naomba jamani kutoka mfuko wa Waziri Mkuu shilingi milioni 200 tu tukawawezeshe vijana wa pale wafanyekazi wawe na uwezo wa *purchasing power* za mapenzi, wasibake watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana tuangaliwe masuala ya huduma za afya tuboreshe, watoto hawa wengine wanabakwa wamekosa nimekuambia ni asilimia tatu katika 11 wanaopata matibabu lakini hata wakienda hospitali sisi tumetoa watoto wengi kuwapeleka Muhimbili pia wakatibiwe baada ya kuwa wamefanyiwa ubakaji hatuna Hospitali ya Wilaya na leo sioni kama imetengwa hapa nimetengewa milioni 500 tu ya kukarabati lakini tuliwaomba tujengewe kwa sababu ile iliyokuwa ya Wilaya mmechukua Mkoa na inahudumia mkoa mzima tunaomba hospitali yetu ya Wilaya ili sisi watoto wetu waweze kutibiwa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme hivi katika masuala ya ukatili haya mimi nasimama leo kama Mheshimiwa Mbunge hapa kwa sababu kuna masuala ya ushirikina yapo ndani yake, sasa ushirikina ni mambo ya rohoni na tunayashughulikia kiroho. Walioko humu ndani watumishi wa Mungu watanielewa, mimi nasema hapa sasa kama Mbunge na ninyi wenzangu kama mnaniunga mkono mtajibu amina mwishoni nasema hivi Mungu tusaidie hatutawafanyia hatutawahasi kama alivyosema Mheshimiwa lakini ninaomba hivi tuachilie nguvu za Mungu kuanzia hapa zikawashughulikie wote kwenye kile kiungo wanachotumia kulawiti watoto wetu, kipigwe nguvu kisifanye kazi na zile mashine mbili zinazozalisha nguvu, zipotee kabisa na madaktari watakapoona mtu mwenye dalili hizo mnitafute ili tumuombee arudi katika hali ya kawaida na tumfanyie *counselling* ili watoto wetu waendelee kuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye masuala ya kiuchumi tuwatengenezee vijana wetu mazingira rafiki ya kufanyakazi tusiwanyanyase mama ntilie sijui akina nani wanapoonekana wanafanyakazi usimwage bidhaa zao, uangalie namna utakavyotumia hekima kuwasaidia ili wajijengee uchumi. Tumesema hapa tuwape vipaumbele Watanzania kwenye miradi tuwape vipaumbele tuwape elimu ili Watanzania waweze kuwa na *purchasing power* ya mahitaji yao ya muhimu ikiwepo suala la mapenzi, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa namuita Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, ajiandae Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, ajiandae Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuongelea Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyotangulia wenzangu kusema Wizara hii inaongozwa na vijana na kwa sababu inaongozwa na vijana wanahaja ya kuacha alama katika Taifa hili, Mheshimiwa Bashungwa watu wengi wamekushauri na mimi pia nakushauri, kuna mambo yanafanyika ndivyo sivyo usipoyasimamia lawama itakupata na utaharibu jina lako na vizazi vinavyofuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia TAMISEMI na hasa kwenye eneo la elimu; elimu ndiyo msingi wa maisha na elimu huanzia kwenye msingi, usipotengeneza jamii yako na hasa kwenye elimu ya msingi kwa watoto wadogo kuanzia hapo unakuwa hujajenga Taifa bora. Mimi ninaamini watu waliosoma elimu nzuri toka elimu ya msingi ndiyo wanaofanya vizuri mpaka sasa. Lakini kumekuwa na uzembe wa Serikali kutokusimamia elimu ya msingi kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ripoti ya *CAG* ya mwaka 2022 inayoishia mwezi wa tatu inasema idadi ya walimu wa shule za msingi wanaohitajika ni zaidi ya walimu 40,000 lakini walimu waliopo ni 23,000 peke yake, huu ni upungufu uko chini ya 41%. Huwezi kuwa na wanafunzi ambao hawana walimu na bahati mbaya sana waathirika wakubwa ni wanafunzi wa vijijini, hao

tumewaonea kwa kuwapa walimu na walimu wanaopangiwa kwenda shule za vijijini wanahama kwa visingizio mbalimbali na kuwaacha watoto wale hawana walimu.

Mimi ninasema Mheshimiwa Waziri, CAG alipoenda kufanya ukaguzi kugundua kwamba idadi hiyo ni ndogo na ninafahamu hamjaajiri zaidi ya miaka sita sasa na mnapozungumzia ajira mnaenda kwenye vyombo vya habari kusema tumetoa ajira na kutoa matangazo mengi, lakini uhalisia walimu wanaoajiriwa ni wachache kuliko wanaohitajika. Ninaomba Wizara yako isimamie hili tupate elimu bora.

**T A A R I F A**

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa dadaangu Mheshimiwa Mwakagenda kwa hoja anayoizungumzia ya ukosefu wa walimu na ni kweli kwamba *foundation* ya mtoto ni wale watoto wa awali wanatakiwa wapate elimu bora ya awali, mwalimu mmoja anafundisha wanafunzi 180; sasa unaweza ukaona kwa wastani mwalimu mmoja wanafunzi 180 tatizo ni kubwa sana.

Kwa hiyo nampa taarifa kwamba aiweke hiyo kumbukumbu kwa sababu ameongelea mafunzo awali ya mtoto kumjengea msingi kwa hiyo ni tatizo kubwa sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia taarif.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipokea taarifa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia elimu bila malipo lengo la elimu hii mlipotoa hilo tamko ni kumsaidia mtoto wa kijijini. Elimu bila malipo mtoto asome vizuri bila michango yoyote, lakini Serikali imekuwa haipeleki fedha kwenye hizo shule kwa ajili ya kusaidia, mmetaja fedha kweli kwa umoja wake mnaweza kusema shilingi bilioni 200 tumepeleka lakini ukienda

kwenye ile shule mwisho kabisa mwalimu mkuu anapata shilingi 200,000 atafanyia kazi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu hii haiwezi kuleta tija kama Serikali haiwezi kusimamia yale inayoyasema. Ripoti ya *CAG* hiyo hiyo ya Machi, 2022 inasema zaidi ya Halmashauri 22 zilizofanyiwa utafiti walikuwa wanahitaji vitabu takribani vitabu 6,000,000 lakini shule hizo zimepata vitabu 1,400,000 tu peke yake unaona upungufu wa vitabu kwenye hizo shule kati ya 6,000,000 kwa 1,400,000 ni vitabu vichache sana tunaomba Wizara yako isimamie kwa sababu huwezi kupeleka watoto shuleni bila kuwa na vitabu vya kiada na ziada. Vitabu hivyo ni vya muhimu na vinavyopungua zaidi ni vitabu vya sayansi tunaomba mtusaidie katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ruzuku bila malipo ambayo inapelekwa kwenye hizo shule nimeshasema hapo mwanzo haziendi sawasawa, watoto masikini ndiyo wanakuwa waathirika, lakini udhaifu wa hizo pesa mnazopeleka kuna maeneo yanapata pesa kwa wakati kuna maeneo yanachelewa kupata pesa. Kuna upungufu zaidi ya shilingi bilioni tano katika fedha hizo mnazopeleka za uzuku kwenye hizo shule, shilingi bilioni tano ni fedha nyingi sana zinapokwenda kwa kuchelewa tunaomba mlisimamie suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa walimu ni changamoto kubwa sana tumesema hapo mwanzo lakini uwiano wa walimu, amenipa hapa mwongozo uwiano wa walimu sawa sawa na ripoti ya *CAG*, kuna baadhi ya wamefanya *research* kuna mahali walimu wanatakiwa 1,300,000 lakini walimu wapo wachache zaidi ya upungufu wa walimu 20,000 mimi ninaomba Mheshimiwa Waziri ulisimamie hilo kwa sababu upungufu na hizo ni Halmashauri chache zilifanyiwa *research* upungufu wa walimu zaidi ya 20,000 ni wengi sana. Tunaomba muajiri kwasababu wasomi wapo waliosoma tayari na wanazunguka mtaani, hawana kazi, tunaomba tuwaajiri watu wafanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wanaojiandikisha shule ya msingi wanajiandikisha kwa wingi na ninafahamu Serikali imejenga madarasa mengi na watoto wanajiandikisha, lakini

katika umaliziaji wa shule elimu ya msingi watoto wengi hawamalizi shule tunaomba mfuate utaratibu kwa Maafisa Elimu wa Wilaya, Mikoa kujua ni sababu gani zinazowafanya watoto wasimalize elimu ya msingi na tumekuwa na watoto mitaani wengi sana ambao sio lugha nzuri kuwaita watoto wa mitaani kwa sababu mtaa hauzai lakini mwisho wa siku watoto wengi wanazurura mitaani, hawana mwelekeo na wakati huo hapa Bungeni tunazungumzia elimu bora, tunazungumzia kujenga madarasa lakini mijini hata hapa Dodoma kuna watoto wanaopita na kuombaomba na sisi kama viongozi tunawaona, hatuchukui hatua yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie ucheleweshwaji wa ruzuku au fedha za maendeleo katika Halmashauri zetu, shilingi bilioni 54.06 bakaa ambayo ilibaki kwa mwaka 2019/2020 zilichelewa kurudi kwenye Halmashauri na katika fedha hizo zilizochelewa karibia bakaa kati ya hizo shilingi bilioni 15 zilikuwa na Mfuko wa Barabara. Sasa usipopeleka na ukapeleka kwa kuchelewa fedha za maendeleo ya Halmashauri tunazungumzia barabara kwa maana ya *TARURA* ina maana wakulima ambao wao wameshalima na kupata mazao wanategemea wasafirishe kwa barabara hizo hawatasafirisha, na kama barabara ni mbovu wachuuzi wanaokwenda kununua bidhaa hizo mikoani na vijijini lazima bidhaa itakuwa bei juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba fedha za Halmashauri zirudi kwa wakati na wala tusione zikicheleweshwa kwa sababu zisizokuwa za rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ucheleweshwaji huo wa fedha za maendeleo umekuwa ni mtindo wa muda mrefu sana kwa sasa, tunaomba mzisimamie lakini sio tu hivyo wito ambao mimi niwawapa Hazina, Hazina iweze kutoa fedha kwa wakati, kama fedha zimekusanywa na zimekwenda Mfuko Mkuu wa Serikali tunaomba fedha hizo zitolewe kwa wakati ili Mfuko wa Maendeleo wa Wilaya na Halmashauri zetu uweze kupata miradi na kuweza kufanya kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo kuna wakati mnatoa fedha wanafanya kwa hiyo tunaita *fast track* haraka haraka ili wakimbizane na muda wa bajeti, fedha inakuwa huwezi kupata *value for money,* lakini pia watu wanafanya kazi kwa haraka haraka kuitisha *tender* za haraka hapo na uhuni unakuwepo wa kupitisha mambo ambayo sisi kama wasimamizi wa fedha za Serikali hatupendi kuona zinafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenzangu hapa amezungumzia suala la ukatili wa kijinsia suala hili limekuwa ni kilio kikubwa sana na kwenye ripoti yako umeizungumzia idadi iliyotajwa ya wanawake na watoto wanaonyanyasika ni kubwa sana kama Taifa tusiposimama ina maana hatuna taifa bora hapo baadaye, wanawake mara nyingi tumesikia kwenye vyombo vya habari na tunafahamu sehemu za vijijini hawana vyombo vya habari itakuwaje wanawake wanauwawa wanawake wanapigwa tu kwasababu hawana usimamizi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, malizia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** … hasa Serikali za Mitaa lakini pia na Wizara husika Kamati imetoa ombi juu ya fedha za UVIKO ambazo zilitolewa tunaomba Wizara yako iundwe kamati…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: …**ili fedha hizi zihakikishwe kama kweli zilifanya kazi iliyotakiwa na wala hawaja *divert* mradi huu. ahsante baada ya kusema hayo.

**NAIBU SPIKA:** Haya ahsante. Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, ajiandae Abdallah Chikota, jiandae Mheshimiwa Mohamed Monni. *(Makofi)*

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma kwa kutuweka hai, lakini nikushukuru wewe kwa kunipa fursa hii ya kuchangia pia naomba nikishukuru Chama

changu cha Mapinduzi kwa kuniamini, naomba pia niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Lulindi kwa kuniombea dua kuniwezesha kutimiza malengo yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote niseme kwamba sina deni kwa Wizara yoyote ile, nasema hivi kwa sababu kwa kadri jinsi walivyokuwa wananipa ushirikiano mara zote nilipokuwa nikihitaji chochote mara zote nilivyoomba msaada wamenipa ushirikiano wa kutosha na ninauhakika kwamba wataendelea kunihakikishia kwamba nitakwenda kuwaomba misaada pale nitakapohitaji kwa maana hiyo ndio maana ninasema sina deni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo sina maana ya kwamba hawataniona, wataniona sana kwa sababu jukumu nililopewa na wana Lulindi ni kuhakikisha kwamba ninawaletea maendeleo pale kwao na maendeleo hayawezi kuja hivi hivi kwa mimi kusimama tu, ina maana kwamba lazima niende kila Wizara kuwaomba hayo maendeleo. Nawaomba msinifukuze, nikija mnikaribishe ndugu zangu, ninyi ndio wenye kunisaidia jukumu hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi Jimbo langu lina uhitaji mkubwa sana kwanini ni Jimbo lina historia na viongozi wakubwa kabisa wa nchi hii, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa aliyekuwa Rais wa nchi hii ndiye nyumbani kwake kwenye Jimbo hili na usingizi wake wa milele umelala pale Lupaso. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kuna kila sababu ya kufanya eneo hili liwe na hadhi inayostahili, mimi peke yangu kama Mchungahela sitaweza ndugu zangu naomba ndugu zangu mnisaidie kuhakikisha kwamba Mkapa anapata stahiki yake, lakini Mheshimiwa Anna Abdallah mwanamke shupavu kabisa katika hii nchi amepigania nchi hii, amejitoa kwa nguvu zake, amelitumikia Taifa hili kwa uzalendo mkubwa kabisa, nyumbani kwake ni Jimbo la Lulindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaomba sana ndugu zangu mumpe heshima Mama Anna Abdallah kwa kumwezesha kila kitu

ambacho kinaweza kikaonekana pale watu wakaona kwamba hapa ni nyumbani kwa Anna Abdallah. Ninayo kila sababu ya kuwaomba ndugu zangu Wabunge kuna baadhi yenu hapa mmejinasibu sana kwamba mmefanikiwa kupata miradi mingi sana katika maeneo yetu basi mkimuona Mchungahela anapewa miradi mingi msiwe na *jealous* ya namna yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaomba sana sana sana mniunge mkono kwa sababu kuna kila sababu sisi tunahitaji upendeleo na upendeleo huu ni wa umuhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine sababu iliyotufanya tumechelewa na mpaka kuhitaji upendeleo ni kwamba eneo letu limejishughulisha sana na shughuli ya kuwasaidia wapigania uhuru wa nchi za Kusini mwa Afrika, baada ya kutumia muda mwingi sisi kujishughulisha na masuala yetu ya kimaendeleo kulijenga jimbo lakini shughuli zetu za kawaida tulijishughulisha sana kuwasaidia sana hawa ndugu zetu wakati tukifanya hivyo tumechelewa kupata maendeleo ya kutosha, kwa hiyo, jamani tunayo kila sababu ya kuonewa jicho la huruma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hapo kama nilivyosema TAMISEMI ni Wizara muhimu sana, mara nyingi sana tunaweza tukasema kama ni *engine* ya bajeti zote ikitumika vizuri tunaweza tukawa na mafanikio makubwa sana kwenye hii nchi na hali hiyo imejitokeza mwaka jana kwa kadri tulivyoona tuliwekewa miradi mingi sana katika maeneo yetu halikadhalika bajeti hii ya mwaka huu inaelekea mwelekeo huo huo, kitu kimoja tu ninawaomba ndugu zangu ambalo tuna jukumu la kufanya kuisimamia hii miradi katika kiwango kinachostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado hatujafanya vya kutosha kusimamia hii miradi, tunalo jukumu la kuhakikisha miradi hii inasimamiwa na ikaweza kunufaisha wananchi kizazi chetu kinachokuja huko mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia elimu ambayo ndio msingi wa Maisha kwa kiwango kikubwa kabisa unatekelezwa na TAMISEMI, lakini utekelezaji wake kwa hali ya sasa ilivyo kwamba

kuna baadhi ya maeneo kuna malalamiko mengi sana kwamba utekelezaji unachelewa. Ninaomba kutumia vyombo vyetu husika ambavyo vinaweza kutusaidia kwa namna moja au nyingine kwa mfano TAKUKURU iweze kuweka jicho katika miradi hii, TAKUKURU isisubiri mpaka waambiwe na mama kwamba jamani kuna suala la kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawomba sana, sana, sana waweke jicho, lakini chombo kingine cha *audit unit* ninaomba sana sana mara hii ilikuwa ni kipindi cha kutengeneza *audit specials* nyingi sana katika maeneo yetu huko kusudi angalau kuwatisha hawa watendaji ambao wenye nia tofauti na mahitaji hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hapo nizungumzie suala la Afya kwenye Jimbo langu nina Kata 18, lakini kituo cha afya kinachofanya kazi vizuri katika jimbo zima ni kimoja tu, kuna vituo vingine viwili ambavyo vilishajengwa havijaisha, lakini pia kuna Kituo cha Nagaga ambacho kinahitaji fedha kumalizia. Katika fedha shilingi 500,000,000 zilizotolewa kituo hiki kilipewa shilingi 400,000,000 peke yake na Kituo cha Chungutwa pia kilipewa shilingi 400,000,000 peke yake hivyo kufanya baadhi ya maeneo au baadhi ya miundombinu inayotakiwa katika hivi Vituo vya Afya kutokukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, alivyopita Makamu wa Rais alituahidi kwamba tushirikiane na TAMISEMI kuhakikisha kwamba tunaangalia ile fedha iliyopungua shilingi 100,000,000 kwa Nagaga na shilingi 100,000,000 kwa Chungutwa inapatikana kwa ajili ya kukamilisha Vituo vya Afya, nasikitika mpaka sasa hivi Mheshimiwa Waziri fedha hii bado haijapatikana licha ya kuwa tumewasiliana mara kwa mara na Wizara yako, sikulaumu lakini najaribu kukumbushia naomba hii shilingi 100,000,000 ya Nagaga ipatikane na shilingi 100,000,000 ya Chungutwa kusudi tuweze kufanikisha ukamilishaji wa Vituo vya Afya hivi, angalau Lulindi na yenyewe ionekane kwamba imepata vituo vya afya vya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo mengi sana ya kuzungumza, lakini nikijaribu kuangalia sana naona kama

yataingia kwenye lawama wakati mimi nilishajielekeza kusifia Wizara zote katika nchi hii na Mawaziri wote, kitu ninachoweza kusema kwa sasa hivi naomba ushirikiano kwa Wabunge wote pale nitakapokuja kwa namna moja au nyingine kuomba msaada wa kunishauri jambo au kunisaidia jambo mnisaidie…

**NAIBU SPIKA**: Ahsante kwa mchango mzuri.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naomba kuunga mkono hoja asilimia moa moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri, Mheshimiwa Abdallah Chikota Mheshimiwa, jiandae Mohamed Monni, jiandae Vedastus Manyinyi. *(Makofi)*

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mezani kwetu na mimi niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya maana ndiye Waziri ambaye ana dhamana ya Wizara hii kwa sababu ni Ofisi ya Rais – TAMISEMI, niwapongeze Mheshimiwa Bashungwa na timu yake Naibu Mawaziri wote, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu na watendaji wote wa TAMISEMI kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utaanzia pale alipoishia Mheshimiwa Jerry Silaa, Meya Mstaafu wa Ilala yeye amezungumzia kwenye ngazi za vijiji na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa ngazi ya Halmashauri. Mimi nitazungumzia kwenye Sekretarieti ya Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma Sheria ya Tawala za Mikoa Sura Namba 97 lakini na *policy paper* ya ugatuaji ile *decentralization* ya mwaka 1998 utakuta majukumu ya *Region Secretariat* ni pamoja na kuzishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile kuzisimamia mamlaka za Serikali za mitaa na kutengeneza mazingira wezeshi ili Mamlaka ya Serikali za Mitaa ziweze kutimiza wajibu wake,

tulitegemea kwenye *Region Secretariat* kuwa na maafisa waandamizi na wabobezi ili wakienda kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa wakashauri, lakini changamoto iliyopo sasa hivi Sekretarieti za Mikoa hazina wataalam hao, unakuta mtaalam anayekwenda kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa kushauri ni *junior* kuliko aliyeko kwenye Halmashauri, kwa hiyo hata ushauri wake hauwezi kusikilizwa na hata cha kushauri hana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, muda umefika sasa na Mheshimiwa Bashungwa tuna matarajio makubwa sana na wewe, hebu tufanye mapitio ya Sheria yetu hii ya Tawala za Mikoa ya mwaka 1997, lakini tufanye *re-structuring* kwenye *RS* je, muundo wa sasa wa *RS* unakidhi mahitaji ya sasa kusimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa? Tumeona hapa juzi Mheshimiwa Aweso ameenda mahali fulani anauliza nionesheni bwana la shilingi milioni 600 na watu wa Mkoa wapo na wao wanashangaa kama tungekuwa na *strong RS* yale yasingetokea Mawaziri msingekimbia kimbia kungekuwa na kazi kubwa zinafanywa na Sekretarieti ya Mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba tufanya mabadiliko, naomba tuziwezeshe tuwe na wataalam mahiri natuwape rasilimali fedha ili ziweze kutekeleza majukumu yake na Mawaziri mtatulia kufanya maamuzi ya kimsingi na sio kwenda kukagua vitu ambavyo Sekretarieti ya Mkoa wangeweza kutekeleza mambo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa pili, unahusu miradi ya kimkakati; nakupongeza Waziri umesema kwamba umeunda timu ya kuzishauri na kuziwezesha Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuandika maandiko ya miradi, lakini Mheshimiwa Waziri nikuombe tu kwamba kuna changamoto ya kuchelewesha maandiko katika ofisi yako, maandiko yamekaa muda mrefu sana na kule kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuna wataalam wa kuandika hayo maandiko, wachumi miongoni mwa *course* ambazo wanazofanya vyuo vikuu ni *project writeup,* sasa nashangaa kwamba wachumi hawa wame-*graduate* vyuoni lakini hawawezi kuandika andiko la mradi tu kujenga ghala kwenye Mamlaka ya Serikali ya Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, muharakishe kupitia hayo maandiko ili fedha zitolewe umesema hapa mwaka jana fedha zilizotumika ni asilimia 32 tu ya fedha zilizotolewa, ina maana kwamba maandiko hayapitishwi kwa wakati, na maandiko mengine Mheshimiwa Waziri yanahitaji maamuzi ya muda mchache tu, nikupe mfano kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa Mkoa wa Lindi na Mtwana tunapolima korosho wengi wameomba kujenga maghala ya kuhifadhi korosho, mamlaka hizi zingepewa fedha wangeweza ku-*back even* kurejesha hivi fedha kwa muda mfupi sana kwa sababu kwa sasa hivi kwa mjengepo wa bei kilo moja ya korosho zinapoingia ghalani inalipwa shilingi 38. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri za Mkoa wa Mtwara mwaka huu zimezalisha tani 178 kwa bei hii kuna ina maana kuna takribani shilingi bilioni tano ingepatikana hawa hata wakiruhusiwa kwenda kukopa kwenye mabenki ya kibiashara uwezekano wa kuridisha ni mkubwa sana kwa kipindi kifupi, hivi andiko kama hili linakaa miaka mitatu linasubiri nini, na ni fedha ipo wazi kwa sababu kila msimu wa korosho yanahitajika maghala kila msimu wa korosho wapo wanunuzi wanakuja wanahitaji haya maghala kila msimu wa korosho kunahitajika maghala ya kuweka pembejeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye stakabadhi ghalani kunahitajika maghala, sasa maandiko kama hayo yanakaa miaka mitatu yanasubiri nini? Mheshimiwa Waziri ebu *fast track* vitu kama hivyo tupunguze Mamlaka ya Serikali za Mitaa kutegemea utegemezi kutoka Serikali Kuu. Hapa tungeruhusu Halmashauri hizi kujenga maghala takribani kila Halmashauri ingekuwa na uhakika kupata shilingi 500,000,000 kila mwaka, sasa hii ingesaidia kufanya vitu vingi sana. Hebu naomba Mheshimiwa Bashungwa fanya maamuzi watu wajenge maghala na fedha hizi ziweze kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ninalotaka kuchangia ni kuhusu mradi wa *TACTIC;* huu mradi nampongeza Waziri kwamba mmeongeza kasi ya mazungumzo ili uanze kutekelezwa na mimi kipekee nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuingiza Halmashauri ya Mji wa Nanyamba katika mradi huu, tupo

kwenye miji 45 na tunausubiri sana kwa hamu. Mheshimiwa Waziri nikuombe kwamba tusifanya makosa yaliyopita huko nyuma miradi hii tujenge kulingana na mahitaji ya sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais ameelekeza kwamba masoko yafuate watu na sio watu wafuate masoko. Tuna miradi mingi pale Mtwara Mjini kwa kaka yangu Mheshimiwa Mtenga limejengwa soko pale Chuno la fedha nyingi, lakini kukawa na mgogoro kati ya wafanyabiashara kwenda kuhamia kwenye lile soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye maeneo mapya tusiruhusu vitu kama hivyo nafahamu huu mradi unachangamoto ya fidia ni bora tutafute fedha mahali tufidie kwenye masoko yaliyopo sasa hivi tujenge ili tuboreshe hapo ili kusiwe na kujenga miradi ambayo haina manufaa. Tukijenga masoko ambapo watu wapo tuna uhakika wa kurudisha hizi fedha. Kwa hiyo pamoja na kuona kwamba kuna miradi hii wafadhili haina fidia basi Mheshimiwa Waziri tafuta chanzo kingine ili tulipe fidia, tujenga miradi maeneo ambayo kuna watu na hasa mradi wa soko na mradi wa vituo vya mabasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie suala la uhaba wa walimu; kama walivyosema wenzangu kuna changamoto kubwa ya upungufu wa walimu na hapa Mheshimiwa Waziri nimeona umekokotoa upungufu kwa kutumia *ratio* ya mwalimu mmoja wanafunzi 60 sijui kama *ratio* hii imebadilika siku hizi lakini mimi ninavyofahamu *ratio* ili mwalimu aweze kufundisha vizuri kwa kiwango chetu tulijiwekea kwamba darasa la *class size* darasa moja watoto 45 na mwalimu hivyo hivyo ahudumie watoto 40, hilo darasa la watoto 60 ni wengi sana darasa la wanafunzi 60 halifundishiki. *(Makofi)*

Kwa hiyo tumeona hapa kwenye takwimu kwamba tunaupungufu mdogo lakini kwa sababu tumetumia *ratio* kubwa tukirudi kwenye *ratio* yetu ya zamani kuna uhaba mkubwa wa walimu hili halikwepeki lazima tutoe kibali maalum kwa walimu ili waboreshe elimu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Monni, jiandae Mheshimiwa Manyinyi.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja hii ya Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nichukue fursa hii kumshukuru Waziri na watalaam wake wote kwa namna ambavyo wamewasilisha hoja hii. Naomba na mimi niseme tu kwamba napongeza kama wenzangu wote walivyopongeza na pongezi zote zilizotolewa ni za kweli na ni sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwanza nataka kuongelea juu ya upungufu wa vyumba vya madarasa lakini lazima ni *declare interest* kwamba mimi jimbo langu nila vijijini yaani hata pale Makao Makuu ya Chemba bado panaitwa kijijini. Sasa labda nitoe takwimu kidogo mahitaji ya vyumba vya madarasa kwenye jimbo langu kwa ujumla ni vyumba 1,562 lakini vilivyopo ni vyumba 700 tu maana yake ni nini? Kuna upungufu wa zaidi ya asilimia 50 na ukweli ni kwamba watu wa vijijini tunafahamiana kwamba ni watu maskini, uwezekano wa kujenga vyumba hivi vingi vyote hivi haiwezekani, kama tulivyofanya kwenye sekondari lazima tuje na mkakati wa makusudi wa kuangalia namna gani tunaweza kwenda kuongeza vyumba hivi vya madarasa hivi shule za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uamuzi ambao aliufanya wa kuidhinisha zile fedha za UVIKO zitumike katika kujenga madarasa ya sekondari. Kwa hoja ile ile mimi nawashauri Wizara ya TAMISEMI lazima waje na mpango mwingine muhimu ili walau kupunguza kwa kiwango fulani upungufu mkubwa wa madarasa kwenye shule hizi za msingi. Hoja hiyo pia iendane pia na upungufu wa walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna upungufu mkubwa sana wa walimu lakini kuna jambo huwa najiuliza sana kwamba unaona kabisa takwimu zinaonesha labda Wilaya ya Chemba ina upungufu mkubwa zaidi kuliko wilaya nyingine, lakini wanavyokuja

kuletwa walimu unaona wamegawiwa kwenye yale maeneo ambayo kuna walimu wengi zaidi. Sasa hili jambo hili nililisema mwaka jana, lakini naomba safari hii lizingatiwe kwamba ndiyo tunaenda kuajiri walimu lakini kwa nini tusiajiri walimu tukawapeleka kule ambapo kuna upungufu mkubwa zaidi. Changamoto hii inaweza ikaendelea kwamba kila siku tunaendelea kuongelea habari ya upungufu wa walimu. Mwaka huu tunaongelea upungufu walimu, walimu wanaajiriwa lakini hatuzingatii ni wapi kuna upungufu mkubwa ili walau tukapunguze *gape* kule kuliko kupeleka kule ambapo kuna walimu wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo shule zangu za msingi zinawalimu wanne na wanafunzi 500 ninamna gani katika mazingira haya walimu hawa wanaweza kufundisha kule kijijini na ni ukweli usiopingika kwamba kuna Mbunge mmoja alitoa hoja ya msingi sana kwamba kuna umuhimu wa kuwaajiri wale walimu ambao wapo tayari kukaa kule porini. Kuna walimu wanajitolea, zilipotolewa ajira wao wakanyimwa wameendelea kujitolea na tunalazimika sisi Halmashauri au vijiji kuchanga fedha kuwalipa wale walimu kufuatana na mazingira yetu, lakini wale wanaojitolea wapo pale hawaajiriwi.

Mimi nafikiri safari hii kuwe na mkakati wa makusudi wa kuangalia kwamba huyu yupo hapa miaka mitatu anajitolea, ajira zimekuja hakuajiriwa, kijiji kinaendelea kuchanga fedha kwa ajili ya kumlipa walau kwa kumuajiri tutakuwa tumepunguza mzigo kwa wale wanakijiji waliopo pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili; nilitaka niongelee kidogo kuhusu na mimi naamini Mawaziri hawa vijana wanaenda kutatua changamoto hii. Kuna changamoto kubwa sana kwenye malipo ya Madiwani hasa zile stahiki ndogo ndogo kama posho, hii ni changamoto kwa Tanzania nzima. Mimi ni mjumbe wa *LAAC* nimejaribu kupita kwenye hizo Halmashauri unaona hapa wanalipwa vingine, hapa wanalipwa vingine. Sasa ni lazima tuje na mwongozo mmoja kwa sababu asilipwe kama hisani hali iliyopo sasa hivi malipo ya Madiwani yale ya posho yanazingatia tu namna gani yule Mkurugenzi anajisikia wakikutana na Mkurugenzi mwenye roho mbaya ni mgogoro kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nini nataka kusema lazima TAMISEMI wenyewe waje na mwongozo mmoja kwa Halmashauri zote ili kila Mheshimiwa Diwani ajue kabisa yeye anapoenda kwenye kikao stahiki zake ni zipi mgogoro huu wa malipo umeharibu sana mahusiano kati ya Mkurugenzi na Madiwani na kazi zinakwama .

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niwaombe vijana mliopo hapa ambao sisi tunawaamini sana kwamba nendeni sasa kuanzia bajeti hii andikeni waraka mmoja na futeni nyaraka nane, tisa zilizopo ambazo hazieleweki na ni kweli ukianza wewe kama Mbunge mara nyingi unajaribu kurekebisha ugomvi kati ya Wakurugenzi na Madiwani, lakini unaona kabisa Madiwani wana hoja wana waraka, Mkurugenzi naye ana waraka sasa sijui inakuwaje! Kwa hiyo, unaanza unakaa unashindwa uchukue waraka wa Mkurugenzi aliokuja nao au waraka wa madiwani waliokuja nao.

Mimi niiombe wizara kwenye bajeti hii njooni na waraka mmoja na futeni nyaraka zingine vyovyote vile ambavyo mtaona itafaa itasaidia kutuliza hali ya migogoro iliyopo kwenye Halmashauri zetu.*(Makofi)*

Mheshimwia Naibu Spika, jambo lingine ni usimamizi wa fedha; usimamizi wa fedha kwenye miradi yetu nimesema mimi ni mjumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali kuna changamoto kubwa sana kwenye fedha hizi zinazopelekwa kwenye miradi, lakini pia na shida hii naiona huku TAMISEMI kwanini labda nitolee mfano mmoja tumeenda kwenye Halmashauri ya Magu kuna jengo limeanza kujengwa mwaka 2011 mpaka leo halijamalizika, lakini pia ukimuuliza Mkurugenzi anasema apewe fedha zilezile ambazo ziliandikiwa *proposal* mwaka huo zitamaliza kujenga jengo lile. Mimi nikamwambia hiki kitu hakiwezekani yaani wakati mfuko unauzwa shilingi 11,000 ndiyo ujenzi ulianza, leo mfuko mara mbili ya bei ile bado anasema fedha ile ikija atamaliza lile jengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi nafikiri hapa kuna shida, lakini shida nyingine kubwa pale kuna mtu anaitwa Mkaguzi wa Fedha za Ndani, Mkaguzi yule yupo chini ya Mkurugenzi, ni

namna gani anaweza kuandika taarifa wakati mtu anayemlipa ni Mkurugenzi? Ni lazima hivi vitu viangaliwe upya kwamba kile kitengo ni cha muhimu sana kwa sababu fedha nyingi ambazo tunapeleka pale, lakini mtu ambaye anaweza kuandika ripoti ya kweli analipwa posho na Mkurugenzi ni kwa namna gani sasa ni vipi ambavyo yeye anaweza akasimama akaandika ripoti ya aina yoyote ya kuhusu Mkurugenzi ambaye yeye ndiye anayemlipa posho anakaa kwenye dawati pale kuandika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka pia nilisemee hilo, lakini la mwisho pengine Mheshimiwa Waziri kwenye jimbo langu alipokuwa Waziri Ummy alikuja na akaahidi kutengeneza barabara ya kilometa 18 kwa kiwango cha changarawe, barabara ile ndiyo inayotumika kila siku, sasa baada ya kuwa ni ahadi ya Waziri sisi hatukuitengea fedha tulizopewa, sasa watu wakipita pale wananitukana mimi, lakini unaona wewe shida imeanza kwenu msingetuahidi mnatujengea barabara ile maana yake nini maana yake ni kwamba sisi tungetenga fedha zile ambazo mmetupa kujenga barabara ile…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaj)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Manyinyi jiandae Mheshimiwa Jumanne Mtaturu jiandae Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye hii hotuba ya Waziri wa TAMISEMI. Nakushuru sana Mheshimiwa Bashungwa pamoja na Naibu Mawaziri mnafanya kazi nzuri ni imani yangu kwamba tukiendelea hivi basi tutaweza walau kutatua changamoto nyingi zinazowahusu wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naendelea kuishukuru sana Serikali kwa maana ya Mheshimiwa Rais Samia tumeweza

kupata fedha za kutosha kujenga vyumba vya madarasa, kujenga zahanati, vituo vya afya pamoja na barabara. Kwa hiyo, nawapongezeni sana, lakini bahati nzuri ni kwamba fedha zimekuja na tumezisimamia vizuri, lakini huu usimamizi mzuri huu kwa namna yoyote ile tusingeweza kusimamia pasipokuwa na madiwani pamoja na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, hiyo kazi nzuri ambayo inafanyika na hata kwa sasa safari hii inaonekana tena fedha nyingi zaidi zitakuja, sasa mimi ombi langu ni vizuri na wale Waheshimiwa Madiwani tukaendelea kuwajali, lakini hali kadhalika na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa kwa sababu hao ndiyo wanaofanya kazi kubwa huko hasa tunapokuwa hatupo majimboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sambamba na hilo katika kuteleleza hayo, maana mimi bahati nzuri nimekuwa Diwani mwaka 2000 kabla sijawa Mbunge mwaka 2005 mojawapo ya mambo yaliyokuwa yanafanyika ilikuwa ni pamoja na kuboresha maslahi ya Madiwani lakini na kuwajengea uwezo ili waweze kuzisimamia. Sasa umezungumza vizuri katika hotuba yako, lakini bado hujazungumza namna ya kuendelea kuwajengea uwezo pamoja na maslahi yao kwa sababu wale watu wanasimamia fedha nyingi sasa, lakini ni kwamba uwezo wao kiuchumi ni mdogo sana. Kwa hiyo, nadhani hilo utakapokuwa unajibu ni imani yangu kwamba utalijibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine pamoja na miradi mingi na fedha nyingi tulizozipata kwangu pale Mheshimiwa Waziri, aidha, mambo yalifanyika kimakosa, aidha, kwa makusudi mfano, kwenye zile fedha zilizokuja fedha za tozo na fedha za UVIKO kwenye barabara mimi nipata shilingi milioni 500 peke yake nilipokuja kuuliza kulikoni nikaambiwa kuna fedha za *TACTICS* pamoja na miradi ya kimkakati. Sasa *at least* katika majimbo mengine zilipatika shilingi bilioni 1.5 mimi nimeambulia shilingi milioni 500 lakini mpaka leo hivi ninavyozungumza hakuna dalili ya fedha za kimkakati wala za *TACTIC*. Kwa hiyo, nitaomba wakati unasimama unieleze hilo, vinginevyo mimi ndiyo nitakuwa wa kwanza kuanza na shilingi yako Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sambamba na hilo ipo ile miradi mfano; fedha zimekuja, lakini vile vituo vya afya vya

zamani vilivyochoka, ninacho Kituo cha Afya cha Bwiru pale, leo ukikiona ni afadhali hata zahanati, lakini zipo shule za msingi kama Mtakuja yaani imechoka yaani ile inahitaji tui-*condemn*. Kwa hiyo, pamoja na mengine yote ningekuomba utakapopata nafasi baada ya Bunge hili twende Musoma nikutembeze na hivi wewe ni mjukuu wangu nitakutembeza mradi kwa mradi uweze kuiona ili uweze kuona kwamba ni kwa kiasi mtaweza kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilidhani kwamba kwenye upande huo Mheshimiwa Waziri hebu basi angalia namna ambavyo tutakavyopata fedha kwa ajili ya kufidia yale mapengo ya barabara ambazo hazikujengwa. Lakini cha ajabu zaidi sasa kwa miaka mitano mfululizo Musoma hatujawahi kupata fedha za maendeleo kwa ajili ya barabara hatujawahi yaani tofauti na fedha tulizo bahatisha za *World Bank* ambazo tumezipigania kwa muda mrefu hakuna fedha yoyote ambayo imeshakuja na ukiangalia kwa muda wa miaka mitano kwa namna ambavyo Madiwani wangu wanafanyakazi nzuri hatujawahi kupata hata hati chafu. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri ni imani yangu kwamba katika yale yote ambayo ni ya kimsingi katika kutusaidia mji wetu wa Musoma ili nao uweze kuendelea basi katika bajeti hii utaweza kusema namna ya kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niseme jambo moja ambalo ninadhani aidha tunaliona, lakini tunajifanya kama hatulioni. Mheshimiwa Waziri umetoa takwimu nzuri kwamba darasa la saba wanamaliza wanafunzi zaidi ya 1,130,000; kidato cha nne wanamaliza wanafunzi zaidi ya 880,000; kidato cha sita wanamaliza wanafunzi 80,000; tafsiri yake ni nini? Kwamba kumbe basi kila mwaka wanafunzi au vijana zaidi ya milioni moja wanaingia kwenye soko la ajira, yaani wanapaswa waanze maisha lakini ukiangalia sasa kama wanapaswa waanze maisha na jukumu mojawapo kubwa la Serikali ni pamoja na kuwapatia wananchi wake ajira, sasa leo ni tatizo ambalo linatutesa, kwangu mimi pale Musoma vijana wangu wengi hawana ajira, lakini hawana ajira sijasikia kwenye bajeti yako ni namna gani mmewatengenezea mazingira kwamba sasa kila wanapomaliza hawa zaidi ya milioni moja wakimaliza shule mmewaandalia

mazingira gani ya ujasiriamali aidha, mazingira gani ya kuweza kupata ajira.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilipomuuliza Mheshimiwa Bashe hapa swali la nyongeza alisema kwenye bajeti hii ameandaa fedha kwa ajili ya miradi ya kilimo kwa ajili ya vijana ili waweze kujiajiri, lakini wanatatizo moja kubwa la maeneo sasa nilitegemea kabisa kwamba na wewe hapo ungeweza ku-*chip in* kwa maana ya kutenga fedha kwenye kila halmashauri ili tuweze kuandaa maeneo ili atakapokuwa na fedha kwa ajili ya vijana basi tayari tuna maeneo ya kuweza kuwa-*accomodate*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine sambamba na hilo wapo vijana wetu wa kimachinga, wapo vijana wetu wa bodaboda, nashukuru kwamba hilo nililipigia kelele mwisho tukawa- *official rise* wanaendelea na shughuli zao pamoja na kwamba bado yapo mambo ya kurekebisha, lakini wale wamachinga wale ni watu ambao wao ili waweze kufanyabiashara wanatafuta watu walipo, sasa cha ajabu kila mnaposema mnawapanga tunawapanga kwenye maeneo ambayo hakuna watu na wao kwa sababu biashara yao ni ndogo ndogo maana yake ni kwamba lazima tuwaandalie maeneo ambayo tayari wapo watu. *(Makofi)*

Sasa kila mara hilo nalo hatujalitekeleza vizuri sana na hata katika bajeti yako sijasikia namna gani umeweza kuwagusa. Kwa hiyo, mimi niombe hapa sasa kwamba pamoja na Wizara yako na wizara zingine ni vizuri kipaumbele chetu kuliko yote ni pamoja na ajira kwa watu wetu ni imani yangu kwamba kila Wizara, juzi nilisikia hapa mfano; *TRA* wametangaza ajira 1000 napo wanajigamba kwamba ajira nyingi zimetoka ajira 1,000 hivi ninyi ajira 1,000 katika watoto zaidi milioni moja ambao kila mwaka wanakuwa tayari kwa ajili ya kuanza maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni imani yangu kwamba kila Wizara iwe na mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba inatoa ajira kwa kila mwaka na kwa kufanya hivyo basi tutakuwa tumewasaidia vijana wetu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nawashukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtaturu, jiandae Mheshimiwa Mafuwe, jiandae Mheshimiwa Kasaka.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mungu wa Rehema kutujaalia uzima na afya na wale wanaotekeleza Mwezi Mtukufu wa Ramadhani tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa neema hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, mama yetu, Rais Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya kwa ajili ya kuwaletea Watanzania maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wake tumeona maono yake, tumeona dhamira yake na kwa hakika tumeona huruma yake kwa ajili ya Watanzania na sisi tunao wajibu wa kuendelea kumuombea na kumuunga mkono sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri kwa kutuwasilishia hotuba nzuri leo asubuhi. Hotuba ambayo imetuonesha dhamira ya dhati ya ofisi hii katika kuwaletea maendeleo wananchi. TAMISEMI ndiko ambapo wananchi walipo wengi. TAMISEMI ndiyo inatoa huduma nyingi kule vijijini. Ukiongelea Halmashauri au Mamlaka za Serikali za Mitaa unaongelea wananchi wa kwenye vitongoji. Maana yake ni kwamba kule tuliko sisi wananchi. Kwa hiyo, leo tumeona dhamira ya Serikali kupitia Wizara hii na kwa hakika nimpongeze sana kaka yangu Mheshimiwa Innocent Bashungwa kwa namna ambavyo amekuwa akitupa ushirikiano kwa muda wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mara tumekuwa tukimpa ushirikiano na kero ambazo zipo kwenye maeneo yetu amekuwa akizitatua kwa wakati, kwa hakika tunasema wewe ni hazina ya Taifa na tunaendelea kukuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo hivyo kwa wenzetu Naibu Mawaziri wake Davis Silinde ndugu yangu pamoja na Ndugu Dkt. Ndugange mnafanya kazi nzuri sana. Kipekee kabisa Profesa Shemdoe pamoja na wenzake wote katika Wizara watendaji mnafanya kazi nzuri ya vijijini na niendelee kukumbusha tu kwamba kule Kipompo ambapo Profesa Shemdoe uliahidi shule ya msingi itapauliwa wananchi washajenga madarasa manne pamoja na nyumba ya mwalimu, tunasubiri mkapaue ili shule ile iweze kusaidia wananchi ambao watoto wanatembea kilometa tisa kutoka pale wanakoishi kitongoji cha Kipompo katika Kata ile ya Mang'onyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwa maana ya mwaka mmoja huu ambao tunauona, Halmashauri ya Ikungi tumepokea zaidi ya shilingi bilioni saba ambazo kwa hakika ni fedha nyingi sana za maendeleo ambazo leo tunaona ziko kwenye maeneo mbalimbali ya vijiji vyetu na zaidi tumeona jambo kubwa lililofanyika la kujenga madarasa 67. Tulipata jumla ya shilingi bilioni 2.6; ni fedha nyingi kwa wakati mmoja. Sisi tunashukuru sana na tunaipongeza Serikali kwa hatua kubwa ya mapinduzi makubwa ya kielimu katika Halmashauri yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikisema hayo pia tumepata eneo la vituo vya afya. Lakini nishukuru sana tumepata Hospitali yetu ya Wilaya imepata shilingi milioni 800 inakwenda kukamilika sasa ambayo tulikuwa hatuna huko nyuma. Lakini kwenye eneo hili niseme tu kwamba katika Kata zangu 13 za Jimbo la Singida Mashariki, Mheshimiwa Waziri mimi nilipata kituo kimoja tu. Kata 13 za Jimbo la Singida Mashariki tumepata Kituo cha Ntuntu. Nashukuru kwamba tumepata shilingi milioni 500 na tunaenda kumaliza kabisa tatizo la afya katika eneo lile la Kata ya Ntuntu ambayo iko mbali na Wilaya. Lakini kwa maana ya Kata 12 zilizobaki, niombe sana kwenye bajeti hii angalau tukipata vituo vingine vitatu tutakuwa tumegusa maisha ya wananchi. Tukiweza kupata Misuwakha, tukiweza kupata katika Kata ile ya Mang'onyi,

tukapata na Kata ya Isuna, tutakuwa tumesambaza vizuri huduma na tutawasaidia wananchi wetu kutembea kwenda kupata huduma mbali. Nikisema hivyo, kwa sababu naenda sambamba pamoja na watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi katika Halmashauri yetu ya Ikungi tuna upungufu wa walimu wengi sana. Walimu ukiangalia hesabu yetu tunahitaji walimu 2,685 lakini tunao walimu 1,305 tu maana yake tuna upungufu wa walimu 1,380. Walimu hawa ni wengi sana katika kuhakikisha kwamba tunaboresha elimu yetu. Leo tunataka ufaulu upande, lakini hatuwezi kupandisha ufaulu bila kuwa na walimu wa kutosha, hatuwezi kusema leo tunaenda kuongeza uwezo wa kufundisha watoto wetu kwenye shule za msingi, unakuta walimu wako watano kwenye shule ya msingi yenye watoto zaidi ya 700 usitegemee mapinduzi ya elimu katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru sana tumeweza kupata fedha katika shule shikizi, shule za Simbikwa, shule za kule Talu Mlimani, shule ya kule Mau, shule ya Mboghantigha tumepata kule ambapo sasa tumepata madarasa na shule zile zinakwenda kusajiliwa. Lakini leo hii tumepanga tusajili zile shule zianze, lakini ina mwalimu mmoja, wawili katika shule, usitegemee mabadiliko makubwa ya kitaaluma katika eneo lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana tuisaidie Idara ya Elimu ipate walimu wa kutosha ili hata Afisa Elimu anaposimamia awe na uwezo mzuri wa kuelekeza namna ambavyo Serikali inataka kuboresha elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiongelea eneo hilo nikikazia zaidi kwenye eneo la afya pia tunao upungufu mkubwa sana. Kuna zanahati unakuta ina mganga au *nurse* mmoja ni kilometa zaidi ya 60 kutoka Makao Makuu ya Wilaya na kila mwezi anatakiwa apeleke *report.* Siku anapeleka *report* au anakwenda benki kutafuta mshahara, ile zahanati inafungwa, huduma haitolewi, ugonjwa hauna taarifa, hauwezi kujua leo umepeleka *report*. Kwa hiyo, wananchi hawawezi kupata huduma kwa sababu hatuna waganga au wahudumu wa afya wa kutosha.

Niombe sana Serikali mnapokuja mje mtuambie mkakati ambao mmeupanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo hili la elimu, lakini pia na kuwasaidia vijana wetu ajira. Mimi niseme tu kwamba naishukuru Serikali tulipata fedha au tulitengewa shilingi bilioni mbili kujenga Chuo cha *VETA* pale Ikungi. Leo tunavyoongea mimi na wewe kile chuo sasa hivi kimesimama ujenzi. Watu wa *VETA* walipewa kandarasi ya kujenga kile chuo, namshukuru sana Naibu Waziri Mheshimiwa Kipanga ulikuja, ulivyokuja ukasema sasa tutabadilisha iende Halmashauri. Hivi ninavyongea wamerudisha tena imekwenda *VETA*, hivi ninavyoongea sasa hivi wale wakandarasi hawajalipwa, mradi umesimama, vifaa hakuna, zaidi ya mifuko ya *cement* 1,800 ilikuwa inaletwa Ikungi imepotea njiani. haijafika. Leo hii imesimama ujenzi, hakuna kinachoendelea na kuna watu wanadai. Usitegemee hawa vijana ambao tunategemea wakasaidiwe elimu pale hawana mahali pa kufundishiwa. Kwa hiyo, usitegemee kwamba tutapata mabadiliko ya kielimu au kusababisha ajira za wananchi wetu. Kwa hiyo, nilitaka nilieleze hili eneo katika kuhakikisha kwamba tunaboresha elimu katika eneo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie na suala la barabara; barabara kweli tumepata fedha shilingi bilioni 1.5 kwenye maeneo yetu imeleta mabadiliko makubwa tunaipongeza Serikali. Lakini kwa barabara za vijijini ambazo tunahitaji vivuko na madaraja, fedha ambazo tunasubiri hizi za pamoja na bajeti hatutengi tutakuwa tunategemea kitu ambacho hatujakipanga.

Kwa hiyo nimeona hapa kuna fedha mmeongeza kweli lakini fedha zile hazitoshi, mngekuwa kwenye fedha za maendeleo zinatoka moja kwa moja *TARURA* tunatenga kwa ajili ya vivuko na madaraja ili Mameneja wa Wilaya wabaki kwenye eneo la kutengeneza barabara tu na matuta. Lakini ukisema leo wafanye kazi ile ile shilingi milioni 800 haifiki hata shilingi bilioni moja kwa mwaka usitegemee mabadiliko ya barabara katika Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo niombe sana tuwe na mpango maalum wa fedha maalum ambazo zinakwenda kwa ajili ya kujenga madaraja na vivuko ili isaidie barabara zetu za vijijini. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE: MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo maneno naomba nirudie tena kushukuru, lakini naomba niseme naunga mkono hoja, kuna mambo ya kimkakati ambayo nitamuandikia Mheshimiwa Waziri kwa ajili ya maboresho. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Mafuwe, jiandae Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, ajiandae na Mheshimiwa Lazaro Nyamoga.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye Hotuba ya Waziri wa TAMISEMI na nianze kwanza kwa kupongeza wananchi wote wa Tanzania kwa namna ambavyo kwa kweli wanaiunga mkono Serikali pale ambapo Serikali inapeleka fedha wao wanaongezea. Tumeona ambavyo Serikali inapeleka shilingi milioni 12 kujenga madarasa wao wanaweka nguvu kazi na michango yao, nawashukuru sana. Lakini niwashukuru watumishi wote wa umma ambao ndiyo wanaosimamia fedha ambazo tunapitisha hapa, nasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwapongeze wasaidizi wa Waziri nikianza na Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu kwa kazi kubwa wanayoifanya, tunawashukuru sana. Lakini majemedari hawa watatu, Naibu Mawaziri wawili na Waziri wao, sisi watu wa Hai tumewapa majina; ndugu yangu Festo kule wanamuita mzee wa *nkwansira* na anajua kwa nini wanamuita *nkwansira* na ndugu yangu Silinde hapo wanamuita mzee wa *makeresho* anajua kwa nini wanamuita hivyo, Waziri nitakupa jina lako nikimaliza kuchangia hotuba yangu wanakuitaje kule Hai. *(Makofi)*

Kwa kweli kwa ujumla tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kutuletea vijana hawa wenzetu wachapakazi ambao kwa kweli wanabeba sura nzuri ya Tanzania, kazi zinakwenda kwa viwango vya hali ya juu. Mheshimiwa Rais tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niombe pia nimshukuru sana Waziri. Ninakushukuru Waziri na watu wa Narumu watu wa Hai kwa ujumla wanasema ahsante sana. Tulikuwa na barabara yetu ya kuanzia Mferejini kwenda Makoa kilometa 18 imeanza kujengwa kwa maandalizi ya kupokea lami, wewe umeniahidi unaenda kumaliza fedha zile ili lami ikamilike ya barabara ile, tunakushukuru sana. Lakini tunakushukuru umetuahidi barabara ile ya Bomango'ombe kwenda *TPC* kilometa 25 na yenyewe itajengwa kwa kiwango cha lami. Tunasema ahsante sana Mheshimiwa Waziri na sisi tunakuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijikite kwenye hotuba ya Waziri na nianze na eneo ambalo tumelijadili sana, mimi ni mjumbe wa Kamati ya USEMI. Eneo la asilimia 10 fedha ambazo zinatokana na mapato ya Halmashauri; fedha hizi zinakopeshwa makundi matatu, kundi la vijana, kundi la walemavu na kundi la wakinamama. Lakini wakati tunapitia taarifa hii kumekuwa na changamoto, fedha hizi zina matatizo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninasimama hapa kumshauri Waziri, na Waziri wewe umeshiriki kwenye Kamati umeona kilicholetwa pale. Fedha hizi zinatumika visivyo, fedha hizi taarifa zake haziko sahihi. Sasa ninaomba sasa hivi ukitazama kuanzia Januari mpaka leo kuna shilingi bilioni 35 ambazo zimekwishakopeshwa. Kwa hiyo, utaona ni fedha nyingi sana, lakini Mikoa imeleta taarifa ambazo zina mapungufu mengi sana ambazo hazioneshi marejesho kiasi gani yamerejeshwa, fedha kiasi gani zimerejeshwa na vikundi. Sasa ninachoshauri hapa; moja, ninaomba tulete sheria ile hapa ifanyiwe mabadiliko. Tufanye mabadiliko kwanza kuongeza kundi la wanaume, maana wakina baba wamesahaulika kwenye hili, nimeshashauri tena Bunge lililopita, lakini narudia tena na kwenye kamati tumesema

tuongeze wigo mpana ili na wanaume nao waweze kukopesheka na wanufaike na hizi pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Waziri kanuni zako ziongeze makali ili kuwe na akaunti maalum ya kupokea fedha hizi, lakini na akaunti maalum ya kupokea fedha za marejesho ili mwisho wa siku tuweze kuona kwenye *10 percent* tumekata kiasi gani, zile za marejesho ziko wapi tujumlishe za marejesho, tujumlishe zile asilimia 10 lakini tutoe fedha zao za usimamizi. Hizi zinazobaki tuone zinakopeshwa kwa kiwango gani. Lakini pia kama ambavyo tulishauri kwenye Kamati, naendelea kusisitiza ni muhimu sana tuwe na mfumo wa ku-*capture* mambo haya. Fedha hizi zitolewe kwa mfumo wa TEHAMA ambavyo Wizara inaweza kuona, *level* la Mkoa inaweza kuona na *level* ya Halmashauri na kwenye *level* zote hizo kuwe na watu ambao wana-*approval* ili kuondoa watu kukopa mara mbili, lakini kuweza kuwabana wale wanaokopeshwa waweze kurejesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba pia nizungumze kuhusu Tume ya Utumishi wa Walimu; Tume hii inafanya kazi nzuri, lakini Tume hii haijawa kamilifu. Walimu nchi hii wana mabosi wengi mno. Sasa nilikuwa naomba hapa Waziri tuone namna sahihi ya kuifanya Tume hii iwe bora, tuiongezee nguvu ili kama tukiamua ndiyo Tume ya kusimamia walimu ifanye hivyo kuliko mwalimu anasimamiwa na TAMISEMI, kila mtu ni kiranja wa mwalimu. Sasa mwisho wa siku tunajikuta hawa Walimu tunawapa mzigo mzito ambao wanashindwa kuisimamia kazi yao ya kitaaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana sana kaeni chini muone namna ya kutuletea tufanye mabadiliko, walimu wawe *centralized somewhere* wasimamiwe na chombo kimoja ambacho kwa mawazo yangu Tume ya Utumishi wa Walimu ingefaa kuwa chombo sahihi cha kusimamia walimu Tanzania na kuwaacha walimu kutokusimamiwa na watu wengi kama ilivyo sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia naomba nishauri jambo linguine, tunaenda kupitisha hapa bajeti na kwenye bajeti hii vifungu vya usimamizi vimeongezeka sana na kupelekea matumizi

ya miradi kushuka zaidi ya asilimia 14 jambo ambalo ni zuri na ofisi ya ma-*DC* zimepata fedha za kutosha.

Naomba kushauri hapa ofisi za Maafisa Tarafa ambapo ni kiungo kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa hao Maafisa Tarafa wamekuwa watu wa kuishi kwa hisani kitu ambacho siyo sawa, sasa ofisi za ma-*DAS* zimepewa fedha. Mimi niombe wapewe *special vote* ya kwao. Kwa sababu ofisi ya Afisa Tarafa inajitegemea wapewe *sub-vote* yakwao ili kwamba kama wanahitaji matumizi yao fedha ziende kule kuliko ilivyo sasa hivi pesa zinapelekwa ofisi ya *DC* halafu inakuwa ni utashi wa *DAS* kuwapa au kutokuwapa. Kwa hiyo, niombe sana hawa watu wanatusaidia kwenye usimamizi wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niombe tutazame tena, wenzangu hapa wamezungumza kuhusu posho za Madiwani. Mimi niseme kwa Madiwani tumefanya vizuri, lakini tuone namna ya kuwaongezea na Wenyeviti wa Mitaa. Tufike mahali pia tutazame hata Watendaji walioko kule, tunafahamu wanapata mishahara yao, lakini hebu tuwatazame namna ya kuwapatia mafunzo ili na wao waweze kufanya kazi kwa wakati. Wakati mwingine tunapeleka tu, tunashindilia maagizo kule kwa Watendaji wa Vijiji, Watendaji wa Kata lakini hatuwapi taaluma ya nini kinatakiwa kufanyika kwa wakati ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ninaomba nizungumze kuhusu miradi ya kimkakati; hii miradi ya kimkakati wenzangu hapa wameeleza masoko maeneo mengi hayakufanya vizuri, kwa sababu walioibua mikakati ile hawakutufikisha mwisho.

Mimi niseme Mheshimiwa Waziri pale Hai tuna soko la Kwa Sadala tayari tumeshakuletea ramani hapo. Mimi niombe hebu tukajifunze pale Hai kwa kujenga hilo soko. Lile soko letu lina kitu cha tofauti, mle ndani tumeweka *sorting industry*, mle ndani tumeweka viwanda vya kufungashia, mle ndani tumeweka viwanda vya kuongeza thamani mazao. Lakini pia tumeweka sehemu ya wakinamama kuwaacha watoto wao wapumzike pale kama *day care center*, na soko liko mjini pale Kwa Sadala. Soko ambalo ukitazama linapokea karibu kata zote na nchi nyingi zinakuja kununua pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niombe huu mradi Mheshimiwa Waziri tafadhari sana mtusaidie na ni ahadi ya Mheshimiwa Rais. Rais mwenyewe ameahidi pale mara mbili soko hili la Kwa Sadala, tafadhalini sana mtusaidie lijengwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme jambo moja jana nilikuwa kwenye msiba kwenye Kata Uroki pale Uswaa. Mheshimiwa Waziri kila aliyekuja kunipa mkono pole Mheshimiwa Mbunge alikuwa ananiambia tuna barabara yetu; barabara ya Uswaa – Kwa Sadala; Uswaa - Bwani kuna mahali ambapo pale Uroki pa kupandia juu hapapitiki kabisa na ile barabara ndiyo tunategemea ipitishe ndizi zile Kwa Sadala, ipitishe ndizi zije Dar es Salaam, zije kwetu hapa Dodoma. *(Makofi)*

Niombe sana, inawezekana nimekuomba maombi mengi ya lami na wewe umeniahidi lakini hii basi hata changarawe, angalia fungu chochote unachoweza kupata hata kwa kipande kile kidogo cha pale kwenye bonde la kushuka Uroki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Kasaka jiandae sasa na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Nyamoga.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na mimi kupata nafasi niweze kuchangia kwenye hotuba nzuri sana ya Ofisi ya TAMISEMI.

Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wake, vijana mahiri, wachapakazi, wanaokimbia huku na huku na mimi nawashukuru sana Waziri pamoja na Naibu Mawaziri wote wameshafika Chunya, tunawashukuru sana kwa kazi nzuri ambayo wamendelea kufanya, lakini pia tuipongeze Serikali yetu ya Awamu ya Sita kwa namna ambavyo imeweza kushusha miradi mingi kupitia TAMISEMI, imeweza kushusha fedha nyingi sana kupitia TAMISEMI, tumpongeze sana Mama yetu Samia Suluhu kwa kazi kubwa

ambayo anaendelea kufanya na ninyi kama wasaidizi wake mmekuwa mnaweza kumsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wote tumekuwa mashahidi namna ambavyo fedha hizi zimekuwa zinakwenda kwenye majimbo yetu na kwenye Wilaya zetu. Nianze tu kuzungumza kwenye upande wa *TARURA*. Tumeona namna ambavyo kila mmoja hapa ameweza kuguswa na pesa nyingi sana ambazo zimekwenda kwenye upande wa kujenga barabara hasa barabara ya *TARURA*. Pesa hizi zimeshuka nyingi ambazo zimeweza kwenda kule kwenye vijiji vyetu, kwenye kata zetu, kwenye Wilaya zetu na ameweza kuchechemua uchumi wa kwenye maeneo yetu yale na kwa mara ya kwanza sisi tumeweza kupata fedha nyingi, kwa Wilaya ya Chunya peke yake tumepata zaidi ya shilingi bilioni 2.3. Ni fedha nyingi ambazo tumezipata kipindi chochote ambacho Wilaya hii imeumbwa, tuipongeze sana Serikali kwa kazi kubwa ambayo imeendelea kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pesa hizi pamoja na kufika huko tumeona namna ambavyo zimeweza kuchechemua uchumi wa nchi, namna ambavyo wakandarasi wameweza kuzidiwa kwa miradi mingi waliyokuwanayo. Leo hii wakandarasi tunawadai kazi siyo pesa, pesa zimekwenda huko nyingi za kutosha, lakini wao ndiyo wamekwama kutekeleza kwa wakati. Aidha, hawana vitendea kazi, hawana wataalam wa kutosha ambao imepelekea mpaka hii miradi kwenda kwa kusuasua. Lakini kwa upande wa Serikali tumeona kwamba fedha zimeweza kwenda kwa wakati. Zimeweza kwenda kwa wakati, tunaweza kuipongeza sana Serikali hii imeweza kufanya mambo makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja nakufanya mambo makubwa haya tuwapongeze tumeona kwenye hotuba yako hapa ya bajeti yale mawazo tuliyokuwa tukiishauri Serikali mara kwa mara mmeweza kuyachukua. Tulikuwa tunawaambia kwamba mwaka wa fedha unaanza Julai, ninyi mlikuwa mnakaa mnasubiri Julai mwaka wa fedha unapoanza ndiyo mlikuwa mnaanza kutangaza *tender* kwa ajili ya kufanya hizi kazi za ujenzi wa barabara. Lakini tumewashauri mara kadhaa, nimeona

kwenye bajeti yako umesema. Sasa haya mmeyapokea na mmeweza kuyafanyia kazi. Sasa hivi mnaanza kutangaza hizi *tender* ili kuanzia mwezi Julai mwaka wa fedha unapoanza maana yake watu wanapewa sasa mikataba hii na kazi zinaanza kwenda kwa wakati. Hii tunawapongeza sana na kwa kweli ule utaratibu wa nyuma ule ulikuwa unatukwamisha sana. Leo hii sisi kwa Chunya unakuta fedha zilitoka toka mwaka jana mwezi wa nane wa tisa leo ndiyo miradi ya barabara inatekelezwa. Watu wamepata shida kipindi chote cha masika wakati fedha zipo. Lakini kwa utaratibu huu ambao mmeanza nao mmetuambia leo kwa kweli tunawapongeza sana mmechukua ushauri wetu uliokuwa mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hayo tumeona kwamba sasa *TARURA* pamoja na kazi nzuri ambayo wanafanya lakini na wao pia kuna changamoto wanazo, wana changamoto za wafanyakazi, za ma-*engineer,* sisi Wilaya yetu ya Chunya tuna ma-*engineer* watatu *almost* kama wanne, Wilaya ni kubwa sana kwa Mkoa wa Mbeya tunakaribu ya eneo la ukubwa zaidi ya asilimia 40 ya Mkoa mzima wa Mbeya, sasa unapotupa wahandisi watatu, na bosi wao mmoja pale Mkuu wa Idara maana yake unatulinganisha sisi na Wilaya nyingine, sisi tunakuwa kwenye wakati mgumu kwenda kusimamia hii miradi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake kule barabara za vijijini zinakosa usimamizi mzuri wa ma-*engineer* hawa waweko kule kwa wakati barabara zinajengwa wakati mwingine wakati mwingine zinajengwa mkandarasi anajenga chini ya kiwango, lakini mainjinia wetu hawa wanashindwa kufika maeneo husika kwa wakati kuweza kusimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi nishauri kwenye ajira ambazo zinakuwa zinatolewa hizi pamoja na kuajiri ma-*engineer* hawa tuajiri pia na wale ma-*engineer* wa kati wale ma-*technician* wawepo, wawe ndio wanashinda kulekule *site* muda wote, wataweza kutusaidia sana kuhakikisha kwamba thamani ya fedha inayotolewa inakwenda sambamba na kazi ambayo inakwenda kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine kwenye upande wa *TARURA* ni vitendea kazi hasa magari. Wilaya zetu hizi zinatofautiana Wilaya za mjini na wilaya za vijijini, Wilaya ya mjini ukiwapata magari ya kawaida, ukiwapa *pickup* za kawaida, wao zinaweza zikawasaidia sana, lakini kwa Wilaya zetu sisi zenye miundombinu mibovu ya barabara kama Wilaya yetu ya Chunya kuweza kuwapa *pickup* ya kawaida ni ngumu sana utekelezaji wake kwenda kusimamia hii miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niombe sana wakati ugawanyaji huu wa rasilimali hizi za magari unafanyika Wilaya sisi hizi zenye miundombinu dume tuweze kupata yale magari ambayo yanaweza yakahimili, tuweze kupata *landcruiser pickup* ziweze kufanya kazi kule. Leo tunapozungumza hapa sisi pale Wilaya ya Chunya tuna *pickup* moja ambayo *pickup* yenyewe bado ni mbovu, leo ni spana mkononi matokeo yake ma-*engineer* wanashindwa kwenda kufanya kazi kufikia miradi kwa wakati, kila siku wanabisha hodi kwa Mkurugenzi kwenda kuomba magari pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niombe sana kwenye bajeti zenu hizi mnapotenga vitendea kazi muone miundombinu ya Wilaya za vijijini hizi tuweze kupata magari ambayo yataweza kutusaidia kuweza kufikia na kuweza kusimamia hii miradi kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine lakuweza kuchangia ni kwenye upande wa elimu, niipongeze Serikali imefanya kazi kubwa, imeweza kujenga miundombinu ya majengo vizuri sana, sisi sote tumekuwa mashahidi tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita ya Mama Samia, tunashukuru sana viongozi wa Wizara, pamoja na kazi kubwa hii iliyofanyika leo hii majengo yetu kule yanakuwa hayajaweza kutumika ipasavyo, majengo yamekamilika watoto wapo lakini hatuna walimu wakuweza kwenda kuwafundisha watoto wetu. Lakini pamoja kwamba shule shikizi zimejengwa kule na leo hapa naona umezungumza kwamba zitaendelea kwenda kujengwa, tuone namna ambavyo hizi shule shikizi tuwapeleke walimu ambao wanaweza wakakaa kwenye mazingira yale, na walimu

wanaweza kukaa kwenye mazingira yale tunao sasa hivi walimu wapo wanaojitolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira zinapotoka hizi wao ndio tuwape kipaumbele kwa sababu tayari wameweza kumudu yale mazingira, ajira zilizopita awamu iliyopita tumeona walimu wanaojitolea wameachwa, sasa tunaomba sana awamu hii walimu wanaojitolea wale waweze kupewa kipaumbele cha kwanza hii itaweza kutusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niwapongeze mnasema mnakarabati shule kongwe sisi pale Chunya tuna shule zetu kongwe za miaka mingi toka enzi hatujapata uhuru, shule ya msingi ya Chunya kati, shule ya msingi ya Mjini pale tumerithi kutoka kwa Wamisionari, zimechakaa zimeharibika zimekuwa za muda mrefu sana sasa shule shikizi zinakuwa ni nzuri kuliko zile shule ambazo zilikuwa muda mrefu na ziko katikati ya mji. Tuombe sana mnapotenga kwenye bajeti yetu zile shule kongwe muweze kuzikumbuka na hizi shule tutaweza sana kuendana sambamba ya utoaji wa elimu bora tunayoendelea nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na haya walimu tutawapeleka kule tuone namna ya kuweza kuwasadia kuwajengea nyumba kule kwenye shule shikizi kule kuna maeneo mengine sisi wanakokaa wafugaji kule hata nyumba ya kupanga mwalimu hakuna, sasa tuone namna ambavyo kupitia Wizara yenu, mkishirikiana pamoja na Wizara ya Elimu kuona namna ambavyo mtaweza kujenga nyumba za walimu ili walimu wetu hawa waweze kufanya kazi katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho nizungumze habari ya afya na yenyewe tunaipongeza Serikali mmefanya kazi vizuri, miundombinu ya afya imejengwa vizuri vituo vya afya vinajengwa, zahanati tunaona zinajengwa na kwa kweli kazi inayofanyika maana yake tunaenda kuwajali Watanzania kuhakikisha kwamba wana afya bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja kwamba miundombinu hii ya majengo yanajengwa lakini bado tuna changamoto ya vifaatiba; vifaatiba kwenye zahanati zetu na

kwenye vituo vya afya hatuna mimi nikupe mfano tuna Kituo cha Afya cha Mtande kimekamilika toka mwaka 2019 lakini mpaka leo hakina vifaatiba pale, sasa hiko ni kimoja ambacho ni Kituo cha Afya cha Mtande, lakini tuna Kituo cha Afya cha Makongolosi kimekamilika, tuna Kituo cha Afya cha Matwiga, na sasa hivi tunaenda kukamilisha Kituo cha Afya cha Kambikatoto vyote hivi havina vifaatiba, tuombe sana Serikali inapofanya mambo haya...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana ya pili hiyo kwa mchango mzuri sasa mchangiaji wetu wa mwisho.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nashukuru na naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Justin Nyamoga.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nichukuwe fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwepo hai hadi wakati huu, lakini jambo la pili niishukuru sana Wizara ikiongozwa na Waziri Mheshimiwa Bashungwa pamoja na Manaibu Waziri na watumishi wote katika wizara hiyo kwa ushirikiano ambao wanaendelea kunipa mimi pamoja na wananchi wa Kilolo katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais pia kwa jinsi ambavyo Kilolo imeanza na inaendelea kukumbukwa sasa kwa mambo mengi tofauti sana katika historia ya Jimbo la Kilolo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo madarasa ya sekondari 73 yamejengwe, shilingi milioni 800 Hospitali ya Wilaya karibu inakamilika kwa mara ya kwanza tangu uhuru tulikuwa na kituo kimoja cha afya, tunajenga vituo vya afya vinne kwa mpigo

Ruaha Mbuyuni, Ilula, Nyarumbu pamoja na Ng'ulule vituo vinajengwa, lakini pia tunayo sekondari Kata ya Kimara haikuwa nayo inajengwa pamoja na mambo mengi nikiorodhesha nitamaliza muda wangu kwa kushukuru tu, lakini sasa naomba niende kwenye mambo mengine.Tunashukuru sana kwa ushirikiano ambao tunaendelea kuupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya kwanza nitakayoizungumzia inahusu mapato ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo; zaidi ya asilimia 50 ya mapato ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo inatengemea mazao ya misitu, mazao ya misitu tunayozungumza maana yake ni pamoja na nguzo, mbao na mazao mengine yanayofanana na hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nieleze ili Wizara ya TAMISEMI ijue athari zitakazotokana na maamuzi ya Wizara au idara nyingine za Serikali kuamua kununua nguzo nje ya nchi hii, tutakapoacha kununua nguzo kutoka kwenye Kiwanda cha *New Forest* kilichopo Wilaya ya Kilolo maana yake ni kwamba tujiandae kupunguza mapato ya Kilolo kutoka shilingi bilioni 4.5 sasa hizi kwenda shilingi bilioni mbili na *point* na kwa hiyo Serikali ijiandae kuleta fedha kuja kuweka hiyo nakisi hatutakuwa na hizo fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kwa hiyo nataka Waziri anapoongea na Mawaziri wengine pamoja na Serikali inapozungumza ilijue hilo, athari za huo uamuzi ni nini kwenye mapato ya Serikali, ninaomba hili lieleweke vizuri ili nitakapokuja hapa kuomba fedha zaidi kutokana na kupunguza mapato baada ya hayo maamuzi ya kununua nguzo nje Serikali ikumbuke kwamba mimi nilisema na hii iwekwe kwenye rekodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu la pili ni kuhusu miradi ya kimkakati; Mheshimiwa Waziri bahati nzuri ulikuwa Wizara ya Viwanda na Biashara na ulitembelea Kilolo na bahati nzuri ulitembelea mashamba ya chai, nataka nikuambie mradi wa kimkakati uliletwa mwaka 2018 kwa ajili ya ununuzi wa mitambo kujenga kiwanda kile cha chai hata jibu hadi leo halijawaji kupatikana kwamba ni mbovu, una nini, hatujapata jibu

na kiwanda hakijajengwa na bahati nzuri na Waziri wa Kilimo yuko hapa anajua tunavyoangaika kutafuta fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mmejenga masoko sawa, mmejenga *stand* huko sawa mngetuambia basi sisi Kilolo tumekosea nini kwenye kuandika ili tuweze kupewa fedha tuweze kujenga kile kiwanda cha chai ambacho kinaajiri watu 2,000 na sisi kwetu watu 2,000 ni wengi, ambacho kitaongeza uzalishaji kwenye chai na tutaongeza mapato ya Halmashauri kwa sababu yale mashamba yanamilikiwa kwa asilimia 40 na Halmashauri, kwa asilimia 10 na Msajili wa Hazina ambayo ni Serikali tena hiyo Hazina inayotoa hela hayo mashamba yanamilikiwa kwa asilimia 50 na wananchi kule hayamilikiwa na taasisi binafsi, inashindikanaje kutoa fedha kwa ajili ya ule mradi wa kimkakati pale?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalo lile andiko kama limepotea au liko mahali niko tayari kukuletea twende mguu kwa mguu Hazina tupate zile fedha kile kiwanda kipate kujengwa na mitambo inunuliwe na zile hela sio nyingi ni kama tu shilingi bilioni tatu ambazo kule mmetoa shilingi bilioni 60 majengo makubwa tunashindwaje kutoa fedha kidogo hivi kwa ajili ya kiwanda cha chai kilichokaa miaka 30 hakijengwi na hela zipo kila siku tusomee miradi ya mkakati ya mijini na sisi tunataka hizo fedha kwa ajili ya mradi wa kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya jambo hili naomba pia nizungumzie kuhusu vifaatiba; ninashukuru sana kwamba umejengwa vituo vya afya vizuri pale Ruaha Mbuyuni mmetupa na hata shilingi milioni 300 juzi tumalizie maana kile kilianza kujenga mwaka wa fedha uliopita na pia pale Ilula tunacho na ninyi mnajua haya ni maeneo ya barabara kuu, sasa hivi karibuni kulitokea ajali pale Ruaha Mbuyuni watu walipelekwa pale nadhani ni kama watu tisa au kumi ambao walihitaji huduma kwanza, madaktari hakuna, lakini vifaatiba havipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa maeneo kama haya tumeambiwa kuna ajira zinakuja maeneo ya barabarani, maeneo yenye Vituo vya Afya ambavyo vinahitaji *attention* kubwa kwanza madaktari wapelekwe, lakini pili tutafute uharaka

wa kupeleka vifaatiba kwa sababu pale sikutakiwa peke yangu nisimame, Wabunge wote humu mnapita Ilula, Wabunge wengi humu mnapita Ruaha Mbuyuni mnapoenda kwenye sehemu zenu huko, hili ni suala la sisi wote na wananchi wote wanaopita mle kwa sababu hatuwezi kujua ya kesho, ninaomba sana vifaatiba kwenye hivi vituo vya afya viwili ambavyo vimekamilika, ninawashukuru sana vifaatiba vipewe kipaumbele kwa sababu ya unyeti na umuhimu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo moja ambalo ningependa kulizungumzia nalo ni suala zima la *TARURA* pamoja na fedha na jinsi zinavyotolewa, mambo mawili; jambo la kwanza ni suala zima la magari ambalo limeshazungumzwa na vifaa, tulipokuwa kwenye Kamati mimi ni mwamakamati wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, tulipokuwa kwenye kamati tuliona kwamba kweli fedha za magari zimetolewa, lakini mamlaka zinazonunua hazijanunua zaidi ya magari 100 na fedha zimeshalipwa, haya magari yangeweza kugawa kwenye hizi Halmashauri yangetosha, kupunguza angalau hiyo kero.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuiombe Serikali kwa sababu ni hiyohiyo tujue kikwazo kinachozuia magari haya kununuliwa na kugawiwa kwa hawa hiyo mamlaka ingekuwa ni taasisi binafsi imepewa fedha za magari zaidi ya 100 hainunui mwaka mzima, hicho ni kiashiria kinaweza kupeleka hadi kwenye karibu na uhujumu, sasa ni Serikali hatuwezi kuita hivyo. tunafanyaje kuhusu watendaji au mahali popote panapokwamisha ununuaji wa haya magari? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili *TARURA* ina sema kwamba wanasajili barabara, sasa barabara inayosajiliwa ni kwamba imetengenezwa yako maeneo kama kule kwangu kwa mfano pale kutoka Idete ili ushuke kule Mngeta ni pori, pana mchoro wa barabara, lakini ni msitu, kila tukienda pale wanasema tengenezeni ili tusajili, atengeneze nani na ile ni hela nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ni lazima itobolewe ile barabara kama ingelikuwa ni ndogo kwa hela ndogo lakini barabara kubwa kama ile lazima itengewe fedha ili itoboke na ile

ni barabara muhimu kiuchumi, ndio tungeweza kusafirisha mbao kwa treni kwenda Dar es Salaam, lakini hatuwezi kuitoboa kwa mikono, walijaribu pale walienda wananchi walishindwa ni sehemu ambayo ni lazima Serikali iwekeze. Ninaomba *TARURA* kwa dharula itenge fedha kwa ajili ya kutoboa barabara ile ili iweze kufanikiwa na kufanya kazi. Nakuomba sana kupitia kwako namuomba sana Waziri aingalie barabara kama hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na barabara nyingine ambazo ni muhimu kiuchumi nataka kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge mkila njegele, viazi na hizo mbogamboga nyingine zote kwa asilimia kubwa zinatoka Kilolo.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara kama ya kutoka Kitoo kwenda Masisiwe, barabara kama ya kutoka Ihimbo kupitia Itimbo kuja kutokea Kitelewasi ambako ndo mahindi mengi mnakula haya ya njiani, barabara ya kutoka Nyanza kwenda Mtandika vitunguu karibu vyote vinatoka huko hizi barabara zinahitaji ile milioni mia tano tu na ndio maana wakati ule nikakuambia mimi nikipata shilingi bilioni 1.5 inapunguza sana hizi kero. Lakini si kwa ajili yangu tu ni kwa ajili ya Watanzania wote wanaoatarajia mazao kutoka kule lakini pia kwa ajili ya kuongeza mapato ambayo yanaweza kutusaidia.*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri.

Nikushukuru sana Kaimu Waziri Mkuu kwa kazi nzuri unayoifanya, Mheshimiwa *Chief Whip* kwa kazi nzuri mawaziri wote na tuombe hili ya nguzo mlitizame vizuri.

Mimi juzi nilikuwa kwenye mkutano wa *European Union* na *African Caribbean and Pacific countries* walikuja na *resolution* za *carbon adjustment mechanism,* wanaanzisha wao utaratibu wa

*green deal* na *green deal* kwao ita-*trickle down* kwetu sisi kwa maana ya *production* zozote za *agro products* ambazo zitaathirika au zitachangia sio tu zitakosa soko na zinaweza zikatozwa kodi kubwa.

Lakini Tanzania tulisimama na tulizirusha na tukaipiga chini sababu itatuuwa kibiashara. Kwa hiyo mtizame kwa wale wanaokwenda kwenye mikataba ya *EPA* lakini swali ikawa hizi nguzo mnapewa masharti kutokuvuna sababu walete nguzo zao, kwa hiyo nasema tu mjaribu kutazama hili muweze kunini. *(Makofi)*

Sasa juzi Waheshimiwa Wabunge nilisema Wabunge Viti Maalum wapitepite pale niwajue, lakini sasa hawaji matokeo yake kaja Getere kaja sijui Kishimba watu ambao wala siwahitaji, niombe tu tuendelee kunini. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, nawapongeza sana kwa michango mizuri na naahirisha shughuli za Bunge mpaka tarehe 19 Aprili saa tatu asubuhi.

*(Saa 7.35 mchana Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumanne, Tarehe 19 Aprili 2022 Saa Tatu Asubuhi)*